**27 APRILI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 27 Aprili, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa niaba yake, Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali kwa Waziri Mkuu. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametuwezesha kushiriki Kikao hiki cha Kumi na Nne cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako tukufu tukiwa buheri wa afya. Aidha, itakumbukwa kuwa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 zimetoa fursa ya uwepo wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu kwa kila siku ya Alhamisi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kanuni hizo nilizozitaja katika kipengele cha 44(4), zimeruhusu Waziri Mkuu kutumia Kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kutoa taarifa au ufafanuzi kuhusu suala lolote linalohusiana na Shughuli za Serikali na lenye maslahi kwa umma. Kwa mantiki hiyo, naomba uridhie nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi kuhusu changamoto mbalimbali zinazojitokeza

katika kusimamia masuala ya uhifadhi na namna ambavyo Serikali imekuwa ikizishughulikia.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kutoa ufafanuzi huu kutokana na mwenendo wa masuala mbalimbali yanayoendelea kwenye jamii yetu kuhusu masuala ya uhifadhi kama vile uvamizi wa maeneo ya uhifadhi, athari zinazotokana na kuongezeka kwa idadi ya wanyama waharibifu na wakali na kudorora kwa mahusiano kati ya wananchi na mamlaka zenye kusimamia uhifadhi huo kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Bunge lako Tukufu katika nyakati tofauti limewahi kupokea hoja kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakilalamikia changamoto hizo hususan kwa yale maeneo yanayopakana na hifadhi zetu. Kadhalika katika ziara zangu kwenye maeneo mbalimbali nchini, nimekuwa nikipokea malalamiko kutoka kwa Wawakilishi wa wananchi na wakati mwingine wananchi wenyewe wamekuwa wakiwasilisha kero hizo.

Mheshimiwa Spika, nyote mtakubaliana nami kwamba ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo, ufugaji na makazi, sambamba na kuimarika kwa shughuli za uhifadhi, kumechangia kwa kiasi kikubwa changamoto nilizotangulia kuzieleza. Kwa mfano, shughuli za kibinadamu zimekuwa chanzo cha wananchi kuingia katika maeneo ya hifadhi kwa kujua ama kwa kutojua na kuendeleza shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Kwa upande mwingine kuimarika kwa shughuli za uhifadhi kumewezesha baadhi ya wanyama kama vile tembo kuongezeka na hivyo kusababisha uharibifu wa mazao na wakati mwingine ulemavu na hata vifo kwa baadhi ya wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na hifadhi.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa hali ya uhifadhi unaonesha kuongezeka kwa uharibifu wa maliasili na mazingira katika maeneo mengi hapa nchini. Miongoni mwa maeneo yaliyoathirika ni misitu. Kwa mfano, kiwango cha kutoweka kwa misitu kwa mwaka kimeongezeka kutoka hekta 372,800 kwa makadirio ya mwaka 2015 hadi hekta 469,420 kwa makadirio ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kueleza kwamba, ongezeko la shughuli za kibinadamu ikiwemo usafishaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo, ufugaji, uchomaji moto holela na matumizi mengine yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu yakichagizwa na ongezeko la idadi ya watu, ni miongoni mwa changamoto kubwa za uhifadhi. Athari za vitendo hivyo tumezishuhudia kwenye baadhi ya maeneo nchini ikiwemo uharibifu katika Hifadhi za Ruaha na Bonde la Mto Ruvu. Hali hiyo inachangia kuleta mabadiliko ya tabianchi na athari zake kama vile ukame, kuongezeka kwa joto, mafuriko na mabadiliko ya misimu ya mvua.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni ongezeko la idadi ya baadhi ya wanyamapori wakali na waharibifu wakiwemo tembo na mamba. Changamoto hiyo ambayo inasababishwa na kuimarika kwa shughuli za uhifadhi pamoja na ongezeko la shughuli za kibinadamu, imekuwa chanzo cha migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Hali hiyo imesababisha madhara kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi, ikiwemo kuuawa na wanyamapori wakali, kuharibiwa mazao yao na wakati mwingine kuingia katika migogoro na mamlaka za uhifadhi ambazo pia zinasimamia maeneo hayo. Baadhi ya maeneo yaliyoathirika na changamoto hizo ni pamoja na Wilaya ya Bariadi, Itilima, Tarime, Serengeti, Liwale, Nachingwea, Chunya na Songwe.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo, sambamba na kuhakikisha tunalinda, kutunza na kufanya maliasili zetu kuwa endelevu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali tena za makusudi katika kufanikisha masuala hayo. Kama mnavyofahamu, Serikali inasimamia maeneo yaliyohifadhiwa kisheria yenye ukubwa wa kilometa za mraba takribani 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 22, eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori 38, maeneo matatu ya Ardhi Oevu chini ya Mkataba wa *Ramsa Site,* Hifadhi za Misitu ya Asili 465, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 20, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 10, Maeneo ya Malikale 133 na vituo saba vya Makumbusho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha maeneo haya muhimu ya urithi niliyoyataja yanalindwa, yanatunzwa na kuendelezwa, Serikali imekuwa ikisimamia kikamilifu Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya mwaka 2009 pamoja na sheria nyingine zinazosimamia maeneo yaliyohifadhiwa. Sheria hizo, pamoja na mambo mengine, zimekataza masuala mbalimbali kufanyika ndani ya maeneo ya hifadhi ikiwemo wananchi kuingia ndani ya maeneo hayo bila vibali, shughuli za kijamii, kilimo, ufugaji, uvuvi, uwindaji haramu na uvunaji haramu wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine ya kuimarisha shughuli za uhifadhi, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Jeshi la Uhifadhi, imepewa dhamana kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama ili kuwa na hifadhi endelevu kwa maslahi ya Taifa letu. Serikali imeendelea kuchukua hatua hizo kwa kutambua umuhimu mkubwa wa maliasili zetu katika kuchangia pato la Taifa na ustawi wa jamii kupitia shughuli za

kiuchumi ikiwemo utalii na uuzaji wa mazao ya misitu pamoja na nyuki. Mathalani asilimia 90 ya vifaa vya ujenzi na samani zinazotumika majumbani zinatokana na misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za misitu na nyuki huchangia asilimia 3.3 ya pato ya Taifa. Asilimia 5.9 ya mapato yotakanayo na biashara ya nje na ajira takribani 4,000,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Vilevile asilimia 90 ya umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji unatokana na vyanzo vya maji ambavyo vingi vipo katika maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, utalii huchangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na uzalisha ajira takribani milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mchango huo mkubwa wa maliasili zetu kwenye uchumi wa Taifa umekuwa chachu ya Serikali kuimarisha shughuli za uhifadhi hapa nchini. Serikali inachukua hatua hizo ili kuhakikisha kuwa urithi huo wa maliasili na malikale umekuwa endelevu na kunufaisha vizazi vilivyopo sasa bila kuvisahau vizazi vijavyo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi kote nchini kwa ujumla tutambue kwamba kama ambavyo sisi tulirithishwa na wazee wetu, tunao wajibu wa kuzilinda, kuzitunza na kuziendeleza maliasili zetu kwa ajili ya vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto kubwa za uhifadhi ambazo Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanaoishi katika maeneo ya mipakani na hifadhi wamekuwa wakiziibua ni pamoja na migogoro ya ardhi kati ya wananchi na hifadhi na kutokuwepo kwa mahusiano mazuri kati yao na mamlaka za uhifadhi. Serikali kwa upande wake inachukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kuwa inashughulikia migogoro hiyo. Mojawapo ya hatua hizo ni kuendelea kudhibiti uvamizi katika maeneo ya uhifadhi, kutatua migogoro inayohusiana na

mwingiliano wa shughuli za wananchi na uhifadhi pamoja na kuimarisha uhusiano bora kati ya uhifadhi na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Serikali imeunda Kamati ya Kitaifa ya Mawaziri wanane kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi hapa nchini;

(ii) Serikali imemega baadhi ya maeneo ya Hifadhi ya Taifa, Mapori Tengefu na Misitu na kugaiwa wananchi ili waweze kuendesha shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Jumla ya vijiji 998; vile vya awali 975 pamoja na vijiji 23 vilivyoongezwa vya kule Mbarali vimefanya jumla ya 998, hivi vyote vimekabidhiwa kwa wananchi kuendesha shughuli zao za kilimo, ufugaji na makazi;

(iii) Kusafisha maeneo ya mipaka ya hifadhi na kuweka vigingi na mabango yenye kutoa uonekano wa kutosha;

(iv) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi endelevu na kushiriki katika ulinzi wa maeneo yaliyohifadhiwa;

(v) Kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi;

(vi) Kutumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za wanyamapori hao kwa kuwafunga vifaa maalum vya kuonesha uelekeo walipo wanyamapori hao ili kurahisisha ufuatiliaji wake;

(vii) Serikali imeanzisha utaratibu wa mawasiliano wa namba za simu za kiganjani za bure ili kuwezesha wananchi kutoa taarifa za wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kupata msaada wa haraka; na

(viii) Serikali imeanzisha vikosi maalum vya muitikio wa haraka vinavyojumuisha Askari wa Hifadhi na Askari wa Vijiji, hususan katika maeneo yenye matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu ikiwemo katika Wilaya za Tunduru, Bunda, Manyoni, Meatu, Itilima, Bariadi, Tarime, Lindi Vijijini, Songwe na Ngorongoro. Pamoja na Serikali kujenga vituo vya askari wa kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya mbalimbali ikiwemo vituo vilivyojengwa katika Kijiji cha Maulwilo Wilaya ya Meatu, Kijiji cha Kirejeshi Wilaya ya Busega, Kijiji cha Milola Wilaya ya Lindi, Kijiji cha Nditi Wilaya ya Nachingwea, Kijiji cha Ngumbu Wilaya ya Liwale, Kijiji cha Milonde Wilaya ya Tunduru, Kijiji cha Kwakoa Wilaya ya Mwanga, Kijiji cha Itulundu Wilaya ya Iringa, Kijiji cha Ubinde Wilaya ya Songwe, Kijiji cha Ndala Wilaya ya Nzega, Kijiji cha Lubungo Wilaya ya Mvomero, Kijiji cha Ilangali Wilaya ya Chamwino na Kijiji cha Mtera Wilaya ya Mpwapwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mafanikio tuliyoyapata kutokana na masuala ya uhifadhi hapa nchini, na ni vyema ifahamike kwamba jitihada za Serikali katika uhifadhi endelevu zimeendelea kujiridhisha na kutambulika ndani na nje ya mipaka yetu ya nchi. Aidha, jitihada hizo zimekuwa kielelezo muhimu katika kutangaza vivutio na kuboresha huduma za utalii na uhifadhi hapa nchini. Miongoni mwa mafanikio ya kujivunia tuliyoyapata ndani ya nchi kwenye maeneo haya yaliyohifadhiwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutambulika kwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa hifadhi inayovutia zaidi Barani Afrika kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021; *(Makofi)*

(ii) Serikali imeendelea kupokea tuzo kutoka kwa *World Traveler Award* ya kuwa nchi inayoongoza kwa shughuli za utalii mzuri Barani Afrika kwa mwaka 2021; *(Makofi)*

(iii) Kuingiza Hifadhi nne za Taifa katika orodha ya Hifadhi 25 Bora Duniani ambazo ni Kilimanjaro, Tarangire na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro zikiongozwa na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na hivyo kupokea Tuzo ya *Traveler's Choice Destination National Park of the World* iliyotolewa na *Trip Advisor; (Makofi)*

(iv) Shirika la Hifadhi za Taifa kutunukiwa cheti cha ubora wa huduma za kiwango cha kimataifa kutokana na kuimarishwa kwa utoaji huduma bora za utalii hapa nchini; *(Makofi)*

(v) Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* kupata tuzo ya utoaji wa huduma zenye viwango kutoka kwa *European Society of Quality Research;* na

(vi) Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuibuka kinara kati ya vivutio 10 bora vilivyoorodheshwa na mtandao wa *safaribookings.com* ulio maarufu duniani kama kivutio kinachofaa kutembelewa zaidi na watalii kote duniani kilichoko huku Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mtakavyoona mafanikio hayo, hayajapatikana kwa bahati mbaya, bali yametokana na juhudi za makusudi zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha shughuli za uhifadhi endelevu hapa nchini. Aidha, mafanikio haya yamechochea ongezeko la shughuli za utalii ambapo watalii wameongezeka kutoka milioni 1.07 mwaka 2012 hadi kufikia 1.45 mwaka 2022. Vilevile katika kipindi hicho mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,712 hadi Dola za Marekani milioni 2,527.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali inatambua kwamba bado zipo changamoto au migogoro ya ardhi inayohusisha wananchi, hususan wanaoishi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi. Pamoja na mambo mengine, changamoto hizo zimesababishwa na kutoshirikishwa

ipasavyo kwa wawakilishi na wananchi wenyewe kwenye maeneo hayo, baadhi ya maeneo kuorodheshwa kimakosa ndani ya hifadhi na kutokuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya wananchi na mamlaka za hifadhi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Serikali inaimarisha uhifadhi endelevu kwa ajili ya ustawi wa jamii na maendeleo ya nchi, nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa mamlaka mbalimbali za Serikali kusimamia masuala yafuatayo: -

(i) Wahifadhi wahakikishie wanazuia mapema wananchi kuanzisha shughuli za kilimo, ufugaji na makazi ndani ya hifadhi ili kuepuka uhitaji wa kuondoa shughuli ambazo zimeshaanzishwa kama vile kuvunja makazi, kufyeka mazao au kukamata mifugo;

(ii) Operesheni zote zifanyike baada ya wananchi wa maeneo husika kushirikishwa na kupewa taarifa za kutosha na siyo kwa kuwavizia; *(Makofi)*

(iii) Mipaka ya hifadhi iimarishwe kwa kuweka nguzo *(beacons)* ndefu zinazoonekana pamoja na mabango kama ilivyofanyika katika Hifadhi za Ruaha, Loliondo na Isawima;

(iv) Wananchi wenye malalamiko ya kunyang'anywa mali, mifugo, kujeruhiwa wahakikishe wanatoa taarifa ya matukio hayo kwa wakati katika vituo vya polisi na mamlaka za wilaya ili iwe rahisi kwa Serikali kuchukua hatua mara moja;

(v) Jeshi la Polisi lichunguze kwa umakini matukio yote yaliyotolewa taarifa na Waheshimiwa Wabunge na wawakilishi kuhusu kuteswa, kuumizwa au kuuawa kwa baadhi ya wananchi waliotuhumiwa kuingia ndani ya hifadhi ili watakaobainika kukiuka sheria wachukuliwe hatua stahiki; *(Makofi)*

(vi) Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye ufuatiliaji wa malalamiko ya wananchi kuhusu tabia ya baadhi ya wahifadhi kuswaga mifugo na kuiingiza hifadhini kwa lengo la kuitaifisha na kujipatia fedha. Aidha, ichukue hatua kali kwa watumishi watakaobainika kufanya vitendo hivyo na kuwadhulumu wafugaji wanaoishi kwenye maeneo hayo; *(Makofi)*

(vii) Wahifadhi waimarishe mahusiano ya ujirani mwema na kutoa elimu kwa wananchi wanaopakana na hifadhi kuhusu manufaa ya uhifadhi endelevu unaohitajika kushirikisha miongoni mwao. Aidha, kwa kadri itakavyofaa, wachangie katika shughuli za kijamii na maendelo ya vijiji jirani ili kufanya ulinzi wa maeneo hayo uwe imara;

(viii) Wizara ya Maliasili na Utalii iendelee kutoa elimu kuhusu vigezo vya kulipwa kifuta machozi na kifuta jasho baada ya athari za matukio ya wanyama pori. Aidha, naielekeza Wizara ifanye mapitio ya kiwango cha kifuta jasho na kifuta machozi ili viendane na uhalisia; *(Makofi)*

(ix) Wizara ya Maliasili na Utalii kwa pamoja na TAMISEMI zipunguze mlolongo wa kushughulikia changamoto zinazotokana na athari za wanyamapori kwa wananchi; *(Makofi)*

(x) Sheria ya Uhifadhi Sura 282 ifanyiwe mapitio ili kuweka ulinganifu wa kiasi kinachopaswa kutozwa kama adhabu na kubainisha wazi kama kiasi tajwa kitahusu mfugo mmoja au kundi zima; *(Makofi)*

(xi) Wizara ya Maliasili kuweka utaratibu wa kisheria utakaolazimu mashauri ya uingizaji wa mifugo katika hifadhi kusikilizwa mapema na kwa haraka ili kuepuka gharama za utunzaji wa mifugo iliyokamatwa huko kwenye maeneo ya hifadhi; na

(xii) Kamati za Ulinzi na Usalama za mikoa na wilaya zishirikishwe kikamilifu pale penye tuhuma dhidi ya wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, natambua uwepo wa migogoro katika Wilaya za Tarime na Serengeti, pamoja na hatua kadhaa zilizoanza kuchukuliwa na Serikali, nitumie nafasi hii kuwaagiza tena Mawaziri wa TAMISEMI na Maliasili na Utalii kuhakikisha wanakwenda Tarime na Serengeti kukutana na wananchi wa vijiji husika kwa ajili ya kutoa elimu na ufafanuzi juu ya sheria zinazohusu uhifadhi kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo nitoe rai kwa wananchi wenzangu kuzingatia sheria hususan zinazosimamia masuala ya uhifadhi na kuheshimu mipaka. Aidha, niendelee kuliahidi Bunge lako tukufu kwamba Serikali inafanyia kazi changamoto zilizopo na itaendelea kushirikiana kwa karibu na Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa maeneo yanayopakana na hifadhi na wadau wengine wote muhimu katika kuhakikisha kwamba shughuli za uhifadhi zinakuwa endelevu na haziwi kikwazo kwa wananchi kuendesha shughuli zao za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu akitoa taarifa ya namna hii katika kipindi cha maswali yanayoelekezwa kwake, Wabunge mnaruhusiwa kumuuliza maswali kuhusu taarifa aliyoitoa hapa mbele. Sasa kwa sababu pamoja na mambo mengine, jambo hili linahusu maeneo mengi na kama mlivyoona kwa kweli taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu inagusa maeneo yote ambayo yana changamoto hizo hapa nchini. *(Makofi)*

Sasa pamoja na hayo, kwa sababu suala hili lilianzia kwenye hoja ya Mheshimiwa Mwita Waitara mwaka jana, nimpe nafasi kama analo swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba niseme kwa niaba ya wananchi wa Tarime Vijijini kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Waziri Mkuu wa viwango; hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nataka nikwambie kwamba hotuba uliyotoa hapa Waheshimiwa Mawaziri na viongozi wakiifanyia kazi Wabunge hawa watafurahi sana na wananchi wetu watafurahi, ume-*cover* karibu kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu; pamoja na hotuba nzuri uliyotoa hapa, ninataka uwasaidie wananchi wa Tarime Vijijini, Serengeti, Bunda; ni lini hawa Mawaziri watakwenda kuwasikiliza wananchi wale ili kutoa elimu na kutambua ile *GN* ya mwaka 1968 ambayo kimsingi ndiyo kilio cha watu wangu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Mheshimiwa Mbunge kutambua jitihada za Serikali katika kufanya utatuzi wa migogoro iliyopo kwenye Wilaya yake, Jimbo lake kule Traime Vijijini, Mkoani Mara, kwamba hatua iliyofikiwa sasa kwenye eneo lile ni kukutana kwa Mawaziri na wananchi ili kuwaelimisha, hayo ndiyo mahitaji makubwa ya wananchi wale, ili waweze kutambua kikamilifu mipaka iko wapi na wananchi wapate nafasi pia ya kuweza kuwasilisha hoja zao, mahitaji yao ili Serikali ifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilishawaagiza waende haraka, na ilikuwa ndani ya mwezi huu, lakini kutokana na

majukumu tuliyonayo ndani ya Serikali na Mawaziri hawa kuwajibika kikamilifu, nataka nikuahidi, kuanzia tarehe 02 Mei baada ya sherehe za Mei Mosi ambazo wao pia watashiriki kule Morogoro, wataanza safari kwenda Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina uhakika kwamba kati ya tarehe 03 na 04 watakuwa Tarime. Na tukualike wewe, tuwaalike Wabunge wa Bunda wanaoguswa na eneo lile la mipaka pamoja na Serengeti kushiriki vikao hivyo kwa sababu hoja zitakazotolewa na Mawaziri zitakuwa zinagusa kwenye maeneo hayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna mifugo, mali nyingi za wananchi zilizokamatwa kwa kuingia hifadhini, na umesema kwamba ipo haja ya kuimarisha mahusiano kati ya wahifadhi na wananchi. Kwa nini usitoe kauli hapa Bungeni kuitaka mifugo yote, mali zote za wananchi zilizokamatwa kwa sababu ziliingia kwenye hifadhi ziachiwe ili kufungua ukurasa mpya tuanze moja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nachelea kama hilo swali liko kwenye taarifa ambayo umeitoa kwa sababu maswali yanayoelekezwa kwa muda huu – acha yale maswali ya kawaida kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu – lakini yanayoulizwa siku kama ya leo ni yale ambayo yanatokana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mimi sijaona alipozungumzia hilo suala isipokuwa amegusia kwa maana ya kwamba watu wapewe elimu ili wajue mipaka ili

wasivuke hiyo mipaka. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili jambo nilitaka niliache lipite. Ama unataka kulizungumzia kidogo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa taarifa nimeitoa hapa leo na kutoa maelekezo kwa vyombo vyote vya Serikali kuchukua hatua hizi. Hatua zote za awali, taratibu, sheria na kanuni ambazo zipo ziendelee kufuatwa ili haki iweze kutendeka kwa haraka sana kama ambavyo nimesisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maelekezo yangu yamebaki, yamekuwa wazi na sahihi. Kwa hiyo, hatua hizo ziharakishwe ili wananchi waweze kutambua haki zao na upande wa Serikali uwajibike kutoa elimu kuanzia sasa na kuendelea. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona wote mmesimama lakini nusu saa imeshapita na muda wa Waziri Mkuu huwa ni nusu saa. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge na kwa taarifa uliyoitoa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, taarifa hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inahitimisha safari tuliyoianza mwaka jana tarehe 09, Juni, 2022, ambapo nilitoa maelezo hapa mbele kuhusu mambo ambayo alikuwa amechangia Mheshimiwa Phillipo Mulugo na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, nikawa nimeielekeza Serikali kwamba ikafanye uchunguzi halafu ilete taarifa ndani ya miezi mitatu ambayo ingetaiwa kuwa Septemba mwaka jana, 2022.

Taarifa ile ni kweli ililetwa na Serikali na sisi tukajaribu kuitazama kama Bunge tukapeleka kwao maswali ambayo tuliona yanatokana na ile taarifa ambayo ilikuwa imeletwa,

yalipoelekezwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri Mkuu akaamua kuifanya hiyo kazi kwa kutumia ofisi yake yeye mwenyewe ili na yeye akajiridhishe na hayo ambayo Bunge lilikuwa limepeleka kama maswali.

Sasa amepewa nafasi leo na ndicho alichokifanya. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo aliyoyatoa kwa sababu mengi ya hayo maelekezo yanakwenda kujibu hoja ambazo Wabunge hawa walikuwa wamezieleza kuhusu changamoto wanazozipitia watu wa maeneo yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kuchukua hatua kwenye jambo hili, na kwa hivyo Waheshimiwa Wabunge jambo hili linafungwa rasmi, siyo kwa maana ya Wabunge kuchangia, hapana, lakini linafungwa rasmi kwa maana ya Taarifa zetu za Bunge sasa zitaonesha jambo ambalo liliagizwa mwaka jana limeshafanyiwa kazi kwa hatua hizi ambazo Serikali imeshazieleza hapa ndani leo. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu tena, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 175

### Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, lini Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu utaanza kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Patrobass Katambi, majibu.

Samahani Mheshimiwa Naibu Waziri; Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri, ili twende vizuri, mnapojibu tukumbuke kutokurejea ile kwa niaba ya. Kwa niaba unasema wakati unapojibu swali la msingi; moja.

La pili, kwa sababu nakuwa nimeshakuita Mbunge anayekuuliza wewe swali, usiwe na wasiwasi, Taarifa Rasmi za Bunge zitakuwa na jina lake, kwa hiyo wewe nenda moja kwa moja kumjibu Mbunge bila kuanza kusema napenda kujibu swali la fulani, nitakuwa nimeshamwita ndiyo maana amepata nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu umeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 57 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010. Katika kutimiza azma ya Serikali ya uanzishwaji wa Mfuko huu, hatua mbalimbali zimeshachukuliwa na Serikali ikiwemo uandaaji wa Mwongozo wa Usimamizi, Uratibu na Uendeshaji wa Mfuko husika pamoja na kufunguliwa kwa akaunti ya mfuko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilika kwa hatua zote muhimu za mfuko kuanza kutekeleza majukumu yake, mfuko huu haujaanza kutoa huduma kutokana na maelekezo ya kuunganisha mifuko yote ya uwezeshaji wananchi kiuchumi yaliyotolewa mwaka 2020. Zoezi hili liliambatana na tathmini ya ufanisi wa utendaji wa mifuko. Aidha, tathimini hii itakapokamilika, wadau wote wataarifiwa juu ya uanzishwaji wa mifuko hiyo ukiwemo Mfuko huu wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hatua zote za uanzishwaji wa mfuko huu zilikwisha kamilika, ninaomba kufahamu tathmini iliyoelezwa kwenye jibu la msingi itakamilika lini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa mfuko huu kwa watu wenye ulemavu, Serikali inaonaje ikauacha mfuko huu ujitegemee kuliko kuuunganisha na mifuko mingine? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tathmini inayofanyika kwa sasa lilikuwa ni suala tu la kibajeti na kwa mwaka huu wa fedha tunakwenda kulikamilisha hilo kwa sababu tayari mipango yote imekwisha kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la mfuko kutokuunganishwa na mifuko mingine. Ni kweli lakini pamoja na

hilo tunatambua kundi hili ni muhimu sana na ni kundi ambalo ni maalum. Kwa umaalum wake tumekwisha kuona katika eneo la tathmini ni pamoja na kutambua kwanza vyanzo vya mapato na sera na sheria ambazo zitaongoza mfuko husika.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni usimamizi wa fedha hizo, na nne, ni jinsi gani ambavyo fedha hizi zinazopatikana, zipo zitakazopatikana kutokana na ruzuku ya Serikali, lakini kwa sababu ya umaalum wake, zipo fedha ambazo zitatokana na wadau ndiko huko kunakopeleka umuhimu wa baadhi ya mifuko kusimama yenyewe kwa sababu msingi wa mfuko huu unaanzishwa na Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ambayo inataka uwepo wa mfuko huu. Kwa hiyo, kuna mifuko ambayo baada ya tathmini haitakuwa imeungwanishwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya tathmini tutakuwa tumepata picha kamili ya namna ya kuongoza mfuko huu ili uweze kuleta tija na faida zaidi kwa ndugu zetu watu wenye ulemavu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa watu wenye ulemavu wameonekana mara nyingi wakiwa wanaombaomba na wakati mwingine kutumiwa kama chambo katika kuomba; je, ni mkakati upi wa Serikali katika kuwasaidia watu hawa kujikwamua kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu namna ya kuwasaidia watu wenye ulemavu kutokana na suala la kuwa ombaomba. Moja ya mikakati ya Serikali ni kutoa elimu; kumekuwa na changamoto sana ya kubadilisha *mindsets* za watu wetu. Na *slogan* ya Serikali ambayo inatumika hapa ni *disability is not inability;* kwa hiyo tumekuwa tukitoa elimu. Sambamba na hilo, Serikali imefungua vyuo vya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha waweze kupata ujuzi wa ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tumekwenda pia kwenye hatua nyingine ya kuweza kutoa mikopo kupitia halmashauri, asilimia mbili, kuwawezesha watu wenye ulemavu. Sambamba na hilo pia tumekwenda katika hatua nyingine ya kuhakikisha kwamba tunawasaidia watu wenye ulemavu katika kutengeneza miongozo mbalimbali ukiwemo huu wa kuweza kuwa na mfuko maalum pamoja na kuwawezesha na kuwaweka kwenye vyama ambavyo vitawasaidia kuweza ku-*raise agenda* zao na kuweza kusaidiwa na Serikali kwa ukaribu na kwa umoja zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hilo la kuendelea kuwa na suala la ombaomba, tayari tumeshaweka mikakati mbalimbali ikiwemo kuweza kuongeza fedha katika mifuko ya watu wenye ulemavu ili waweze kupata elimu ya ujasiriamali na kujikwamua zaidi.

Mheshimiwa Spika, upande wa elimu, tayari tuna *inclusive education* ambapo kwa wale wenye uwezo wa kwenda shule Serikali imekuwa ikiwachukua. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, amekwisha kutoa zaidi ya bilioni tatu kwa ajili ya kurekebisha vyuo vya watu wenye ulemavu na kutoa huduma za utengemavu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana, ningeomba kujua kwenye hii Wizara ilitolewa milioni 60 kwa ajili mafuta ya watu wenye uarubino. Nataka nifahamu ni lini sasa yale mafuta yataanza kusambaa Tanzania nzima, kwa sababu nina amini kuna Wabunge hapa wananiuliza kila siku wanahitaji haya mafuta? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE.PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hili ni la kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu aliona umuhimu huo. Tulikuwa tunapata mafuta kutoka nje ya nchi sasa yanatengenezwa pale *KCMC,* na gharama zinalipwa na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Awamu ya sita. Suala la usambazaji na ufikaji wa mafuta ni suala la uratibu tu ambalo nitaomba Mheshimiwa Mbunge niwasiliane naye kama kuna changamoto sehemu za wao kuweza kuyapata; lakini pia tutaweka utaratibu wazi wa kuweza kuona ni namna gani kila eneo wataweza kuyapata mafuta haya muhimu kwa ajili ya watu wetu wenye ulemavu, ahsante sana

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, kwa kuwa matibabu ya watu wenye ulemavu ni ya ghali sana kwa namna ya kuwapeleka hospitali lakini na hata matibabu yenyewe.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka ruzuku ya bima ya afya kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kuwapunguzia adha wazazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ahsante, moja ya jitihada za Serikali ni pamoja na kuandaa mwongozo huo wa mwaka 2020 ambao umekamilika katika kuona na kuratibu masuala ya changamoto, kwanza kutambua changamoto za watu wenye ulemavu lakini pili kuona namna gani tunaweza kuwahudumia zaidi. Kwa hiyo kuwepo kwa mfuko wa watu wenye ulemavu utatatua changamoto nyingi sana ambazo zitasaidia sana kuona namna gani tunaenda kutatuta changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la bima, kwa kuwa tuko kwenye utaratibu sasa wa kupata *universal health care*, mfuko wa bima ya afya kwa wote tutaona pia umaalum wake kwa sababu kundi hili ni muhimu kuweza kuliangalia kwa umaalum wake na kulifanya hilo. Kwa hiyo niseme tu nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na kwamba tutaufanyia kazi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Venant Protas Mbunge wa Igalula sasa aulize swali lake.

Na. 176

**Upungufu wa watumishi wa afya na elimu – Igagula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta watumishi wa afya na elimu katika Jimbo la Igalula ili kuondoa kero wanayoipata wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais *TAMISEMI*, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daud Protas Venant, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitoa ajira ili kukabiliana na upungufu wa watumishi katika kada za afya na elimu unaotokana na kustaafu, kuacha kazi, kufukuzwa na kufariki. Tangu mwaka 2018/2019 hadi 2021/2022, Serikali imeajiri jumla ya walimu 26,598 wakiwemo 16,640 wa shule za msingi na 9,958 wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, watumishi wa kada za afya 7,736 waliajiriwa na kupelekwa kwenye maeneo mbalimbali nchini kulingana na uhitaji uliokuwepo. Mkoa wa Tabora ulipata walimu 565 wakiwemo wa shule za msingi 301 na shule za sekondari 264. Aidha, kwa upande wa kada za afya Serikali ilipeleka kwenye Mkoa wa Tabora jumla ya watumishi 265 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilipata watumishi wa kada ya afya 50.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari imetangaza nafasi za ajira za walimu na watumishi wa kada ya afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Jumla ya ajira 13,130 kada ya elimu na 8,070 kada ya afya zitatolewa hasa kwa kuzingatia maeneo yenye upungufu mkubwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas swali la nyongeza.

**MHE. DAUD P. VENANT:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nipongeze Serikali kwa majibu mazuri. Wilaya ya Uyuwi ina upungufu ya watumishi zaidi ya 2,000 lakini pamoja na upungufu huo Serikali imebadilisha utaratibu wa watumishi hasa walimu na madaktari kuwa wakandarasi. Yuko darasani anaambiwa huku mfuko wa simenti umepotea huku anatibu anaambiwa vibarua hawajalipwa.

Je, Serikali haioni haja ya kubadilisha mfumo ili hawa ambao tunao pamoja na upungufu wao wafanye kazi kikamilifu?

Swali la pili, Jimbo la Igaula hatukuwa na shule ya *five na six,* nashukuru Serikali imetuletea, lakini shule ile ina mchepuo wa sayansi hatuna walimu wa sayansi.

Je, kwenye ajira hizi hauoni unipe upendeleo maalum kwenye ile shule ili iweze kufanya vizuri kwa sababu imeshaanza kufundisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza hili la nyongeza analo sema kwamba walimu sasa au watumishi kwa ujumla wamegeuka kuwa wakandarasi na kuacha kufanya kazi zao; naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine humu ndani, kwamba wale wakuu wa shule na walimu wakuu ni nafasi za madaraka. Hivyo wao ndio *accounting officers* katika zile shule zao. Ni kama mtu anapokuwa Katibu Mkuu wa Wizara, anapokuwa Katibu Tawala wa Mkoa, yeye ndiye *accounting office*. Zile pesa zinaingia kwenye *account* ya shule husika kwenye mradi. Sasa ni wajibu wao kuhakikisha matumizi ya zile fedha yanakuwa ni mazuri na ya uwajibikaji. Sasa nitolee kwa ujumla kwamba halmashauri bado ina mkono kuhakikisha zile

kamati za manunuzi kwenye *force account*, kamati ya mapokezi na kadhalika zinafanya kazi kwa miongozo na wataalam wa halmashauri kusimamia; lakini bado ni wajibu wa Mkuu wa Shule, ni wajibu wa Mwalimu Mkuu kuhakikisha matumizi ya zile fedha yanakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la walimu wa sayansi kupatikana katika hii shule ambayo tayari imeshafanywa kuwa *A-level* ndani ya halmashauri yake. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge. Ninyi wote ni mashahidi, katika kipindi kifupi cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maeneo yote yamepata watumishi wa kutosha katika kipindi cha miaka hii miwili; na tayari kuna ajira hizi ambazo zimetangazwa. Kwa hiyo nikutoe mashaka Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hizi ajira zilizotangazwa tutahakikisha pia na wewe kule katika shule uliyoitaja mnapata walimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka kufahamu ni lini sasa Serikali italeta watumishi wa afya katika Jimbo la Msalala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, watumishi wa afya kwenda Msalala naamini katika hizi ajira zilizotangazwa sasa ambazo Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha kuweza kuajiri watumishi wa afya wa kutosha na Msalala vile vile nanyi mtapata watumishi wa afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. halmashauri ya Kyerwa inawatumishi wa kada ya afya 252 ikiwa na mahitaji ya watumishi 1022 ni upungufu wa asilimia 75.

Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha kwenye hii halmashauri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, katika ajira hizi ambazo Serikali imetangaza tutahakikisha pia na Halmashauri ya Kyerwa ina pata watumishi wa kwenda kwenye kada ya elimu na kada ya afya vile vile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itapeleka madaktari kwenye hospitali ya kanda iliyojengwa Mitengo Mkoani Mtwara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutashirikiana na Wizara ambayo ndio wasimamizi wa hospitali hizi za kanda kuhakikisha kwamba Hospitali hii ya Kanda ya Mtwara kule inapata madaktari katika ajira hizi kwa sababu Wizara ya Afya nao wametoa ajira hizi kupitia mfumo wao.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Doctor Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Hospitali ya Manispaa ya Kahama inatibu kama hospitali ya mkoa; ni nini kauli ya Serikali kuhusu kuongeza idadi ya watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye ajira hizi ambazo Serikali imetangaza na ambazo mchakato unaendelea tutahakikisha hospitali ya Manispaa ya Kahama nayo inapata watumishi wa kutosha kuweza kusaidia wananchi wa pale Kahama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, mbali na Serikali kutoa ajira nyingi, Jimbo la Sumve limeendelea kuwa na tatizo la upungufu mkubwa wa watumishi hasa katika sekta ya elimu, kiasi kwamba Shule kama Nyang'enge, Bukala zina walimu kati ya watano mpaka saba.

Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kutoa upendeleo maalumu katika ajira zinazofuata kwa Jimbo la Sumve ili kukidhi mahitaji ya walimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilikuwa nimeshasema awali kwamba katika kipindi hiki cha miaka miwili ya uongozi wa Doctor Samia Suluhu Hassan, Serikali imejitahidi sana kuhakikisha inaajiri walimu wengi, na ninyi ni mashahidi kwenye halmashauri zenu

Waheshimiwa Wabunge mmepata walimu wa kutosha. Kwenye hizi ajira mpya tutahakikisha Sumve pia nanyi mnapata Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 177

**Kuhuisha Mpango wa Upanuzi wa Manispaa ya Moshi**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itahuisha mpango wa upanuzi wa Manispaa ya Moshi kutoka kilometa 58 hadi 146 pamoja na kuwa Jiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tarehe 25 novemba, 2015 ilipokea ombi la uendelezaji wa Manispaa ya Moshi kuwa Jiji kwa kuongeza ukubwa wa mipaka ya kiutawala kutoka kilomita za mraba 58 hadi kilomita za mraba 142 kwa kuongeza vijiji kutoka Halmashauri za Wilaya za Moshi na Hai.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Uanzishaji wa Maeneo ya Utawala wa mwaka 2014, kigezo cha ukubwa wa

kuanzisha halmashauri ya jiji ni kilometa za mraba 1,000 na Halmashauri ya Wilaya ni kilometa za mraba 5,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mamlaka nyingi zilizoanzishwa bado zinaupungufu wa miundombinu mbalimbali yakiwemo majengo ya utawala na huduma za kijamii, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa hitaji letu ni uhalisia kuliko nadharia, kutokana na uhalisia kwamba hata eneo la dampo sasa tumenunua Moshi Vijijini; na moja ya changamoto ni kwamba barabara inayoelekea kwenye dampo hatuwezi kuikarabai sisi kwa sababu haiwezi kuingia kwenye bajeti ikafanye kazi Moshi Vijijini. Na Moshi Vijijini pia haiko kwenye vipaumbele vyao kwa hiyo inatusababisha sisi tuna *operate* kwa gharama kubwa sana. Lakini pia inasababisha kwa mfano hospitali ya halmashauri inayojengwa Moshi Mjini inabidi ijengwe kwa ghorofa jambo ambalo ni karibu mara mbili ya gharama za kutengeneza maeneo mengine.

Je, tukiachana na Suala la Jiji ni lini mtakubali tupanue kuendana na *GN* namba 219 ya tarehe 15, July 2016 ikiwa ni pamoja na kupata maeneo ya makaburi ambayo hatuna?

Swali la pili; yapo maeneo kwenye kata, kwa mfano kata ya Shirimatunda, eneo la Boniti ambalo lilikuwa la viwanda lakini sasa hivi limesharasimishwa kuwa makazi lakini haliwezi kuendelea ili watu wapate hati zao kwa sababu ya kusubiri mchakato huo.

Je, hamuoni kwamba kuna uwezekano wa kutoa upendelea kwa Moshi Mjini kwanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la kwanza la Mheshimiwa Tarimo la uhitaji huu ni uhalisia; Serikali inatambua umuhimu wa kutanua mipaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Lakini kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba kwa sasa kipaumbele kikubwa ni kuhakikisha tunaimarisha yale maeneo ambayo ni mapya na halmashauri ambazo ni mpya. Ni muda si mrefu halmashauri nyingi zilihamia katika maeneo yao ya utawala, na kwa sasa Serikali hii ya Awamu ya Sita imeweka kipumbele kuhakikisha majengo ya utawala,kuhakikisha huduma za hospitali za Wilaya, kuhakikisha mashule na kadhalika yanajengwa, na hivyo baada ya haya kukamilika Serikali itaanza kutenga bajeti kuhakikisha maeneo mapya ya kiutawala yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, niseme tu kuwa Serikali inalichukua hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumza la Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kupewa upendeleo maalumu kwa sababu tayari *GN* ilikuwepo. Pale ambapo tutamaliza ukamilishaji wa ujenzi wa miundo mbinu katika halmashauri mpya basi Moshi Mjini Manispaa nayo itapewa kipaumbele.

**SPIKA:** Mheshimiwa Doctor Alfred J. Kimea Mbunge wa Korogwe Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 178

**Ukarabari Hospitali ya Magunga – Korogwe**

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa Hospitali Kongwe ya Magunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 17.1 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali 19. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 kiasi cha shilingi bilioni 12.95 zimekwishatolewa kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya hospitali Kongwe kumi na nne (14).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itatenga shilingi bilioni 27.9 kwa ajili ya ukarabati wa hospitali kongwe 31 ikiwepo Hospitali ya Mji wa Korogwe ya Magunga ambayo imetengewa shilingi milioni 900.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Alfred J. Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi hospitali yetu hii ni kongwe sana inawezekana ni kati ya hospitali kongwe zaidi Tanzania ambayo ilijengwa mwaka 1952.

Je, Serikali inatupa *commitment* gani kwamba tutapewa fedha hizi maana tumekuwa tukiahidiwa mara nyingi tunaletewa fedha za ukarabati na hatujawahi kupewa.

Je, Serikali ina tupa *commitment* gani kwamba fedha hizi zitakuja ili hospitali yetu hii ipate kukarabatiwa?

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa majibu yangu ya msingi katika mwaka wa fedha 2023/2024 hospitali hii kongwe ya Mjini Korogwe ya Magunga imeshatengewa shilingi milioni 900 kwa ajili ya ukarabati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Idunda kata ya Kimara wamekarabati jengo lao wenyewe ili liwe zahanati na limekamilika.

Je, Waziri yuko tayari kuagiza Serikali kupeleka watumishi na vifaa tiba mara moja kwa sababu wanatembea zaidi ya kilometa 40 kupata huduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye zahanati hii ya Idunda katika ajira hizi ambazo Serikali imetangaza za elimu na afya tutahakikisha kwamba zahanati hii inapata watumishi. Lakini vilevile kuhusu vifaa tiba naomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako hili kumuelekeza kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilolo kuhakikisha anaanza kuweka fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba na sisi huku Wizarani tutaona ni lipi ambalo

linaweza likafanyika ku-*complement* jitihada za Mkurugenzi wa Halmashauri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona wote mliosimama lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hili swali liko chini ya Naibu Waziri mwingine sivyo? Nadhani Wabunge wengi wamesimama ila nadhani nikikupa nafasi ya kujibu maswali yote nitakuwa nakuonea.

Waheshimiwa Wabunge, wote mliosimama mmeonwa mumuone Mheshimiwa Naibu Waziri ili afuatilie haya mambo kwa sababu hili swali lilitakiwa lijibiwe na Naibu Waziri mwingine, kwa hiyo yeye ameshajibu maswali ya kutosha kwenye ilo eneo.

Tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 179

**Kukarabati Kituo cha Polisi Mkoani – Pemba**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakarabati upya Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mkoani Pemba pamoja na nyumba za kuishi askari wa kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jengo la kituo cha Polisi cha wilaya ya Mkoani, mkoa wa kusini Pemba ni chakavu na halifai kwa matumizi ya kutoa huduma za Polisi. Mwezi Disemba 2022 Serikali imetoa kiasi cha fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi kipya cha Daraja B eneo hilo. Taratibu za ujenzi zimeshaanza na ujenzi unatarajia kukamilika mwezi Agosti, 2023.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya uchakavu kwa ajili ya kufanya ukarabati wa nyumba ya makazi ya askari ya kuishi familia nne ambayo iko eneo la kituo imeshafanyika na kubaini kwamba shilingi milioni 46.27 kinahitajika kwa ajili ya kubadilisha paa, dari, miundombinu ya maji safi, maji taka na umeme, kuziba nyufa na kupaka rangi. Fedha hizo zitaombwa kutoka kwenye mfuko wa tuzo na tozo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, nina swali moja la nyongeza. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa majibu yake mazuri. Je, Waziri yuko tayari kwenda kukikagua Kituo hicho cha Polisi ambacho Waziri amesema kitamalizika Agosti, 2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimewahi kukitembelea kituo hiki na kuona kasi ya ujenzi unavyoendelea, inanitia moyo kwamba inaweza ikamalizika. Hata hivyo, kwa vile hakuna zida mbovu, niko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge kukamilika ili kwenda

kuangalia maendeleo ya ujenzi na kujiridhisha kwamba kitakamilika katika muda uliopangwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Maswa ni wilaya Kongwe katika Mkoa wa Simiyu, lakini haina Kituo cha Polisi kabisa. Ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Wilaya ya Maswa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunatambua uwepo wa baadhi ya wilaya kongwe kama ilivyo Maswa ambazo hazina Kituo cha Polisi. Mara kadhaa tumetoa ahadi hapa, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti zetu zinazofuata tutaangalia uwezekano wa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza wa ujenzi wa Kituo cha Polisi ngazi ya wilaya katika Wilaya ya Maswa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Liwale pamoja na kwamba ni ya mwaka 1975 haijawahi kuwa na jengo la Kituo cha Polisi, lakini Serikali walituahidi kutujengea Vituo vya Polisi katika Kata za Kimambi, Lilombe na Kibutuka. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tumewahi kueleza hapa na naomba nirudie kwamba katika wilaya zetu hasa kwenye kata, mpango wa Serikali ni ku-

*support* pale ambapo juhudi zimeoneshwa na wananchi na halmashauri zao za ujenzi wa vituo hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge akitusaidia kupitia Mfuko wa Jimbo, akaanzisha ujenzi, kwa vyovyote vile *IGP* kupitia fungu lake atatoa fedha za kusaidia kukamilisha vituo vyake. Kwa hiyo, nimtie moyo, hizi kata tatu ambazo zina changamoto za uhalifu, tuanze kwenye ngazi ya halmashauri na Mfuko wa Jimbo ili ngazi ya wizara kupitia Jeshi la Polisi liweze kusaidia kukamilisha, nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe Maswali mafupi, maswali mafupi. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru. Wananchi wa Kata ya Mazinde kwa kushirikiana nami Mbunge wao tumeshirikiana kujenga Kituo cha Polisi mpaka boma limekamilika. Je, ni lini Serikali itatusaidia kumaliza Kituo hicho cha Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kupitia bajeti ya mwaka 2023/2024, tutaona uwezekano wa kupata fedha kutoka Mfuko wa Tuzo na Tozo kukamilisha Kituo cha Mazinde ambacho Mheshimiwa Mbunge amekizungumzia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Polisi wote nchini wanapitia Shule ya Polisi Moshi inayojulikana kama *CCP,* shule hiyo ni chakavu, mbovu, barabara hazipitiki na wakija wageni wanapitishwa kwenye geti kubwa na sio hili la Moshi Sekondari. Je, ni lini sasa Serikali itakarabati chuo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimekitembelea Chuo cha Polisi Moshi na kubaini uchakavu anaousema na kupitia ziara yangu tulikubaliana na uongozi wa Manispaa ya Moshi kupitia Mamlaka ya Barabara za Mjini na Vijijini *(TARURA)* kwa sababu chuo hiki kipo kwenye himaya yake waanze kutenga fedha. Nimtie moyo Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara kuu inayoingia tayari ukarabati umefanyika na tutaendelea kufanya ukarabati huo kwenye barabara zote nyingine zilizopo kwenye chuo hicho, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kituo cha Polisi Kwamtoro ni kituo cha majengo ya mkoloni, kimechakaa, hakitamaniki, hakithaminiki. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kulingana na upatikanaji wa bajeti tunaendelea kuvikarabati Vituo vyote vya Polisi vilivyochakaa. Hiki cha Kwamtoro pia tutakiingiza kwenye mpango wa matengenezo kadri tutakavyopata fedha kutoka Serikalini, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa. Kutoka Makambako mpaka unaingia Mafinga hali ya usalama sio nzuri kwa sababu hakuna Kituo cha Polisi na tayari jitihada zimekwishaanza kufanywa na wananchi kwa kutenga eneo na hata mimi mwenyewe Mbunge kupeleka *cement.* Je, Wizara iko tayari kupeleka fedha kuhakikisha kwamba Kituo cha Polisi cha Nyololo kinakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa jitihada ambazo zimekwishafanywa na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wake wizara itamuunga mkono kukamilisha kituo hicho, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Gari lililopo katika Kituo cha Polisi Magugu ni chakavu. Je, ni lini Serikali itawapatia kituo hicho gari ili kurahisisha utendaji kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunao mpango katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Polisi kununua magari na kuzipatia Wilaya zote za Kipolisi nchini Tanzania. Naamini gari hiyo itakapopatikana, basi magari yaliyopo kwenye ngazi ya wilaya yanaweza kupelekwa kwenye kituo hicho kama kutaonekana kuna uhitaji mkubwa wa gari, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Mtenga, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtwara Mjini ndio kwenye Kituo Kikuu cha Polisi. Kituo hicho kilijengwa toka mwaka 1962, kwa sasa kituo hicho ni chakavu mno na inapelekea Askari kufanyia kazi kwenye mwembe. Je, ni lini Serikali itakwenda kufanya ukarabati kwenye kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tunatambua hali ya uchakavu wa Kituo cha Polisi ngazi ya

Wilaya Mtwara. Hata hivyo, katika bajeti yetu ya mwaka 2023/2024, fedha zimetengwa za kuanza kufanya ukarabati kwenye kituo hicho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na matumaini kwamba mwaka 2023/2024 kituo hicho kitakarabatiwa, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 180

**Kupelekwa umeme wa *REA* vijiji 23 – Mkalama**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* kwenye Vijiji 23 Wilayani Mkalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, katika Wilaya ya Mkalama unatekelezwa na Mkandarasi *CRJE – CTCE Consortium*. Mradi unalenga kupeleka umeme katika vijiji vyote 25 vya Wilaya ya

Mkalama ambavyo havina umeme na Mkandarasi yupo katika eneo la *site* akiendelea kuwasha umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mradi huu wa kusambaza umeme katika Wilaya ya Mkalama unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2023, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca David Kishoa, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Moja ya changamoto kubwa inayopelekea miradi hii ya *REA* kutotekelezwa kwa wakati ni pamoja na ukosefu wa nguzo. Nataka kusikia kauli ya Serikali imejipangaje kwa ajili ya kutatua changamoto hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna makampuni yasiyo na uaminifu katika kutekeleza miradi hii ya *REA* jambo ambalo linasababisha kuendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi hii, mfano kampuni ya *TONTAN* ambayo imetumia zaidi ya bilioni 3.8 kinyume na utaratibu. Nataka kujua kauli ya Serikali imekwishachukua hatua gani mpaka sasa dhidi ya kampuni hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la nguzo kwa ajili ya usambazaji wa umeme tunaendelea kuvihamasisha na kuviwezesha viwanda vyetu vya ndani kuhakikisha kwamba vinatosheleza soko. Hata hivyo, ni kwa sababu kazi zimekuwa nyingi na miradi imekuwa mingi na hivyo viwanda vinaonekana kuzidiwa na kazi ambazo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amewezesha zifanyike katika nchi yetu. Hata hivyo, tunajitahidi na viwanda vimekuwa vikizalisha nguzo na kwa sehemu kubwa tatizo huilo limepungua na endapo litakuwa kubwa sana tutahakikisha tunazipata kokote zinakowezekana kupatikana ili hilo tatizo liishe.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili, kuhusiana na wakandarasi ambao wanalegalega katika katika utekelezaji wa kazi zao. Kama ambavyo tumekuwa tukisema tunao wakandarasi wa *lot* kama saba ambao tumekuwa tukikamatana nao kwa nguvu zaidi kuhakikisha kwamba wanakamilisha kazi zao. Vile vile, tumewekeana malengo na mikakati na muda utakapofika endapo watashindwa kukamilisha, basi tutavunja mikataba hiyo ili tuweze kupata watu wengine wa kukamilisha kazi kwa wakati. Hata hivyo, kwa sasa tunaendelea vema katika ambayo tumeweka utaratibu wa kufuatilia siku kwa siku kwa kuajiri wale vijana wetu ambao tumewapeleka katika maeneo yetu ya majimbo na hivyo tunapata taarifa za mara kwa mara na usimamizi unakuwa wa karibu. Tunaamini kazi zitakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika Wilaya ya Namtumbo tuna Vijiji viwili cha Ligunga na cha Msisima chenye Shule ya Sekondari ya Kata ya Msisisima iliyojengwa kwa gharama ya shilingi milioni 600, kilirukwa katika awamu hii na awamu ya tatu mzunguko wa pili. Vile vile, tuliomba viingizwe na vikapata *proof* na mkandarasi amefanya *survey* ameleta…

**SPIKA:** Mheshimiwa swali lako.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali lini itampa kibali aendelee kufanya kazi hiyo ya kuweka umeme katika Kijiji cha Msisima na Ligunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, vijiji vyote ambavyo havikuwa na umeme vitawekewa umeme na mikataba tuliyokuwa nayo inaisha Desemba, 2023, vile vilivyokuwa kwenye miradi ya awali na vile ambavyo vilikuja kuongezwa vyote vitafanyiwa kazi kwenye *scope* hii ambayo tunakwenda nayo na vitakamilika katika awamu hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Jimbo la Newala Vijijini lina vijiji zaidi ya 60 ambavyo havijapatiwa umeme. Je, ni lini Mradi wa *REA*, mzunguko wa pili, utaenda kumaliza tatizo hili? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa *REA*, awamu ya tatu, mzunguko wa pili, unaendelea na tunatarajia utakamilika ifikapo Desemba, 2023. Katika Jimbo la Newala Vijijini napo mradi huu utatakiwa ukamilike na vijiji vyote vilivyopo vitapata umeme.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushuru. Kutokana na mpango wa umeme vitongojini kwa Wilaya ya Tunduru bado haujaanza na kuna taasisi mbili za kidini ambazo hazina umeme na ziko vitongojini. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya umeme kwenye taasisi hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, tayari Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,

imetoa fedha za nyongeza za kupeleka umeme katika kilometa mbili za ziada ukiachana na ile moja ambayo tulikuwa nayo katika Mradi wa *REA III Round II*. Kwa hiyo, naamini katika nyongeza hiyo ya kilomita mbili itazidi kuingia kwenye maeneo ya vitongoji na taasisi hizo zikiwekwa ni za kipaumbele, basi Mkandarasi atafikisha umeme kwenye maeneo hayo kwa kipindi hiki ambacho tumepata nyongeza ya pesa ya kupeleka umeme katika kilomita mbili za ziada ukijumlisha na ile moja ambayo itagusa vitongoji vingi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika shule zote za msingi, sekondari na taasisi za dini katika wilaya zote Mkoa wa Kigoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, katika mpango wa *REA III, Round II,* tuliokuwa nao sasa tunafikisha umeme katika vijiji vyote na katika maeneo ya vitongoji baadhi kwa kilomita moja ukiongeza na zile kilomita mbili. Hata hivyo, tayari Serikali inatafuta fedha ya kuhakikisha inapeleka umeme katika vitongoji vyote Tanzania takribani 36,000 ambavyo havina Umeme kwa gharama ya shilingi 6,500,000,000,000. Pesa hiyo itakapokuwa imepatikana taasisi na maeneo mengine yote yanayohitaji umeme yatafikishiwa umeme kulingana na upatikanaji wa fedha ambao tunaamini zitapatikana katika muda mfupi ujao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, sasa aulize swali lake.

Na 181

**Somo la Kilimo kuwa la lazima Vyuo vya Ufundi**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italifanya somo la kilimo kuwa la lazima kwenye Vyuo vya Ufundi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mkenda, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Vyuo vya Ufundi Stadi kutoa mafunzo yanayozingatia shughuli za kiuchumi za maeneo husika na Taifa kwa ujumla ili kuwawezesha wananchi kutumia kikamilifu fursa na rasilimali zilizopo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA),* imekuwa ikifanya upembuzi yakinifu kabla ya uanzishaji wa fani za ufundi ili kubaini mafunzo yanayofaa kutolewa katika vyuo hivyo kulingana na fursa na rasilimali zilizopo katika maeneo husika. Kozi ya kilimo ni miongoni mwa Kozi zinazotolewa katika Vyuo vya Ufundi Stadi vya Kihonda, Dakawa, Katavi, Arusha na Manyara. Aidha, katika Vyuo vipya 64 vya Wilaya vinavyojengwa, kutakuwa na karakana moja kwa kila

chuo kwa ajili ya kutoa mafunzo yatakayozingatia shughuli za kiuchumi katika eneo husika ikiwemo kilimo, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na swali moja la nyongeza. Kwa kuwa imethibitika pasipo shaka kwamba maendeleo sio miujiza. China wana Vyuo karibu 7,294 vya shule za ufundi. Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Sera ya kuwa na vyuo kama ilivyokuwa kwenye Sera ya Afya kwamba kila Kata, sasa Sera hii iende kwenye kila jimbo na hasa majimbo ya vijijini ili tuwafundishe sasa watu wetu kulima katika maeneo madogo, tija kubwa pia ili waweze sasa kubadilisha udongo badala ya kuchoma majani wawe wanafukia? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa elimu ya mafunzo ya amali ambayo mara nyingi tunaita mafunzo ya ufundi stadi na ndio maana sasa hivi tume-*register* vyuo takribani 809, vya Serikali 77 na vingine vilivobaki ni vya watu binafsi na bado vile vile Serikali inaendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundi stadi 65, kimoja cha Mkoa wa Songwe na Vingine 64 kwa ajili ya kila wilaya. Pamoja na hivyo kama ambavyo tutakuja kulieleza Bunge lako katika Semina ambayo tutakuja kukuomba, Mabadiliko ya Sera na Mitaala ambayo yanafanyika yataongeza ufundishaji wa elimu ya amali (ufundi stadi katika Shule za Serikali) ili kuhakikisha kwamba kweli tunaongeza ujuzi kwa wanafunzi wetu wanaohitimu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelibert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni sasa aulize swali lake.

Na. 182

**Kuanza ujenzi wa kivuko kipya – Kigamboni**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa kivuko kipya ya Kigamboni utaanza baada ya kutengewa fedha mwaka 2022/2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GEDFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* katika mwaka wa fedha 2022/2023 umetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya katika Kituo cha Magogoni – Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, uzoefu uliopatikana kwa kutumia vivuko vidogo *(sea taxi)* vilivyokodishwa toka Kampuni ya Azam *Marine* umeonesha kuwa vivuko hivyo vina ufanisi zaidi katika kutatua kero ya ucheleweshwaji wa abiria. Hivyo, Serikali imeamua

kununua vivuko vidogo viwili. Taratibu za manunuzi ya vivuko vidogo viwili kwa ajili ya abiria *(Sea Taxi)* ambavyo vitakuwa na uwezo wa kubeba abiria 250 kila kimoja zinaendelea, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa mwaka wa fedha 2023/2024 umebaki miezi miwili.

Je, ni lini wananchi wa Kigamboni watarajie vivuko hivyo viwili vidogo kama Mheshimiwa Naibu Waziri anavyoongea?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa *TEMESA* ni Taasisi ya Umma inayotoa huduma za ufundi na umeme pamoja na huduma za vivuko.

Je, Serikali haioni sasa umefika muda muafaka wa kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma ya vivuko ili kuongeza ufanisi na kuongeza wigo wa huduma hususani kwa wananchi wa Kigamboni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GEDFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, mwaka huu tulitegemea tuanze manunuzi ama utengenezaji wa kivuko na kazi hiyo tumeshaanza, kwa sababu tulitangaza tenda kununua hivi vivuko viwili lakini ilionekana watu hawa walikuwa wame-*bid,* wote walikuwa wame-*tender* bei za juu wakati wa kufanya *evaluation,* hivyo tunatangaza upya tena

tenda, kwa hivyo tupo kwenye utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kigamboni na Magogoni kwamba hizo taratibu zinaendelea tutakapopata Mkandarasi sahihi shughuli hizo zitaanza mwaka huu wa fedha na tayari tumeshaanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, tayari yalikuwa pia ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba taasisi zote ambazo zinafanya biashara kama kuna uwezekano wa watu binafsi kufanya biashara basi waruhusiwe, hivi ninavyoongea tayari Azam ameshaonesha nia ya kutaka kufanya shughuli katika kivuko hiki cha Kigamboni na sasa itakuwa ni kwa vivuko vyote tunategemea Serikali ikishakamilisha taratibu basi wale wafanyabiashara ambao wanataka kufanya biashara sambamba na *TEMESA* taratibu zikishakamilika wataruhusiwa kufanya hivyo. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa kifupi, Mheshimiwa Jafari Chege swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninataka nijue tu ni lini Serikali itarejesha kituo cha MV Musoma kilichokuwa kinatoa huduma kati ya Kinesi kwa maana ya Rorya na Musoma Mjini hasa ukizingatia kituo kilichopo ni kidogo na hakikidhi mahitaji ya watu lakini pia ni hatari kwa maisha ya wananchi wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GEDFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Musoma - Kinesi kiliazimwa kwenda kufanya kazi kati ya Kisolya na Lujezi, Musoma tulipeleka kivuko cha *Chato One*. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunategemea mwishoni mwa mwezi huu Tarehe 30 Kivuko cha Kisolya- Lugeza ambacho kilikuwa kinatengenezwa kitakamilika na mwanzoni mwa mwezi unaokuja kivuko cha MV Musoma kitarudishwa kwa ajili ya kutoa huduma iliyokuwa imezoeleka kati ya Musoma na Kinesi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwenye mradi wa *SGR* kwenye eneo la Kikongo pamoja na Msuwa kuna uhitaji wa kuweka kivuko na *TRC* waliahidi kuweka ni muda mrefu sasa.

Je, Waziri atakuwa yuko tayari kutoa agizo kwa Mkururgenzi wa *TRC* kukamilisha mradi huo kabla haujaanza utekelezaji wake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakamo Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumejadili na Mheshimiwa Mbunge na tayari nilishatoa maelekezo kwa Mtendaji wa *TRC* ili waweze kuangalia eneo hilo ambalo ni muhimu sana kuwa na kivuko kwa waenda kwa miguu ili waweze kuangalia uwezekano wa kujenga kivuko mahali aliposema Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Gati la kushukia abiria jengo la mizigo ya wasafiri, jengo la abiria Bandari ya Manda Wilayani Ludewa utaanza lini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Gati la Manda upo kwenye mpango, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha kwamba tunajenga gati hili la Manda ili wananchi wasipate changamoto ambayo wanaipata sasa hivi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa pesa nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa kivuko cha Mwaya – Kajunjumele; je, ni sababu gani zinafanya mpaka sasa hivi kisianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kati ya Mwaya- Kajunjumele tuna kivuko ambacho kilitoka Luhuhu kiko *site* na tunachosubiri sasa hivi ni kwamba maji yaweze kupungua ili tuweze kurekebisha rampu halafu baada ya hapo kivuko hicho kitaanza kutoa huduma kati ya Mwaya na Kajunjumele, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Katika Jimbo la Singida Kaskazini Kijiji cha Kinyeto na Ilongero kuna bwawa la Ntambuko ambalo wananchi wanapata shida..

**SPIKA:** Swali lako.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa Serikali italeta kivuko katika bwawa la Ntambuko linalounganisha Kijiji cha Itamuka, Ilongero na Kinyeto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tumelichukua hilo na *TEMESA* watakwenda kufanya *study* ili waone kama kivuko kinaweza kikajengwa kwenye hilo bwawa alilolisema kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi wa pande hizo mbili. *(Ahsante)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Ahmed Pathan Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 183

**Ukarabati Viwanja vya Ndege Lindi na Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa Ndege Lindi kwa kiwango cha lami pamoja na kukarabati Uwanja wa Ndege Nachingwea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya kufanya marejeo ya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi kwa kiwango cha lami. Marejeo ya usanifu wa kina yalifanyika ili kuzingatia mahitaji ya sasa ya kiwanja, ikiwemo kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Gesi katika maeneo hayo. Kwa sasa, Serikali inakamilisha maandalizi ya makabrasha ya zabuni hiyo ili iweze kutangazwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kiwanja cha Ndege cha Nachingwea, Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya miundombinu ya kiwanja hicho ili kiendelee kutumika ambapo mwaka 2020 ilikamilisha ukarabati mkubwa wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Kiwanja cha Ndege Nachingwea, Serikali inaendelea na utwaaji wa eneo la ziada ili kujenga kiwanja hicho kwa kiwango cha lami. Aidha, mnamo mwezi Machi, 2023 wataalam wa Wizara walifanya uhakiki wa daftari la fidia na kuwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa idhini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Viwanja hivi vilitumika kwa kupigania uhuru Kusini mwa Bara la Afrika. Je, ni nini tamko la Serikali hasa kwamba viwanja hivi lini vitawekwa lami vyote viwili?

Swali pili, Je, ni lini wananchi waliotwaliwa maeneo yao kwa ajili ya kuongeza eneo kwenye uwanja wa ndege wa Nachingwea watalipwa fidia zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni lini vitajengwa viwanja hivi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa maeneo hayo kwamba katika bajeti ya mwaka huu Kiwanja cha Lindi kimetengewa ama tumetenga takribani bilioni 2.5 na fedha hizi zitatumika kwa ajili ya Mkandarasi Mshauri ambae ataandaa *document* kwa Ajili ya kutangaza viwanja hivi ili viweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, suala la pili anataka kuja ni lini wananchi watalipwa fidia. Ni kweli tathmini imekwishafanyika na mwezi Machi daftari ambalo limeshaandaliwa kwa ajili ya malipo liliwasilishwa kwa Mthamini Mkuu na Mthamini Mkuu ataleta Wizarani na Wizara tutapeleka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hawa katika kiwanja hiki cha Nachingwea. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Ezra Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kutokana na umuhimu wa Serikali kukuza utalii hususani katika mbuga yetu ya Burigi – Biharamulo, naomba kujua ni lini sasa uwanja wa ndege wa Biharamulo sasa utakarabatiwa ili uweze kuwa kiungo muhimu cha kuleta watalii katika eneo letu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chiwelesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kiwanja cha Ndege cha Biharamulo ni miongoni mwa viwanja 11 ambavyo tumevitengea fedha na kwa kiwanja cha Biharamulo pekee tumetenga takribani Milioni 400 kwa jili ya ukarabati kiwanja hiki cha Biharamulo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Je, ni lini uwanja wa ndege wa Bukoba Mjini utawekewa taa na mnara wa kuongoza ndege ili kuongeza usalama wa watumiaji wa uwanja huo?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kiwanja cha ndege cha Bukoba kwenye mwaka wa fedha ujao na kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais tumetenga takribani bilioni 2.9 kwa ajili ya ujenzi

wa *control tower* pamoja na taa za kuongozea ndege katika kiwanja hiki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Mbogwe ni kubwa iliyo na vyanzo vingi vya mapato, tumeshatenga eneo la kujengewa uwanja wa ndege tayari. Lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Mbogwe?*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge naomba mara baada ya kipindi cha maswali na majibu nionane naye ili niweze kuangalia bajeti kiasi gani tumetenga kwa bajeti ijayo katika eneo lake. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Lake Manyara *Airport* utajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, uwanja alioutamka Mheshimiwa Mbunge ni miongoni mwa viwanja ambavyo vipo chini ya Benki ya Dunia na tayari tupo katika mchakato wa kutangaza tenda ili viwanja hivi viweze kujengwa kikiwemo na Kiwanja cha Tanga, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 184

**Ujenzi wa barabara ya Kigonsera – Matiri na Mbinga – Litembo**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa kiwango cha lami barabra ya Kigonsera hadi Matiri na Mbinga hadi Litembo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imetangaza zabuni kwa ajili ya kupata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya Mbinga – Litembo – Mkiri sehemu ya Mbinga – Litembo/Mbuji kilometa 22 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami ambapo zabuni zimefunguliwa tarehe 19 Aprili, 2023 na uchambuzi wa zabuni unaendelea. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana Serikali itatafuta fedha za kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa barabara ya Kigonsera – Matiri – Mbaha kilometa 55, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ambayo yanatia moyo wananchi hawa wa Wilaya ya Mbinga kwa maana ya barabara hii ya Litembo ambayo imesubiriwa kwa muda mrefu na inaahadi za Marais Watatu kujengwa kwa kiwango cha lami, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Matiri kwa maana ya Kigonsera hadi Matiri ambako kuna kilimo kikubwa cha maharage na mahindi inapitika kwa shida sana, sasa wakati tunasubiri mchakato huo kuendelea, Serikali inampango gani wa kuifanya hii barabara iweze kupitika kwa msimu mzima?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, barabara ya kutoka Liyombo kuja hadi Rwanda kupitia Mdunduwalo ambayo Makaa ya Mawe yanapita hivi sasa ama haipitiki baadhi ya siku, ama inapitika kwa shida sana, tumeleta maombi maalum ni lini sasa Serikali itaitengeneza barabara hii kupitisha makaa ya mawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Matiri - Kigonsera kama alivyoisema kweli ni barabara ya changarawe ambapo sasa hivi ni kipindi kikubwa ambacho mvua kubwa sana inanyeesha naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshatoa taarifa kwa mameneja wote wa *TANROADS* Tanzania kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo zinachangamoto waweze kuzisimamia kwa ukaribu na narudia

tena kumsisitiza Meneja wa Mkoa wa Ruvuma ahakikishe kwamba barabara ya Matiri – Kigonsera inapitika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili la kutoka Liyombo hadi Rwanda hii ndiyo barabara ambayo inasafirisha sana Makaa ya Mawe na kuna migodi kama minne, ambayo pia Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo tuweze kuitengeneza.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii tutahakikisha kwamba inapitika na kama nilivyosema kwamba kwenye barabara zingine Mkandarasi yuko *site* kwenye hayo maeneo lakini inategemia na hali ya hewa. Kwa hiyo, Mkandarasi yuko *site* kuhakikisha kwamba patakapotokea nafuu ya hali ya hewa wataendelea kuitengeneza hiyo barabara ili iweze kupitika. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kufahamu ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kutujengea barabara ya Mlowo – Kamsamba? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, babrabara ya Mlowo - Kamsamba naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ni barabara ambayo imepigiwa sana kelele katika Bunge hili, kwa hiyo tunategemea kwamba itakuwa kwenye mapendekezo kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Norah Mzeru, swali la nyongeza.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara ya Isimilo -

Kilombero ili kuwasaidia wakulima kupitisha mazao yao kwa urahisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii naamini inatengenezwa na inakarabatiwa, changamoto kubwa ambayo tunayo sasa hivi ni barabara nyingi katika kipindi hiki cha mvua kunatokea changamoto, pia nitoe tu maelekezo tena kwa Meneja wa Singida kuhakikisha kwamba anaisimamia hii barabara na inapitika muda wote wakati huu wa kilimo kwa wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya Makambako - Songea hasa eneo la Madaba kuanzia Igewisinga mpaka Mtiangimbole limebomoka vibaya sana kiasi cha kuhatarisha usalama wa watumiaji. Je, ni lini sasa Serikali itaijenga hii barabara kwa uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemuelewa vizuri hii ni barabara kubwa ya kutoka Makambako kwenda Songea, hii barabara ipo kwenye mpango wa kukarabatiwa na *World Bank,* sasa hivi tutaanzia Lutukila kwenda Songea ikiwa ni pamoja na

*bypass* ya Songea Mjini, wakati huo sasa inatafutwa fedha kuanzia Makambako hadi Lutukila.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa, Serikali imeshatoa Milioni 300 kwa ajili ya upembuzi wa barabara ya kutoka Kahama - Nyang'wale – Busolwa - Busisi - Sengerema kwa kiwango cha lami, na huwa unanijibu majibu ya kisiasa nataka leo unijbu, ni lini upembuzi huo utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tukishatenga fedha kwenye bajeti nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita iko makini, ikishatenga maana yake tunatekeleza, isipokuwa tu ni hatua kuwa hatua ndefu.

Mheshimiwa Spika, barabara inayotwa siyo barabara fupi Kahama Nyang'wale - Ngoma hadi Busisi ni parefu, kwa hiyo iko tayari inafanyiwa kazi nakuhakikishia baada ya kukamilika ndiyo sasa tutajua gharama ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Sabu Swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, ahsante; je, ni lini barabara ya Bariadi – Ngulyati kwenda Magu itajengwa kwa

kiwango cha lami kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pia hii barabara ni kati ya barabara ambazo zimeongelewa sana. Namwomba Mheshimiwa Mbunge tusubiri, tutakapoleta bajeti yetu watupitishie, na ninaamini itakuwa ni moja ya barabara ambazo zitakuwepo kwenye mpango, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Barabara ya Iringa – MR – Itunundu iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi zaidi ya miaka 30. Ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, kwanza itatakiwa iingizwe kwenye usanifu wa kina, baada ya hapo tukishafanya hiyo kazi, ndiyo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tunatambua kwamba iko kwenye Ilani, ifanyiwe usanifu na ninaamini kazi hiyo tutaifanya katika kipindi hiki cha miaka mitano, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Barabara ya kutoka Hoteli Tatu – Pande – Lihimalyao iko chini ya *TARURA,* lakini Bodi ya Barabara pamoja na Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Lindi ilipendekeza barabara hii iapandishwe hadhi, ichukuliwe na *TANROADS*; ni lini *TANROADS* itaichukua barabara hii? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Swali hilo ni la muhimu sana lakini sina hakika kama unayo majibu sasa, kwa sababu ni barabara mahususi na inataka majibu mahususi. Kama huna majibu, ataleta kama swali la msingi, kama unayo mjibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kuleta swali mahususi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kilometa 52 kutoka Kilindoni mpaka Rasi Mkumbi, Kisiwani Mafia ni lini zitakamilika kwa ujenzi wa lami? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyotaja Mheshimiwa Mbunge tumeitengea bajeti mwaka huu unaoendelea na tutaendelea kuitengea katika mwaka unaokuja hiyo barabara ambayo iko katika Kisiwa cha Mafia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Tumeshuhudia mvua kubwa zinazoendelea nchi nzima na kufanya mawasiliano katika baadhi ya maeneo kukatika na hivyo kuchukua muda mrefu kuzitengeneza kwa wakati ili wananchi waweze kuendelea na usafiri na usafirishaji, lakini kuokoa uhai wa watu kwa wale ambao labda wanahitaji huduma hizo kwenda hospitali na vinginevyo:-

Nini mkakati wa Serikali wa haraka endapo inatokea changamoto ya namna hiyo, inafanyika kwa haraka na mawasiliano yanarudi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunategemea tutaoa taarifa, kama alivyoongea hata juzi Mheshimiwa Kunambi. Barabara nyingi ambazo tunazo Tanzania, ni Kilometa kama 36,000 ambazo tunazihudumia. Kati ya hizo, ni kilometa 12,000 tu ambazo zina lami. Kwa hiyo, barabara hizi zenye urefu wa kilometa kama 24, nyingi ni za changarawe na nyingine zipo mabondeni ambazo tumeshatoa taarifa kwa wakuu wa barabara kwa maana ya Meneja wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba barabara zote ambazo zinakuwa na changamoto wanazi-*attend* kwa muda.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambapo ni kwenye madaraja, tuna madaraja ya muda ya chuma ambayo kama ni daraja linaweza lakini bahati mbaya unakuta siyo tu daraja limeondoka, lakini ni tuta pengine la kilometa moja mpaka mbili limeondoka na wakati mvua inanyesha inakuwa ni ngumu kuweza kufanya hiyo kazi wakati pana maji, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta tangazo la wageni, halafu baadaye kuna maelezo ambayo nitayatoa. Kuna mtu amesimama kule nyuma, sijui kama ni Mbunge au ni nani amesimama, nami nimesimama hapa mbele.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; kwanza, tutaanza na mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Mheshimiwa Omary Said Kumbilamoto; karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni viongozi wa watendaji kutoka Wizarani, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hiyo, wakiongozwa na Ndugu Kheri Mahimbali ambaye ni Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Msafiri Mbibo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, yupo Profesa Idris Kikula, Mwenyekiti Tume ya Madini; *Major General Retired* Michael Isamuhyo, Mwenyekiti Bodi ya *STAMICO;* Profesa Justian Ikangula, Mwenyekiti Bodi ya *GST*; Dkt. George Mofulu, Mwenyekiti *TGC;* Ndugu Abdulrahman Mwanga, Kamishna wa Madini; Ndugu Daniel Kidesheni, Mratibu Kituo cha *TGC*; Ndugu Deusdedith Magala, Kaimu Mkurugenzi *STAMICO*; Ndugu Mariam Mgaya, Kaimu Katibu Mtendaji, *TEITI*; Mhandisi Yahya Samamba, Katibu Mtendaji Tume ya Madini; Dkt. Mussa Budeba, Mkurugenzi Mtendaji *GST*; Ndugu Ally S. Ally, Meneja Mkuu *STAMIGOLD*; Ndugu Augustini Ollal, Mkurugenzi wa Sera, Mipango wa Wizara ya Madini; Ndugu Issa Nchasi, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu; na Ndugu Jullieti Moshi, Mkurugenzi wa Sheria, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wadau wa madini kutoka Makampuni ya Uchimbaji wa Madini ambayo Serikali ina ubia. Sijui kama wanajifahamu hawa, wanaweza kusimama. Makampuni ya uchimbaji ya madini ambayo Serikali ina ubia. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yapo pia Makampuni ya Uchimbaji wa Madini; wapo pia kutoka *Chamber of Mines*; lipo pia Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini Tanzania *(FEMATA)*; wapo pia Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania *(TAMIDA);* kipo pia Chama cha Wanunuzi Wadogo wa Madini Tanzania *(CHAMATA);* wapo Chama cha Kuendeleza Wanawake katika Madini *(WIMO);* na pia tunao Chama cha Wanawake katika Madini *(WIMA),* karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo wadau kutoka Haki Rasilimali; Thamani Madini; Mahakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Bukombe; Ipo pia Benki ya Azania; ipo pia Benki ya *CRDB*; na vile vile wapo Benki ya *NMB,* karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile ipo Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Bukombe ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ambaye ni Mheshimiwa Said Nkumba, karibuni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambao ni wapiga kura wake kutoka jimboni kwake Bukombe, Mkoani Geita wakiongozwa na Ndugu Philip Shigaka, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo mgeni mwingine ambaye nafikiri hakuandikwa hapa, huyu ni Chifu kutoka Ruvuma, Chifu wetu kutoka Ruvuma huyo na… *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sijamaliza utambulisho, kwa hiyo, simama kidogo Chifu. Unajua ni Bungeni pekee ndipo unaweza kumwambia Chifu asimame.

Sawa, sasa huyu ni Chifu kutoka Ruvuma, lakini pamoja na hayo, anatoka Jimbo la Peramiho kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, pia ni mjomba wake Mheshimiwa Mhagama. Ahsante sana Chifu wetu, karibu sana. *(Makofi/Kicheko)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini, na hii ni familia yake kutoka Jijini Arusha; yupo Ndugu Agnes Kiruswa ambaye ni mke wake; yupo pia mtoto wake ambaye ni Seyian Kiruswa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Ndugu Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu; yupo pia Ndugu Neema Msitha, Katibu Mtendaji BMT; yupo pia Ndugu Ally Tembele, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo; na Ado Komba, Mkurugenzi Msaidizi Maendeleo ya Michezo, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Gabriel Geay, Mwanariadha ambaye ameshika nafasi ya pili katika mbio kubwa za Kimataifa za *Boston Marathon,* haya, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Ngoja nimalize utambulisho huu maalum; Bwana Gabriel Geay, Wabunge kama wanaendelea kupiga makofi unakuwa umesimama mpaka yaishe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ngoja nimalize utambulisho basi; huyu ni mwanariadha ambaye ameshika nafasi ya pili katika

mbio kubwa za Kimataifa za *Boston Marathon* akimpita mkimbiaji mwenye kasi zaidi duniani ambaye ndio aliyekuwa anashikilia hiyo, nadhani itakuwa imeondoka kwa sasa, lakini amempita mkiambiaji mwenye kasi zaidi duniani Bwana Eliud Kipchoge. Kwa hiyo, huo ni utambulisho wa muhimu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Ahsanteni sana, pia mwaka 2022 alikuwa mshindi wa pili kwenye Mbio za *Valencia Marathon* na kumfanya kushika nafasi ya nane duniani. Kwa hiyo, huyu ni mkimbiaji namba nane duniani. Nadhani kwa ushindi wake wa kuwa wa pili kwenye hii nyingine labda itakuwa nafasi imesogea sogea kule juu. Tunakutakia kila la heri. Ahsante sana kwa kulitea Taifa letu heshima, unaweza kuketi sasa. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Alphonce Simbu ambaye ni mwanariadha. Huyu ni mwanariadha ambaye ameshiriki mbio kubwa za *Osaka Marathon* nchini Japan na kushika nafasi ya tatu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia Simbu ni Mshindi wa Medali ya Fedha katika Mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika *Birmingham* na kufungua pazia la medali nchini. Nadhani wote tulimsikia wakati huo, angalau sasa medali zimeanza kufululiza. Kwa hiyo, tunakushuru sana Alphonce Simbu kwa heshima ambayo umeliletea Taifa hii na sasa tunaona medali nyingi zikiendelea kuja, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Sasa kumbe huku ndio alikuwa amewekwa Chifu wetu, sasa kwa sababu nilishamtambulisha, labda sasa nimtaje tu jina lake anaitwa Chifu Emmanuel Zulu Gama, Chifu wa Songea, ahsante sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 51 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni wanafunzi wa

Kitivo cha Sheria Chuo cha Makumira cha Jijini Arusha. Wapo wageni wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wa Mkoa wa Manyara, Ndugu Janes Darabe na Ndugu Mohamed Farah ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM kutoka Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Nusrat Hanje ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe cha Mjini Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Justine Nyamoga kutoka *Shamba FM* Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya kutoka Ngara Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Vitalis Ndailagije na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa *Col.* Mathias Kahabi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni Wahadhiri na Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Iringa wakiongozwa na Ndugu Crispin Nyomoye. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni mabondia kutoka nchini Afrika ya Kusini na hawa ni Ndugu Kuvesa Katembo ambaye ni bondia aliyepigana na Hassan Mwakinyo. Katika hao yupo Ndugu John Butodi ambaye ni kocha, yupo pia Ndugu Bonyele Intole ambaye ni daktari, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa sitaki kuzizungumzia sana ngumi ambazo niliogopa kumvunja Mheshimiwa Ngw'asi Kamani, si mnajua alivyo, ningemvunja sasa ingekuwa mtihani humu ndani. Kwa hiyo, nikaona nimlindie uhai wake. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanachama 85 wa CCM, Jamii Mpya kutoka Ilala, Jijini Dar es Salaam. Hii kweli hatari kabisa! Eh, hii ni hatari, maana kwa suti hizo tumemwelewa Mheshimiwa Zungu, ahsanteni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo pia watumishi 12 wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, sijui wamekaa upande gani hawa? Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao asubuhi hii hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo maelezo yangu kuhusu Azimio la Bunge la Kuidhinisha kufuta hasara ama upotevu wa fedha na vifaa va Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2022.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba siku ya tarehe 25 Aprili, 2023 wakati wa mjadala wa Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria hapa Bungeni, Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, aliomba ufafanuzi kuhusu Azimio la Bunge la kuidhinisha kufuta hasara ama upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022 ambalo alieleza kwamba halikuwahi kupitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika maelezo yake Mheshimiwa Lusengekile alifafanua kwamba siku ya tarehe 16 Septemba, 2022 ambapo Azimio hili liliwekwa kwenye orodha ya shughuli kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Bunge, Waziri husika pamoja Mwakilishi wa Kamati inayohusika waliwasilisha Mezani Hati za Azimio hilo. Isipokuwa kwamba, ilipofika wakati wa Mtoa wa Hoja kuwasilisha Azimio hilo liliondolewa na hayakuwahi kuwa Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutoa ufafanuzi wa hoja hiyo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro alikiomba kiti kiangalie uwezekano wa kupata ushahidi na uthibitisho kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* ili kujiridhisha kama ilikuwa ni kosa au siyo ili masahihisho stahiki yaweze kufanywa kwa mujibu wa mwongozo utakaotolewa na kiti.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kiti kilipokea hoja zote zilizotolewa na kuahidi kuzifanyia kazi, napenda kuliarifu Bunge hili kwamba ni kweli Azimio la Bunge la kuidhinisha kufuta hasara ama upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2022 iliwekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Nane wa Bunge, lilijadiliwa na Kamati husika na hatimaye kupangwa kujadiliwa na kupitishwa na Bunge tarehe 16 Septemba, 2022 ambapo hati za azimio hilo ziliwasilishwa mezani.

Waheshimiwa Wabunge, aidha kutokana na sababu mbalimbali na kuwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, Serikali iliahirisha kuwasilisha azimio hilo kwa wakati huo hadi wakati mwingine muafaka na hivyo halikuwahi kupitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa ni kawaida kwa Bunge kupitisha azimio lenye maudhui haya kila mwaka wa fedha natumaini Serikali itakamilisha utaratibu unaotakiwa kuhusu azimio hilo ili Bunge liweze kufanya kazi yake ya kulipitia azimio hilo na kisha kufanya maamuzi. Kwa hiyo, tunaamini watafanya hivyo ndani ya Bunge hili ili kutoa nafasi kwa ajili ya mwezi Septemba kuletewa azimio linalohusu mwaka mwingine sasa unaokuwa unafuata. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo huo ndiyo mwongozo kuhusu jambo hili na kwa hivyo kwa kadri tulivyokuwa tumehojiwa

kuhusu azimio hili, wakati ikijadiliwa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria taarifa hiyo inaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge lakini pia kwenye taarifa za Wizara zinazohusika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba yetu. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko aje awasilishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Madini naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali, kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yenye kurasa 116 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa kwenye Ofisi za Bunge. Kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini na kuendelea kuipa kipaumbele sekta hii katika kutoa miongozo, maelekezo na maagizo mbalimbali katika kipindi cha uongozi wa Awamu ya Sita. Tumeshuhudia mafanikio katika sekta ya madini ikiwemo kuzilinda rasilimali madini, kuvutia wawekezaji na kuongeza ushiriki wa Watanzania kwenye sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha kuwa rasilimalimadini zinawanufaisha Watanzania na taifa kwa ujumla. Vile vile nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na maelekezo yake aliyoyatoa ili kufanikisha utendaji Serikalini ikiwemo Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa umahiri, hekima, busara na ubunifu mkubwa. Aidha nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyo tuongoza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze kwa dhati kabisa Dunstan Luka Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa namna wanavyoiongoza Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako tukufu kwa kazi nzuri ambayo limekuwa likiifanya

katika kuisimamia na kuishauri Serikali ikiwemo Wizara ya Madini. Aidha napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali wanazozisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru watu wema wa Bukombe kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wao. Naahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu na kutekeleza shughuli za maendeleo Jimboni kwetu. Daima kusema na kutenda uendelee kuwa msingi Wilayani kwetu Bukombe.

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze kwa dhati Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mbunge), Naibu Waziri wa Madini, Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Bw. Msafiri Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa kuaminiwa kuiongoza Wizara hii ya Madini. Aidha, niwashukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga Kamishna wa Madini, Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati mke wangu mpenzi Benadetha Clement Mathayo na watoto wetu wapendwa kwa kunivumilia na kunipa ushirikiano wakati wote ninapotekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa niungane na wenzangu kutoa pole kwa Wananchi wa Jimbo la Amani Zanzibar, kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa. Vilevile, natoa pole za dhati kwa wananchi wote walipoteza ndugu na mali zao kutokana na majanga mbalimbali. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2022/2023; na Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa madini nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu ambayo huchangia takriban asilimia 80 ya mapato yote yanayotokana na rasilimali madini. Kwa kipindi kuanzia Julai mwaka 2022, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda kutoka wastani wa dola za Marekani 1,736.37 hadi kufikia dola za Marekani 1,854.5 Machi, 2023. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhitaji mkubwa wa madini hayo hapa duniani.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko la mahitaji ya baadhi ya madini ikiwemo dhahabu, *palladium, nickel, aluminium, cobalt* na madini mengine ya kinywe. Ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo vita vya Urusi na Ukraine hivyo kusababisha mahitaji ya madini haya kuwa yanahitajika kwa sababu nchi zinazohusika katika vita hizo ni wazalishaji wakubwa wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini ya almasi, bei ya madini hayo ilipungua kutoka kwenye soko la dunia kutoka dola za Marekani 296.63 kwa karati hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 265.8 kwa karati katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Kushuka kwa bei ya madini ya almasi kumesababishwa na upungufu wa mahitaji wa madini hayo, uliosababishwa na mtikisiko dunia hususan katika nchi za Bara la Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Wizara inachukua hatua mbalimbali ili kunufaika na mahitaji ya madini duniani kwa upande wa madini ya almasi, Wizara inatafuta masoko mengine ya kimataifa zikiwemo Nchi za Falme za Kiarabu zenye uhitaji mkubwa wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara inaendelea kuhimiza uwekezaji na utafutaji na uchimbaji wa madhini mkakati ili kuhimiza uongezaji thamani ya madini nchini kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuangalia uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya tozo ili kuvutia uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 894.27. Hadi kufikia Machi 2023, Wizara imekwisha kukusanya shilingi bilioni 548 katika kipindi rejewa. Fedha hizo shilingi bilioni 509.32 zilipelekwa Hazina na shilingi bilioni 38.68 zimekusanywa na kutumika na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitengewa Bajeti ya shilingi bilioni 83.44 kwa ajili ya matumizi na taasisi zake. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 22 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 20.6 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 40.83 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 23, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 47.86 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15.04 ni mishahara ya watumishi, shilingi bilioni 28.22 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 4.6 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 23 shilingi bilioni 9.42 zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ambapo shilingi bilioni 4.6 kutoka kwenye bajeti ya maendeleo na shilingi bilioni 4.8 kutoka katika akaunti ya amana. Miradi iliyotekelezwa ni

pamoja na kukamilisha ujenzi wa Vituo vya Umahiri Songea, Mpanda na Chunya, ujenzi wa ghala la kuhifadhia miamba choronge na ununuzi wa vifaa vya maabara na utafiti kwa ajili ya *GST*, ununuzi wa mawe mawili ya Tanzanite na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imetekeleza vipaumbele vifuatavyo; kwanza kuimarisha ukusanyaji wa maduhuri na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele hicho, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali ya mipaka nchini, viwanja vya ndege, bandari na kuanzisha na kuimarisha masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 93. Hadi kufikia Machi, 2023 mauzo katika masoko ya vituo hayo yamefikia shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kudhibiti utoroshaji wa madini hapa nchini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali. Jitihada hizi zimesaidia kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi milioni 532.44, madini hayo yamekamatwa katika mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Kahama, Songwe na Singida.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wafanyabiashara wa madini kufanya kazi kwa uaminifu, kuzingatia sheria na kanuni na taratibu zilizowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizo, kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuri ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 23, shilingi bilioni 509 zimekusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina na ikilinganishwa na shilingi bilioni 461.6 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha uliopita. Ongezeko hilo ni sawa na 10.34%.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la taifa umeendelea kuimarika, 4.4% mwaka 2017 hadi kufika 7.2% mwaka 2021. Aidha katika kipindi cha robo cha mwaka cha Julai hadi Septemba mwaka 2022. Sekta ya madini ilikua kwa 9.8%. vilevile katika kipindi hicho hicho, mchango wa Sekta ya Madini katika pato la taifa uliongezeka na kufikia 9.7% ikilinganishwa na 7.9% katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Mwenendo huu wa ukuaji wa Sekta ya Madini unatupa imani kuwa kiwango kilichowekwa cha 10% cha kuchangia ifikapo mwaka 2025 tutakifikia.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta ya Madini katika kuliingizia taifa fedha za kigeni umekuwa ukiimarika. Mwaka 2022 madini yenye thamani ya dola za Kimarekani 3,395.3 yaliuzwa nje ya nchi sawa na 56% ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 3,116.4 sawa na 45.9% mwaka 2021. Aidha mwaka 2021/2022 mchango wa mapato ya kodi za ndani umefika shilingi trilioni 2.09 sawa na 15.84% ya mapato yote ya kodi za ndani ikilinganishwa na mapato ya shilingi trilioni 1.08 sawa na 10.31% ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kingine ni kuendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki kwenye uchumi wa madini. Wizara ilitoa elimu jinsi ya kushiriki katika shughuli za madini kwa wachimbaji wadogo katika Mikoa ya Geita, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Njombe, Ruvuma, Kigoma, Mara, Iringa na kugawa nakala 400 za miongozo kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, *GST* pia ilitoa mafunzo ya uchukuaji wa sampuli kwa wachimbaji wapatao 2,200 katika Mikoa ya Lindi, Morogoro. Aidha ilifanya utafiti maalum katika maeneo ya wachimbaji wadogo katika Wilaya ya Gairo ambapo matokeo ya awali yameonyesha uwepo wa mwendelezo wa mkondo wa

dhahabu katika Kijiji cha Kitaita na Reshata. Vilevile *STAMICO* imetoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya kemikali na vilipuzi kwa wachimbaji wadogo 829 katika vituo vya mfano vya Katente, Rwamgasa na Itumbi.

Mheshimiwa Spika, taasisi za fedha na benki nchini zimeendelea kuonyesha mwitikio mzuri katika kuwawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia fedha na vifaa. Taasisi zilizotoa mikopo ni pamoja na Benki ya NMB, NBC, AZANIA, CRDB, KCB. Hadi kufikia Machi 2023, shilingi bilioni 145 zimekopeshwa kwa wachimbaji wadogo ikilinganishwa na shilingi bilioni 36 zilizokopeshwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana taasisi za fedha, mabenki na kuwaomba waendelee kuwaamini wachimbaji wadogo kwa sababu wachimbaji wa sasa siyo kama wachimbaji wa zamani.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini ambapo inaandaa mkakati wa uongezaji thamani madini. Lengo ni kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na madini na kuwezesha uwekezaji wa ndani na nje. Vilevile mfumo wa biashara ya madini ya Tanzanite umeandaliwa ili kudhibiti bei na kuongeza thamani ya madini hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara imeanza shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya *TGC* ambapo kwa sasa taratibu za ujenzi wa jengo la kisasa litakalotumika kwa ajili ya mafunzo na uongezaji thamani nchini zimekamilika. Aidha watumishi wanne walifanya ziara za mafunzo katika Nchi ya Thailand, India kwa ajili ya kuongeza ujuzi katika uongezaji thamani madini, uendeshaji wa viwanda na kuchakata madini utoaji wa huduma za maabara za madini ya vito na kutengeneza bidhaa za usonara.

Mheshimiwa Spika, aidha, watumishi watatu wanahudhuria mafunzo ya kuongeza thamani ya madini ndani ya nchi na watumishi sita wamehudhuria mafunzo hayo katika nchi za Thailand, China pamoja na India.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kipaumbele cha kuhamasisha biashara na uwekezaji katika sekta ya madini kuanzia Julai 2022 hadi Machi 23 Tume ya Madini imetoa leseni kubwa ya uchimbaji wa madini ya kinywe kwa kampuni ya *Faru Graphite Corporation Limited* na leseni ya uchimbaji wa kati wa madini ya Tanzanite kwa kampuni ya *Franone Mining Limited* kwa ajili ya kitalu *C* Mirerani. Thamani ya uwekezaji katika miradi hiyo inatarajiwa kuwa na takribani dola za Kimarekani milioni 538.925.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini imetoa leseni 6,381 katika shughuli za utafutaji, uchimbaji na biashara na uongezaji thamani madini. Kwa mwaka 2021, shughuli za madini zimezalisha takribani ajira 14,742 kwenye migodi mikubwa. Kati ya ajira hizo, 14,308 ni ajira za Watanzania sawa na 97% na ajira 434 pekeyake sawa na 3% ni ajira za wageni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesaini mikataba ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini muhimu na madini mkakati hapa nchini kwa kampuni ya *Evolution Energy Minerals Limited, EcoGraf Limited* na *Peak Rare Earth Limited* za Australia tarehe 17 Aprili, mwaka huu. Mikataba hiyo yote ina thamani ya dola za Marekani milioni 667 ikihusisha uchimbaji wa madini ya kinywe katika eneo la Chilalo Wilayani Ruangwa na Epanko Wilaya ya Ulanga pamoja na madini adimu ya *rare earth elements* katika eneo la Ngualla Wilaya ya Songwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa makubaliano hayo, miradi hiyo itasimamiwa na kampuni za ubia baina ya Serikali na wawekezaji za *Kudu Graphite Limited* kwa mradi wa Chilalo,

*Duma TanzGraphite* kwa mradi wa Epanko na *Mamba Minerals Corporation* kwa mradi wa Ngualla.

Mheshimiwa Spika, kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa shughuli za migodi nchini, Wizara imeendelea na jukumu hili katika kipindi cha Julai 22 hadi Machi 23, migodi mikubwa sita ya *Williamson Diamond*; *Buckreef*; *North Mara, Geita Gold* Bulyanhulu na Buzwagi na migodi mingine 66 ya kati na migodi midogo 19,528 ilikaguliwa katika maeneo mbalimbali. Katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ambapo wahusika walielekezwa kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake pamoja na Sheria ya Utunzaji wa Mazingira ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kuzijengea uwezo taasisi, *GST* imewezeshwa kununua vitendeakazi ikiwemo basi kwa ajili ya watumishi, vifaa vya *geoscience* na maabara pamoja na kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za madini choronge zilizojengwa katika eneo la Kizota Dodoma. *STAMICO* imewezeshwa kununua mitambo mitano ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo na mitambo mikubwa miwili ya uzalishaji wa mkaa mbadala *(Coal briquette)*. *TGC* imewezeshwa kununua magari manne kwa ajili ya kufanikisha shughuli za kituo na fedha kwa ajili ya mafunzo kwa kuwaongezea ujuzi watumishi wa Tume ya Madini vile vile inaendelea na ujenzi wa jengo la makao makuu.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi Wizara imeajiri watumishi 30 na kujaza nafasi zilizokuwa wazi 26 kwa utaratibu wa uhamisho; kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya makao makuu ya Wizara na kuwawezesha watumishi 114 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maeneo mbalimbali; kwanza ufatiliaji na usimamizi wa shughuli za baruti. Katika kuhakikisha shughuli za biashara na uhifadhi wa baruti zinafuata matakwa ya Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963, Wizara imefanya ukaguzi wa maghala 79 ya kuhifadhi baruti katika mikoa wa Geita, Mbeya, Songwe, Mwanza, Tanga na Pwani. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi katika kiwanda cha kutengeneza baruti cha Kampuni ya *Mbogo Mining and General supply*. Katika kaguzi hizo baadhi ya maghala yalibainika kuwa na mapungufu na wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo, na walitekeleza maelekezo hayo kama walivyopewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala ya kuhifadhia baruti ya Kampuni za *Tanga Cement* iliyooomba maghala yao kuvunjwa. Kupitia ukaguzi huo kibali cha kubomoa maghala ya kuhifadhi baruti kilitolewa pia ulifanyika ukaguzi mwingine katika maeneo ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi baruti kama Kampuni ya *Siontinto* ilipewa kibali cha ujenzi. Vibali na leseni za baruti zilitolewa na vimepatia Serikali jumla ya shilingi milioni 376.5.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea na zoezi la kurekebisha sheria mbalimbali na kurekebisha Sheria ya Madini Sura ya 123 kupitia marekebisho mbalimbali. Marekebisho hayo ni pamoja na kuanzisha leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini, kumpa Waziri mamlaka ya kurejesha Serikalini maeneo ya leseni za madini zilizofikia ukomo, kuipa *GST* mamlaka ya kisheria ya kufanya utafiti wa kina kwa madini mkakati. Kuweka muda wa kuhuisha leseni na utafutaji wa madini kwa kipindi cha pili na kuweka muda wa kuanza shughuli za uchimbaji baada ya kupewa leseni kwa wamiliki wa leseni ndogo za uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara imetunga Kanuni za Madini (Ufifilishaji wa Makosa) za Mwaka 2022 na kutangazwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 549 la tarehe 2 Septemba, 2022. Kanuni hizi

zinaweka masharti mbalimbali ikiwemo utaratibu wa kufifilisha makosa, ulipaji wa fedha kwa kosa lililofifilishwa, utaratibu wa kukaza hukumu ya ufifilishaji iliyotolewa na Tume ya Madini, utunzaji wa fedha zinazotokana na ufifilishaji wa makosa na utoaji wa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imetunga Kanuni mpya za Madini za Ushiriki wa Serikali *(State Participation)* za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 574 la tarehe 23/9/2022. Kanuni hizi pamoja na masuala mengine zinaweka masharti ya leseni zinazorejeshwa Serikalini, masharti ya umiliki wa hisa zisizofifishwa *(non-dilutable shares)* na haki zake za kimsingi za kuingia ubia kati ya Serikali na kampuni za madini; usimamizi wa kampuni za ubia na *models* za mkataba wa msingi wa ubia na katika kampuni ya wanahisa katika ubia huo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Madini ilipokea na kupitia jumla ya mipango 510 ya ushirikishwaji wa Watanzania katika sekta ya madini ambapo mipango 505 iliidhinishwa. Mipango mitano haikukidhi vigezo na hivyo haikuidhinishwa na kupewa muda wa kurekebisha. Aidha, Tume ya Madini ilipokea maombi 513 kutoka kwa wamiliki wa leseni na wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya idhini ya kuendelea na hatua mbalimbali za ununuzi wa huduma na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara; Wizara ina jukumu la kusimamia taasisi tano ambazo ni Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia ya Utafiti nchini, Shirika la Madini la Taifa, Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Kituo cha Jemolojia Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume ya Madini imetekeleza kama ifuatavyo; imetoa leseni za uchimbaji madini jumla ya leseni 6,381 kati ya leseni 6,116

zilizopangwa kutolewa katika kipindi husika. Aidha, leseni 16 za utafutaji wa madini zimetolewa, leseni 18 za uchimbaji wa kati wa madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutokuzingatia matakwa ya sheria. Vilevile leseni 12 za utafutaji wa madini na leseni 13 za uchimbaji wa kati zilifutwa baada ya kushindwa kurekebisha makosa hayo.

Mheshimiwa Spika, shughuli za usimamizi wa biashara ya madini kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 zilifanyika kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ambapo Tume ya Madini ilikusanya jumla ya shilingi 117,616,806,020.64 kutokana na mrabaha na ada ya ukaguzi kwenye masoko ya madini 42 na vituo vya ununuzi wa madini 93. Katika makusanyo hayo, shilingi 101,405,400,832.03 zilitokana na mrabaha; na shilingi 16,211,405,188.61 zilitokana na ada ya ukaguzi wa madini.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa mitambo ya kuchenjulia madini ya dhahabu. Tume ya Madini ilifanya ukaguzi wa mitambo ya kuchenjulia madini ya dhahabu kama ifuatavyo; mitambo 646 ya *vat leaching*, 10 ya *CIP* na 97 ya *elution*. Aidha kaguzi hizo zilibaini maeneo ya udongo wa mabaki ya dhahabu *(tailings),* kutowekewa mifereji ya kuyazunguka kwa lengo la kuzuia utiririshaji wa maji kwenye maeneo.

Mheshimiwa Spika, wahusika walielekezwa kuyafanyia kazi mapungufu hayo na viwanda viwili vya kusafisha dhahabu vya *African Eyes Company Limited* na Banjul *Limited* vilikamilisha na vilikidhi vigezo na kupewa leseni.

Mheshimiwa Spika, kupitia taarifa ya mpango ya ufungaji wa migodi; katika kipindi hiki jumla ya mipango ya ufungaji wa migodi tisa ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi. Kati ya mipango hiyo, mipango sita iliidhinishwa, mipango ya migodi mitatu ambayo ni *Minjingu Mines and Fertilizers, CATA Mining Company Limited* na *MMG Gold Mine* haikukidhi vigezo kutokana

na mapungufu yaliyobainika. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo yaliyobainishwa ili waidhinishiwe mipango yao.

Mheshimiwa Spika, jumla ya sampuli 6,047 za wateja mbalimbali zilipokelewa na kituo chetu cha *GST* na Tume ya Madini. Kati ya sampuli hizo sampuli 179 zilitoka migodi mikubwa ya dhahabu kwa ajili ya kuwezesha Serikali kukokotoa mapato stahiki na sampuli 4,351 zilitoka kwa wateja binafsi ambapo Serikali ilikusanya kiasi cha shilingi 336,136,000.00.

Mheshimiwa Spika, utambuzi na uthaminishaji wa madini yaliyoingizwa nchini na yaliyosafirishwa nje ya nchi; katika hatua ya kuimarisha na kusimamia biashara ya madini nchini, Tume ya Madini imetoa vibali 90 vya kuingiza madini nchini yenye thamani ya dola za Marekani 12,732,417.06 kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, aidha katika mwaka 2022, jumla ya vibali 10,318 vyenye thamani ya Mola za Marekani milioni 3,240.35 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 5,526 vilivyotolewa mwaka 2021 vyenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3,046.23. Ongezeko la vibali hivyo kwa kiasi kikubwa limetokana na ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume ya Madini imefanya ukaguzi wa kampuni 12. Kati ya kampuni hizo, tatu ni za viwanda vya saruji na tisa ni za miradi ya barabara. Kaguzi hizo zimewezesha kuibua hoja mbalimbali zinazohusiana na kutolipwa kwa malipo mbalimbali ya Serikali ya shilingi 5.3. Hadi kufikia Machi, 2023, shilingi 261 zimekusanywa kutokana na ukaguzi huo. Tume ya Madini inaendelea kufuatilia malipo yaliyobaki ili yalipwe na wahusika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kusogeza huduma kwa wananchi, Tume ya Madini imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua mfisi mpya katika mkoa wa kimadini wa Mahenge hivyo kuwa na jumla ya ofisi 30 za Maafisa Madini *Wakazi (RMOs)* zilizopo nchi nzima. Nitoe wito kwa wadau wa sekta ya madini nchini kuzitumia ipasavyo ofisi hizo ili kupata huduma ili kuwa na uchimbaji salama na wenye tija kwao.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO);* katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika limetekeleza miradi ifuatayo; kwanza limechimba tani 88,077.82 za makaa ya mawe katika mradi wa Kabulo-Kiwira ambapo tani 40,909.99 zenye thamani ya shilingi 4,520,488,032.86 ziliuzwa ndani na nje ya nchi na kubakiwa na Tani 47,167.83. Shirika limeanza uchimbaji wa makaa ya mawe katika kitalu E kilichopo eneo la Kabulo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha miundombinu ya kusafirishia makaa ya mawe, Shirika limekamilisha kujenga kituo cha kuhifadhi makaa ya mawe katika Bandari ya Mtwara. Mradi wa *coal briquettes* Shirika limeendelea na kufanya majaribio ya uzalishaji wa mkaa mbadala kutokana na makaa ya mawe ambapo limepata cheti cha hidhibati kutoka shirika la viwango nchini *(TBS)*. Bidhaa hiyo inatambulika kwa jina la *Rafiki Briquettes.* Aidha, Shirika limeagiza mitambo minne ya kuzalisha tani 20 kwa saa kila mmoja. Mitambo miwili imeshafika nchini na maandalizi ya kusimika mitambo hiyo yanaendelea katika eneo la Kiwira Songwe na mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa vituo vya mfano ni shughuli nyingine inayofanywa na Shirika letu la Madini la Taifa *(STAMICO)*. Shirika limeendelea kusimamia na kuimarisha huduma katika vituo vya mfano ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya gramu 30,475.72 za dhahabu zenye thamani ya shilingi 3,600,089,338.50 zilizalishwa na shilingi 279,659,530.20 zililipwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Kampuni Tanzu ya *STAMIGOLD* katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 mgodi umezalisha wakia 8,740.42 za dhahabu na wakia 1,001,770.65 za madini ya fedha zote zikiwa na thamani ya shilingi 36,365,275,161.79 ambapo Serikali imepata shilingi 2,654,665,072.86 kutokana na mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kusogeza huduma kwenye mgodi huu, Shirika la umeme nchini tayari limekwisha kuunganisha umeme wa *TANESCO* kwenye mgodi huu ambao kwa muda mrefu ulikuwa unatumia mafuta. Sasa naomba kutoa taarifa kuwa kuanzia jana shirika hili limeondokana na mfumo wa utumiaji wa mafuta na tunatumia umeme wa *TANESCO;* na kwa kweli naomba nitumie nafasi hii niwashukuru sana *TANESCO* na Wizara ya Nishati kwa wepesi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza kinaendelea na kupata ithibati *(ISO)* ili dhahabu itakayosafishwa kwa wateja wa ndani na nje ya nchi itambuliwe kimataifa. Taratibu hizo zinahusisha vigezo sita na kwa sasa kiwanda kimetekeleza vigezo vitatu. Aidha vigezo vinavyoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na utekelezaji wa taratibu zilizoandaliwa kwa nyaraka. Ukaguzi wa ndani na nje, usajili na utoaji wa cheti cha ithibati. Hatua ya ukaguzi inahitajika kwenda sambamba na uzalishaji endelevu ili ukaguzi uweze kufanyika na hatimaye cheti kiweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Dhahabu wa *Buckreef* umezalisha wakia za dhahabu 15,036.28 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 26 na kulipa Serikalini shilingi 4,544,586,358.9 kama mrabaha, ada za ukaguzi na ushuru wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea na kandarasi ya uchorongaji katika Mgodi wa *GGM*, *STAMIGOLD* na Mgodi wa *Buckreef*. Shirika imepata kandarasi mpya ya Kampuni ya *Miner*

*Station* wenye thamani ya shilingi milioni 600 na kuongezwa kwa mkataba wa kandarasi ya uchorongaji katika Mgodi wa *GGM* wenye thamani ya shilingi bilioni 55.25 na kusaini kandarasi ya Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef* wenye thamani ya shilingi bilioni 3.65.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Jiolojia imeendelea na majukumu yake kwanza kufanya tafiti za jiosayansi na kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini. Kuboresha huduma za maabara hapa nchini, kuratibu majanga ya asili ya jiolojia na kutoa elimu kwa wananchi. Aidha, *GST* imeendelea kuimarisha uwezo wa taasisi na kusogeza huduma kwa wadau kwa kusogeza huduma hizo katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi ya uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali madini, mafuta na mesi asilia *(TEITI)*. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 TEITI imetekeleza majukumu yafuatayo; kukamilika na kuwekwa wazi kwa umma ripoti ya mwaka 2019/2020 ya ulinganishi wa malipo ya kodi kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia yaliyopokelewa na Mamlaka za Serikali. Pamoja na mambo mengine ripoti hii inaainisha kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Juni, 2020 Serikali imekiri kupokea kiasi cha shilingi trilioni 1.2 kutoka kwenye kampuni 40 zilizofanyiwa ulinganisho. Taarifa hiyo inapatikana kwenye tovuti ya *TEIT*

Mheshimiwa Spika, *TEITI* imeendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi na umuhimu wa takwimu na ripoti zake kupitia runinga, redio, tovuti, mitandao ya kijamii na kwenye maonesho mbalimbali. Aidha, *TEITI* ilifanya warsha kuhusu matumizi ya takwimu za ripoti za *TEITI*, katika Mikoa ya kimadini ya Mwanza, Lindi, Mererani, Songwe na Mtwara zikiwa na lengo la kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani na watunza hazina wa halmashauri, waandishi wa habari, wachimbaji madini wadogo na asasi za kiraia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kituo chetu cha Jemolojia Tanzania *(TGC)* katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 imetekeleza majukumu ya utoaji mafunzo na udahili wa wanafunzi, uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa wadau wa madini kuendelea kuimarisha miundombinu ya kituo na kuwajengea uwezo watumishi wa kituo.

Mheshimiwa Spika, *TGC* inakusudia kujenga jengo jipya la kituo ambapo tayari Mshauri Elekezi amekamilisha michoro na Kituo kipo kwenye taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Makadirio na Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo;

i. Mwongozo wa kitaifa wa maandalizi ya bajeti wa Mwaka 2023/2024;

ii. Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi mwaka 2020;

iii. Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano 2021/2022 – 2025/2026;

iv. Sera ya Madini ya Mwaka 2009;

v. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025,

vi. Maelekezo ya Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Madini itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo;

i. Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuendeleza madini muhimu na madini mkakati hapa nchini;

ii. Kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo;

iii. Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;

iv. Uhamasisha uwekezaji na biashara katika sekta ya madini;

v. Uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la vipaumbele mwaka ujao wa fedha 2023/2024 wizara imeongeza maeneo mapya mawili ambayo ni uendelezaji madini muhimu na madini ya kimkakati kwenda sambamba na mahitaji ya sasa ya dunia yatakayokuwa yanahitajika kwa kiasi kikubwa katika vifaa vya *electronic* yaani betri na magari kwenye vifaa vya uzalishaji vinavyotumia nishati. Pili uanzishwaji wa minada ya maonyesho ya madini ya vito kwa lengo la kuinua biashara ya madini ya vitu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelezwa na Taasisi, Tume ya Madini imetekeleza kazi zifuatazo;

i. Kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa maduhuli,

ii. Kuimarisha ufatiliaji na ukaguzi wa usalama, afya ya mazingira na uzalishaji wa madini,

iii. Kuimarisha ukaguzi wa fedha na kodi, kuendelea kuboresha mazingira ya kuwawezesha wananchi kufaidika na rasilimali madini pia kuwaelimisha umma juu ya sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, upande wa *GST* imepanga kutekeleza mambo yafuatayo kwanza kufanya tafiti za jiosayansi na kuboresha kanzidata ya Taifa, kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kufanya tafiti za jiosayansi, kuboresha huduma za maabara na kuboresha uratibu wa majanga asilia ya jiolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa *STAMICO* imepanga kutekeleza kazi zifuatazo; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuendelea na uzalishaji wa makaa ya mawe pamoja na mkaa wa kupikia, kuimarisha shughuli za uchorongaji, kuendeleza leseni za shirika, kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo na kuimarisha vituo vya mfano.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa *TEITI*, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo;

i. Kuweka wazi ripoti za *TEITI* za ulinganisho za mwaka wa fedha 2021/2022,

ii. Kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta, gesi asilia,

iii. Kuweka wazi orodha za wamiliki wa hisa, kampuni za madini, mafuta gesi asilia na kuanzisha kanzidata za takwimu zitakazoifanya *TEITI* kuwa kitovu cha taarifa za takwimu za madini, mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Jemolojia Tanzania kimepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

kutoa mafunzo ya uongezaji thamani nchini, kuzalisha bidhaa zinazotokana na madini ya miamba na kuendeleza ujenzi wa kituo cha mfano.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa Serikali ya awamu ya sita imeendelea na juhudi kubwa sana ya kuhakikisha kuwa uchumi wa madini nchini unaimarika. Kasi kubwa ya utekelezaji na utendaji anayoendelea nayo Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadhihirisha kuwa nchi yetu inaendelea kukua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kutumia fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo yake. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Daktari Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo ambayo ameendelea kutupa katika kusimamia Wizara hii ya Madini. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo ametupa mwelekeo mpya wa usimamizi wa Serikali ikiwemo sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Daktari Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini kwa jinsi anavyoendelea kutoa ushirikiano katika kusimamia sekta ya madini. Amekuwa ni msaada mkubwa sana kwangu katika kuhakikisha kwamba sekta ya madini inatimiza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru watendaji wanaonisaidia wizarani wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu Wizara ya Madini Bwana

Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa ukuzaji wa sekta ya madini na watendaji wote wa wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Wenyeviti wa Bodi kwa moyo wa dhati kwa namna wanavyosimamia Taasisi hizi. Pia niwashukuru Wakuu wa Vitengo, Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Taasisi, wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa na kujituma kwao bila kuchoka katika kutekeleza majukumu yao. Nikiri kwamba bila wao mafanikio haya isingekuwa rahisi kuyafikia.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji wa madini, wachimbaji, wamiliki wa mitambo, wachenjuaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Hii imerahisisha kwa kiasi kikubwa usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, aidha, nishukuru Taasisi za Fedha hususani mabenki ambao tunao hapa leo kwa namna ambavyo wanaendelea kuiamini Sekta ya Madini na kuendelea kutoa mikopo. Naomba niwashukuru sana Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutuhakikishia usalama kwenye maeneo ya shughuli za madini bila kusahau Vyombo vyote vya Habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, sasa ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyopangwa ikiwemo kukusanya maduhuli ya Sh.1,006,705,169,300, naomba Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha makadirio ya Sh.89,357,491,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Sh.23,172,500,000 ikiwa ni Fedha za Maendeleo; Sh.66,184,941,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo Sh.20,307,498,000 ni kwa ajili ya Mishahara na Sh.45,877,443,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na Vielelezo kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na masuala ya kitakwimu muhimu kwenye sekta ya madini tumeambatanisha kwenye hotuba hii. Hotuba hii vile vile inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa kikoa cha www.madini.go.tz.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. DOTO MASHAKA BITEKO (MB.), WAZIRI WA MADINI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

***1. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua bajeti ya Wizara ya Madini, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Madini na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***2. Mheshimiwa Spika,*** kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kuijalia nchi yetu

amani na utulivu na kutuwezesha kushiriki katika mkutano huu wa 11 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mbele ya Bunge lako Tukufu.

***3. Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Madini. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii kwa kutoa Miongozo, Maelekezo na Maagizo mbalimbali. Pia, namuahidi Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu pamoja na Watanzania wote kwamba, tutaendelea kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na maarifa ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inakuwa yenye manufaa kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla.

***4. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita, tumeshuhudia uthubutu, ujasiri, uchapakazi na ubunifu mkubwa ambao umekuwa chachu ya mafanikio katika Sekta ya Madini ikiwemo kuzilinda rasilimali madini, kuvutia uwekezaji katika shughuli za uchimbaji madini, uchenjuaji, uongezaji thamani madini na kuongeza ushiriki wa Serikali katika shughuli za madini.

***5. Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yake mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha kuwa rasilimali madini zinawanufaisha Watanzania na Taifa kwa ujumla. Vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake makini na maelekezo anayoyatoa ili kufanikisha utendaji kazi Serikalini, ikiwemo Wizara ya Madini. Viongozi hawa wamekuwa tayari

kutusikiliza na kutupa miongozo na maelekezo mbalimbali na hivyo busara zao zimetusaidia katika kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi.

***6. Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa umahiri, hekima, busara na ubunifu mkubwa. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuna imani kuwa mtaendelea kuliongoza Bunge katika kufanya maamuzi makini kwa maslahi mapana ya Taifa.

***7. Mheshimiwa Spika,*** naomba niwapongeze Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati. Pia, nawapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kuteuliwa kuunda Kamati hiyo. Tunaipongeza Kamati kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yanasaidia kuongeza ufanisi na umakini wa utendaji kazi wa Wizara. Naahidi kuendelea kuipa Kamati ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inaendelea kukua na kuimarika huku ikiendelea kuwanufaisha watanzania.

***8. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Bunge lako Tukufu kwa kazi nzuri ambazo limekuwa likifanya katika kuisimamia na kuishauri Serikali, ikiwemo Wizara ya Madini. Kupitia kwako, naliomba Bunge liendelee kutupatia ushirikiano ili kuiendeleza Sekta hii muhimu katika kujenga uchumi imara na maendeleo endelevu ya Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Vilevile, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri

wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kusimamia Sekta ya Madini.

***9. Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge wao. Kutokana na majukumu ya kitaifa kama Waziri wa Madini kuna wakati wananikosa jimboni, lakini kwa wema wao wanaendelea kunivumilia na kunipa ushirikiano mkubwa. Nawaahidi kuendelea kuwa mtumishi wao mwaminifu katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya Jimbo letu.

***10. Mheshimiwa Spika,*** napenda niwapongeze kwa dhati Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri, Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu na Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa kuaminiwa kuiongoza Wizara ya Madini. Aidha, namshukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga Kamishna wa Madini pamoja na wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini pamoja na wafanyakazi wote kwa ushirikiano na utendaji kazi mzuri katika kutekeleza majukumu yao.

***11. Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kumshukuru mke wangu mpendwa Benadetha Clement Mathayo kwa maombi na upendo wake wa dhati kwangu na watoto wetu. Amekuwa mvumilivu kipindi chote ninapokuwa natekeleza majukumu ya ubunge na uwaziri na kukubali kubeba baadhi ya majukumu ya kifamilia. Aidha, nawashukuru watoto wangu pamoja na familia yangu kwa ujumla kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kuwalinda.

***12. Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na wenzangu kutoa pole kwa wananchi wa jimbo la Amani

Zanzibar, kwa kuondokewa na aliyekuwa mbunge wao Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa. Vilevile, natoa pole za dhati kwa wananchi wote ambao walipoteza ndugu na mali zao kutokana na ajali, maafa na maradhi yaliyotokea sehemu mbalimbali hapa nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

***13. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa shukrani na pole, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mahsusi ya hotuba hii ambayo ni: Mwenendo wa Biashara ya Madini Duniani; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## B. MWENENDO WA BIASHARA YA MADINI DUNIANI

***14. Mheshimiwa Spika,*** uchumi wa madini nchini kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu ambayo huchangia takriban asilimia 80 ya mapato yatokanayo na rasilimali madini. Kwa kipindi cha kuanzia julai, 2022, bei ya madini ya dhahabu kwa wakia ilipanda kutoka wastani wa dola za Marekani 1,736.37 hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 1,854.54 Machi, 2023. Kuongezeka kwa bei ya dhahabu kunatokana na sababu mbalimbali ikiwemo mahitaji makubwa ya madini hayo duniani.

***15. Mheshimiwa Spika,*** kumekuwa na ongezeko la mahitaji baadhi ya madini ikiwemo dhahabu, palladium, nickel, aluminium, cobalt na madini ya kinywe (graphite). Ongezeko hilo limetokana na sababu mbalimbali ikiwemo vita kati ya Urusi na Ukraine. Hali hiyo inatokana na baadhi ya madini hayo yanayozalishwa na Urusi kuwekewa vikwazo kuingia kwenye masoko ya dunia, na hivyo kutengeneza fursa ya uhitaji mkubwa kwenye nchi nyingine zinazozalisha madini hayo. Hii imeongeza

fursa za uwekezaji kutokana na bei za madini hayo kuendelea kupanda.

***16. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa madini ya almasi, bei ya madini hayo ilipungua katika soko la dunia kutoka wastani wa dola za Marekani 296.63 kwa karati hadi kufikia wastani wa dola za Marekani 265.78 kwa karati katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Kushuka kwa bei ya madini ya almasi kumesababishwa na kupungua kwa uhitaji wa madini hayo, uliosababishwa na mtikisiko wa kiuchumi hususan katika nchi za Bara la Ulaya, kutokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine.

***17. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inachukua hatua mbalimbali katika kutafuta masoko mengine ya kimataifa ya almasi yenye bei nzuri kama Nchi za Falme za Kiarabu ambazo zina uhitaji mkubwa wa almasi, kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na kuangalia uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya kodi na tozo kwa wachimbaji ili kuwaongezea wigo wa faida na kuchochea uzalishaji zaidi.

***18. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inaendelea kuhimiza uwekezaji katika madini mkakati ikiwemo *palladium, nickel, aluminium, cobalt, lithium* na kinywe (graphite) ili kunufaika na ongezeko la mahitaji ya madini hayo duniani. Aidha, Wizara inaendelea kuhimiza uongezaji thamani madini nchini ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na madini.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

### I. Mapato

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 894,278,406,800.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kati ya

fedha hizo, shilingi 822,028,205,000.00, sawa na asilimia 91.92 zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na shilingi 72,250,201,800.00, sawa na asilimia 8.08 zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

***20. Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2023, Wizara ya Madini imekusanya jumla ya shilingi 548,008,929,816.01 sawa na asilimia 61.28 kwa kipindi rejewa. Kati ya fedha hizo shilingi 509,320,355,707.01 zilipelekwa Hazina na shilingi 38,688,574,109.00 zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ajili ya matumizi ya taasisi husika.

**II. Matumizi**

***21. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ilitengewa bajeti ya shilingi 83,445,260,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na taasisi zake. Kati ya fedha hizo, shilingi 22,000,000,000.00 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na shilingi 61,445,260,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi 20,609,600,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na shilingi 40,835,660,000.00, kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

***22. Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi 47,868,045,919.70 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 4,601,640,975.30 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi 43,266,404,944.40 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa, shilingi 15,045,584,058.52 zimetumika kulipa mishahara ya watumishi na shilingi 28,220,820,885.88 ni matumizi mengineyo.

## III. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

***23. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Fedha za Maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 9,421,031,881.01 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi 4,601,640,975.30 ni kutoka kwenye bajeti ya maendeleo na shilingi 4,819,390,905.71 ni kutoka katika Akaunti ya Amana.

***24. Mheshimiwa Spika***, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya umahiri katika shughuli za madini vya Songea, Mpanda na Chunya; ujenzi wa ghala la kuhifadhia miamba choronge (Core Shade) eneo la Kizota Dodoma; ununuzi wa vifaa vya maabara na utafiti pamoja na vitendea kazi kwa ajili ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); ununuzi wa mawe mawili (2) ya Tanzanite yenye uzito mkubwa wa kilo 3.74 na 1.48; na ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Wizara awamu ya pili katika Mji wa Serikali – Mtumba. Kwa upande wa fedha za maendeleo kiwango kidogo kilichopokelewa kimetokana na wakandarasi kutowasilisha hati za madai mbalimbali ili walipwe. Hati hizo zinategemewa kuwasilishwa ndani ya nusu ya pili ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

## IV. Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

***25. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini;

kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi; kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu kwa ufanisi; na kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**(a) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa**


***26. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa, Wizara imeimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, mipaka ya nchi, viwanja vya ndege, bandari pamoja na kuanzisha na kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 93 vimeanzishwa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 mauzo katika masoko na vituo vya ununuzi yamefikia shilingi 1,676,948,980,375.3. Uwepo wa masoko na vituo hivyo umechangia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

***27. Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine za kuimarisha ukusanyaji maduhuli zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha udhibiti wa biashara haramu na utoroshaji wa madini. Katika kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali imefanikiwa kukamata madini ya aina mbalimbali yenye thamani ya shilingi 532,440,693.21 katika Mikoa ya kimadini ya Mara, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Kahama, Songwe na Singida. ***Napenda kutoa wito kwa wafanyabiashara wa madini kufanya kazi kwa uaminifu na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Sekta.***

***28. Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudi hizo kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 shilingi 509,320,355,707.01

zimekusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ikilinganishwa na shilingi 461,602,428,366.97 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2021/2022, sawa na ongezeko la asilimia 10.34.

***29. Mheshimiwa Spika***, kutokana na juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali, ukuaji wa Sekta ya Madini na mchango wake kwenye Pato la Taifa umeendelea kuimarika. Mchango wa sekta katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.4 mwaka 2017 hadi asilimia 7.2 mwaka 2021. Aidha, katika kipindi cha robo mwaka cha Julai hadi Septemba, 2022, Sekta ya Madini ilikua kwa asilimia 9.8. Aidha, katika kipindi hicho, mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa uliongezeka hadi kufikia asilimia 9.7 ikilinganishwa na asilimia 7.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021. Mwenendo huu wa mchango unatupa tumaini kwamba Sekta ya Madini itaweza kuchangia hadi asilimia 10 kwenye Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 kama ilivyo kusudiwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025.




***Kielelezo Na. 1:*** *Mwenendo wa Mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa*

***30. Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Sekta ya Madini katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni umekuwa ukiimarika. Mwaka 2022 madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,395.3 yaliuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 56 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 3,116.4 sawa na asilimia 45.9 mwaka 2021. Aidha, mapato ya kodi za ndani yatokanayo na Sekta ya Madini yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mwaka 2021/2022 mchango wa mapato ya kodi za ndani umefikia shilingi 2,091,256,445,986.27 sawa na asilimia 15.84 ya mapato yote ya kodi za ndani ikilinganishwa na mapato ya shilingi 1,081,982,345,036.43 sawa na asilimia 10.31 ya mwaka 2020/2021.

**(b) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo na Kuwawezesha Wananchi Kushiriki katika Uchumi wa Madini**

***31. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hicho, Wizara ilitoa elimu jinsi ya kushiriki katika shughuli za madini kwa wachimbaji wadogo katika Mikoa ya Geita, Tabora, Singida, Dodoma, Lindi, Mtwara, Njombe, Ruvuma, Kigoma, Mara na Iringa. Aidha, nakala 400 za Mwongozo wa Wachimbaji Wadogo kuhusu usimamizi wa mazingira, Sheria ya Madini na Kanuni zake zilisambazwa kwa wachimbaji wadogo ili wazitumie katika kuboresha shughuli zao.

***32. Mheshimiwa Spika,*** *GST* ilitoa mafunzo ya uchukuaji wa sampuli kwa ajili ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini na namna bora ya kufanya tafiti kwa wachimbaji wadogo 2,200 katika Mikoa ya Lindi na Morogoro. Aidha, utafiti maalum wa kuangalia sifa za miamba na mikanda ya madini ya dhahabu kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ulifanyika katika Wilaya ya Gairo ambapo matokeo ya awali yanaonesha uwepo wa mwendelezo wa mkondo wa dhahabu kati ya Kijiji cha Kitaita na Leshata.



***Picha Na.1:*** *Wataalamu wa GST wakitoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo katika Mkoa wa Lindi.*

***33. Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* imeendelea kusimamia shughuli za wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali hususani kupitia vituo vya mfano vilivyopo Katente, Lwamgasa na Itumbi. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Shirika limetoa huduma za mafunzo kwa wachimbaji wadogo 829 kuhusu matumizi sahihi ya kemikali na vilipuzi. Aidha, *STAMICO* kupitia vituo hivyo imekuwa ikitoa huduma bora ya uchenjuaji wa dhahabu na kwa gharama nafuu kwa wachimbaji wadogo na hivyo kuweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2.96.

***34. Mheshimiwa Spika,*** taasisi za fedha na benki nchini zimeendelea kutoa mikopo pamoja na vifaa kwa wachimbaji wadogo. Taasisi hizo ni pamoja na benki za *NMB*, *NBC, AZANIA, CRDB* na *KCB*. Hadi Machi, 2023 taasisi hizo zimekopesha jumla ya shilingi bilioni 145 kwa wachimbaji wadogo ikilinganishwa na shilingi bilioni 36 zilizokuwa zimekopeshwa hadi kufikia Machi, 2022. ***Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa taasisi za fedha kuendelea kuwaamini na kuwakopesha wachimbaji wadogo.***

## (b) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini

***35. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini kwa lengo la kuyafanya madini yawe na manufaa zaidi kwa watanzania na uchumi wa nchi kwa ujumla. Aidha, ili kuhakikisha kuwa kusudio hilo linafikiwa, Wizara inaandaa Mkakati wa kuwezesha Uongezaji Thamani Madini kwa lengo la kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotokana na madini na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje.

***36. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeandaa Mfumo wa Biashara ya Madini ya Tanzanite ili kudhibiti bei na kuongeza thamani ya madini hayo. Mfumo huo ulipitiwa na wadau mbalimbali wakiwemo uongozi wa Mkoa wa Manyara, Wilaya ya Simanjiro, Wabunge wa mkoa wa Manyara, Wabunge wa Majimbo yanayopakana na Wilaya ya Simanjiro ambayo ni Kilimanjaro, Arusha na Arumeru, Baraza la Biashara la Taifa (TBNC), wachimbaji pamoja na wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite nchini na kutoa maoni yao.

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza juhudi za uongezaji thamani madini, Wizara imeanza shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya TGC kwa kuanza ujenzi wa jengo la kisasa ambalo litatumika kutoa mafunzo ya ukataji madini, utambuzi, utengenezaji wa bidhaa za usonara na kuifanya TGC kuwa kituo cha umahiri katika uendelezaji madini ya vito nchini. Vilevile, kama sehemu ya juhudi hizo watumishi wanne (4) walifanya ziara ya mafunzo katika nchi za India na Thailand kwa lengo la kujifunza na kuongeza ujuzi kuhusu uongezaji thamani madini, uendeshaji wa viwanda vya kuchakata madini, utoaji wa huduma za maabara za madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Aidha, watumishi watatu (3) wanahudhuria mafunzo ya uongezaji thamani madini ndani ya nchi na

watumishi sita (6) wamehudhuria mafunzo hayo katika nchi za Thailand, China na India.



***Picha Na.2:*** *Wanafunzi wa Kituo cha Jemolojia Tanzania wakiwa kwenye mafunzo ya uongezaji thamani madini ya vito.*

***38. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kwa kuanzisha leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini (Primary Processing Licence) ili kurasimisha shughuli za uchenjuaji zinazofanyika katika mialo na makarasha.

**(c) Kuhamasisha Biashara na Uwekezaji katika Sekta ya Madini**

***39. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini ili kuongeza mchango wa Sekta katika Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Tume ya Madini imetoa leseni kubwa ya uchimbaji wa madini ya kinywe kwa *Kampuni ya Faru Graphite Corporation Limited* (FGCL) pamoja na leseni ya uchimbaji wa kati wa madini ya Tanzanite kwa kampuni ya *Franone Mining Limited* kwa ajili ya kuendeleza Kitalu "C" Mirerani. Aidha, kutokana na uhamasishaji ambao umefanyika katika Sekta ya Madini, jumla ya leseni 6,381 zilitolewa katika shughuli za utafutaji, uchimbaji, biashara na uongezaji thamani madini kati ya leseni 6,116 zilizopangwa kutolewa katika kipindi husika.

***40. Mheshimiwa Spika***, thamani ya uwekezaji katika miradi ya uchimbaji wa madini ya kinywe na uchimbaji wa kati wa madini ya Tanzanite inatarajiwa kuwa kiasi cha takriban dola za Marekani milioni 538.925 sawa na shilingi trilioni 1.26. Uwekezaji huu utaongeza ajira, kodi, tozo mbalimbali, manufaa yatokanayo na uwajibikaji wa kampuni za madini kwa jamii (CSR) na ushirikishwaji wa watanzania katika uuzaji wa bidhaa na utoaji huduma katika shughuli za madini (Local Content). Aidha, takriban ajira 14,742 zimezalishwa kwenye migodi mikubwa kwa mwaka 2021. Kati ya ajira hizo 14,308 ni za watanzania ambazo ni asilimia 97 na ajira 434 sawa na asilimia 3 ni za wageni. Ajira hizi zitaendelea kuongezeka kutokana na matakwa ya leseni na Kanuni za Ushirikishwaji wa watanzania.

***41. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imesaini mikataba ya uchimbaji mkubwa na wa kati wa madini muhimu na madini mkakati na kampuni za Evolution Energy Minerals Limited, EcoGraf Limited na Peak Rare Earth Limited zote za Australia tarehe 17 Aprili, 2023. Mikataba hiyo ina thamani ya dola za Marekani milioni 667 ikihusisha uchimbaji wa madini ya kinywe katika eneo la Chilalo Wilaya ya Ruangwa na Epanko Wilaya ya Ulanga pamoja na madini adimu (rare earth elements) katika eneo la Ngualla Wilaya ya Songwe.

***42. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa makubaliano hayo, miradi hiyo itasimamiwa na Kampuni za ubia baina ya Serikali na Wawekezaji za Kudu Graphite Limited kwa mradi wa Chilalo, Duma TanzGraphite kwa mradi wa Epanko na Mamba Minerals Corporation kwa mradi wa Ngualla. Aidha, katika uwekezaji huo Serikali itakuwa na umiliki wa hisa asilimia 16 zisizoshuka thamani. Kupitia miradi hiyo, Serikali itapata manufaa mbalimbali ikiwemo kodi mbalimbali, mrabaha, ada ya ukaguzi na tozo za huduma *(service levy)*, ajira, maendeleo ya miundombinu, uhaulishwaji

wa teknolojia mbalimbali, huduma kwa jamii na ununuzi wa bidhaa na huduma zinazopatikana hapa nchini.

***43. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na jitihada za kutangaza fursa za uwekezaji na kutoa elimu kwa umma kupitia ziara mbalimbali za viongozi; kwenye vyombo vya habari; majukwaa ya ushirikishwaji wa watanzania; mikutano ya kitaifa; kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliandaa na kushiriki mikutano mbalimbali ikiwemo: mkutano wa nchi za Afrika zinazozalisha Almasi (ADPA) uliofanyika Jijini Arusha na Victoria Falls nchini Zimbabwe; mkutano wa kupambana na vitendo vya utoroshaji wa madini katika nchi za Maziwa Makuu (ICGLR) uliofanyika nchini Zambia; kongamano la 91 la Jumuiya ya Umoja wa Watafutaji na Wawekezaji wa Rasilimali za Madini (PDAC) nchini Canada; mkutano wa Uchumi wa Bahari uliofanyika nchini Jamaica; kongamano la ushirikiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Afrika Kusini; na mkutano kuhusu uwekezaji katika madini mkakati uliofanyika Riyadh - Saudi Arabia. Mikutano hiyo imewezesha kubadilishana uzoefu na kuimarisha ulinzi wa rasilimali madini.



***Picha Na. 3:*** *Katibu Mkuu Wizara ya Madini Bw. Kheri A. Mahimbali akishiriki katika mkutano wa nchi za Afrika zinazozalisha Almasi (ADPA) uliofanyika nchini Zimbabwe.*

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kushiriki maonesho ndani na nje ya nchi ikiwemo maonesho ya 5 ya teknolojia ya Madini yaliyofanyika Mkoani Geita, Maonesho ya kwanza ya teknolojia ya Madini yaliyofanyika Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya na Maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara yaliyofanyika *Bangkok* nchini *Thailand* (Thailand Gem and Jewelry Fair). Maonesho ya ndani yalihusisha washiriki zaidi ya 600 wakiwemo wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa, pamoja na taasisi za kifedha.

***44. Mheshimiwa Spika,*** katika maonesho ya ndani ya nchi pia, Wizara iliendesha kliniki ya mambo ya Madini iliyosikiliza migogoro mbalimbali na kuitolea ufafanuzi. Kupitia maonesho na mikutano ya nje, tumeendelea kujifunza na kuongeza ujuzi kutoka nchi nyingine kuhusu masuala mbalimbali ya namna ya kuboresha usimamizi katika Sekta ya Madini, teknolojia za kisasa na kujenga mahusiano ya kidiplomasia ambayo ni msingi wa ustawi wa biashara na uwekezaji baina ya nchi yetu na nchi nyingine.




***Picha Na. 4:*** *Maonesho ya kwanza ya teknolojia ya Madini Mkoa wa Mbeya yaliyofanyika katika Viwanja vya Sinjiriri Wilaya ya Chunya.*

### *(d)* Kusimamia Mfumo wa Ukaguzi wa Shughuli za Migodi

***46. Mheshimiwa Spika,*** shughuli za ukaguzi wa migodi na mazingira zinahusisha ukaguzi wa usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti katika shughuli za uchimbaji wa madini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 migodi mikubwa (6) ya Williamson Diamond, Buckreef, North Mara, Geita Gold, Bulyanhulu, na Buzwagi; migodi 66 ya kati na migodi midogo 19,528 ilikaguliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

***47. Mheshimiwa Spika,*** kaguzi hizo zilifanyika katika Mikoa ya Kimadini ya Dar es Salaam, Pwani, Mara, Kahama, Njombe, Shinyanga, Geita, Rukwa, Lindi, Ruvuma, Mtwara, Tanga, Mirerani, Manyara, Mwanza, Singida, Kigoma, Dodoma, Mbeya, Chunya, Morogoro, Mahenge, Songwe na Katavi.

***48. Mheshimiwa Spika,*** katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo kutokutekelezwa kwa maelekezo ya Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi, utunzaji usiofaa wa taka ngumu ikiwemo kuchanganya taka ngumu na mabaki ya baruti, kutowasilishwa kwa taarifa ya usanifu wa eneo la kuhifadhia miambataka, kutofukiwa kwa mashimo na kutokutumia vifaa kinga na matumizi yasiyo sahihi ya vilipuzi. Wahusika walielekezwa kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake, pamoja na Sheria ya Utunzaji wa Mazingira ya Mwaka 2004.



***Picha Na. 5:*** *Wataalamu kutoka Tume ya Madini wakikagua mgodi wa dhahabu wa North Mara.*

**(f) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ili Ziweze Kutekeleza Majukumu kwa Ufanisi**

***49. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zake zinatekeleza majukumu yao kwa ufanisi ili kusaidia Sekta kuendelea kuongeza mchango katika Pato la Taifa. Katika kuzijengea uwezo, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) imewezeshwa kununua vitendea kazi ikiwemo basi kwa ajili ya watumishi, vifaa vya jiosayansi na maabara pamoja na kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhifadhia sampuli za miamba choronge linalojengwa katika eneo la Kizota – Dodoma.

***50. Mheshimiwa Spika,*** STAMICO imewezeshwa kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo na mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa mkaa mbadala (Coal briquette). Aidha, TGC imewezeshwa kununua magari manne (4) kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Kituo na fedha kwa ajili ya mafunzo ya kuwaongezea ujuzi watumishi. Vilevile, Tume ya Madini inaendelea na ujenzi wa jengo la ofisi makao makuu.

**(g) Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

***51. Mheshimiwa Spika,*** rasilimaliwatu na mazingira ya kazi ni muhimu kuimarishwa wakati wote ili kufikia malengo yaliyowekwa. Wizara imefanya yafuatayo katika kutekeleza kipaumbele hiki: kuajiri watumishi wapya 30 na kujaza nafasi zilizo wazi 26 kwa utaratibu wa uhamisho kwa watumishi wenye sifa na ujuzi unaostahili; kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi ya makao makuu ya Wizara; kuwawezesha watumishi 114 kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 100 kupata mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi; kufuatilia na kuhakikisha kuwa maslahi na stahiki za watumishi zinapatikana ikiwemo upandishaji vyeo kwa wakati.

**D. UTEKELEZAJI WA MAENEO MENGINE**

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya utekelezaji kwenye maeneo mengine kama ifuatavyo;

**(i) Ufuatiliaji na Usimamizi wa Shughuli za Baruti**

***53. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha shughuli za biashara na uhifadhi wa baruti zinafuata matakwa ya Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963, Wizara imefanya ukaguzi wa maghala ya kuhifadhi baruti 26 katika mkoa wa Geita, 20 katika mkoa wa Mbeya, 14 katika mkoa wa Songwe, 9 katika mkoa wa Mwanza, 7 katika mkoa wa Tanga na 3 katika mkoa wa Pwani. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi katika kiwanda cha kutengeneza baruti cha kampuni ya *Mbogo Mining and General supply* katika kijiji cha Ihayabuyaga Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza kuhakikisha shughuli za utengenezaji baruti zinazingatia Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963. Baadhi ya maghala yaliyobainika kuwa na mapungufu kama ukosefu wa vipima joto, *fire extinguisher*, mpangilio hatarishi wa vilipuzi na maghala kuzungukwa na nyasi.

Wahusika walipewa siku 14 za kurekebisha mapungufu hayo na walitekeleza maelekezo waliyopewa.

***54. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilifanya ukaguzi wa maghala ya kuhifadhia baruti ya kampuni za *Tanga Cement* iliyooomba maghala yao kuvunjwa. Kupitia ukaguzi huo kibali cha kubomoa maghala ya kuhifadhi baruti kilitolewa kwa mhusika baada ya kuona maghala yaliyoainishwa na kampuni hiyo yanastahili kuvunjwa kwa mujibu wa Sheria ya Baruti ya Mwaka 1963.

***55. Mheshimiwa Spika,*** Ukaguzi mwingine katika maeneo kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi baruti ulifanyika kwa kampuni ya Siontinto katika kijiji cha Mitunduliani Wilaya ya Bagamoyo Mkoani Pwani. Kupitia ukaguzi huo kibali kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhi baruti kilitolewa kwa mhusika baada ya kuona eneo lililopendekezwa kwa ajili ya ujenzi linafaa kwa mujibu wa Sheria ya Baruti Sura, 56. Aidha, vibali na leseni za baruti vilivyotolewa vimeipatia Serikali jumla ya shilingi 376,528,000.

**(ii) Ununuzi wa Madini ya Tanzanite**

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 mawe mawili (2) ya madini ya Tanzanite yenye uzito mkubwa, moja likiwa na kilo 3.74 na lingine lenye kilo 1.48 yenye jumla ya thamani ya shilingi 2,245,571,543.46 yalinunuliwa na Serikali na kuhifadhiwa Benki Kuu ya Tanzania.



***Picha Na. 6:*** *Naibu Waziri wa Madini Dkt. Steven Kiruswa akiwa ameshika vipande viwili vya madini ya Tanzanite yaliyopatikana kutoka mgodi wa Anselm Kawishe uliopo Mirerani Wilaya ya Simanjiro.*

## (iii) Marekebisho ya Sheria na Uandaaji wa Kanuni

***57. Mheshimiwa Spika,*** ili kupanua wigo wa shughuli za madini nchini, Serikali imefanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya Mwaka 2022. Marekebisho hayo ni pamoja na kuanzisha leseni ndogo ya uchenjuaji wa madini (Primary Processing Licence); na kumpa Waziri mamlaka ya kurejesha serikalini maeneo ya leseni za madini zilizofikia ukomo kwa mujibu wa Sheria ili ikionekana yanafaa yaweze kutengwa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti na GST. Marekebisho hayo ya Sheria yamewezesha kurasimisha shughuli za uchenjuaji wa madini na kuiwezesha Serikali kujua makadirio ya mashapo kupitia tafiti za *GST* na kufanya majadiliano yenye tija na kampuni za madini ambazo Serikali inashiriki kupitia ubia.

***58. Mheshimiwa Spika,*** marekebisho ya Sheria pia yameipa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini (GST) mamlaka ya kisheria ya kufanya utafutaji wa kina wa kimkakati wa madini; kuweka muda wa uhuishaji wa leseni za utafutaji wa madini (Prospecting Licence) wa kipindi cha pili; na kuweka muda wa kuanza shughuli za uchimbaji baada ya kupewa leseni kwa wamiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji (Primary Mining Licence).

***59. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetunga Kanuni za Madini (Ufifilishaji wa Makosa) za Mwaka 2022 (compounding of offences) na kutagazwa katika Tangazo la Serikali Na. 549 la tarehe 2/9/2022. Kanuni hizi zinaweka masharti mbalimbali ikiwemo utaratibu wa kufifilisha makosa, ulipaji wa fedha kwa kosa lililofifilishwa, utaratibu wa kukazia amri ya ufifilishaji iliyotolewa na Tume ya Madini, utunzaji wa fedha zinazotokana na ufifilishaji wa makosa na utoaji wa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Aidha, ufifilishaji wa makosa ya jinai chini ya Sheria ya madini unamtaka mtu aliyetenda kosa kukiri kutenda kosa la jinai na hivyo kuwa na hiari ya kulipa kiasi kilichofifilishwa badala ya kushtakiwa mahakamani.

***60. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imetunga Kanuni mpya za Madini (Ushiriki wa Serikali) za Mwaka 2022 na kutangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 574 la tarehe 23/9/2022. Kanuni hizi pamoja na masuala mengine zinaweka masharti ya leseni zinazorejeshwa Serikalini, masharti ya umiliki wa hisa za serikali zisizofifishwa (non dilutable shares) na haki zake, misingi ya kuingia ubia kati ya Serikali na Kampuni za Madini, usimamizi wa kampuni za ubia na models za mkataba wa msingi wa ubia na Katiba ya Kampuni ya wanahisa katika ubia.

### (iv) Ushirikishwaji wa Watanzania na Wajibu wa Kampuni kwa Jamii katika Sekta ya Madini

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara kupitia Tume ya Madini ilipokea na kupitia jumla ya mipango 510 ya ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini ambapo mipango 505 iliidhinishwa. Mipango mitano (5) haikukidhi vigezo vya kuidhinishwa na hivyo wahusika walipewa muda wa kurekebisha. Aidha, Tume ya Madini ilipokea jumla ya maombi 513 kutoka kwa wamiliki wa leseni na wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya idhini ya kuendelea na hatua mbalimbali za ununuzi wa huduma na bidhaa.

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utekelezaji wa Kanuni za ushirikishwaji wa watanzania katika Sekta ya Madini na kuhakikisha watanzania wananufaika na uwepo wa migodi, jumla ya kampuni tatu (3) za kitanzania zimeonesha nia ya kujenga viwanda vya kutengeneza vifaa vinavyotumika migodini. Vifaa hivyo ni *wiremesh*, *coretrays* na *bolts* zinazotumika migodini ambazo kwa sasa zinaagizwa kutoka nje ya nchi. ***Nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa watanzania wenye uwezo wa kuanzisha viwanda hapa nchini vya vifaa vinavyotumika migodini kuchangamkia fursa hii.***

***63. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya madini unaimarika, Tume ya Madini iliandaa jukwaa la Ushirikishwaji wa Watanzania ambalo liliambatana na Maonesho ya bidhaa na huduma kutoka kwa wamiliki wa leseni za Madini na Watoa huduma migodini (contractors) Jijini Arusha ambapo zaidi ya washiriki 560 walishiriki katika Jukwaa hilo. Kaulimbiu ilikuwa "*Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini kwa kufungamanisha na Sekta Nyingine kwa uchumi imara wa Nchi*". Kauli mbiu hii inaenda sambamba na utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009. Aidha, Tume ya Madini pamoja na mambo

mengine itahakikisha bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini zinapewa kipaumbele migodini kwa mujibu wa Kanuni za Ushirikishwaji wa Watanzania.

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tunaendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia na kutimiza matakwa ya Kanuni za ushirikishwaji wa Watanzania, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Madini imeunda Mfumo wa uendeshaji na Usimamizi wa Ushirikishwaji wa Watanzania katika Sekta ya Madini (LCCR-MIS). Mfumo huu ndo utakaotumika katika shughuli zote za ushirikishwaji wa watanzania (Local content) na utarahisisha shughuli zote za ununuzi na uwasilishaji wa mipango ya ushirikishwaji wa Watanzania.

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kampuni za madini zinatekeleza wajibu wake kwa jamii (CSR), Wizara imeandaa Rasimu ya Kanuni za Madini (Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii) za Mwaka 2023 na kuiwasilisha katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Aidha, Rasimu hiyo imezingatia maoni ya wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini.

**(v) Masuala Mtambuka**

***66. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Masuala Mtambuka, Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojitokeza kwa kuwapatia fedha taslimu kwa ajili ya huduma ya lishe bora na vifaa kinga ili kupambana na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI. Aidha, mafunzo yameendelea kutolewa kuhusu kudhibiti Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) na Kifua Kikuu kwa watumishi pamoja na kuhamasisha watumishi kushiriki katika michezo na kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha afya na kuepuka uwezekano wa kupata Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY). Aidha, Wizara imeendelea kushawishi watumishi kupima afya

kwa hiari. Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Wizara dhidi ya Rushwa.

## E. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

***67. Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jukumu la kusimamia taasisi tano (5), ambazo ni Tume ya Madini; Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) na Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC).

### (a) Tume ya Madini

***68. Mheshimiwa Spika***, Tume ya Madini inasimamia na kudhibiti shughuli zote zinazohusiana na Sekta ya Madini zikiwemo utafutaji, uchimbaji, ukaguzi wa migodi na usimamizi wa baruti, uongezaji thamani na biashara ya madini. Taasisi imetekeleza kazi zake kama ifuatavyo: -

### (i) Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini

***69. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume ya Madini imetoa jumla ya leseni 6,381 kati ya leseni 6,116 zilizopangwa kutolewa katika kipindi husika. Leseni zilizotolewa ni kama ifuatavyo: Leseni ya Uchimbaji Mkubwa wa Madini (SML) – 01; Leseni za Uchimbaji wa Kati wa Madini (MLs)- 08; Leseni za Utafutaji wa Madini (PLs) -218; Leseni za Uchimbaji Mdogo (PMLs) – 3,865; Leseni kubwa za biashara (DLs) – 618; Leseni ndogo za biashara (BLs) – 1,649; na Leseni za Uchenjuaji wa Madini (PCLs) – 25.

***70. Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, katika kipindi rejewa, leseni 19 za utafutaji wa madini, leseni 18 za uchimbaji wa kati wa

madini zilipewa hati za makosa kutokana na kutozingatia matakwa ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Aidha, leseni 12 za utafutaji madini na leseni 13 za uchimbaji wa kati zilifutwa baada ya kushindwa kurekebisha makosa.

**(ii) Uendelezaji na Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA**

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za utoaji na usimamizi wa leseni, Tume imeendelea kuimarisha mfumo wake wa usimamizi na utoaji wa leseni za madini kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA*)* ili kuendana na kasi ya uchakataji wa maombi ya leseni yanayopokelewa kila siku.

**(iii) Ukaguzi na Biashara ya Madini**

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika ukaguzi na biashara ya madini shughuli zifuatazo zilitekelezwa: kudhibiti utoroshaji wa madini; kusimamia shughuli za uthaminishaji madini nchini; kushiriki minada ya madini; kuandaa bei elekezi; usimamizi wa shughuli za maabara; na kufanya ukaguzi wa fedha, kodi na Ushirikishwaji wa Watanzania (Local Content) katika Sekta ya Madini.

***73. Mheshimiwa Spika,*** shughuli za usimamizi wa biashara ya Madini kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 zilifanyika kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali ambapo Tume ya Madini ilikusanya jumla ya shilingi 117,616,806,020.64 kutokana na mrabaha na ada ya ukaguzi kwenye masoko ya madini 42 na vituo vya ununuzi wa madini 93. Kati ya makusanyo hayo, shilingi 101,405,400,832.03 zilitokana na mrabaha; na shilingi 16,211,405,188.61 zilitokana na ada ya ukaguzi wa madini.

**(iv) Shughuli za Ukaguzi wa Migodi, Mazingira na Usimamizi wa Baruti**

***74. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 shughuli za ukaguzi migodi na mazingira zilihusisha ukaguzi uliolenga usalama, afya, mazingira na matumizi salama ya baruti katika shughuli za uchimbaji wa madini kama ifuatavyo:

**Ukaguzi katika Migodi Mikubwa**

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, migodi Mikubwa Mitano (5) ya *Williamson Diamond*; *Buckreef*; *North Mara, Geita Gold* na Buzwagi ilikaguliwa. Mapungufu yaliyobainika ni kupasuka kwa sehemu ya bomba la maji kutoka shimo la Gokona kwenda kwenye bwawa la kuhifadhia maji katika Mgodi wa North Mara; kutowasilisha taarifa ya usanifu wa eneo la kuhifadhia miambataka (*Waste Rock Dump* - WRD) na mpango wa uchimbaji katika Mgodi wa Buckreef*;* kutokuwepo kwa taarifa ya usanifu ya ufungaji wa bwawa la zamani la topesumu katika Mgodi wa Geita; uwepo wa mmomonyoko wa udongo katika baadhi ya maeneo ya kuhifadhia miambataka hali inayoweza kusababisha ukuta kutokuwa imara katika Mgodi wa Buzwagi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na migodi kuelekezwa kurekebisha mapungufu yote yaliyobainika kwa kufuata Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

**Ukaguzi katika Migodi ya Kati**

***76. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, jumla ya migodi 66 ya uchimbaji wa kati wa madini ilikaguliwa katika Mikoa ya kimadini ya Dar es Salaam, Pwani, Mara, Kahama, Njombe, Shinyanga, Geita, Rukwa, Lindi, Ruvuma, Mtwara, Tanga, Mirerani, Manyara, Mwanza, Singida, Kigoma, Dodoma, Mbeya,

Chunya, Morogoro, Mahenge, Songwe na Katavi. Katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo kutokutekelezwa kwa maelekezo ya Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi, utunzaji usiofaa wa taka ngumu na kutowasilishwa kwa taarifa ya usanifu wa eneo la kuhifadhia miambataka. Wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza kwa kufuata Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na marekebisho yake pamoja na kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

**Ukaguzi katika Migodi Midogo**

***77. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, ukaguzi ulifanyika kwenye migodi 19,528 katika Mikoa ya kimadini ya Morogoro, Tabora, Arusha, Kahama, Mwanza, Tanga, Manyara, Iringa, Njombe, Mbogwe, Shinyanga, Dodoma, Kigoma, Kagera, Chunya, Geita, Mara, Mbeya, Rukwa, Lindi, Ruvuma, Mtwara, Songwe, Pwani, Dar es Salaam na Katavi. Katika kaguzi hizo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwemo kutofukiwa kwa mashimo na kutotumia kwa usahihi vifaa kinga na vilipuzi. Wahusika walielekezwa kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainika ili kuwa na uchimbaji wenye tija.



***Picha Na. 7****: Waziri wa Madini Dkt. Doto Biteko (MB.) akiwa kwenye ukaguzi wa mgodi wa uchimbaji mdogo wa dhahabu Chunya.*

**Ukaguzi wa Maghala, Stoo na Masanduku ya Kuhifadhia Baruti**

***78. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, jumla ya maghala na stoo za kuhifadhia Baruti 243 yalikaguliwa. Kaguzi hizo zilifanyika katika Mikoa ya kimadini ya Shinyanga, Geita, Pwani, Dar es Salaam, Katavi, Rukwa, Iringa, Mtwara, Lindi, Mwanza, Singida, Mirerani, Kigoma na Morogoro. Katika kaguzi hizo masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo mpangilio usiofaa wa utunzaji baruti, wamiliki kutokuwa na leseni za uendeshaji wa maghala na kutokulipwa kwa ada ya mwaka ya leseni. Wahusika walielekezwa kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainika ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza.

**Ukaguzi wa Mitambo ya Kuchenjulia Dhahabu (Vat Leaching, CIP na Elution)**

***79. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume ya Madini ilifanya ukaguzi wa mitambo ya kuchenjulia dhahabu kama ifuatavyo: 646 ya *Vat leaching,* 10 ya *CIP* na 97 ya *elution* ilikaguliwa katika Mikoa ya kimadini ya Dodoma, Geita, Katavi, Lindi, Mara, Mbogwe, Mtwara, Mwanza, Iringa, Chunya, Shinyanga, Tanga, Songwe na Ruvuma. Aidha, kaguzi hizo zilibaini maeneo yenye udongo wa mabaki ya dhahabu (tailings), kutowekewa mifereji ya kuyazunguka kwa lengo la kuzuia utiririshaji wa maji taka kwenda kwenye mazingira na baadhi ya *elution plants* kutokuwa na mfumo wa kuchuja hewa wakati wa uoshaji. Wahusika walielekezwa kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

***80. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 viwanda viwili (2) vya kusafisha dhahabu (refineries) vya *African Eyes Company Ltd* ya Geita na *Banjul Ltd* ya Dar es Salaam vilikaguliwa kwa lengo la kujiridhisha kama viwanda hivyo vimekidhi vigezo vya kuanza uzalishaji, ikiwemo

ukamilishaji wa ujenzi na usimikaji wa mitambo. Ukaguzi huo ulibaini kuwa viwanda hivyo vimekidhi vigezo na vinajiandaa kwa uzalishaji.

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi rejewa, jumla ya mabwawa ya topesumu (TSF) 18 yalikaguliwa kwa lengo la kutoa vibali vya ujenzi au kutumia mabwawa hayo. Ukaguzi huo ulilenga kuangalia maeneo yanayopendekezwa kwa ajili ya ujenzi kama yanafaa. Katika ukaguzi huo *TSF* 10 zilikidhi vigezo na kupewa vibali na *TSF* nane (8) ambazo ni Maweni *Gold Mines Limited, GGM*, *Xinyuan Tanzania Co. Ltd A.S, Lulila – PCL, Waja General C. Ltd* - Mbogwe, *Waja General C. Ltd* Mwakitolyo, *Bukreef Gold Mine* na *Mawe Meru Gold Limited* - Mwakitolyo hazikukidhi vigezo, hivyo wahusika walielekezwa kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa.

***82. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini ilifanya ukaguzi maalumu wa mabwawa 63 ya kuhifadhia topesumu yaliyopo katika Mikoa mbalimbali ya kimadini hapa nchini kwa lengo la kujiridhisha na usalama wake. Ukaguzi huo ulibaini kuwa mabwawa hayo yapo katika hali inayostahimili matumizi kwa kuzingatia miongozo ya uendeshaji wake.

**Kupitia Taarifa za Mipango ya Ufungaji Migodi (MCP)**

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika jumla ya Mipango ya Ufungaji Migodi tisa (9) ilijadiliwa na Kamati ya Kitaifa ya Ufungaji Migodi (NMCC). Kati ya Mipango hiyo, Mipango ya migodi sita (6) iliidhinishwa, ambayo ni *Wiliamson Diamond Limited, Mbeya Cement Company Limited*, *North Mara Gold Mine, Buckreef Gold Company Limited*, *STAMIGOLD Biharamulo Mine* na *GGML Old TSF*. Mipango ya migodi mitatu (3), ambayo ni *Minjingu Mines and Fertilizers, CATA Mining Company Liimited na MMG Gold Mine* haikuidhinishwa kutokana na mapungufu yaliyobainika yanayohitaji maboresho.

## (v) Utoaji wa Huduma za Maabara

***84. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya sampuli 6,047 za wateja mbalimbali zilipokelewa na kuchunguzwa kupitia maabara ya Tume ya Madini. Kati ya sampuli hizo, sampuli 1,679 zilitoka migodi mikubwa ya dhahabu kwa ajili ya kuwezesha Serikali kukokotoa mapato stahiki na sampuli 4,351 zilitoka kwa wateja binafsi ili kuwasaidia kufanya maamuzi sahihi katika uzalishaji na biashara ya madini. Huduma iliyotolewa iliwezesha Serikali kupata makusanyo ya kiasi cha shilingi 336,136,000.00.



***Picha Na. 8:*** *Mtaalamu wa Maabara ya Tume ya Madini akiwa katika shughuli ya upimaji wa sampuli za madini.*

## (v) Utambuzi na Uthaminishaji wa Madini Yaliyoingizwa Nchini na Yaliyosafirishwa Nje ya Nchi

***85. Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha na kusimamia biashara ya madini nchini, Wizara kupitia Tume ya Madini ilitoa jumla ya vibali 90 vya uingizaji madini nchini yenye thamani ya dola za Marekani 12,732,417.06 kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023.

***86. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022, jumla ya vibali 10,318 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,240.35 vya kuuza madini nje ya nchi vilitolewa ikilinganishwa na vibali 5,526 vilivyotolewa mwaka 2021 vyenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,046.23. Ongezeko la vibali hivyo kwa kiasi kikubwa limetokana na ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe nje ya nchi.

**(vi) Mchango wa Sekta ya Madini Katika Kuliingizia Taifa Fedha za Kigeni**

***87. Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Sekta ya Madini katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni umekuwa ukiimarika mwaka hadi mwaka. Mwaka 2022 madini yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3,395.3 yaliuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 56 ya mauzo yote ya bidhaa nje ya nchi ikilinganishwa na mauzo ya dola za Marekani milioni 3,116.4 sawa na asilimia 45.9 mwaka 2021.

**(vii) Ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Kodi**

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume ya Madini imefanya ukaguzi wa kampuni 12. Kati ya kampuni hizo, tatu (3) ni za viwanda vya Saruji na tisa (9) ni za miradi ya barabara. Kaguzi hizo zimewezesha kuibua hoja mbalimbali zinazohusiana na kutolipwa kwa malipo mbalimbali ya Serikali ya shilingi 5,300,640,044.28. Aidha, shilingi 261,079,078.13 zimekusanywa kutokana na ukaguzi huo hadi kufikia Machi, 2023. Tume ya Madini inaendelea kufuatilia malipo yaliyobaki ili yalipwe.

**(viii) Utoaji wa Elimu kwa Wadau wa Sekta ya Madini**

***89. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tunaepusha masuala ya migogoro inayoweza kutokana na shughuli za madini nchini,

Tume ya Madini imeendelea kutoa elimu ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini. Aidha, mafunzo maalum yametolewa kwa wachimbaji wadogo wapatao 500 katika mikoa ya Dodoma, Singida na Mara. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uelewa kuhusu Sekta ya Madini.

***90. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua Ofisi mpya katika Mkoa wa kimadini wa Mahenge hivyo kuwa na jumla ya Ofisi 30 za Maafisa Madini Wakazi (RMOs) zilizopo nchi nzima. Pia, Tume ya Madini ina Ofisi 13 za Maafisa Migodi Wakazi (MROs). ***Nitoe wito kwa Wadau wa Sekta ya Madini nchini kuzitumia ipasavyo ofisi hizo ili kupata huduma mbalimbali ili kuwa na uchimbaji salama na wenye tija.***



***Picha Na. 9:*** *Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Doto Biteko (Mb.) akizindua Ofisi mpya ya Afisa Madini Mkazi Mahenge.*

## *(b)* Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

***91. Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Madini la Taifa linawekeza katika miradi ya kimkakati kwa niaba ya Serikali na kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Katika kipindi cha Julai,

2022 hadi Machi, 2023 Shirika limetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

**(i) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

***92. Mheshimiwa Spika,*** Shirika linamiliki na kusimamia miradi mitano (5) ambayo ni: mradi wa makaa ya mawe wa Kabulo-Kiwira; mradi wa makaa ya kupikia (Coal Briquettes); mradi wa kuuza kemikali na vilipuzi; mradi wa huduma za uchorongaji; na mradi wa usimamizi wa vituo vya mfano vya wachimbaji wadogo.

**Mradi wa Makaa ya Mawe wa Kabulo - Kiwira**

***93. Mheshimiwa Spika***, kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 shughuli zifuatazo zimefanyika katika mradi wa Kabulo - Kiwira: uchimbaji wa tani 88,077.82 ambapo tani 40,909.99 za makaa ya mawe yenye thamani ya shilingi 4,520,488,032.86 yaliuzwa ndani na nje ya nchi. Tani 47,167.83 zilizobaki zinatarajiwa kuuzwa nje ya nchi. Shirika pia limeanza uchimbaji wa makaa ya mawe katika kitalu E kilichopo eneo la Kabulo.



***Picha Na 10:** Uchimbaji wa makaa ya Mawe katika eneo la Kabulo- Kiwira.*

***94. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha miundombinu ya kusafirishia makaa ya mawe Shirika limekamilisha kujenga kituo cha kuhifadhi makaa (coal storage facility) katika bandari ya

Mtwara na kufanikiwa kupata Cheti cha Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA Certificate) kinachoruhusu kutekelezwa kwa mradi wa utunzaji na usafirishaji wa makaa ya mawe.

**Mradi wa Makaa ya Kupikia (Coal Briquettes)**

***95. Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea na uzalishaji wa majaribio wa mkaa mbadala kutokana na makaa ya mawe kwa kutumia mtambo wenye uwezo wa kuzalisha tani mbili kwa saa na kufanikiwa kupata cheti cha ubora wa bidhaa kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambapo bidhaa hiyo inatambulika kwa jina la *Rafiki Briquettes*. Aidha, Shirika limeagiza mitambo minne (4) ya uzalishaji yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa kila mmoja. Mitambo miwili imefika nchini na maandalizi ya kusimika mitambo hiyo yanaendelea katika eneo la Kiwira Songwe na mkoa wa Pwani.



***Picha Na. 11:*** *Mtambo wa kuzalisha mkaa mbadala utokanao na makaa ya mawe.*

***96. Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha jamii inashirikishwa kwenye matumizi ya mkaa mbadala wa *Rafiki Briquettes*, Shirika limetembelea na kuelimisha Taasisi zinazotumia majiko ya kuni na mkaa zikiwemo shule, vyuo na magereza ili kuanza kutumia nishati safi ya *Rafiki Briquettes*. Aidha, Shirika linaendelea kuutangaza mkaa huu katika maeneo tofauti ndani na nje ya nchi ili kupata masoko zaidi.

**Mradi wa Kuuza Kemikali, Baruti na Vilipuzi**

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika linatekeleza miradi ya kuuza kemikali, baruti na vilipuzi kwa wachimbaji wadogo kwenye vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi na katika mgodi wa *STAMIGOLD*. Aidha, mpango wa kuanza kuuza kemikali na vilipuzi katika migodi mingine unaendelea ili kusogeza huduma hiyo karibu na wachimbaji wadogo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika limepata mapato ya shilingi 4,866,795,500.00 kutokana na mauzo ya kemikali na vilipuzi. Pia, mradi huu umesaidia kuondoa uhaba wa kemikali zinazotumika kwenye shughuli za madini hapa nchini na hivyo kusaidia kupunguza mfumuko wa bei hususan kwa wachimbaji wadogo.

**Usimamizi wa Vituo vya Mfano**

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kusimamia na kuimarisha huduma katika vituo vya mfano ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya gramu 30,475.72 za dhahabu zenye thamani ya shilingi 3,600,089,338.50 zilizalishwa na fedha kiasi cha shilingi 279,659,530.20 zililipwa Serikalini. Aidha, taratibu za kuongeza uwezo wa vituo vya mfano zimeanza baada ya Mshauri Elekezi kutembelea kituo cha Lwamgasa ambapo ameainisha mahitaji na gharama ili upanuzi wa mtambo uanze ndani ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Kampuni Tanzu ya STAMIGOLD Biharamulo**

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, *STAMIGOLD* ni mgodi unaomilikiwa na Serikali kupitia *STAMICO* inayomiliki hisa asilimia 99 na Ofisi ya Msajili wa Hazina inamiliki hisa asilimia moja (1). Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 mgodi umezalisha wakia 8,740.42 za dhahabu na wakia 1,770.65 za madini ya fedha zote zikiwa na thamani ya shilingi 36,365,275,161.79 ambapo Serikali

imepata shilingi 2,654,665,072.86 kutokana na mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma. Aidha, kazi ya kuunganisha mgodi katika gridi ya Taifa ipo katika hatua za mwisho na zinafanywa na TANESCO kupitia kampuni tanzu inayoitwa ETDCO.

**(ii) Utekelezaji wa Miradi ya Ubia**

**Kiwanda cha Kusafisha Dhahabu Mwanza**

***100. Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda kinaendelea na taratibu za kupata Ithibati (ISO) ili dhahabu itakayosafishwa kwa wateja wa ndani na nje ya nchi itambuliwe kimataifa. Taratibu hizo zinahusisha vigezo sita na kwa sasa kiwanda kimetekeleza vigezo vitatu ambavyo ni; mafunzo na tathmini kwa watumishi wa idara zote; kuainisha mapungufu ambapo wakaguzi kutoka *Bureau Veritas* wamekamilisha kazi hiyo; na kukamilisha maandalizi ya nyaraka zote na taratibu za kufanyia kazi.

***101. Mheshimiwa Spika,*** vigezo vinavyoendelea kufanyiwa kazi ni pamoja na utekelezaji wa taratibu zilizoandaliwa kwenye nyaraka; ukaguzi wa ndani na nje; na usajili na utoaji cheti cha ithibati. Hatua ya ukaguzi inahitaji kwenda sambamba na uzalishaji endelevu ili ukaguzi uweze kufanyika na hatimaye cheti kutolewa.

**Mradi wa Dhahabu wa Buhemba**

***102. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni wa ubia kati ya *STAMICO* inayomiliki hisa asilimia 35 na kampuni ya *GOODFIELD International DMCC* ya Dubai inayomiliki hisa asilimia 65. Shughuli zilizofanyika ni ujenzi wa miundombinu ya mgodi kwa kushirikiana na mbia mwenza pamoja na uchorongaji wa awali ili kuongeza kiasi cha mashapo ambapo jumla ya mita 4,600 za RC na 1,940 za DD zimechorongwa. Shughuli za uzalishaji zitaanza baada ya

kutolewa kwa matokeo ya upimaji kutoka maabara na kukadiriwa kwa rasilimali za madini zilizopo.

**Mgodi wa Dhahabu wa *Buckreef***

***103. Mheshimiwa Spika,*** mgodi wa dhahabu wa *Buckreef* uliopo mkoani Geita unamilikiwa kwa ubia kati ya *STAMICO* na *TANZAM2000*. Katika ubia huo Shirika linamiliki hisa asilimia 45 na mbia ana hisa asilimia 55, ambapo thamani ya uwekezaji katika mradi ni dola za Marekani milioni 19.6. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, mgodi umezalisha wakia za dhahabu 15,036.28 zenye thamani ya dola za Marekani 26,415,952.53 sawa na shilingi 60,888,770,581.65 na kulipa Serikalini shilingi 4,544,586,358.9 kama mrabaha, ada za ukaguzi na ushuru wa huduma.



***Picha Na. 12:*** *Mtambo wa Kuchenjua dhahabu wa mgodi wa Buckreef*

**Kandarasi za Uchorongaji**

***104. Mheshimiwa Spika***, Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) linaendelea na kandarasi ya uchorongaji katika Mgodi wa *GGM*, *STAMIGOLD* na mgodi wa *Buckreef* ambao unahusisha uchorongaji wa *Reverse Circulation* (RC*)* na *Diamond Drilling* (DD). Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika limepata kandarasi mpya na kusaini mkataba na Kampuni ya

*Miner Station* wenye thamani ya shilingi milioni 600 na kuongezwa kwa mkataba wa kandarasi ya uchorongaji katika Mgodi wa *GGM* wenye thamani ya shilingi 55,253,496,000 utakaotekelezwa kwa muda wa miaka miwili kuanzia Aprili, 2023 hadi Aprili, 2025.




***Picha Na. 13:*** *Mtendaji Mkuu wa STAMICO Dkt. Venance Mwase akisaini mkataba wa uchorongaji na Kampuni ya GGM.*

***105. Mheshimiwa Spika***, Shirika pia limesaini kandarasi na mgodi wa dhahabu wa *Buckreef* wenye thamani ya shilingi bilioni 3.65. Katika kuimarisha shughuli za uchorongaji, *STAMICO* imeendelea kununua mitambo ya uchorongaji ambapo hadi sasa inamiliki mitambo 14.



***Picha Na. 14:*** *Moja ya mitambo ya uchorongaji inayomilikiwa na STAMICO*

### (c) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)

***106. Mheshimiwa* Spika**, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ni mhifadhi mkuu wa taarifa zote zinazohusu miamba na madini hapa nchini na inatoa takwimu na taarifa za jiosayansi kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi katika uwekezaji endelevu. Vilevile, Taasisi inaratibu majanga ya asili ya jiolojia na kutoa elimu kwa umma ya namna ya kujikinga kabla na baada ya kutokea majanga hayo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Taasisi imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

### (i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini

***107. Mheshimiwa Spika,*** *GST* imefanya ugani wa jiolojia kwenye QDS mbili (2) mpya (QDS 203 na QDS 204) zilizopo Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Lengo la ugani huo ni kubaini miamba na madini yanayopatikana kwenye maeneo hayo. Matokeo ya awali ya utafiti huu yanaonesha uwepo wa madini ya viwandani aina ya *kaolin* ambayo hutumika kwenye utengenezaji wa

karatasi, marumaru, kauri na rangi; chokaa ambayo hutumika kwenye utengenezaji wa saruji, mbolea, rangi na *gypsum board*; udongo mfinyanzi (ball clay) ambao hutumika kutengenezea kauri; *silica sand* ambayo hutumika kutengenezea vioo, kauri, urembo, chupa, rangi na kuchuja maji; na *heavy mineral sands* ambayo hubeba madini ya *titanite*, *zircon* na *monazite* ambayo pia hubeba metali adimu (rare earth elements) ambazo hutumika kutengeneza vifaa vya teknolojia, rangi nyeupe na teknolojia ya uchimbaji wa visima vya mafuta na gesi.



***Picha Na.15:*** *Wataalam wa GST wakiendelea na ugani wa jiolojia katika maeneo ya Mkoa wa Pwani (QDS 203 na 204).*

***108. Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, ushauri elekezi wa jiosayansi ulitolewa kwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kuhusu uimara na muundo wa miamba na udongo katika eneo wanalotarajia kujenga ofisi zao Jijini Dodoma. Lengo la ushauri huo ni kusaidia kuepusha kufanya ujenzi katika maeneo yenye mipasuko ya miamba. Aidha, ushauri elekezi ulitolewa kwa wachimbaji wadogo kuhusu mwelekeo wa miamba yenye madini pamoja na namna bora ya uchukuaji sampuli na uchenjuaji ili kuongeza tija katika shughuli zao za uchimbaji.

***109. Mheshimiwa Spika,*** utafiti maalumu ulifanyika kwa lengo la kubaini jiolojia na uwepo wa madini yenye thamani katika eneo

la Mahenge Wilaya ya Ulanga. Matokeo ya awali ya utafiti huo yameibua maeneo mapya yenye madini ya kinywe (graphite) ambayo hayakuwa kwenye kanzidata ya awali. Madini haya ni muhimu sana duniani kwa sasa kwani hutumika kutengeneza betri za magari yanayotumia nishati ya umeme ambayo ni teknolojia mpya.



***Picha Na.16:*** *Wataalam wa GST wakifanya utafiti maalum wa jiolojia katika Wilaya ya Ulanga.*

***110. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika utafiti huo *GST* ilifanikiwa kuibua chanzo kipya kikubwa cha mchanga ambacho kilikuwa hakijulikani. Chanzo hiki kitaongeza wingi wa madini ya ujenzi katika Wilaya ya Ulanga.

***111. Mheshimiwa Spika,*** utafiti kwa njia ya jiofizikia, jiokemia na jiolojia umefanyika kujua chanzo na ubora wa chumvi kwenye vijiji vya Majiri na Kinangali, Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida. Taarifa za awali zinaonesha kuwa chumvi katika maeneo haya inatokana na chemichemi za maji zinazotoka chini ya ardhi. Aidha, chumvi katika maeneo haya ina ubora unaoanzia asilimia 45 hadi 98 huku baadhi ya maeneo yakiwa na kiasi kikubwa cha magadi.




***Picha Na. 17**: Wataalam wa GST wakiwa kwenye shughuli za uchunguzi wa ubora wa chumvi katika maeneo ya Wilaya ya Manyoni.*

***112. Mheshimiwa Spika,*** utayarishaji wa andiko la madini muhimu (critical minerals) kwa Tanzania unaendelea na unatarajia kukamilika kabla ya mwisho wa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Taasisi imefanya uchambuzi wa awali na kukusanya taarifa na takwimu zenye kuelezea madini muhimu na mkakati kwa nchi. Takwimu hizo zimekusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi za Serikali kama vile: Tume ya Madini, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Wizara ya Kilimo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI) na pia taarifa kutoka Kanzidata ya Taifa ya Jiosayansi iliyopo *GST*.

***113. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, wadau muhimu kama vile wamiliki wa viwanda vya saruji, chuma na viwanda vya mbolea wametoa takwimu ili kusaidia uandaaji wa andiko hili muhimu. Uchakataji wa takwimu na uhakiki wa maeneo yenye madini husika unaendelea na orodha yake itajumuishwa kwenye andiko.

***114. Mheshimiwa Spika,*** jumla ya ripoti 448 kutoka kwa wamiliki wa leseni za utafiti na uchimbaji madini (kampuni 25)

zilipokelewa na kufanyiwa uchambuzi wa awali na kuhifadhiwa kwenye Kanzidata ya Taifa ya Jiosayansi. Aidha, GST imekamilisha kuandaa toleo jipya la kitabu cha "Madini Yapatikanayo Tanzania".

**(iii) Kuboresha Huduma za Maabara**

***115. Mheshimiwa Spika,*** *GST* imeendelea kutoa huduma za maabara ambapo imechunguza jumla ya sampuli 12,559 kati ya sampuli 11,333 zilizopangwa kuchunguzwa kwa kipindi husika. Idadi hii inajumuisha sampuli za uchunguzi wa dhahabu, metali mbalimbali, vito na madini ya viwandani kutoka kwa wateja wa ndani na nje. Jumla ya vyungu vya kuyeyushia dhahabu (crucibles) 7,067 vimezalishwa. Aidha, ukaguzi wa nje kupitia shirika linalodhibiti ubora wa huduma za maabara katika nchi zilizopo Kusini mwa Bara la Afrika (SADCAS) ulifanyika tarehe 1 Desemba, 2022 na Taasisi imekidhi vigezo vya kuendelea kuwa na ithibati. ***Kupitia Bunge lako Tukufu napenda kutoa wito kwa wachimbaji wa madini kuendelea kuzitumia maabara za GST kwa matokeo ya uhakika ya uchunguzi wa sampuli za miamba, madini, udongo na maji.***

**(iv) Kuratibu Majanga ya Asili ya Jiolojia na Kutoa Elimu kwa Wananchi**

***116. Mheshimiwa Spika,*** matengenezo ya vifaa, ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za mitetemo kutoka katika vituo vinne (4) vya Dodoma, Geita, Mbeya na Arusha ulifanyika ambapo matokeo yanaonesha kuwepo kwa matukio ya matetemeko ya ardhi kwenye ukanda wa Bonde la Ufa la Afrika Mashariki katika mikoa ya Manyara, Arusha, Singida, Mara, Dodoma na Ruvuma. Matetemeko hayo yalikuwa na ukubwa wa kati ya 4.4 na 5.0 katika kipimo cha *Richter*. Hata hivyo, hakuna madhara yaliyotokea kutokana na matetemeko hayo. *GST* inaendelea

kuelimisha umma kuhusu kuchukua tahadhari katika kujikinga na majanga ya asili ya jiolojia.

**(v) Uimarishaji wa Uwezo wa Taasisi na Kusogeza Huduma kwa Wadau**

***117. Mheshimiwa Spika,*** ili kusogeza huduma za ugani na utafiti kwa wadau *GST* imeanza ujenzi wa ofisi na maabara katika wilaya ya Chunya. Aidha, *GST* imewezesha watumishi 20 kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali za taaluma ili kuwajengea uwezo kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

***(d)* Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia *(TEITI)***

***118. Mheshimiwa Spika,*** *TEITI* ina jukumu la kuhamasisha Serikali kuweka mifumo ya uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia ili kuongeza mapato na manufaa yatokanayo na Sekta ya Uziduaji. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi imetekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

**(i) Kukamilika na Kuwekwa Wazi kwa Umma Ripoti ya TEITI ya Mwaka 2019/2020**

***119.Mheshimiwa Spika****, TEITI* imekamilisha na kuweka wazi kwa Umma Ripoti ya Mwaka 2019/2020 ya ulinganishi wa malipo ya kodi kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopokelewa na Mamlaka za Serikali. Pamoja na mambo mengine ripoti hii iliainisha kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Juni, 2020 Serikali imekiri kupokea kiasi cha shilingi 1,220,455,246,248.63 kutoka kwenye kampuni 40 zilizofanyiwa ulinganisho.

***120. Mheshimiwa Spika**,* ripoti ya Mwaka 2019/2020 imeweka wazi taarifa mbalimbali zikiwemo za uzalishaji na mauzo ya rasilimali madini, mafuta na gesi asilia; taarifa za wamiliki wa hisa katika Sekta ya Uziduaji na taarifa za ushirikishwaji wa Watanzania (local content) ili kuhakikisha kuwa matokeo ya ripoti hii yanawafikia wananchi wengi zaidi. Aidha, taarifa hiyo inapatikana kwenye tovuti ya https://www.teiti.go.tz/dashboard/

***121. Mheshimiwa Spika**,* taarifa hiyo imeandaliwa kwa lugha za kiswahili, kingereza na lugha ya alama (nukta nundu) kwa watu wenye uono hafifu ili kuwapa fursa ya kuelewa masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

### *(ii)* Elimu kwa Umma Kuhusu Matumizi ya Ripoti za *TEITI*

***122. Mheshimiwa Spika,*** TEITI imeendelea kuelimisha Umma kuhusu matumizi ya ripoti zake kupitia runinga, redio, tovuti, mitandao ya kijamii na kwenye maonesho mbalimbali yakiwemo maonesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba yaliyofanyika Julai, 2022 Dar es Salaam na maonesho ya Nanenane yaliyofanyika Agosti, 2022 Jijini Mbeya. Elimu kuhusu umuhimu wa kutumia takwimu pamoja na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi takwimu hizo hutolewa ili wananchi waweze kutumia takwimu hizo kuboresha sekta ya uziduaji na kuhamasisha mijadala kuhusu manufaa yanayotokana na utafutaji na uvunaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia hapa nchini. Ripoti za TEITI zinapatikana: https://www.teiti.go.tz.

***123. Mheshimiwa Spika,*** *TEITI* pia ilifanya warsha katika Mikoa ya kimadini ya Mwanza, Lindi, Mirerani, Songwe na Mtwara kwa lengo la kuwajengea uwezo Waheshimiwa Madiwani, Watunza Hazina wa Halmashauri, waandishi wa habari, wachimbaji wadogo wa madini na Asasi za Kiraia kuhusu matumizi ya takwimu zilizopo katika ripoti za *TEITI*.

### *(e)* Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)

***124. Mheshimiwa Spika,*** *TGC* inatoa mafunzo ya uongezaji thamani madini ikiwa ni pamoja na utambuzi, uchongaji wa vinyago vya miamba na madini, ukataji na ung'arishaji wa madini ya vito na utengenezaji wa bidhaa za usonara. Kituo kimetekeleza majukumu yake katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kama ifuatavyo: -

#### (i) Utoaji wa Mafunzo na Udahili wa Wanafunzi

***125. Mheshimiwa Spika,*** Kituo kimedahili jumla ya wanafunzi 88 wa *National Technical Awards* (NTA) *Level* 4, 5 na 6 katika fani ya Teknolojia ya Madini ya Vito na Usonara. Aidha, wanafunzi 19 walidahiliwa kujiunga na mafunzo ya muda mfupi katika fani za utambuzi wa madini ya vito, usonara, ukataji na ung'arishaji madini hayo. Vilevile, wanafunzi 39 walihitimu Stashahada katika Teknolojia ya Madini ya Vito na Usonara.

#### (ii) Uzalishaji wa Bidhaa na Huduma kwa Wadau wa Madini

***126. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Kituo kilizalisha jumla ya bidhaa 1,323 kati ya 2,000 zinazotokana na madini zilizotarajiwa kuzalishwa kwa mwaka. Bidhaa hizo ni pamoja na vinyago vya miamba na madini, tuzo, ramani, rozari, *bracelet, chain, necklace, keyholders, pendants, tablemats,* hereni na shanga (beads).




***Picha Na. 18:*** *Baadhi ya bidhaa zilizozalishwa na TGC*

**(iii) Kuhuisha Mitaala**

***126. Mheshimiwa Spika,*** Kituo kimehuisha mitaala ya mafunzo kwa kushirikisha wadau na kuiwasilisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET)* kwa ajili ya kuridhiwa kutumika kuanzia Mwaka wa Masomo 2023/2024. Mitaala iliyohuishwa ni ya *Basic Technician in Gem and Jewellery Technology* (NTA Level 4), *Technician in Gem and Jewellery Technology* (NTA Level 5) na *Ordinary Diploma in Gem and Jewellery Technology* (NTA Level 6) ambayo imejumuisha mahitaji ya soko yaliyopo kwa sasa.

**(iv) Kuendelea Kuimarisha Miundombinu ya Kituo na Kuwajengea Uwezo Watumishi**

***128. Mheshimiwa Spika,*** TGC inakusudia kujenga jengo jipya la Kituo ambapo tayari Mshauri Elekezi amekamilisha michoro na Kituo kipo kwenye taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi. Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 baadhi ya watumishi wa Kituo walipatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi yaliyolenga kuwajengea uwezo na kubadilishana uzoefu

kwenye tasnia ya uongezaji thamani madini ya vito na usonara. Mafunzo hayo pia yalikusudia kupata uelewa na ujuzi juu ya uendeshaji wa viwanda vya kuchakata madini na utoaji wa huduma za maabara ya madini ya vito, utengenezaji wa bidhaa za usonara na usimamizi wa tasnia ya uongezaji thamani madini.

***129. Mheshimiwa Spika,*** ziara ya kupata uzoefu katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za uongezaji thamani madini ya vito na biashara ya usonara ilifanyika katika nchi za India na Thailand ambazo zimebobea kwenye shughuli za uongezaji thamani madini. Kupitia ziara hiyo, Wizara ilipata uelewa wa namna bora ya kuendeleza shughuli za uongezaji thamani madini na usonara. Aidha, katika ziara hiyo pia fursa za uwekezaji katika uongezaji thamani madini nchini zilitangazwa.

***130. Mheshimiwa Spika,*** nchi hizo zimeonesha utayari wa kushirikiana na Tanzania katika utoaji wa mafunzo ya uongezaji thamani madini na biashara ya madini. Vilevile, kampuni za India zimeonesha nia ya kuwekeza katika madini mkakati na makaa ya mawe.

## F. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

***131. Mheshimiwa Spika,*** katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imezingatia miongozo ifuatayo: Mwongozo wa Kitaifa wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2023/2024; Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022– 2025/2026; Sera ya Madini ya Mwaka 2009; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa waliyoyatoa kwa nyakati tofauti; pamoja na Maelekezo ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini yaliyotolewa kwa nyakati tofauti.

## I. Vipaumbele vya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

***132. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Madini itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:- kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; Kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; kuwaendeleza na kusogeza huduma za ugani kwa wachimbaji wadogo; kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini; kuhamasisha uwekezaji na biashara katika Sekta ya Madini, uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; na kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ya Madini ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

### (i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Maduhuli na Kuongeza Mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa

***133. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:- kuimarisha udhibiti na usimamizi wa uchimbaji mkubwa, wa kati na mdogo wa madini ili uweze kunufaisha nchi na wawekezaji; kutekeleza mikakati itakayowezesha kudhibiti vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchini.

***134. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini nchini; kuweka mazingira yatakayowezesha kuanzishwa na kusimamia migodi mipya ya uchimbaji mkubwa, wa kati na mdogo; na kuendeleza mikakati ya kuimarisha usimamizi wa madini ya ujenzi na viwandani, soko

la Tanzanite na vito vingine hapa nchini ili kuongeza mapato yatokanayo na madini hayo.

**(ii) Kuendeleza Madini Muhimu na Madini Mkakati**

***135. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza madini muhimu na madini mkakati (critical and strategic minerals), Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:- kufanya tafiti na kutangaza fursa za madini mkakati na muhimu zilizopo; kuhamasisha uwekezaji katika utafutaji na uchimbaji wa madini mkakati na madini muhimu; kutoa leseni za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini mkakati na madini muhimu; na kuandaa Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa shughuli za uchimbaji wa madini mkakati nchini.

***136. Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa madini mkakati ambayo yatapewa kipaumbele katika utafiti ni pamoja na madini ya kinywe, nikeli, rare earth elements, cobalt, lithium, manganese, vanadium, niobium, titanium na tin. Madini haya yanahitajika kwa kiasi kikubwa kwenye vifaa vya kielektroniki, betri za magari yanayotumia nishati ya umeme, vifaa vya ndege na vyombo vingine vinavyoruka angani, vifaa vinavyozalisha nishati ya umeme kupitia upepo na mwanga wa jua, na vifaa vya kisasa vinavyotumika katika kulinda usalama wa nchi. Aidha, mpango wa muda wa kati na mrefu ni kuyatumia madini hayo kuzalisha bidhaa/teknolojia mbalimbali hapa nchini.

**(iii) Kuwaendeleza na Kusogeza Huduma za Ugani kwa Wachimbaji Wadogo**

***137. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo:- kubuni na kuimarisha utekelezaji wa mipango ya kuwawezesha wachimbaji wadogo ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija na kuendelea kuwatengea maeneo au kuwapatia leseni kwenye maeneo ambayo yana

taarifa za msingi za jiolojia; kutoa huduma za utafiti kwa gharama nafuu; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kuwa wa kati na hatimaye kuwa wachimbaji wakubwa; na kuwawezesha wachimbaji wadogo, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo, kuwawekea mazingira mazuri ili waweze kukopesheka.

***138. Mheshimiwa Spika,*** pia wachimbaji wadogo watapatiwa mafunzo kuhusu uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini; na kufanya tafiti za jiosayansi na kuboresha kanzidata ya taifa ya taarifa za miamba na madini.

**(iv) Kuhamasisha Shughuli za Uongezaji Thamani Madini**

***139. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini, Wizara itafanya yafuatayo:- kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya uchenjuaji, uyeyushaji, usafishaji na utengenezaji wa bidhaa za madini; kuvutia uwekezaji na kusimamia shughuli za uongezaji thamani madini; kujenga na kuimarisha miundombinu ya Kituo cha Jemolojia ili kiweze kutoa mafunzo ya uongezaji thamani madini kwa ufanisi. Kuweka mazingira rahisi kwa *refineries* zilizopo nchini kuhakikisha zinapata malighafi madini kwa ajili ya kusafisha kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi. ***Napenda kutoa wito kwa wachimbaji na wafanyabiashara wa madini ya dhahabu kutumia refineries zilizopo nchini kusafisha madini hayo***.

**(v) Kuhamasisha Uwekezaji na Biashara katika Sekta ya Madini, Uanzishwaji wa Minada na Maonesho ya Madini ya Vito**

***140. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo:- kuweka mazingira yatakayohamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini bila ya kuathiri ustawi na matarajio ya nchi kutokana na uwekezaji huo; kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kufanya tafiti za madini ya Kimkakati na

madini muhimu, madini ya viwandani na madini ya metali; kushiriki mikutano na makongamano mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika Sekta ya Madini; na uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito na bidhaa za usonara nchini.

**(v) Kuzijengea Uwezo Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi**

***141. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kipaumbele hiki, Wizara itafanya yafuatayo: kuiimarisha *STAMICO* ili ishiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini; kuiimarisha Tume ya Madini ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kukusanya maduhuli na takwimu za madini kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.

***142. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itaendelea kuiimarisha *GST* ili iweze kufanya tafiti zaidi za madini ili kuvutia uwekezaji kwenye Sekta ya Madini unaoenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia; kuiimarisha *TEITI* kwa kuipatia vitendea kazi ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo; na kuiimarisha *TGC* ili iweze kutoa mafunzo ya usonara, ukataji na ung'arishaji ili kiwe Kituo bora cha uendelezaji madini ya vito.

**II. Kazi Zitakazotekelezwa na Taasisi Zilizo 2023/2024 (a) Tume ya Madini (i) Kuimarisha Usimamizi wa Sekta ya Madini na Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali Chini ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha**

***143. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Madini itatekeleza yafuatayo: kuongeza wigo wa ukusanyaji wa maduhuli ikiwemo kuhimiza matumizi ya *PoS* katika ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na madini ujenzi na viwandani; kuongeza kasi ya utoaji wa leseni kwa kuimarisha Mfumo wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni; kuendelea kutangaza fursa za madini zilizopo nchini ili

kuchochea na kuvutia wawekezaji wa madini; kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa migodi kwenye masuala ya usalama, afya na matumizi bora ya baruti; kusimamia uzalishaji wa madini ya ujenzi kwa kuhakikisha Mfumo wa Ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na madini haya (*MiMS*) unafanya kazi kikamilifu nchi nzima. Aidha, kuhakikisha maeneo ambayo hayafikiki kwa sasa na yana uzalishaji wa madini ya ujenzi na viwandani yanafikiwa na maduhuli ya Serikali yana kusanywa. Suala hili litafanywa kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango.

***144. Mheshimiwa Spika,*** hatua nyingine ni kutatua migogoro katika maeneo mbalimbali yenye shughuli za uchimbaji; kuboresha huduma katika masoko ya madini nchini ikiwa ni pamoja na kudhibiti mianya ya utoroshaji wa madini kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Serikali pamoja na kusajili mialo ya wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuweka mazingira mazuri ya kikodi ikiwemo kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) ili wachimbaji na wafanyabiashara wa madini wahamasike kufanya biashara kwenye masoko, *refineries* na vituo vya ununuzi wa madini na kuacha kutorosha madini.



***Picha Na. 19:*** *kutoka kushoto ni Wakaguzi Wasaidizi wa Madini Ujenzi wakikusanya maduhuli kwa kutumia Mashine ya PoS*

**(iii) Kuimarisha Ufuatiliaji na Ukaguzi wa Usalama, Afya, Mazingira na Uzalishaji wa Madini kwa Wamiliki wa Leseni**

***145. Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na uchimbaji madini salama, endelevu na wenye tija, Tume ya Madini itaendelea kufanya ukaguzi wa mazingira kwa kukagua miundombinu ya migodi kama vile mabwawa ya kuhifadhia topesumu, mashimo ya uchimbaji, maeneo ya kutunzia miambataka, maghala na stoo za kuhifadhia baruti na kukagua mitambo ya uchenjuaji madini. Vilevile, itaendelea kusimamia mipango ya uendelezaji na ufungaji migodi kwa wamiliki wa leseni kubwa na za kati.

**(iv) Kuimarisha Ukaguzi wa Fedha na Kodi**

***146. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa kodi na tozo mbalimbali zinazotokana na uchimbaji na biashara ya madini zinalipwa ipasavyo, Tume ya Madini itaendelea kufanya ukaguzi huu kwa wenye leseni za Madini ili kuhakikisha stahiki za Serikali zinapatikana na kulipwa kwa usahihi. Suala hili litaendana na kuimarisha maabara ya Tume ambayo inapima ubora na wingi wa madini yanayochimbwa nchini.

***147. Mheshimiwa Spika,*** majibu yanayotoka kwenye maabara hii yatasaidia kufanya usuluhishi wa mrabaha na ada ya ukaguzi. Pia, kufanya uchambuzi wa kina wa moduli za kifedha na upembuzi yakinifu kwa waombaji wa leseni za uchimbaji madini ili kujiridhisha kama miradi hiyo ina tija.

**(v) Kuendelea Kuboresha Mazingira ya Kuwawezesha Wananchi Kufaidika na Rasilimali Madini**

***148. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Watanzania wananufaika na Rasilimali Madini, Tume ya Madini itaendelea kutenga na kugawa maeneo kwa wachimbaji wadogo nchini, kusimamia ushirikishwaji wa watanzania (Local Content) kwenye shughuli za

madini kwa mujibu wa Sheria, kuhakikisha kampuni za uwekezaji katika Sekta ya Madini zinatumia bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na huduma zinazotolewa na Watanzania, na kusimamia wenye leseni za uchimbaji madini kutimiza takwa la uwajibikaji kwa jamii zinazowazunguka kwa kutekeleza Miradi ya Kijamii (CSR). Aidha, Tume itaendelea kutoa elimu kwa Taasisi za kifedha kuhusu Sekta ya Madini ili kuendelea kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo kuongeza ushiriki katika shughuli za madini.

**(v) Kuelimisha Umma na Kuboresha Wadau wa Sekta ya Madini Upatikanaji wa Taarifa Mbalimbali kwa**

***149. Mheshimiwa Spika,*** ili kujenga uelewa kuhusu shughuli za madini, Tume ya Madini itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Madini ikiwa ni pamoja na namna ya kupata leseni ya madini, upatikanaji wa Sheria na Kanuni za usimamizi wa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini, biashara ya madini, utunzaji wa mazingira na ulipaji wa kodi na tozo za madini. Vilevile, Tume itaendelea kuimarisha Kitengo cha Habari kwa kuboresha tovuti ya Tume ya Madini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za Sekta ya Madini kwa wadau.

**(vi) Kuendeleza Rasilimaliwatu na Kuboresha Mazingira ya Kufanyia Kazi**

***150. Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na usimamizi wa Sekta ya Madini, Tume ya Madini itaendelea kuboresha mazingira ya kazi na vitendea kazi; kuwaendeleza watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi; na kuboresha Muundo wa Tume ya Madini.

**(b) Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)**

***151. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2023/2024, *GST* imepanga kufanya utafiti maalumu (strategic mineral potential mapping) katika QDS mbili (2) zilizopo mikoa ya Njombe na Ruvuma. Utafiti huo unalenga maeneo yenye jiolojia inayoshabihiana na uwepo wa madini kama vile chuma, *nickel,* kinywe, *manganese,* makaa ya mawe, ambayo baadhi ni madini muhimu yanayohitajika sana kwa sasa duniani.

**(i) Kufanya Tafiti za Jiosayansi na Kuboresha Kanzidata ya Taifa ya Taarifa za Miamba na Madini.**

***152. Mheshimiwa Spika,*** *GST* inakusudia kufanya utafiti wa jiolojia na jiokemia katika QDS mbili (2) mpya (QDS 221 na QDS 222) zilizopo Mkoa wa Pwani na kuchora ramani zake. Utafiti huo pamoja na kuhuisha Kanzidata ya Taifa ya miamba na madini, unalenga kuibua madini ambayo ni malighafi muhimu kwa baadhi ya viwanda hapa nchini.

***153. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi itafanya tafiti nne (4) maalumu za jiosayansi; utafiti wa kina mmoja wa madini yakiwemo, madini ya viwandani, helium, vito mfano tanzanite, na dhahabu; kufanya tafiti moja (1) kwa lengo la kuibua uelewa kwa wadau na kuchapisha kwenye jarida linalotambulika; kutoa ushauri elekezi kwa wadau/kampuni 15 kwenye nyanja za jiolojia, jiokemia, jiofizikia na uchenjuaji madini.

***154. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya *GST* inakusudia kutengeneza (digitization) ramani 24, kudurusu ramani 30 na kuchakata picha za *satellite*; ku-scan ramani na ripoti 500, kuingiza taarifa/*specimen*/machapisho 500 kutoka katika mfumo wa karatasi kwenda katika mfumo wa dijitali; kukusanya, kuhakiki na kutathmini taarifa/takwimu kutoka kwa wamiliki 40 wa leseni za utafutaji/uchimbaji madini nchini ili kuzifanyia uchambuzi kwa

ajili ya kujua kiasi cha rasilimali madini kilichopo; kuhuisha kanzidata ya rasilimali madini zinazopatikana nchini na Kitabu cha Madini Yapatikanayo Tanzania; na kukusanya miamba choronge mita 1,000 na kuchakata taarifa zake.

**(ii) Kuwaendeleza Wachimbaji Wadogo kwa Kufanya Tafiti za Jiosayansi**

***155. Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaendeleza wachimbaji wadogo na wa kati, *GST* inalenga kufanya utafiti wa jiosayansi na kutoa mafunzo kwa lengo la kutambua ulalo, mwelekeo na tabia za mbale katika maeneo mawili (2) ya wachimbaji wadogo yaliyopo mikoa ya Kigoma na Katavi; na kufanya utafiti wa jiosayansi kwa lengo la kubaini uwepo wa madini katika eneo moja (1) lililotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**(iii) Kuboresha Huduma za Maabara kwa Wadau wa Sekta ya Madini, Kilimo na Ujenzi**

***156. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha Huduma za Maabara, *GST* imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:- kufanya uchunguzi kwa kuzingatia matakwa ya ithibati ili matokeo ya uchunguzi wa maabara yaendelee kutambulika kimataifa; kuanzisha maabara katika maeneo ya Chunya kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wachimbaji na watafutaji wa madini; utafiti wa malighafi na kutengeneza vyungu (crucibles) 300,000 na *cupels* 50,000 kwa ajili ya kuyeyusha sampuli za dhahabu; uchunguzi wa sampuli za udongo miamba au madini 18,000; kusogeza huduma za uchunguzi wa sampuli maeneo ya Geita na Chunya; uandaaji wa sampuli rejea za dhahabu, shaba, silva, zinki, chuma na kobati; na ukarabati wa *Induced Coupled Plasma*.

### (iv) Kuboresha Uratibu wa Majanga ya Asili ya Jiolojia

***157. Mheshimiwa Spika,*** *GST* inakusudia kutekeleza yafuatayo: kukusanya takwimu kutoka vituo vitano (5) vya kudumu vilivyoko Arusha, Dodoma, Geita, Mtwara na Mbeya vya kupimia matetemeko ya ardhi ili kujua matukio mbalimbali ya mitetemo; kuchakata takwimu zilizokusanywa kutoka katika vituo vyote vitano (5) na kuhuisha ramani inayoonesha vitovu vya matetemeko ya ardhi nchini; kufanya matengenezo na kuvihudumia vifaa vya kunakili mitetemo vilivyofungwa katika vituo vyote vitano (5); kuendelea na kazi ya kuunganisha vituo viwili (2) vya kupimia mitetemo vilivyopo Dodoma na Arusha katika mfumo wa mubashara (*real time*) ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa wakati mara tetemeko linapotokea.

***158. Mheshimiwa Spika,*** vilevile *GST* itatoa elimu kwa Umma juu ya namna bora ya kujikinga au kupunguza athari za majanga ya asili ya jiolojia kupitia machapisho, semina na vyombo vya habari; na kusimika kituo kipya mkoani Kigoma cha kufuatilia matetemeko kwa ukanda wa Bonde la Ufa Mkondo wa Magharibi.

### (v) Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika Kutoa Huduma

***159. Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uwezo wa *GST* wa kutekeleza majukumu pamoja na ukusanyaji wa mapato, mambo yafuatayo yanatarajiwa kufanyika: kuboresha mifumo ya ndani ya uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa na takwimu za jiosayansi za upatikanaji wa madini; kuwajengea uwezo watumishi 35 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi katika nyanja mbalimbali.

***160. Mheshimiwa Spika,*** vilevile *GST* itahakikisha kuwa mazingira ya utendaji kazi yanaboreshwa kwa kununua vitendea kazi mbalimbali, ukarabati wa majengo na kuboresha maslahi ya

watumishi; kuendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji, usimamizi na matumizi ya fedha za Serikali; kuboresha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu na fedha; kutangaza zaidi (marketing) bidhaa/huduma zitolewazo na *GST*; kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala mtambuka kama vile kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, mapambano ya kuzuia rushwa na madhara yake; na kuendelea na hatua za kukamilisha kufanya mapitio na maboresho ya Muundo wa Taasisi ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu.

**(c) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)**

***161. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2023/2024, *STAMICO* inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo:

**(i) Kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani**

***162. Mheshimiwa Spika*****,** Shirika limepanga kuongeza usimamizi kwenye uwekezaji uliopo ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa wakati ambapo uwekezaji huo unahusisha miradi ya Buhemba; kiwanda cha kusafisha dhahabu cha Mwanza; mradi wa dhahabu wa *Buckreef*; mradi wa kuzalisha mkaa mbadala wa Rafiki Briquettes; mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe (Kabulo-Kiwira); mradi wa kuuza vilipuzi na kemikali za madini; na kuimarisha shughuli za uchorongaji.

**(ii) Kuendelea na Uzalishaji wa Makaa ya Mawe pamoja na Mkaa wa Kupikia (Rafiki Briquettes)**

***163. Mheshimiwa Spika*****,** Shirika litaendelea na uzalishaji mkubwa wa makaa ya mawe katika eneo la Kabulo-Kiwira kwa kununua vifaa vya uchimbaji na kufanya utafiti zaidi ili kuongeza mashapo yanayotarajiwa kuchimbwa na kuuzwa kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. Vilevile, kwa kutumia makaa

hayo, Shirika linatarajia kuongeza uzalishaji wa mkaa wa kupikia (Rafiki briquette) kwa kununua vifaa na mitambo minne (4) yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa kila mmoja. Shirika kwa kushirikiana na TANESCO litaendelea kutekeleza mpango wa kuzalisha umeme kiasi cha *Megawatt* 200 kutokana na makaa ya mawe kwa mujibu wa makubaliano kati ya Shirika na TANESCO.

**(iii) Kuimarisha Shughuli za Uchorongaji**

***164. Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kutangaza na kutafuta kandarasi za kudumu za muda mrefu katika migodi mikubwa na ya kati nchini na nje ya nchi. Aidha, Shirika litanunua vifaa vya kisasa vitakavyowezesha uchorongaji wenye tija. Ili kukidhi ongezeko la huduma za uchorongaji nchini na nje ya nchi, Shirika limepanga kuongeza mitambo ya uchorongaji hadi kufikia 18.

**(iv) Kuratibu Shughuli za Uchimbaji Mdogo na Kuimarisha Vituo vya Mfano**

***165. Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* itaendelea kuratibu shughuli za uchimbaji mdogo kwa kununua mitambo mitano (5) ya uchorongaji maalumu kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kutekeleza mpango wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali nchini; kuongeza uwezo wa vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi kwa kuimarisha miundombinu iliyopo; kuendelea na ujenzi wa vituo viwili vipya vya mfano katika Mkoa wa Tanga na Lindi; na Kuendelea kuwaunganisha wachimbaji wadogo na taasisi za fedha.

**(v) Kuendeleza Leseni za Shirika**

***166. Mheshimiwa Spika,*** *STAMICO* itaendelea kutekeleza mkakati wa utafiti (Exploration Strategy) ili kuendeleza leseni zake

ikiwemo leseni ya uchimbaji wa dhahabu Kigosi pamoja na leseni za madini mkakati na muhimu ya shaba, *lithium,* kinywe (graphite) na *rare earth element.*

**(vi) Kuboresha Mazingira ya Kazi kwa Watumishi**

***167. Mheshimiwa Spika***, *STAMICO* itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na mazingira ya kazi kwa kuwapatia vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa jengo la makao makuu ya Shirika Jijini Dodoma.

***168. Mheshimiwa Spika,*** Shirika pia, limepanga kuongeza usimamizi kwenye miradi yake ya ubia inayohusisha *Buckreef*, Buhemba, Mwanza Refinery pamoja na kampuni Tanzu ya *STAMIGOLD* ili kuongeza ufanisi na hivyo kuwezesha ukusanyaji wa mapato stahiki kutoka kwenye miradi hiyo. Aidha, Shirika litaendelea kuiwezesha *STAMIGOLD* kuendelea kufanya utafiti zaidi wa maeneo ya leseni zake ili kubaini mashapo zaidi na kuongeza uhai wa mgodi.

**(e) Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia (*TEITI*)**

***169. Mheshimiwa Spika**,* katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 *TEITI* imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kuweka wazi ripoti ya *TEITI* ya ulinganishi wa Malipo ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia na Mapato ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; kuweka wazi mikataba ambayo Serikali imeingia na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; kuweka wazi orodha za wamiliki wa hisa katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia; kufanya utafiti utakaokuja na mapendekezo ya namna bora ya kufungamanisha Sekta ya Madini na Sekta nyingine za uchumi nchini.

***170. Mheshimiwa Spika***, vilevile, *TEITI* itajenga mfumo wa kielektroniki utakaotumiwa na kampuni pamoja na Taasisi za Serikali kutoa taarifa za malipo yaliyofanywa na kampuni hizo kwa Serikali; kufanya tafiti mbalimbali za namna wananchi wanavyonufaika na wanavyoweza kunufaika zaidi na rasilimali madini, mafuta na gesi asilia; na kuanzisha kanzidata ya takwimu itakayoifanya *TEITI* kuwa kitovu cha taarifa na takwimu za madini, mafuta na gesi asilia nchini.

**(f) Kituo cha Jemolojia Tanzania (TGC)**

***171. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kituo cha Jemolojia Tanzania kinatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

**(i) Utoaji wa Mafunzo**

***172. Mheshimiwa Spika,*** Kituo kitaongeza udahili wa wanafunzi wa muda mrefu (stashahada) katika fani ya teknolojia ya madini ya vito na usonara (*gem and jewellery technology);* kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utambuzi wa Madini ya Vito, Ukataji na Ung'arishaji wa Madini ya Vito na Utengenezaji wa Bidhaa za Usonara.

***173. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Kituo kitatoa huduma za maabara kwa madini ya vito na bidhaa za usonara; utengenezaji wa bidhaa za mapambo na urembo (usonara); kutoa ushauri na ugani kwa wadau wa madini; kufanya tafiti za kuyaongezea thamani madini; na kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

**(ii) Uzalishaji wa Bidhaa**

***174. Mheshimiwa Spika***, Kituo kitaongeza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zitokanazo na madini ya vito na miamba zikiwemo

vinyago, mikufu, hereni na bidhaa nyingine za urembo na mapambo.

**(iii) Kukijengea Uwezo Kituo**

***175. Mheshimiwa Spika**,* katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara kupitia *TGC* imepanga kuimarisha miundombinu ya kutolea mafunzo kwa kuendelea na ujenzi wa jengo lenye huduma za madarasa, karakana za uongezaji thamani madini, ofisi, kantini, maduka ya kuuzia bidhaa za madini na mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500.

***176. Mheshimiwa Spika,*** Kituo kinatarajia kuwaendeleza watumishi 12 katika kozi za muda mfupi na mrefu katika vyuo vilivyobobea kwenye masuala ya uongezaji thamani madini. Aidha, ili kuboresha utendaji kazi wa kituo cha TGC, Wizara imepanga kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za ukufunzi.

**G. SHUKRANI**

***177. Mheshimiwa Spika,*** nikiri kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na juhudi kubwa za kuhakikisha kuwa uchumi wa nchi yetu unaimarika. Kasi kubwa ya utendaji kazi anayoendelea nayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadhihirisha kuwa nchi yetu itaendelea kukua kiuchumi.

***178. Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo mazuri anayotupatia katika Sekta ya Madini ambayo yanaifanya Sekta kuendelea kukua na kuvutia wawekezaji kwa manufaa ya Taifa.

***179. Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maelekezo na miongozo mbalimbali ambayo amekuwa akiitoa katika kusimamia utendaji wa shughuli mbalimbali kwa manufaa ya Taifa. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

***180. Mheshimiwa Spika,*** kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa (Mb.), Naibu Waziri wa Madini kwa jinsi anavyoendelea kutoa ushirikiano katika kusimamia Sekta ya Madini. Amekuwa ni msaada mkubwa kwangu katika kuhakikisha Sekta ya Madini inatimiza malengo yake.

***181. Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa niwashukuru Bw. Kheri Abdul Mahimbali, Katibu Mkuu, na Bw. Msafiri Lameck Mbibo, Naibu Katibu Mkuu kwa namna wanavyosimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, niwashukuru Dkt. AbdulRahman Shabani Mwanga, Kamishna wa Madini, Profesa Idris Suleiman Kikula, Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Profesa Justinian Rwezaula Ikingura, Mwenyekiti wa Bodi ya *GST*, Meja Jenerali (Mstaafu) Michael Wambura Isamuhyo, Mwenyekiti wa Bodi ya *STAMICO*, Dkt. George Patrick Mofulu, Mwenyekiti wa Bodi ya *TGC,* Bw. Ludovick Silemwa Utouh, Mwenyekiti wa Kamati ya *TEITI*, Makamishna wa Tume ya Madini na wajumbe wa Bodi zote kwa kusimamia kwa umakini na weledi uendeshaji wa Sekta ya Madini.

***182. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, niwashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa na kwa kujituma bila kuchoka katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

***183. Mheshimiwa Spika,*** niwashukuru pia wadau wa Sekta ya Madini wakiwemo watafutaji, wachimbaji, wamiliki wa mitambo ya uchenjuaji pamoja na wafanyabiashara wa madini kwa kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi. Hii imerahisisha usimamizi wa Sekta ya Madini. Aidha, nizishukuru Taasisi za Fedha hususan mabenki kwa kuendelea kuwapa mikopo wachimbaji, Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutuhakikishia usalama kwenye maeneo yenye shughuli za madini bila kusahau vyombo vyote vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kuitangaza Sekta ya Madini.

***184. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo la Bukombe ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na Taifa. Nawaahidi na kuwahakikishia nitaendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote na kwa kipaji nilichojaliwa na Mwenyezi Mungu katika kuleta maendeleo ya jimbo na Taifa kwa ujumla.

***185. Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kumshukuru kipekee mke wangu mpendwa Benadetha Clement Mathayo pamoja na watoto wangu wapendwa Elshadai, Elvin, Elis, Abigael, Amon, Abishai na Moses kwa kunivumilia, kuniombea kwa dhati kwa Mwenyezi Mungu na kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu ya ubunge na uwaziri katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa.

## H. HITIMISHO

***186. Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyopangwa ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ya shilingi 1,006,705,169,300.00, naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kupitisha makadirio ya shilingi 89,357,491,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa mchanganuo ufuatao:

(i) Shilingi 23,172,550,000.00 ikiwa ni fedha za maendeleo; na

(ii) Shilingi 66,184,941,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 20,307,498,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 45,877,443,000.00 ni Matumizi Mengineyo.

***187. Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Majedwali na vielelezo mbalimbali kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala na takwimu muhimu kuhusu Sekta ya Madini vimeambatishwa pamoja na hotuba hii. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Madini kwa kikoa cha www.madini.go.tz.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ataingia Mwenyekiti punde ili aendelee na ratiba iliyo mbele yetu, lakini kuna matangazo mawili.

La kwanza nimejulishwa hapa na Mheshimiwa Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe kwamba kuna wageni wake ambao ni viongozi wa bodaboda kutoka Kyela hawajatambulishwa. Sijui wako upande gani? Haya karibuni sana sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote. Wabunge Wanawake na Wabunge Wanaume kuwa kesho tarehe 28 Aprili, 2023 kutakuwa na Sherehe ya Usiku wa Mwanamke wa Bunge. Itakayofanyika katika Viwanja vya Bunge mara baada ya Bunge kuahirishwa kesho jioni. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote ni Usiku wa Mwanamke wa Bunge lakini Wabunge Wanaume wote mnaalikwa na mnatarajiwa wote kuhudhuria. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa Mwenyekiti anakuja kuendelea na ratiba. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Daniel S. Baran) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini awasilishe maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Madini - Fungu 100 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa. Mimi pamoja na Wajumbe wa Kamati tunawahakikishia ushirikiano katika kuliendesha Bunge letu. Aidha, kipekee napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa imani kubwa waliyonipa mimi na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula kwa kuona tunafaa

kuwaongoza katika kutekeleza majukumu ambayo tumekasimiwa. Tunawaahidi ushirikiano na tutahakikisha Kamati yetu inatekeleza majukumu yake kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri unaostahili kwa Wizara hii na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini - Fungu 100 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti Pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo na Kamati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ; uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulijikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023; Kamati ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi miwili inayohusu Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi Wakala wa Jiolojia Nchini *(GST)* Dodoma na Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia *(coal Briquette)* Msasani, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi wa Wakala wa Jiolojia Nchini *(GST);* katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya mradi

huu na kufikia Februari, 2023 shilingi bilioni 1.66 zilipelekwa na kuwezeshwa ununuzi wa vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ambayo *GST* imepata kutokana na upatikanaji wa fedha, lakini bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama inavyoonekana kwenye taarifa ukurasa wa tano, zikiwemo za miundombinu chakavu na ufinyu wa bajeti. Kamati ilishuhudia miundombinu ambayo haiendani na kazi inayofanywa na Taasisi hii. Asili ya kazi za maabara za taasisi kama hii zinapaswa kuwa na kamera ambazo wakati Kamati inatembelea hazikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ukaguzi wa Mradi ya Makaa ya Mawe ya Kupikia *(coal briquette)* Msasani, Jijini Dar es Salaam, Mradi wa Makaa ya Mawe ya kupikia ambao unatekelezwa na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* katika eneo la Msasani, Dar es Salaam, unahusika na kutengeneza mkaa usiokuwa na moshi *(Smokeless Briquette)* na pia usiyokuwa na harufu, wala hewa chafu na wenye kuwaka kiurahisi. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati mbadala ili kupunguza ukataji wa miti ambao umeleta madhara makubwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, shilingi bilioni 1.66 zilitengwa na wakati Kamati inatembelea mradi mwezi Machi, 2023, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepelekwa. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa *STAMICO* iliendelea kufanya shughuli za kiwanda kwa kutumia mapato ya ndani ambapo jumla ya shilingi milioni 260, zimetumika. Kamati inashauri fedha zilizotengwa zitoke kabla mwaka huu wa fedha haujakwisha ili mradi uweze kutekelezwa kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wastani wa upatikanaji wa fedha kwa Miradi hiyo miwili ambayo Kamati

ilitembelea ni asilimia 33.3 kama inavyoonekana kwenye kielelezo namba moja ukurasa wa nane wa Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati.

(a) Kwa kuwa Mradi wa ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi Wakala wa Jiolojia Nchini *(GST)* umeonyesha kuleta tija katika kuboresha kazi za *GST* ipo haja ya Wizara kufanya yafuatayo: -

i) Kuboresha mazingira na miundombinu ya *GST* ikiwemo Maabara ambayo hayaridhishi; na

ii) Katika kujenga imani zaidi na kuweka uwazi wa upimaji wa sampuli, *GST* ifunge Kamera katika maeneo yote ya maabara.

(b) Kwa kuwa Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia ni moja kati ya miradi yenye faida kiuchumi na kimazingira:-

i) Ni vyema Serikali ikasimamia kikamilifu ufungwaji wa Mitambo mipya na kuhakikisha inaanza kazi kwa wakati;

ii) Wizara ya Madini, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira zinapaswa kuwa na mwelekeo wa pamoja katika kuhakikisha mkaa huu unaleta tija kwa ustawi wa wananchi na mazingira;

iii) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha miradi hii zitoke zote na kwa wakati; na

iv) *STAMICO* ihakikishe Mkaa wa *coal briquette* unakuwa na ubora na unakidhi vigezo vya soko ikiwemo kuwaka kwa urahisi, kutokuwa na moshi, harufu na hewa chafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; Kamati imefanya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara na kubaini kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji unaridhisha. Kutokana na mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa tisa hadi wa 10. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa ambapo umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 7.8 mwaka 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 9.7 mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Madini ilipangiwa kukusanya Maduhuli yenye thamani ya Shilingi Bilioni 894.27 kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kufikia februari, 2023 Shilingi Bilioni 457.23 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 55.6 na kuwasilishwa Hazina ambayo ni chini ya wastani kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.3 cha Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa makusanyo ya Taasisi zilizo chini ya Wizara, Shilingi Bilioni 33.33, sawa na asilimia 46.12 zilikusanywa kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilihoji sababu za makusanyo kutofikia lengo na ilielezwa sababu mbalimbali kama inavyoonekana Taarifa ya Kamati ukurasa wa 11 hadi 13. Kamati inasisitiza Wizara kuhakikisha kufikia tarehe 30 Juni, 2023, lengo la makusanyo liwe limefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 kuhusu upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Madini ilihidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya

Shilingi Bilioni 83.44 na kufikia Februari 2023 Wizara imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 42.88, sawa na asilimia 51.3 ya Bajeti yote iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye kiambatanisho Na.5 cha Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Miradi ya Maendeleo imepokea asilimia 20.9 tu. Kamati inatoa rai kwa Wakandarasi kutekeleza kazi kwa wakati na kuwasilisha hati za madai mapema ili kulipwa. Aidha, mapungufu yote yaliyojitokeza katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yafanyiwe kazi ili kuwezesha utekelezaji bora wa miradi hii kwa maendeleo ya sekta na kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; katika Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa jumla ya maoni tisa ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla. Kamati imepitia Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati na kubaini kwa kiasi kikubwa Wizara imezingatia na kutekeleza vizuri. Kwa ambayo bado, Kamati inaendelea kusisitiza yafanyiwe kazi kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati, ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha uliopita 2022/2023. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa fedha 2023/2024; Kamati imepitia vipaumbele vya Wizara na kubaini kuwa vipaumbele hivyo kwa mwaka 2022/2023 vilikuwa saba na kwa Mwaka 2023/2024 vipaumbele ni sita kikiwemo kipaumbele kipya kimoja kinachohusu kuendeleza utafutaji na utafiti wa Madini ya Kimkakati. Maelezo ya kina ni kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Wizara kwa kuakisi utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mpango wa Maendeleo kwa kuwa suala hili litasaidia mpango bora na wa muda mrefu wa madini muhimu ambayo yamekuwa na soko kubwa duniani na pia ni muhimu katika kuelekea kwenye nishati safi. Rai ya Kamati kuwa utekelezaji wa mkakati huu usimamiwe kikamilifu na kupewa uzito wa kipekee kwa manufaa mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Madini inakadiria kukusanya Shilingi Trilioni 1.006 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.6 cha Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Makadirio hayo yameongezeka kwa asilimia 12.5 ikilinganishwa na mwaka 2022/2023 kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.7 cha Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo la makadirio ya makusanyo kwa ujumla hasa ikizingatiwa kuwa kufikia Februari, 2023, wastani wa lengo la makusanyo kwa makadirio ya mwaka 2022/2023 lilikuwa halijafikiwa. Wizara ilieleza sababu mbalimbali kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Madini inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 89.35. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.17 ni kwa ajili ya Maendeleo; shilingi bilioni 20.30 kwa ajili ya Mishahara; na shilingi bilioni 45.87 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha Bajeti ya Wizara kati ya mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 na imebaini kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa asilimia 7.08 kama inavyooneka kwenye kielelezo namba tisa. Maelezo ya kina kuhusu bajeti hii ni kama inavyooneka kwenye Taarifa ya Kamati ukurasa wa 21 hadi 22. Ni rai ya Kamati kuwa miradi hii itekelezwe na kusimamiwa vizuri na kwa ufanisi ili kuwezesha ukuaji zaidi wa Sekta ya Madini na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa; Kamati imefanya uchambuzi wa kulinganisha asilimia ya Bajeti ya Wizara hii dhidi ya Bajeti ya Taifa kati ya mwaka 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kuwa pamoja na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 kuongezeka kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na mwaka uliopita asilimia ya Bajeti ya Wizara ya Madini - Fungu 100 dhidi ya Bajeti ya Taifa imebaki kuwa ni ileile ya mwaka uliopita ambayo ni asilimia 0.20, kama inavyoonekana kwenye kielelezo Na. 10 cha Ripoti ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara ambayo ina mchango mkubwa kwenye pato la Taifa ambayo pia inakabiliwa na changamoto nyingi katika Taasisi zake ambazo ndizo zinazochangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Baada ya uchambuzi huo. Ufafanuzi wa yale yote yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Bajeti, Kamati inatoa maoni ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa bajeti ya 2022/2023 umekuwa chini ya malengo na hususan mradi wa jengo la Kituo cha Jemolojia Tanzania (*TGC)*. Ni vyema tathmini ya kutosha ikafanyika kabla ya kuanza utekelezwaji wa miradi hii ili kuwezesha kukamillka kwa wakati bila kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo katika Halmashauri. Kutokana na baadhi ya Halmashauri kutunga Sheria Ndogo *(By Laws)* zinazohusu tozo mbalimbali ambazo baadhi zinakinzanna na Sheria Mama na hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa wachimbaji wa madini wakimwemo wa madini wa ujenzi na viwandani, Serikali ifanyie kazi na kuondoa mgongano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa watumishi. Kwa kuwa kuna uhaba wa watumishi katika Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara kama Wakala wa Jiolojia *(GST)*, Shirirka la Madini *STAMICO* na kituo cha Jemologia *(TGC*), mamlaka husika zichukue suala hili kwa uzito wa kipekee na kuhakikisha vibali vya ajira vinatoka ili Taasisi hizi ambazo zinajiendesha kibiashara ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za ununuzi wa umma kuchukua muda mrefu. Kamati imebaini moja ya changamoto inayokwamisha utendaji wa taasisi nyingi nchini ni taratibu za ununuzi ambazo zinachukua muda mrefu. Ni wakati muafaka sasa sheria hii ifanyiwe marekebisho ili kuondoa changamoto hiii

na kuwezesha taasisi zinazojiendesha kibiashara kuweza kushindana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Madini la Taifa - *STAMICO*. Ili kufikia lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira na kuhakikisha mkaa wa *coal briquette* unawafikia wananchi wengi, *STAMICO* ihakikishe inaweka mazingira rahisi kwa mawakala ikiwa ni pamoja na kuondoa masharti magumu kama vile dhamana ya shilingi 50,000,000. Aidha mawakala waruhusiwe kununua mkaa kwa thamani halisi ya mzigo. Wizara zinazohusika na Mazingira na Madini na TAMISEMI ziwe na muelekeo wa pamoja kuhakikisha mkaa huu wa *coal briquette* unaleta manufaa katika kuokoa mazingira na kuwainua wananchi kiuchumi ili kuendana na malengo mahsusi ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2021/2022 hadi 2025/2026 Sura ya Kwanza, Sehemu ya Kwanza kipengele cha Saba unaolenga kuongeza kasi ya ukuaji uchumi jumuishi na shirikishi kupitia mikakati ya kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya jamii pamoja na uwezo wa uzalishaji kwa vijana, wanawake na makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inarejea ushauri wake wa mwaka 2022 kuhusu *STAMICO* kuongeza juhudi za ulipaji madeni ambayo *STAMIGOLD* inadaiwa na wazabuni. Aidha, Serikali ione namna ya kulichukua deni hilo kwa kuhakikisha juhudi zinazoendelea na utekelezaji wake zinakamilika kwa haraka. *STAMICO* ihakikishe mitambo ya uchorongaji inayotarajia kufika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024, mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, izingatie mgawanyo kwenye maeneo yenye uhitaji kwa uwiano unaofaa. Aidha gharama za utumiaji wa mitambo hiyo ziwe rafiki kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *STAMICO* ishirikiane na *TANESCO* ili kuwa na mkakati wa kutumia makaa ya mawe katika kuzalisha umeme na kuhusu uunganishaji wa umeme kwa mgodi wa

*STAMIGOLD,* kwa kuwa kwa taarifa ya Waziri kuanzia jana mgodi wa *STAMIGOLD* umeanza kutumia umeme wa *TANESCO,* napenda kuipongeza Wizara kwa kuingiza umeme katika mgodi wa *STAMIGOLD* jambo litakalopelekea kupunguza gharama kubwa za nishati ya *diesel* iliyokuwa inatumika kuendesha mitambo hiyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Madini. Kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa. Ukaguzi na usimamizi wa miradi mipya ya uwekezaji katika madini uimarishwe. Tathimini ya athari za kimazingira ifanyike kwa mabwawa yote ya tope na tope sumu, zinazoweza kutokea iwapo yataharibika ama yatapasuka. Aidha, Wizara ihakikishe kwamba inakamilisha mapitio ya kanuni za usalama afya na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kuwa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya uendelezaji wa madini ya aina mbalimbali, kuendelea kuwaumiza wananchi wanaomiliki maeneo hayo kutokana na fidia zisizoendana na uhalisia. Serikali ihakikishe inasimamia suala hili ili fidia ziendane na tathmini halisi ya eneo. Aidha, Wizara inaweza kufikiria na kufanya kazi na wananchi ambao wako tayari kupewa hisa *(free carried interest)* katika maeneo yao wanayopisha. Ili kupunguza changamoto za baadhi ya wamiliki wa leseni kuwafukuza wananchi katika maeneo yao, elimu itolewe kwao ili wafahamu umuhimu wa kukubaliana *(sound negotiation*) na wananchi ili kupisha maeneo yao kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Jiolojia nchini (*GST)*. Ujenzi wa Ofisi za Kanda upewe kipaumbele hii itasaidia kusogeza huduma karibu Zaidi na jamii na kufikia wahitaji wengi zaidi. Ili kuongeza usalama na imani kwa wateja Wakala wa Jiolojia nchini Wakala ihakikishe inaimarisha mifumo ya usalama kwa kufunga kamera katika maabara zake. Pia *GST* ijitangaze zaidi

hasa baada ya kuboresha huduma zake kwa kununua vifaa vipya vyenye ubora. Elimu hii izingatie zaidi maeneo yenye wateja wa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Jemolojia Tanzania (*TGC*). Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majengo ya *TGC*, ni rai ya Kamati kuwa utekelezaji wa mradi huu uende kwa kasi na kukamilika kwa wakati ili kuondoa changamoto ya miiundombinu duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Spika wetu Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Waziri wa Madini Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko na Naibu Waziri Dkt. Steven Lemomo Kiruswa pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Heri Mahimbali kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati muda wote. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Katibu Mkuu kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kwa nafasi hiyo. Kamati itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kufikia malengo ya Wizara na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, namshukuru pia Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Kipekee zaidi nawashukuru sana Makatibu wa Kamati ya Nishati na Madini, Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Onesmo Laulau, Ndugu Jesca Sanga na Msaidizi wa Kamati Ndugu Rukia Shabani kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini - Fungu 100 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mhe Najma Murtaza Giga (Mb), Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb) na Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb) kwa kuchaguliwa kuwe Wenyeviti wa Bunge. Mimi pamoja na

Wajumbe wa Kamati tunawahakikishia ushirikiano katika kuliendesha Bunge letu. Aidha, kipekee napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini kwa imani kubwa waliyonipa mimi na Mwenyekiti wangu Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb) na kuona tunafaa kuwaongoza katika kutekeleza majukumu ambayo wewe Spika umetukasimu. Tunawaahidi ushirikiano na tutahakikisha Kamati yetu inatekeleza majukumu yake kwa maslahi ya nchi kwa kutoa ushauri unaostahili kwa Wizara hii na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023[1], naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa Bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yameelezwa katika Fasili ya 7(1)(a) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023[2].

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na muundo wa taarifa;

---

[1] Baada ya Waziri kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mujibu wa fasili (1), Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika thelathini kila mmoja

[2] 7,-(1) Majukumu ya Kamati za Kudumu ya Bunge za Kisekta yatakuwa yafuatayo:-

(a) Kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

b) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

d) Sehemu ya Nne ni Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulijikita katika maeneo makuu matano (5) kama ifuatavyo:-

a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023;

b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

c) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli;

d) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 kuhusu upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023; na

e) Uchambuzi wa utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## 2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Iliyotengewa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023[3], Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Madini. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 14 na 21 Machi 2023 katika Mkoa wa Dodoma na Dar Es Salaam mtawalia ambapo Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi miwili ifuatayo:-

a) Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi – GST, Dodoma (Mradi Na. 1119); na

b) Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briquette*) – Msasani, Dar Es Salaam (Namba ya Mradi 1119).

### 2.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

### a) Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi – GST, Dodoma (Mradi Na. 1119)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi katika Taasisi ya Jiolojia Tanzania (GST) unalenga katika kuboresha upimaji wa sampuli. Maabara ya GST imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni Sehemu ya Kemia na Sehemu ya Utambuzi miamba na Uchenjuaji Madini.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bunge liliidhinisha **Shilingi Bilioni 2.4** kwaajili ya mradi huu na hadi kufikia

[3] 117.-(1) Baada ya kuwasilishwa kwa mapendekezo ya mpango na kiwango cha ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa Wabunge, Kamati za Bunge za kisekta zitatembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa siku zisizozidi saba.

Februari 2023 kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.66** sawa na **asilimia 69.1** kilikuwa kimepokelewa. Kupitia fedha hizo, maabara ya GST ilipata mashine na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uchunguzi na utambuzi wa sampuli za madini, uchenjuaji madini pamoja na utambuzi wa tabia za miamba kwa ajili ya shughuli za uchimbaji na ujenzi. Mashine na Vifaa hivyo ambavyo Kamati iliviona vimesaidia katika kuongeza na kuboresha utendaji kazi kwa kuongeza idadi ya wateja, idadi ya sampuli za uchunguzi na kuongeza makusanyo ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ambayo GST imepata kutokana na upatikanaji wa fedha, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama:-

i) Taratibu za ununuzi wa Umma kuchukua muda mrefu na hivyo kukwamisha utekelezaji bora wa majukumu ya Taasisi;

ii) Upungufu wa watumishi;

iii) Miundombinu chakavu ya Maabara hasa majengo na mifumo yake ya maji na umeme; na

iv) Ufinyu wa bajeti katika kuwezesha kazi za Maabara.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyobainishwa kwenye changamoto, kazi inayofanywa na GST ni kubwa hata hivyo, mazingira ya Maabara hayaridhishi. **Kamati imeshuhudia miundombinu chakavu ambayo haiendani na kazi inayofanywa na taasisi hii. Asili ya kazi za maabara za Taasisi kama hii zinapaswa kuwa na kamera ili kuongeza ubora, lakini wakati Kamati inatembelea hazikuwepo.**

**b) Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briquette*) – Msasani, Dar Es Salaam (Namba ya Mradi 1119)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Makaa ya Mawe ya kupikia ambao unatekelezwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) katika eneo la Msasani, Dar Es Salaam, unahusika na kutengeneza mkaa usiokuwa na moshi (*smokeless briquette)*, harufu, wala hewa chafu na wenye kuwaka kirahisi. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa nishati mbadala ili kupunguza ukataji wa miti ambao umeleta madhara makubwa kwenye mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka huu wa fedha 2022/2023, STAMICO ilitengewa **Shilingi Bilioni 1.66** kwa ajili ya uendelezaji wa mradi huu. Kufikia Machi 2023 wakati Kamati inatembelea mradi huu, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepokelewa. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa STAMICO iliendelea kufanya shughuli za kiwanda kwa kutumia mapato ya ndani ambapo jumla ya **Shilingi Milioni 260** zimetumika. **Kamati inashauri fedha hizi zitoke kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha ili mradi uweze kutekelezwa kama ulivyopangwa.**


**Mheshimiwa Spika**, tangu kuanza kwa uzalishaji wa majaribio *(Pilot Plant)* Aprili, 2022 kufikia Februari 2023, jumla ya **tani 556** zimezalishwa za mkaa huu. Aidha, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji Shirika limeagiza mitambo minne (4) ya uzalishaji yenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa saa kila mmoja. Mitambo miwili imeshafika nchini na maandalizi ya maeneo ya kusimika mitambo yanaendelea katika eneo la Kiwira – Mbeya na Mkoa wa Pwani. Aidha, mitambo mingine miwili inatarajiwa kufika kabla ya Mwaka huu wa Fedha 2022/2023 kuisha na itasimikwa katika Mkoa wa Geita na Dodoma. Shirika pia linatarajia kuongeza mitambo mingine zaidi ya minne na kuweka katika maeneo mengine ya nchi katika mwaka wa fedha 2023/2024. **Ni rai ya**

**Kamati kuwa mipango hii itekelezwe kama ilivyopangwa ili kupunguza kasi ya ukataji miti nchini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua na jitihada mbalimbali ilizochukua zikiwemo za kuanza kuwasili kwa mitambo miwili. Ni imani ya Kamati kuwa matakwa ya Ilani ya uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 Uk.108 sehemu ya 65 (n) ***Serikali ya CCM itahakikisha sekta ya Madini inachangia zaidi katika Pato la Taifa na kupunguza umaskini nchini na ili kufikia malengo hayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaimarisha Shirika la STAMICO ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.*** **Hivyo Kamati inaona ni muhimu STAMICO kuhakikisha mradi huu unaleta ustawi wa wananchi na kukuza Pato la Taifa kwa ujumla.**

**Mheshimiwa Spika**, wastani wa upatikanaji wa fedha kwa miradi hiyo miwili (2) ambayo Kamati iliitembelea ni **asilimia 33.3** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.1.

**Kielelezo Na. 1: Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati kufikia Februari, 2023**




***Chanzo: Taarifa ya Wizara ya Madini na usanifu wa Kamati***

### 2.1.2 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati

a) Kwa kuwa Mradi wa Ununuzi wa Vifaa vya Jiosayansi – GST umeonyesha kuleta tija katika kuboresha kazi za GST ipo haja Wizara kufanya yafuatayo:-

i) Kuboresha mazingira na miundombinu ya GST ikiwemo Maabara ambayo hayaridhishi; na

ii) Katika kujenga imani zaidi na kuweka uwazi wa upimaji wa sampuli, GST ifunge Kamera katika maeneo yote ya maabara.

b) Kwa kuwa Mradi wa Makaa ya Mawe ya Kupikia (*Coal Briquette*) ni moja kati ya miradi yenye faida kiuchumi na kimazingira:-

i) Ni vyema Serikali ikasimamia kikamilifu ufungwaji wa Mitambo mipya na kuhakikisha inaanza kazi kwa wakati;

ii) Wizara ya Madini, TAMISEMI na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira zinapaswa kuwa na mwelekeo wa pamoja katika kuhakikisha Mkaa huu unaleta tija kwa ustawi wa Wanachi na mazingira;

iii) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanikisha miradi hii muhimu zitoke zote na kwa wakati; na

iv) STAMICO ihakikishe Mkaa wa *coal briquette* unakuwa na ubora na unakidhi vigezo vya soko ikiwemo kuwaka kwa urahisi, kutokuwa na moshi, harufu na hewa chafu.

**2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Madini inajukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Madini nchini kwa kuweka mifumo madhubuti kwa ajili ya kusimamia ufuatiliaji, uchimbaji, uongezaji thamani na biashara ya madini kwa lengo la kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa unaongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ilijiwekea vipaumbele saba (7) vifuatavyo ambavyo pia vimeelezwa na Waziri mwenye dhamana: -

i) Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa;
ii) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi wa madini;
iii) Kuhamasisha shughuli za uongezaji thamani madini;
iv) Kuhamasisha biashara na uwekezaji katika Sekta ya Madini;
v) Kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi;
vi) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na
vii) Kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa vipaumbele hivi na kubaini kuwa, kwa kiasi kikubwa utekelezaji unaridhisha. Kwa mfano, Wizara imefanikiwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, masoko ya madini, vituo vya uuzaji wa madini pamoja na mipaka ya nchi. Juhudi hizo zimesaidia katika kuimarisha mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa kutoka wastani wa asilimia 7.8 Mwaka 2021 hadi kufikia wastani wa asilimia 9.7 Mwaka 2022 katika kipindi kama hicho. Mwenendo huu wa mchango unatoa mwelekeo chanya kuwa Sekta ya Madini itaweza kuchangia

asilimia 10 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua hii muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) imefanikiwa kuimarisha na kutanua wigo wa shughuli zake kwa kuimarisha shughuli za uchorongaji kwa kuongeza kununua mitambo ya kazi hizo ambayo imesaidia Shirika kupata kandarasi na Mgodi wa GGM wenye thamani ya Shilingi Bilioni 55.2 na kazi nyingine nyingi. Hii ni kutokana na imani ya makampuni hayo kwa STAMICO.

**Mheshimiwa spika** katika kipaumbele cha kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi katika kudhibiti vitendo mbalimbali vya utoroshaji madini, Wizara imefanikiwa kukamata madini yenye thamani ya **Shilingi 393,948,829.15** Mwaka 2022/2023 katika mikoa ya Dar Es Salaam, Mwanza, Mbeya, Kahama, Songwe na Singida. Takwimu hizi zinaonyesha kushuka kwa matukio hayo ambayo Mwaka 2021/22 kipindi kama hicho madini yenye thamani ya **Shilingi 501,223,895.65** yalikamatwa hivyo matukio ya utoroshaji yanaonyesha kushuka kwa **asilimia 78.5. Kamati inasisitiza Wizara kuendelea kuboresha mifumo ya udhibiti matukio ya utoroshaji ili kuhakikisha Madini yananufaisha nchi na kukuza Pato la Taifa.**

**Kielelezo Na. 2: Madini yaliyokamatwa katika matukio mbalimbali ya utoroshaji**




***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara na usanifu wa Kamati***

**2.3 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** ilipangiwa kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 894,278,406,800.00** kutoka vyanzo vyake mbalimbali. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 822,028,205,000.00** zilipangwa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina na **Shilingi 72,250,201,800.00** zilipangwa kukusanywa na kutumiwa na taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha ambazo zilipaswa kukusanywa na kuwasilishwa Hazina kufikia Februari 2023 **Shilingi 457,238,525,245.70** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 55.6** ambayo ni chini ya wastani kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3**.

**Kielelezo Na. 3: Ukusanyaji wa Maduhuli kufikia Februari, 2023**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI KUFIKIA FEBRUARI 2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **MAKADIRIO** | **MAKUSANYO** | **ASILIMIA** |
| **Mapato mengineyo** | 2,000.00 | 0 | - |
| **Marejesho ya fedha za Serikali** | 10,000,000.00 | 5,221,553.00 | **52.22** |
| **Ada ya Mwaka ya Leseni** | 37,298,204,306.00 | 19,429,797,387.01 | **52.09** |
| **Ada ya Ukaguzi** | 109,154,809,317.00 | 68,109,107,689.11 | **62.4** |
| **Ada za kijiolojia** | 15,680,436,817.00 | 5,901,272,774.38 | **37.63** |
| **Mrabaha** | 655,666,352,351.00 | 361,808,789,510.67 | **55.18** |
| **Adhabu na Faini za Malimbikizo ya Ada** | 3,618,400,209.00 | 1,704,341,399.67 | **47.1** |
| **Malipo ya huduma za Maabara** | 600,000,000.00 | 279,994,931.86 | **46.67** |
| **JUMLA** | **822,028,205,000.00** | **457,238,525,245.70** | **55.62** |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa KamatI***


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo madogo ambayo yamesababisha Wizara kushindwa kufikia wastani wa makusanyo wa angalau **asilimia 66.6** mwezi Februari 2023 na ilielezwa sababu mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Kushushwa kwa asilimia ya tozo za mrabaha kwa madini ya viwandani na nishati yanayouzwa nchini kutoka **asilimia 3 hadi asilimia 1;** na

b) Kusimama uzalishaji kwa baadhi ya migodi kutokana na sababu mbalimbali kama vile: uwepo wa maji mengi chini ya ardhi; Mgodi wa Sunshine kuathiriwa na changamoto ya umeme; kusimama kwa uzalishaji kwa mgodi wa Edenville kutokana na mgogoro wa umiliki; Kusimama kwa uzalishaji katika mgodi wa Williamson Diamonds Limited (Kishapu) na kuchelewa kuanza kwa uzalishaji wa Miradi mipya ya Pu Bo Mining (Singida), Shanta Mining (Singida) na Lindi Jumbo (Lindi).

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa makusanyo ya **Shilingi 72,250,201,800.00** ambayo yalipangwa kukusanywa na kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara, kufikia Februari 2023 **Shilingi 33,324,065,932.50** sawa na **asilimia 46.12** zilikuwa zimekusanywa kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.4.**

**Kielelezo Na. 4: Ukusanyaji wa maduhuli ya Taasisi kufikia Februari, 2023**




***Chanzo: Taarifa ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji sababu za makusanyo hayo ya Taasisi kutofikia lengo na ilielezwa ni kutokana na sababu zifuatazo:-

a) STAMICO: Kuchelewa kufika kwa mitambo miwili (2) ya kuzalisha mkaa mbadala wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briquettes*) kutokana na changamoto za Uviko 19 nchini China inakotengenezwa mitambo hiyo*;*

b) GST: Kushindwa kuanza uzalishaji na uuzaji wa vyungu vya kuyeyushia dhahabu (*crucibles*); na

c) TGC: Malipo ya ada za mafunzo na michango mingine hufanyika katika kipindi cha Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaisisitiza Wizara kuhakikisha kufikia 30 Juni, 2023 lengo la Makusanyo liwe limefikiwa na hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya changamoto ambazo Kamati imeelezwa zimeshaanza kupatiwa utatuzi.


## 2.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 kuhusu upatikanaji wa fedha kufikia Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** ambayo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 83,445,260,000.00**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 40,835,660,000** sawa na **asilimia 48.9** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC), **Shilingi 20,609,600,000.00** sawa na **asilimia 24.6** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi(PE) na **Shilingi 22,000,000,000.00** sawa na **asilimia 26.3** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kufikia Februari, 2023, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 42,886,208,301.01** sawa na **asilimia 51.3** ya bajeti yote iliyoidhinishwa[4]. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya fedha hizo zilizopokelewa, Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 24,890,765,885.89** sawa na **asilimia 60.9**, Mishahara **Shilingi 13,398,616,582.24** sawa na **asilimia 65** na Miradi ya Maendeleo **Shilingi 4,596,825,832.88** sawa na **asilimia 20.9** ya bajeti iliyoidhinishwa kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na.5.**

[4] Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023: Fedha zilizopokelewa kufikia Februari 2023 uk.3

**Kielelezo Na. 5: Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2023**




| | Matumizi Mengineyo (OC) | Mishahara ya Watumishi (PE) | Miradi ya Maendeleo |
|---|---|---|---|
| KILICHOIDHINISHWA | 40,835,660,000.00 | 20,609,600,000.00 | 22,000,000,000.00 |
| KILICHOPOKELEWA | 24,890,765,885.89 | 13,398,616,582.24 | 4,596,825,832.88 |
| ASILIMIA | 60.95 | 65.01 | 20.89 |

***Chanzo: Taarifa ya utekelezaji ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini sababu mbalimbali zilizochangia Miradi ya Maendeleo kupata fedha kwa wastani wa **asilimia 20.9** kuwa ni pamoja na kutowasilishwa kwa hati za madai ya kandarasi mbalimbali. **Kamati inatoa rai kwa Wakandarasi kutekeleza kazi kwa wakati na kuwasilisha hati za madai mapema. Aidha, mapungufu yote yaliyojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yafanyiwe kazi ili kuwezesha utekelezaji bora wa miradi hii kwa maendeleo ya Sekta na kwa uchumi wa Taifa.**

### 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa jumla ya maoni 9 ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla. **Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na kubaini kwa kiasi**

**kikubwa Wizara imezingatia na kutekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati. Kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati inasisitiza Wizara kufanyia kazi ushauri huo wa Kamati. Kwa mfano suala la Uunganishaji wa Mgodi wa STAMIGOLD Bulyanhulu katika Gridi ya Taifa , Kamati imeelezwa kuwa Ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme (sub-station) umekamilika. Hatua inayoendelea ni TANESCO kwa kushirikiana na Mkandarasi TANELEC kuweka miundombinu wezeshi kwenye kituo hicho ambapo kazi imekamilika kwa asilimia 90.15 na kwamba umeme unatarajiwa kuwashwa kwa majaribio ya uzalishaji mgodini mwishoni mwa mwezi huu wa Aprili 2023. Ni rai ya Kamati kuwa umeme uwashwe STAMIGOLD ili kupunguza gharama ya kununua mafuta ya dizeli kuendesha mitambo.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA WIZARA YA MADINI (FUNGU 100) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini **(Fungu 100)** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha uliopita (2022/2023)[5].Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

[5] Baada ya kutembelea miradi, Kamati za Bunge za Kisekta, kwa kipindi kisichozidi isku tisa, zitafanya vikao vya kuchambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoisha na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa fedha unaofuata.

b) Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

d) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

### 3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 umebaini kuwa, Wizara imezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025[6] na Sera ya Madini ya Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha mipango hiyo inatekelezwa kikamilifu, Kamati imepitia vipaumbele vya Wizara na kubaini kuwa vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka 2022/2023 vilikuwa Saba (7) na kwa Mwaka 2023/2024 vipaumbele ni sita (6).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata nafasi ya kuhoji sababu ya mabadiliko hayo ya vipaumbele na ilielezwa kuwa vipaumbele ambavyo havionekani katika Mwaka huu wa fedha ni Kipaumbele Na. 5 kinachohusu kusimamia mfumo wa ukaguzi wa shughuli za migodi ambacho kinatekelezwa na Tume ya Madini kupitia maeneo yaliyobainishwa katika vipaumbele vyake. Hivyo, Wizara itaendelea kuhakikisha Tume inatekeleza ipasavyo kipaumbele hicho. Aidha, kipaumbele cha kuendeleza rasilimaliwatu na kuboresha mazingira ya kufanya kazi ni

[6] Ilani ya Chama cha Mpainduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 (Uk. 108 -110).

endelevu na ni mtambuka hivyo uendelezaji rasilimaliwatu utatekelezwa kupitia malengo ya Wizara kwa Mwaka 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika** Kamati iliweza kubaini pia kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kuna kipaumbele kipya (Namba 2) ambacho hakikuwepo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kinachohusu *"kuendeleza utafutaji na utafiti wa Madini ya Kimkakati"*. **Kamati inaipongeza Wizara kwa kuakisi utekelezaji wa Ilani ya CCM na Mpango wa Maendeleo kwani suala hili litasaidia mpango bora na wa muda mrefu wa madini muhimu ambayo yamekuwa na soko kubwa Duniani na pia ni muhimu katika kuelekea kwenye Nishati safi. Ni Rai ya Kamati kuwa, utekelezaji wa Mkakati huu usimamiwe kikamilifu na kupewa uzito wa kipekee kwa manufaa mapana ya nchi yetu.**

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,006,705,169,300.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 822,128,205,000.00** sawa na **asilimia 81.6** zitakusanywa kupitia Idara, Vitengo vya Wizara na Tume ya Madini na zitawasilishwa Hazina**.** Aidha**, Shilingi 124,576,964,300.00** sawa na **asilimia 12.3** zitakusanywa na kutumika na Taasisi zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 6.**

**Kielelezo Na. 6: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli 2023/2024**

| Maduhuli yatakayokusanywa na Kuwasilishwa Hazina | | |
|---|---|---|
| **CHANZO** | **2023/2024** | **ASILIMIA** |
| **WIZARA** | 7,000,000.00 | **0** |
| **TUME YA** | 882,121,205,00 | **87.6** |

| | | |
|---|---|---|
| **MADINI** | 0.00 | |
| **Jumla Ndogo** | **882,128,205,000.00** | **87.6** |
| | | |
| **Maduhuli yatakayokusanywa na Kutumika na Taasisi** | | |
| **CHANZO** | **2023/2024** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 122,091,964,300.00 | **12.1** |
| **GST** | 2,235,000,000.00 | **0.22** |
| **TGC** | 250,000,000.00 | **0** |
| **Jumla Ndogo** | **124,576,964,300.00** | **12.3** |
| **JUMLA KUU** | **1,006,705,169,300.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio hayo yameongezeka kutoka **Shilingi 894,278,406,800.00** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 1,006,705,169,300.00** Mwaka 2023/2024 ambayo ni ongezeko la **Shilingi 112,426,762,500.00** sawa na **asilimia 12.5** kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo na. 7.** Ongezeko zaidi linaonekana STAMICO kwa **asilimia 74.2** kutoka **Shilingi 70,047,726,800.00** kufikia **Shilingi 122,091,964,300.00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo la makadirio ya makusanyo kwa ujumla hasa ikizingatiwa kuwa kufikia Februari 2023, wastani wa lengo la makusanyo kwa Makadirio ya Mwaka 2022/2023 lilikuwa halijafikiwa. Wizara ilieleza miongoni mwa sababu zilizofanya ongezeko la makadirio ya makusanyo ni pamoja na:-

a) Kuanza uzalishaji kwa Mgodi wa Williamson Diamond Limited (WDL) na miradi ya Zem Shinyanga, Shanta Mine, Sunshine, Peponi, Pu Bo, Xinyuani Tanzania na Lindi Jumbo.
b) Kuanza uzalishaji wa kampuni zinazochimba madini ya Kinywe (Lindi Jumbo)
c) Kuongeza usimamizi wa madini ujenzi na Viwandani kwa kutumia mawakala na TAMISEMI
d) **STAMICO**: Kufanya huduma ya uchorongaji na ushauri wa kijiolojia, pamoja na mradi wa *Coal Briquette*
e) **GST:** Ada ya Ushauri Elekezi, Tozo za huduma za maabara na Tozo za ramani na machapisho ya jiosayansi.
f) **TGC:** Ada za wanafunzi Ngazi ya Cheti katika mafunzo ya ukataji na usanifu wa vito; na mauzo ya bidhaa na huduma.

**Kielelezo Na. 7: Ulinganisho wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**


| Maduhuli ya kuwasilishwa Hazina | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2022/2023** | **2023/2024** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **WIZARA/TUME YAMADINI** | 822,028,205,000 | 882,128,205,000.00 | 60,100,000,000.00 | 7.3 |
| **Maduhuli ya kutumika na Taasisi** | | | | |
| **CHANZO** | **2022/2023** | **2023/2024** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **STAMICO** | 70,047,726,800 | 22,091,964,300 | 52,044,237,500 | 74.2 |
| **GST** | 2,000,800,000 | 2,235,000,000 | 234,2000,000 | 11.7 |
| **TGC** | 201,675,000 | 250,000,000 | **48,325,000** | 9.7 |
| **Jumla Ndogo** | **72,250,201,800** | **124,576,964,300** | **24,770,604,333** | **34.2** |
| **JUMLA KUU** | **894,278,406,800** | **1,006,705,169,300** | **112,426,762,500** | **12.5** |

***Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Madini **(Fungu 100)** inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 89,357,491,000.00.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 23,172,550,000.00** sawa na **asilimia 26** ni kwa ajili ya Maendeleo na **Shilingi 66,184,941,000.00** sawa na **asilimia 74** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambazo zinajumuisha **Shilingi 20,307,498,000.00 (asilimia 23)** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 45,877,443,000.00 (asilimia 51)** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) kwa Wizara na Taasisi zake kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 8.**

**Kielelezo Na. 8: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**





***Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha bajeti ya Wizara kati ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024 na imebaini kwa ujumla bajeti imeongezeka kwa **asilimia 7.08** kutoka **Shilingi 83,445,260,000.00** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 89,357,491,000.00** Mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa fedha za Miradi ya Maendeleo zimeongezeka kutoka **Shilingi 22,000,000,000.00** Mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 23,172,550,000.00** Mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la **asilimia 5.3.** Ongezeko hilo litawezesha utekelezaji mzuri wa Miradi ya Usimamizi endelevu wa Rasilimali za Madini (SMMRP) ambapo itatumia **asilimia 69.7** ya Fedha zote za Maendeleo. Kupitia miradi hii Wizara imepanga kununua mitambo miwili (2) ya uzalishaji wa makaa ya mawe ya kupikia (*coal briqquette*) na ununuzi wa mtambo wa kuchakata madini ya chokaa (STAMICO); ununuzi wa vifaa vya maabara ya jiosayansi (*geoscientific equipment and tools*) na kusogeza huduma za ugani kwa wadau (GST); uanzishwaji wa minada ya madini ya vito, kujenga uwezo wa usimamizi endelevu wa Sekta ya Madini na ujenzi wa jengo la Afisa madini Mkazi Geita(Tume ya Madini). Aidha, fedha nyingine za maendeleo zimeelekezwa katika Mradi wa Kituo cha Jemolojia Tanzania (Tanzania Gemological Center-) ambao utatumia **asilimia 30.2** ya Bajeti yote ya Maendeleo. **Ni Rai ya Kamati kuwa Miradi hii itekelezwe na kusimamiwa vizuri na kwa ufanisi ili kuwezesha ukuaji zaidi wa Sekta ya Madini na kuongeza mchango katika Pato la Taifa.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Mishahara, Kamati imebaini imepungua kutoka **Shilingi 20,609,600,000.00** hadi kufikia **Shilingi 20,307,498,000.00** sawa na upungufu wa **asilimia 1.46** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 8. **Kamati ilihoji sababu za kushuka kwa bajeti ya Mishahara wakati bajeti zote zimepanda na ilifahamishwa kuwa upungufu huo unatokana na baadhi ya Watumishi kuhamishiwa Taasisi nyingine na wengine kustaafu**. **Kamati imeendelea kusisitiza Wizara kuziba mapema sehemu ambazo watumishi wake wameondoka kwa sababu tajwa ili kuondoa upungufu wa aina yoyote unaoweza kurudisha nyuma ufanisi na uwezo wa kiutendaji.**

**Kielelezo Na. 9: Ulinganisho wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**




***Chanzo: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati***

### 3.4 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti ya Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya madini inachangia sana katika pato la Taifa kama ambavyo imeonekana kufikia 2022 mchango ni **asilimia 9.7**. Kamati imefanya uchambuzi kwa kulinganisha asilimia ya Bajeti ya Wizara hii (Fungu 100) dhidi ya Bajeti ya Taifa kati ya Mwaka 2022/2023 na 2023/2024 na kubaini kuwa pamoja na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/2024 kuongezeka kwa **asilimia 7.0** ikilinganishwa na Mwaka 2022/2023, asilimia ya bajeti ya Wizara ya Madini (Fungu 100) dhidi ya bajeti ya Taifa imebaki kuwa ni ileile ya Mwaka 2022/2023 ambayo ni **asilimia 0.20** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 10. Aidha, Kamati imebaini kuwa OC imepungua kutoka **asilimia 0.91** hadi **asilimia 0.82**, Mishahara kutoka **asilimia 0.21** hadi asilimia **0.19,** Fedha za Maendeleo ndani zimeongezeka kutoka **asilimia 0.18** hadi

**asilimia 0.19** na Fedha za Maendeleo nje kutoka **asilimia 0** hadi **asilimia 0.04. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali ione umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Wizara hii yenye mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ambayo pia inakabiliwa na changamoto nyingi katika Taasisi ambazo ndiyo zinazochangia katika Pato la Taifa.**

**Kielelezo Na. 10: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara dhidi ya Bajeti Kuu ya Taifa 2022/2023 na 2023/2024**

| BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2022/2023 | | | |
|---|---|---|---|
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI MADINI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 4,493,500,000,000.00 | 40,835,660,000.00 | 0.91 |
| **MISHAHARA** | 9,740,800,000,000.00 | 20,609,600,000.00 | 0.21 |
| **MAENDELEO NDANI** | 12,122,100,000,000 | 22,000,000,000 | 0.18 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,399,200,000,000 | 0 | - |
| **DENI LA SERIKALI** | 11,308,400,000,000.00 | 0 | - |
| **JUMLA** | **41,064,000,000,000.00** | **83,445,260,000.00** | **0.20** |
| | | | |
| **BAJETI YA WIZARA DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2023/2024** | | | |
| **AINA** | **BAJETI TAIFA** | **BAJETI MADINI** | **ASILIMIA** |
| **OC** | 5,578,433,000,000 | 45,877,443,000.00 | 0.82 |
| **MISHAHARA** | 10,882,126,000,000 | 20,307,498,000 | 0.19 |
| **MAENDELEO NDANI** | 11,873,900,000,000 | 22,000,000,000 | 0.19 |
| **MAENDELEO NJE** | 3,282,100,000,000 | 1,172,550,000 | 0.04 |
| **DENI LA** | | 0 | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **SERIKALI** | 12,771,500,000,000 | | |
| **JUMLA** | **44,388,059,000,000.00** | **89,357,491,000.00** | **0.20** |

***Chanzo: Taarifa ya Mapendekezo ya Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24 na Randama ya Wizara ya Madini 2023/2024***

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi huo, ufafanuzi wa yale yote yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

### 4.1 MAONI YA JUMLA

#### 4.1.1 Kusuasua kwa utekelezaji kwa Miradi ya Maendeleo

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa bajeti ya 2022/2023 umekuwa chini ya malengo na hususan Mradi wa Jengo la TGC, ni vyema tathmini ya kutosha ikafanyika kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hii ili kuwezesha kukamilika kwa wakati bila kuchelewa.

#### 4.1.2 Tozo katika Halmashauri

Kutokana na baadhi ya Halmashauri kutunga Sheria ndogo (*by laws*) zinazohusu tozo mbalimbali ambazo baadhi zinakinzana na Sheria mama na hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa wachimbaji wa madini wakiwemo wa madini ya ujenzi na viwandani, Serikali ifanyie kazi na kuondoa mgongano huu.

#### 4.1.3 Uhaba wa Watumishi

Kuna uhaba wa Watumishi katika Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara kama vile GST, STAMICO na TGC. Mamlaka husika

zilichukue suala hili kwa uzito wa kipekee na kuhakikisha vibali vya ajira vinatoka ili Taasisi hizi ambazo zinajiendesha kibiashara ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

### 4.1.4 Taratibu za ununuzi wa Umma kuchukua muda mrefu

Kamati imebaini moja ya changamoto inayokwamisha utendaji wa taasisi nyingi nchini ni taratibu za ununuzi ambazo zinachukua muda mrefu. Ni wakati muafaka sasa Sheria hii ifanyiwe marekebisho ili kuondoa changamoto hii na kuwezesha Taasisi zinazojiendesha kibiashara kuweza kushindana.

## 4.2 SHIRIKA LA MADINI LA TAIFA (STAMICO)

**4.2.1** Ili kufikia lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira na kuhakikisha mkaa wa *coal briquette* unawafikia wananchi wengi, STAMICO ihakikishe inaweka mazingira rahisi kwa mawakala ikiwa ni pamoja na kuondoa masharti magumu kama vile dhamana ya Shilingi Milioni 50. Aidha, Mawakala waruhusiwe kununua mkaa kwa thamani halisi ya mzigo.

**4.2.2** Wizara zinazohusika na Mazingira, Madini na TAMISEMI ziwe na mwelekeo wa pamoja katika kuhakikisha mkaa huu wa *coal briquette* unaleta manufaa katika kuokoa mazingira na kuwainua wanachi kiuchumi ili kuendana na malengo Mahsusi ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo 2021/22 – 2025/26 Sura ya kwanza, sehemu 1.2 (viii) unaolenga "*kuongeza kasi ya ukuaji uchumi jumuishi na shirikishi kupitia mikakati ya kupunguza umaskini na kuleta maendeleo ya jamii pamoja na uwezo wa uzalishaji kwa vijana,wanawake na makundi maalumu*".

**4.2.3** Kamati inarejea ushauri wake wa mwaka 2022 kuhusu STAMICO kuongeza juhudi za ulipaji madeni ambayo STAMIGOLD inadaiwa na wazabuni. Aidha, Serikali ione namna ya kulichukua deni hilo kwa kuhakikisha juhudi zinazoendelea za utekelezaji wake zinakamilika kwa haraka.

**4.2.4** STAMICO ihakikishe mitambo ya uchorongaji inayotarajiwa kufika ndani ya robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu, izingatie mgawanyo kwenye maeneo yenye uhitaji kwa uwiano unaofaa. Aidha, gharama za utumiaji wa mitambo hiyo ziwe rafiki kwa wachimbaji wadogo.

**4.2.5** Uunganishaji wa umeme kwa Mgodi wa STAMIGOLD Bulyanhulu ambao taarifa ilitolewa upo hatua za mwisho. Wizara kwa kushirikiana na TANESCO wahakikishe umeme unaingia mapema iwezekanavyo ili kupunguza gharama kubwa za nishati ya dizeli katika kuendesha mitambo hiyo.

**4.2.6** STAMICO ishirikiane na TANESCO ili kuwa na mkakati wa kutumia Makaa ya Mawe katika kuzalisha umeme.

**4.2.7** STAMICO itanue wigo wa utoaji Elimu kwa wachimbaji wadogo Kwa kuwa nakala 400 za mwongozo kuhusu usimamizi wa mazingira, sheria za Madini na kanuni ambazo zilitolewa hadi kufikia Feb,2023 bado ni chache na hazikidhi uhitaji.

## 4.3 TUME YA MADINI

Kutokana na umuhimu wa Tume ya Madini katika kuhakikisha mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa:-

**4.3.1** Ukaguzi na usimamizi wa miradi mipya ya uwekezaji katika Madini uimarishwe;

**4.3.2** Tathmini ya athari za kimazingira ifanyike kwa mabwawa yote ya tope na tope sumu zinazoweza kutokea iwapo yataharibika au kupasuka. Aidha, Wizara ihakikishe inakamilisha mapitio ya kanuni za usalama, afya na utunzaji wa mazingira;

**4.3.3** Kutokana na ukweli kuwa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya waendelezaji wa madini ya aina mbalimbali kuendelea kuwaumiza wananchi wanaomiliki maeneo hayo kutokana na fidia zisizoendana na uhalisia, Serikali ihakikishe inasimamia suala hili ili fidia ziendane na thamani halisi ya eneo. Aidha, Wizara inaweza kufikiria na kufanyia kazi uwezekano wa wananchi ambao wako tayari kupewa hisa (*Free carried interest*) katika maeneo yao wanayopisha.

**4.3.4** Ili kupunguza changamoto za baadhi ya wamiliki wa leseni kuwafukuza wananchi katika maeneo yao, Elimu itolewe kwao ili wafahamu umuhimu wa kukubaliana (*sound negotiation)*na wananchi ili kuweza kupisha maeneo yao kwa amani.

## 4.4 WAKALA WA JIOLOJIA NCHINI (GST)

**4.4.1** Ujenzi wa Ofisi za Kanda upewe kipaumbele hii itasaidia kusogeza huduma karibu zaidi na Jamii na kufikia wahitaji wengi zaidi;

**4.4.2** Ili kuongeza usalama na imani kwa wateja, GST ihakikishe inaimarisha mifumo ya usalama kwa kufunga kamera katika maabara zake; na

**4.4.3** GST ijitangaze zaidi hasa baada ya kuboresha huduma zake kwa kununua vifaa vipya vyenye ubora. Elimu hii izingatie zaidi maeneo yenye wateja wa maabara.

## 4.5 KITUO CHA JEMOLOJIA TANZANIA (TGC)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga **Shilingi Bilioni 7** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Majengo ya TGC. Ni Rai ya Kamati kuwa utekelezaji wa mradi huu uende kwa kasi na kukamilika kwa wakati ili kuondoa changamoto ya miundombinu duni.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa huu kukushukuru sana Spika wetu Mhe. DKt. Tulia Ackson (Mb), Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini kwa ushirikiano wao wakati wa kutekeleza majukumu ya Kamati na kushiriki vizuri katika uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Judith Salvio Kapinga, - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. David Mathayo David, Mb
4. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
5. Mhe. Constantine John Kanyasu, Mb
6. Mhe. Seif Khamis Gulamali, Mb
7. Mhe. Hamis Mwagao Tabasam, Mb
8. Mhe. Iddi Kassim Iddi, Mb
9. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
10. Mhe. John Marko Sallu, Mb

11. Mhe. Juliana Didas Masaburi, Mb
12. Mhe. Nicodemas Henry Maganga, Mb
13. Mhe. Saada Mansour Hussein, Mb
14. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
15. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
16. Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda, Mb
17. Mhe. Martha Festo Mariki, Mb
18. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
19. Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
20. Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb
21. Mhe. Ndaisaba George Ruhoro, Mb
22. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru sana Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko(Mb) na Naibu Waziri Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mb) pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndg. Kheri Mahimbali kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati wakati wote. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Katibu Mkuu kwa kuaminiwa na Mhe.Rais na kuteuliwa kwa nafasi hiyo. Kamati itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha katika kufikia Malengo ya Wizara na Nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi (*ndc*). Namshukuru pia Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto *(ndc)*kwa ushirikiano na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Kipekee zaidi nawashukuru sana Makatibu wa Kamati Ndg. Pamela Pallangyo, Ndg. Onesmo Laulau, Ndg. Jesca Sanga na Msaidizi wa Kamati Ndg. Rukia Shabani kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali

kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini (Fungu 100) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja .

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Dunstan Luka Kitandula
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
27 APRILI, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Kapinga, Makamu Mwenyekiti wa Nishati na Madini, kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo kidogo; kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Madini moja ni wageni kutoka kampuni za uchimbaji wa madini ambazo Serikali ina ubia. Tunaanza na *Twiga Minerals Cooperation Limited* wakiongozwa na Ndugu Mtagahwa, ahsante karibuni. *(Makofi)*

Wengine kutoka *Tembo Nickel Cooperation Limited* wakiongozwa na Ndugu Benedict Basunzu; wengine wametoka Nyati *Minerals Science Limited* wakiongozwa na Ndugu Heri Ngombera. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine kutoka *Faru Graphite Cooperation* wakiongozwa na Ndugu Alimia Othman Munge; wageni kutoka *Mamba Minerals Cooperation Limited* wakiongozwa na Ndugu Ismail Diwani; wageni kutoka *Sotta Mining Cooperation Limited* wakiongozwa na Dkt. Joas Kabete; wageni kutoka *Duma Tanz Graphite Limited* wakiongozwa na Ndugu Chrispine Muhingo; wageni kutoka *Kudu Graphite Limited* wakiongozwa na Dkt. Mary Mwanjelwa; wageni kutoka *Williamson Diamond Limited*

wakiongozwa na Ndugu Shagembe A. Mipawa, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine kwenye kampuni ya uchimbaji wa madini, tutaanza na *Geita Gold Mining Limited* wakiongozwa na Ndugu Simon Shayo; wageni kutoka *Shanta Gold* wakiongozwa na Ndugu Honest Mrema; wageni kutoka Busolwa *Mining Limited* wakiongozwa na Ndugu Masumbuko T. Buyi; na wageni kutoka *Franone Mining and Gems Company Limited* wakiongozwa na Ndugu Vitus M. Ndakize, ahsante na karibuni sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu sasa tutaanza mjadala kwa hoja iliyoko mbele yetu na hapa ninayo orodha ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Madini ambayo inatamani tupitishe Bajeti ya shilingi 89.3 kwa ajili pia ya malengo makubwa ya kukusanya maduhuli yanayofikia Trilioni 1.006 na nitangulie kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho yetu ya madini kama sekta ni kesho njema na hivyo tuunge hoja mkono kwa kupitisha Bajeti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ambazo tumeshuhudia ukuaji wake mwaka hadi mwaka ni sekta ya madini na ni kweli kwamba kwa mwendo ambao tunakwenda nao ile asilimia 10 ya kuchangia Pato la Taifa kufikia Dira yetu ya Taifa ya mwaka 2025 itaweza kufikiwa bila shida. Hii inatokana na maono makubwa ya Wakuu wetu wa Nchi lakini pia na uongozi mzuri wa Wizara na Taasisi zilizo chini yao, pia na uelewa mkubwa wa wadau kwa maana ya wachimbaji wakubwa na wadogo pamoja na watu wote ambao wanajihusisha na sekta ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitoe pongezi za dhati na za pekee sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa diplomasia yake ya hali ya juu. Hii ni kwa sababu katika ile ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani tulisikia ahadi ya kujengewa kiwanda kinachotengeneza betri kwa kutumia madini yetu ya *nickel.* Huu ni ukombozi mkubwa na lazima tumpongeze sana Rais jinsi ambavyo anajua kutumia diplomasia yake katika kuvutia uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachochagiza ukuaji huu wa sekta pamoja na mambo mazuri ambayo tunayashuhudia ni pamoja na yale mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017. Ni kweli kwamba hatua kubwa imepigwa na hasa katika kuwawezesha Watanzania kushiriki kutoa huduma katika migodi lakini pia na kuwahudumia wachimbaji wadogo, kama kuna Wizara inatamani kujua namna *local content* inavyotekelezwa waende Wizara ya Madini. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kujivunia na tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo katika miaka hii Sita ya kuwepo kwa Sheria ya Madini ni muhimu pia tukafanya tathmini kuona kama zile fikra tulizokuwa nazo mwaka 2017 zinatekelezeka zingine au zingine hazitekelezeki na kwa jinsi hiyo kuna mambo ambayo kama Wizara wanaona kwamba hayakuwa sawa na matarajio basi yanaweza yakaletwa ili kwamba yaweze kurekebishwa na moja ya mambo kama hayo ni leseni hodhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni hodhi zimerudishwa Serikalini kwa njia ya sheria lakini wawekezaji nao bado ni kama hawana ridhaa nalo, lakini pia wachimbaji wadogo wanaziangalia na kuzichokonoa fulani kwa hiyo unakuta kwamba siyo sisi wala Serikali wala wawekezaji wanaonufaika nadhani hili Mheshimiwa Waziri anaweza akaona kama ndani ya muda huu linamletea shida, basi anaweza likafanyiwa marejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wakati Tume ya Madini inaanzishwa ilileta pamoja watumishi ambao walikuwa na viwango tofauti vya mshahara, na ilitegemewa katika kuleta upatanifu na ulinganifu, wale wadogo wasogezwe katika wale waliokuwa na mshahara mkubwa, lakini jambo hili halikufanyika hivyo badala yake wale wakashushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linapunguza *morale* na wakati ambapo ndio watu unaowategemea waweze kukusanya maduhuli ya trilioni moja. Sasa hawa ni watumishi, walikuwa juu halafu wakashushwa na ukiangalia hiyo *payroll* kama mtu alikuwa ana *commitment*s zake huko nyuma, wengine walipata mshahara *negative* (hasi), anaendaje kukusanya maduhuli huku hana fedha? Kwa hiyo, hili nadhani liko kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Simbachawene Wizara ya Utumishi hebu vuta mafaili ungalie hawa watu, kwa sababu pia wakati mwingine Serikali tujifunze kulipa ujira sawasawa na kazi ya mtu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakwenda Mererani kilomita mbili anakwenda kuchukua *Tanzanite* ya bilioni tatu halafu anapoileta juu badala ya kuthaminisha mshahara wake unahesabika maelfu kadhaa. Nadhani tujifunze kulipa kwa kadri ya ujira wa mtu. Siyo sawa mtu aliyezama kilomita Mbili analeta madini ya thamani ya bilioni tatu mshahara wake mwisho wa mwezi unahesabika. Yeye si naye ana roho, nyama na damu jamani au? Kwa hiyo, hilo nadhani Mheshimiwa Simbachawene unaweza ukaliangalia hebu livute katika mafaili yako wasaidie hawa watumishi wa Tume ya Madini ili *morale* yao ipande ili waweze kukusanya maduhuli ya Trilioni 1.006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye hoja yangu ambayo nataka kuichangia asubuhi hii ya leo. Siasa za Kimataifa zina makundi ya wenye uchumi Nchi Saba tunawaita *G7,* pia siku za karibuni kuna kundi la watu wanaitwa *BRICS* hawa ni Brazil, Urusi, India pamoja na China na Afrika Kusini. Hawa watu katika

kujaribu kuondoa matumizi ya dola kwa sababu ni kama ni makundi yanayoshindana wameamua kwamba wao watakalolifanya kubwa ni kununua dhahabu kwa wingi, kuweka akiba katika nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naleta siasa hizi za Kimataifa katika mjadala wangu asubuhi ya leo? Hoja hapa ni kwamba kama hawa ambao wanajaribu kuona kwamba ili uchumi wao uweze kutengemaa wanaiona dhahabu kuweka akiba kama njia ya kuimarisha uchumi kwa maana ya kwamba wakati ujao yawezekana nani ajuaye dola yawezekana isiwe na nguvu katika kufanya biashara ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba na kwa sababu pia sheria yetu inaturuhusu Kifungu cha 88 cha Sheria ya Madini, Kifungu Kidogo cha Pili kinasema mrabaha hapo mbele uweze kukusanywa kwa thamani ya madini yaliyosafishwa *(refined gold)* ili itusaidie na sisi kama nchi tuweze kuwa na akiba ya dhahabu, ili tuweze kulinda na kutegemeza uchumi wetu ambao unaendelea kukua siku kwa siku.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba dhahabu tunayo, *refinaries,* tunazo hebu sasa tufikirie yaani ifikie mahali tunapopanga mipango yetu ya uchumi na kuukuza basi tununue dhahabu na kuiingiza katika benki yetu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine niongee habari ya Liganga na Mchuchuma kidogo, pamoja na kwamba inapenda kuongelewa katika Wizara ya Viwanda lakini bado ni madini na wala siyo bidhaa hadi pale yalipo kwa hiyo ni sawa tu kuiongelea katika muktadha wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liganga kuna chuma, *vanadium* na *titanium*. Madini yote ambayo yana thamani kubwa sana, lakini pia Mchuchuma kuna makaa ya mawe mazuri kabisa na

kimsingi ndio huwa kuelelezo cha makaa ya mawe katika mfuatano wa madini Tanzania. Sasa hawa watu walipewa leseni kwenye kampuni ya ubia mwaka 2014 na sheria zetu za madini zinawaruhusu angalau miezi 18 wawe wameanza uchimbaji hawajaanza.

**MWENYEKITI:** Malizia mchango wako Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninakushukuru kwa hayo, wakati mwingine Mungu akijaalia.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Namuita Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii nami nichangie Wizara hii muhimu, hasa kwa uchumi wetu. Nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri wa Madini kwa kazi nzuri waliyoifanya kuisimamia hii sekta ya madini ambayo imeonesha mwelekeo mzuri. Ukiangalia hata kwenye pato la Taifa sekta ya madini imekuwa ikichangia kwa wastani mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania siyo kisiwa, ni sehemu ya dunia na tunaona mabadiliko makubwa ya kiuchumi duniani. Nasi rasilimali zetu tulizonazo inabidi tuzitumie vizuri na rasilimali mojawapo ambayo inaweza kuibadilisha Tanzania kwa haraka ni hii sekta ya madini. *Speed* tuliyonayo pamoja na hayo mafanikio, inabidi iongezwe kidogo kwa sababu, ukiangalia mtangulizi wangu hapa amezungumzia kuhusu mradi wa Mchuchuma au Liganga na Mchuchuma. Angalia muda mrefu ulivyopita, lakini kuna miradi mingi ambayo inaendana pamoja na hiyo, kwa

sababu, hizi rasilimali tusipozitumia leo baadaye zinaweza kugeuka zisiwe na thamani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara iangalie namna gani kwa kushirikiana na Wizara nyingine Serikalini kuvutia wawekezaji ili kuhakikisha hizi rasilimali zinabadilishwa na zinatafsiri kuongeza uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, napendekeza Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha kuwa miradi kama Liganga na Mchuchuma inaenda kwa *speed* ya haraka ili tupate pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo enaendana sawa na Liganga na Mchuchuma, kuna mradi wa *Niobium* hapa. Nafikiri Mheshimiwa Waziri nisingesema hili neno angenishangaa. Nitaendelea kulisemea hilo kwa sababu inaelekea wenzetu bado hawaoni zile fursa tulizonazo kama Tanzania. Kuleta kiwanda cha uchenjuaji *Niobium* cha kwanza Afrika, cha nne duniani na mahitaji ya *ferroniobium* ni makubwa mno duniani. Kwa kweli ni jambo ambalo linabidi lichukuliwe kwa haraka ili Tanzania ibadilike hapa tulipo. Tumekuwa tukifanya vizuri kwenye uchumi wa nchi yetu, lakini hatujafanya vizuri sana kama tungeweza kutumia rasilimali hizi tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *ferroniobium* ninayoizungumzia ambayo inapatikana Mbeya, yale madini ndiyo yangetumiwa kwenye ujenzi wa madaraja yetu, ujenzi wa reli yetu tunayoijenga sasa hivi, na vilevile haya madini yanahitajika zaidi huko nje. Ukiwa na hiki kiwanda ina maana hata nchi Jirani, haya madini yao yatakuja kutengenezwa au kuongezwa thamani hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, naona kabisa ya tunaitaka Tanzania ya viwanda. Kwa hiyo, ukiwa na kiwanda cha namna hii, ndiyo unafikia yale malengo ambayo yamo kwenye *millennium goals*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kulisema hilo, kwa ajili ya muda, mwenzangu amezungumzia kuhusu umuhimu wa dhahabu kuwa sehemu ya fedha za kigeni ambayo itatunzwa na Benki Kuu. Dunia imebadilika sana. Mataifa makubwa leo hii yanaachana na kutumia zile fedha za kigeni tulizozizoea kama Dola, *Sterling Pounds* au *Euro* kama sehemu ya kuwekeza, yamekuwa sasa hivi yananunua dhahabu na kuwekeza kwenye hizo benki na kuwa sehemu ya pesa zao za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili umuhimu wake mkubwa kwa sababu, dhahabu thamani yake mara nyingi inaongezeka kwa haraka zaidi wakati Dola inapungua. Kwa hiyo, ukiangalia huo mtazamo kwa muda mrefu, nilikuwa naangalia takwimu za mwaka 2022 Desemba, ukilinganisha na leo, miezi minne tu, bei ya dhahabu imepanda kwa asilimia 11 ambayo hiyo ni asilimia kubwa sana. Ina maana nchi yetu ingeweza kuwekeza kwenye dhahabu, hiyo thamani kubwa tungeweza kuipata badala ya kuendelea kuwekeza pesa zetu kwenye pesa za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwekeza pesa za kigeni kwenye benki za wenzetu inawezekana hata wengi hawajui, ni sawa na kuwakopesha. Kwa hiyo, zile thamani ya pesa tulizonazo sisi kule, ina maana tumewakopesa, lakini ukiwa na dhahabu ambayo umeinunua Tanzania hapa hapa na tunazalisha Tanzania hapa hapa, utakuwa umetumia shilingi yetu kununua hiyo dhahabu na ukaibadilisha ikawa pesa ya kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumzia urari wa biashara ambao sasa hivi tuliona kwa kiasi kikubwa ulikuwa hauendi vizuri sana, kwa hiyo, kwa kununua dhahabu, Benki Kuu ikianza huo mpango itawezesha nchi yetu kuwa na urari wa biashara ambao ni mzuri. Labda ni kuchukua tu tahadhari ya kwamba huko nyuma hawakufanya vizuri, kwa hiyo, sasa hivi kinachohitajika, wajifunze kutokana na upungufu uliokuwepo, ili

tuweze kurekebisha taratibu zetu tuhakikishe kuwa kile tutakachonunua kitatuletea faida badala ya kutuletea hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wake, sasa hivi kuna mashirika makubwa sana ambayo yanalisimamia hilo. Kwa hiyo, hutanunua dhahabu kama dhahabu, utanunua dhahabu ambayo itaongezwa thamani kufikia mpaka asilimia 99.95 mpaka 99.99 ambayo inasimamiwa na mashirika makubwa kama lile la *London Bullion Market Association.* Ninashauri kuwa Benki Kuu waanzishe haraka hiyo ili tuepukane na kuweka fedha zetu kwenye Dola ambayo mpaka leo hatuoni kama itaendelea kutuletea faida hasa kulingana na mitikisiko ya kiuchumi na hii mivutano iliyoko hapa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tungelitumia vizuri kwa Wizara ya Madini; tumeona bei za mbolea zikipanda kwa haraka mno. Hizi mbolea zinatengenezwa kwa madini ambayo yanapatikana Tanzania. *Calcium* tunayo, *phosphate* tunayo, *lime* tunayo, *natural gas* tunayo, hatuna sababu ya kuendelea kutegemea mbolea za kutoka nje. Kwa hiyo, tujipange vizuri tuangalie ni namna gani nchi yetu ianze kutumia hizi rasilimali zetu tuweze kupeleka mbolea nje badala ya sisi kuwa waagizaji wa mbolea kutoka nje. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, ajiandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya

njema kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na leo kuwa miongoni mwa wachangiaji kwenye hotuba hii ya Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiongoza nchi yetu na ninaamini kabisa kupitia Wizara hii malengo na mafanikio ya kujenga uchumi imara yanaenda kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa, nilikuwa nikipitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini na katika maelezo yake kwamba, sekta hii ya madini hadi kufikia Septemba, 2022 imechangia takribani asilimia 9.7 kwenye pato la Taifa. Ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naamini kabisa kwamba jitihada hazijafanyika za kutosha kwa sababu nchi hii maeneo mengi yana madini. Wachimbaji wadogo wadogo na wachimbaji wa kati bado hawajawezeshwa hatimaye kuweza kuisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yake hii Mheshimiwa Waziri, imeonesha pia kwamba, madini yamechangia kiasi cha Dola milioni 3,395 ambayo ni sawa na asilimia 56 ya mauzo ya nje. Hili ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, zipo changamoto ambazo wenzetu wa Wizara ya Madini ni lazima wakubali kuzipokea na waweze kuwasaidia hususan wachimbaji wadogo wadogo. Moja ya maeneo ambayo nilikuwa nataka niyaseme na ambayo nimeona Serikali ya Mheshimiwa Rais imefanya ni ya kupeleka umeme katika maeneo ya wachimbaji. Ni jambo la kupongeza sana. Ni takribani kama miezi miwili iliyopita, Mheshimiwa Rais alikutana na Wizara ya Nishati akisaini mikataba.

Moja ya maelekezo yake ilikuwa ni kutoa maelekezo kwamba miradi ile mikubwa iende katika migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameona kwamba madini haya hayachimbwi ipasavyo. Uwekezaji umekuwa una gharama sana kwa sababu, wachimbaji wanakuwa wanatumia mafuta ya dizeli, sasa kitendo cha Mheshimiwa Rais na Serikali yake kuamua kupeleka umeme mkubwa kwenye machimbo haya maana yake unaenda kuwezesha uchumi wa wananchi hatimaye na Taifa kwa ujumla. Ni jambo la kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuchangia ni Sheria yetu ya Leseni ambayo inaruhusu kukata leseni kupitia mtandao. Ni sheria nzuri sana, lakini sheria hii ina matobo ambayo ni lazima sisi kama Waheshimiwa Wabunge tuiangalie na tuweze kuirekebisha. Leo hii mtu anaweza kuomba leseni akapata leseni hata katika jengo letu la Bunge hili bila kutazama kwamba hapa pana nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliseme hili kwa sababu, limekuwa likileta migogoro sana, hususan katika maeneo ambayo yana wachimbaji, kama Kilindi na maeneo mengine. Mtu anapata leseni halafu anamkuta mwenye shamba pale. Sheria hii inatenganisha Sheria ya Ardhi na Madini. Sasa haimpi haki mwenye ardhi, au mwenye shamba. Sasa hili limekuwa na mgogoro mkubwa sana; na hili kwa kweli lazima tulitazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji anaweza akapata leseni pale, akaanza kuchimba, anaanza kuingia mgogoro na mwenye ardhi. Sasa ni lazima tutazame na tujifunze kupitia maeneo mengine. Tutembee maeneo mengine tuone: Je, wenzetu wameweza kuepuka migogoro namna gani? Tuone namna ambavyo kama mwekezaji akipata aneo akamkuta

mkulima pale, basi zile *shares* zisiwe *diluted*. Hii ndiyo namna pekee ambayo inaweza kumsaidia mwenye eneo lake. Hili limeweza kufanikiwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matobo mengine ambayo ni mabaya kabisa, sheria hii kwa kiasi kikubwa inachangia kuongeza deni la Taifa. Naomba niliseme hili kwa mifano. Unakuta barabara inatakiwa kujengwa, mkandarasi anapotaka kuanza kujenga barabara anakuta sehemu ya mawe. Anapotaka kutengeneza kokoto, siku mbili kabla hajaanza *site,* kuanza kujenga barabara anakuta eneo limetolewa leseni. Mtu katumia shilingi 50,000, yule aliyepewa leseni anaanza kuomba kuanza kufidiwa. Sasa hili limeleta shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano mmoja. Tunayo barabara yetu ambayo inatoka Handeni – Kiberashi hadi Singida, mkandarasi aliweza kuchelewa zaidi ya miezi minne kwa sababu, eneo ambalo alikuwa anataka kuchimba kokoto, alikuta tayari mwekezaji kapewa leseni na muda wote alikuwa hajapewa leseni. Jambo hili ukitaka kuangalia, kuna *syndicate* kati ya watumishi wachache wa Wizara ya Ujenzi na wenzetu wa Madini. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuona namna gani ya kubadilisha sheria yetu ili isiweze kuruhusu Serikali kuingia gharama kubwa kutokana na sheria ambayo tumeitunga wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigua. Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nashukuru pia kwa kupata nafasi ya kuchangia. Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana

Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake nzuri ambayo ameitoa. Kipekee naipongeza Serikali kwa ujumla, Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa kazi nzuri ambayo tunaendelea kushuhudia inafanyika kwenye diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulialikwa juzi kwenda kushuhudia uwekaji sahihi wa uwekezaji wa madini; niyaite madini adimu *(rare minerals)*. Hizi ni dalili kwamba tunaendelea kuungwa mkono huko nje na watu wanaendelea kutuelewa; na ni dalili kwamba Wizara inafanya kazi yake vizuri. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana watu wote wanaofanya kazi na Mheshimiwa Waziri na kumpongeza sana Katibu Mkuu mpya kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kielelezo cha kwamba kazi zinakwenda vizuri ni mafanikio ambayo yamefika sasa kwenye asilimia 9.7 ya malengo ambayo yaliwekwa na Serikali na Bunge hili ili kuweza kuchangia uchumi kwenye bajeti ya nchi. Jambo hili haliwezi kufanikiwa kama Wizara haizungumzi lugha moja. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio makubwa ya Wizara hii yanatokana na mchango mkubwa wa wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo kwa taarifa ya Wizara, wanachangia takribani asilimia 40 ya mauzo ya dhahabu nje ya nchi. Jambo hili ni kubwa na hatuwezi kuliacha lipite hivi hivi. Kwa nini tumefanikiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanikiwa kuondoa usumbufu uliokuwa unawakuta wachimbaji wadogo; tumeondoa urasimu uliokuwa unasababisha sekta hii haikui; tumefanikiwa kuimarisha na kuongeza masoko ambayo sasa siyo tena jambo la ajabu kusikia kwamba kuna soko kila kona ya nchi hii. Sasa Serikali ina jambo moja tu la kufanya katika eneo hili. Ni kufanya sera yake ya kodi kwenye eneo la wachimbaji wadogo iweze kutabirika na

iweze kueleweka. Naishukuru sana Serikali, wanafanya utafiti na utafiti huu utawapeleka kwenye kuamua aina gani ya kodi wafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa kwamba, fedha tunazoziona kwenye mauzo ya dhahabu ya mchimbaji, siyo faida. Mchimbaji mpaka anafikia kwenda sokoni kuuza dhahabu, *investment* yake aliyoiweka wakati mwingine ni asilimia 200 ya anachoenda kukiuza. Kwa hiyo, ni vizuri sana tuwe na sera zinazotabirika na zinazoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ili uweze kufikia malengo sasa unayokwenda zaidi ya Shilingi trilioni moja *point;* aliwahi kuzungumza Mheshimiwa Kishimba, hakuna Chuo cha Wizi, Serikali inafundisha tu namna ya kumdhibiti mwizi, lakini kuna watu wanajifunza namna ya kuiba. Mikakati yote ambayo mnafanya, lazima pia mjue kuna watu wanajifunza namna ya kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu, kuna watu wanafanya mkakati wa ku-*lower purity* ya dhahabu, lakini kuna watu wanafanya *smuggling* na hii *smuggling* inatuathiri sisi wenye Halmashauri tunazotegemea kupata *Service Levy* kutoka kwenye mauzo ya dhahabu. Sasa lazima Serikali nzima ifanye kazi kwa pamoja; vyombo vyote, ili tuweze kufikia malengo haya ambayo mimi nayaona tunaenda kufikia, kwa sababu, tayari tumeanza kukaribisha wawekezaji wengine katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kulichangia, nataka kuishukuru sana Serikali. Tumekuwa na mgogoro wa muda mrefu Geita wa vigingi pamoja na mipasuko. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Shigela. Baada ya kufika Mheshimiwa Shigela amekuja na *formula* tofauti na Wakuu wa Mikoa wengine. Kwanza ameshirikisha makundi

yote kwa kukaanayo, akawashirikisha wawekezaji, baadaye akaunda kamati ambayo imefanya kazi yake. Sina uhakika na taarifa ya Kamati, lakini nina imani kubwa, Kamati ile kwa mchanganyiko wake na muundo wake, itakuwa inakwenda kuleta suluhu ya wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu Mheshimiwa Waziri, jambo hili lifike mwisho. Wananchi walikusikia tarehe 09 Januari, ulitoa miezi mitatu, miezi mitatu imekwisha. Wengi wanaomba namba yako wakupigie ili waweze kujua limefikia wapi, lakini siwezi kuwapa namba, nina imani kwamba utakwenda kusema sasa jambo hili linaishaje. Nani analipwa fidia, nani halipwi fidia na kazi zinaendelea kwa staili gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa sababu umeonesha dalili ya kwamba unataka lifike mwisho. Ninawaahidi wananchi wa Geita kwamba Serikali yao inawapenda na kuwasikiliza, na mwakilishi wao ambaye wamenituma hapa sasa wawe na uhakika kwamba nakwenda kulimaliza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; tulifanya mabadiliko ya sheria hapa kuhusu *local content*. Naomba kuipongeza Serikali; imefanikiwa sana kwenye utekelezaji wa *local content*. Ni miongoni mwa halmashauri ambazo mtu akitaka kujifunza namna ambavyo *local content* inasaidia kukuza uchumi wa wananchi aje ajifunze Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana *GGM,* ninawapongeza katika maeneo yote. Kwenye michezo nadhani mnafahamu habari ya *Geita Gold*. Tunayo timu nzuri, tumepandisha timu nyingine ya wanawake, *Geita Gold Queens,* ambayo na yenyewe tunawashukuru sana *Geita Gold* kwa sababu bila mchango wao hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru *Geita Gold* kwa sababu *local content* imesaidia sasa wananchi wa Geita wanaweza kushiriki kwenye uchumi mkubwa ambao ni uchumi wa madini. Sasa…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu; Twiga *Mining* pamoja na *Geita Gold* na mashirika mengine, kwa mfano Twiga *Mining* wameweka *middleman* pale katikati ili uweze kufanya biashara na mgodi, inawaongezea gharama wafanyabiashara. Tunashukuru kwa nafasi hiyo lakini tunaomba tupunguze huo urasimu ili kusaidia wananchi wengi kushiriki kwenye uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassor Amar.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ambayo tunategemea ukuaji wake na mchango wake ni mkubwa sana kwenye maendeleo ya nchi yetu hii na kwenye Pato la Taifa. Nakupongeza Mheshimiwa Waziri na wataalam wako wote Wizarani; mnafanya kazi kubwa na nzuri na kila mwananchi wa Tanzania anaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Madini imeendelea kukua miaka hadi miaka. Kwenye uchangiaji wa Pato la Taifa pia imeendelea kufanya vizuri na ukuaji wake kila mtu anauona. Tunawapongeza sana kwa hili na kwa kweli tuna imani kwamba ile mipango ya kufikia zaidi ya asilimia kumi na itaweza kufika kwa wakati na pato lake kwa Taifa litakuwa linaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapowapongeza hawa lazima pia tuwapongeze wachimbaji wadogo, wachimbaji wetu wadogo nao pia wameendelea kufanya vizuri. Wameweza kuendelea kuongeza uzalishaji na kuweza kuchangia kwenye pato la Taifa. Katika madini yote ambayo yanapatikana, asilimia 40 yanapatikana kutoka kwa wachimbaji wadogo; lazima tuwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo hawa ambao wanachangia zaidi ya asilimia 40, maisha yao ambayo wanaishi hayaakisi kile ambacho wao wanakizalisha. Na hayaakisi hivi kwa sababu ya kodi nyingi na ada mbalimbali ambazo wao wanatozwa. Leo hii baada ya Wizara na mfumo mzima wa uchimbaji kuwa vizuri, sasa taasisi nyingine zote za kimapato zinaangalia uchimbaji huu mdogomdogo kama vyanzo vyao vya kutafuta mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza kodi ambazo zinamkabili mchimbaji mdogo ni nyingi sana kiasi kwamba inasababisha mchimbaji huyu anazalisha kwa nguvu kubwa sana lakini tija kwake yeye binafsi inakuwa ndogo sana. Niombe kama Serikali muweze kukaa muone namna bora zaidi za kumpunguzia kodi mchimbaji huyu mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizi pia ziweze kukaa ziwe na utaratibu mzuri zaidi wa kumuwezesha badala ya kuwa wao kazi yao ni kuzuia. Leo mchimbaji mdogo anapoanza kufanya kazi yake zinakuja taasisi nyingine, badala ya kumsaidia,

kumshauri vizuri, wao kazi yao wanakuja pale kumuwekea vikwazo ambavyo vinasababisha mchimbaji huyu ashindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anakuja kudai jambo dogo tu anakwambia sasa hapa tunasimamisha uzalishaji wako mpaka ulipe hii kodi au ulipe hii ada. Na hiyo inakwenda kwenye ngazi kuanzia ya *TRA* wenyewe, hizi taasisi zinazozunguka mpaka kwenye ngazi ya kijiji. Leo mpaka mtendaji wa kijiji anafika pale anakwambia kwamba hujalipa *service levy* au ada hii hapa ndogo, uzalishaji usimame mpaka ulipe. Namna hii hatutaweza kumkomboa mchimbaji mdogo, lazima hizi sheria pia ziweze kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo upande wa *STAMICO.* Wamefanya kazi nzuri, tunawapongeza sana. Kutoka kuwa shirika mfu ambalo lilikuwa linataka kufutwa mpaka ilifikia hatua wanashindwa kulipa mishahara yao. Lakini sasa hivi wameweza kupiga hatua kubwa sana na wameweza kuzalisha faida ya zaidi ya bilioni 70 kwa mwaka; hii ni hatua kubwa sana. Tuwapongeze na tuwape moyo, wanaweza wakafanya mambo makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, Serikali iliangalie sana Shirika la *STAMICO,* linaweza likafanya miradi mikubwa na ya kimkakati na uzalishaji ukaongezeka na uchangiaji kwenye pato la Taifa ukawa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza habari ya *STAMICO,* tuangalie sheria ya uanzishaji wake. Tunaweza tukaibadilisha sheria ya uanzishaji wa *STAMICO* na yenyewe ikawa wasimamizi badala ya Serikali kwenye ule uchimbaji wa madini mwingine wowote ambao Serikali inaingia, badala ya kuanzisha kampuni ndogondogo za kila siku, yenyewe sasa ikasimama badala ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikwenda ikulu pale kushuhudia makubaliano na kusaini mikataba lakini kulikuwa na makampuni mbalimbali ambayo yameanzishwa na Serikali ambayo yameingia ubia na hayo makampuni ya nje kwa ajili ya uzalishaji. Sasa badala ya kuanzisha makampuni madogo madogo mengi kila tunapotaka kuanza uchimbaji sasa tuipe jukumu hili *STAMICO* ili waweze kuifanya kazi hiyo. Nina imani *STAMICO* wanaweza wakafanya kazi hiyo vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia kwenye *STAMICO* hapa namna ambavyo wameendelea kwenda na ubunifu na sasa wamekuja na mkaa rafiki. Ni teknolojia ambayo wameanza nayo na ni nzuri, na ikiendelea hivi itasaidia sana mkaa huu kwenda kuwa mbadala wa ile mikaa ambayo inatumiwa ya miti na kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanaendelea kuwa safi na salama kwa muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mkaa rafiki ambao unazalishwa na *STAMICO,* hii teknolojia ambayo wao wameifanya, mimi nishauri kwamba badala ya kuendelea nayo wao waiuze kwa Taasisi nyingine kama *SIDO* au *VETA* ili wao sasa waje waipeleke kwenye jamii huku chini na baadaye uzalishaji wake uweze kufanyika huko. Badala ya wao kuibuni na wao pia waendelee kuweza kuzalisha na kuuza huko mtaani. Wao wabakie na mambo makubwa makubwa kama ambayo wanaendelea nayo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiendelea na mambo makubwa haya ambayo sisi tunayasema ili kuweza kuifanya *STAMICO* ikue kwa uwanda mpana zaidi. Leo mfano tunazungumza makaa ya mawe, haya makaa ya mawe ndiyo ambayo leo yanazalisha umeme. Je, sisi kutumia *STAMICO* tunaisadia vipi hii nchi yetu *STAMICO* iweze kuzalisha umeme mkubwa zaidi uweze kuingia kwenye Gridi yetu ya Taifa ili uweze kutusaidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kwamba sasa badala ya *STAMICO* kwenda kuzalisha hii miradi mingine midogo midogo, ijiwekeze kwenda kwenye kuzalisha umeme uwe mkubwa zaidi, tutoke sasa hivi tunataka tuzalishe kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere megawati elfu mbili na, twende kupitia makaa ya mawe chini ya *STAMICO* tufikirie miaka 10, 20 mbele uzalishaji wa umeme uweze kufikia megawati 10,000 mpaka 15,000 kupitia makaa ya mawe. Jambo ambalo linawezekana, ni kuwawezesha tu *STAMICO* waweze kufanya kazi hiyo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa *STAMICO* wakati Mheshimiwa Rais anapokea Ripoti ya *CAG* tuliona alisema kuna baadhi ya mashirika na taasisi nyingine yamekuwa hayana faida kwa sasa hivi. Tutolee mfano *NDC; NDC* imekuwa inasimamia Mradi ule wa Liganga pamoja na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu imekuwa ni stori ya miaka nenda rudi, niombe sana kuishauri Serikali iweze kubadilisha sheria ili ule Mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma uweze kutoka kule ulipokuwepo kwa maana ya Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya *NDC* uweze kuja sasa Wizara ya Madini na isimamiwe na *STAMICO* ili sasa uchimbaji uweze kufanyika na baadaye iweze kuleta tija kubwa sana kwenye nchi yetu hii. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia *STAMICO* na itakuwa ina miradi mikubwa na sisi tutakuwa tumeweza kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya *GST, GST* pamoja na kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya bado wanapata bajeti ndogo na mazingira yao ya kazi siyo mazuri. Tukiweza kuwekeza vizuri kwenye utafiti maana yake wachimbaji wetu hawa wadogo wadogo na wa kati wataweza kufanya kazi zao kwa kujua nini ambacho wanakifanya, nini ambacho

watakipata chini badala ya sasa hivi tunafanya uchimbaji wa kupiga ramli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwawezeshe hawa *GST* waweze kufanya kazi yao vizuri zaidi, wawe na vifaa vya kutosha. Leo wameagiza mitambo ya kuchoronga mitano na mingine inakuja, ni mwanzo mzuri lakini tuweze kwenda mbali zaidi na taarifa zao za *GST* ziweze kuwafikia wachimbaji wadogo hawa, ndiyo itakuwa ukombozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa kwenye mapato haya ambayo yamepatikana ya uchimbaji asilimia 40 yamezalishwa na wachimbaji wadogo lakini wachimbaji wadogo hawa hatujaweza kuwawezesha vizuri kuhakikisha kwamba uchimbaji wao utakuwa na tija na kuweza kuwasaidia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasaka, malizia mchango wako.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Hoja iliyoko mbele yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa uhai na afya njema kwa siku ya leo kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Ni hoja nzuri na nilikuwa nimejipanga vizuri sana kuweza kuchangia lakini kwa bahati nzuri hoja hii kwa kweli

imenifilisi kwa kiasi kikubwa, lakini nitaendelea kutoa ushauri kwa sababu nilikuwa nimejipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri wa Madini, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Katibu wa Wizara pamoja na timu yote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika Wizara hii; hongera sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo yangu ni machache sana; kuipongeza na kuishauri Serikali kupitia hii Wizara ya Madini. Nianze kwanza kwa kuwapongeza wachimbaji wadogo ambao wanaendelea kuchangia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa, kwa asilimia 40, kwa dhahabu yote ambayo inapatikana Nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemi wanasema unapotaka kumkamua ng'ombe ili akutolee maziwa mengi ni vyema ukamnenepesha. Kwa nini nasema hivyo; nizishukuru taasisi za kifedha kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wachimbaji wadogo, lakini naomba iendelee kutoa zaidi na kupunguza masharti kwa wachimbaji wetu wadogo ili waweze kupata vifaa vya kisasa waweze kuzalisha dhahabu kwa wingi na kuweza kuzidi asilimia ambayo sasa hivi wanachangia, asilimia 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vichache sana kwa hawa wachimbaji wadogo ambavyo vinahitajika ni kama vile *compressor, crusher, bombing, winch, digger,* vilipuzi na vifaa vingine. Vifaa hivi wakiweza kukopeshwa wachimbaji wetu wadogo wakaondoka kwenye uchimbaji duni uliopo hivi sasa wa kutumia kushusha ama kupandisha mawe kutoka chini kwa kutumia *roller* ama kuingia ndani kwa kutumia *mock* wanaita ukweli uzalishaji utakuwa ni mkubwa na mapato yao yatakuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naiomba Wizara izidi kuzishawishi taasisi za kibenki ziweze kupunguza masharti ili kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo waweze na wao kunufaika na mali hii iliyoko chini ambayo ni aina ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mchimbaji mdogo ninaomba Wizara hii iweze kuwasaidia wachimbaji wadogo, hususan wenye leseni kupitia *GST* waweze kuchimba maeneo ambayo yameshafanyiwa utafiti. Lakini pia GST ipunguze gharama zake za kuwafanyia utafiti hawa wachimbaji kutoka kwenye gharama ya shilingi 432,000 kwa mita na waweze kushusha angalau ifike hata shilingi 200,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakifanya hivyo watakuwa wamewasaidia sana hawa wachimbaji wadogo, pamoja na kwamba mnawakopesha wanakwenda kuchimba kwa kutumia ramli mafanikio hayatakuwepo. Lakini *GST* mkiwapunguzia hawa wachimbaji gharama za uchorongaji na mkaingia nao makubaliano, hata kama kwa malipo kidogo kidogo, watakuwa wanaifanya kazi kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nadhani unanisikia, nakuomba ulichukue hili. Washauri sana *GST* waweze kupunguza gharama za utafiti za uchorongaji ili wananchi wetu waweze kunufaika na uchimbaji wao kuliko kutumia uchimbaji unaoitwa uchimbaji wa ramli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa madini unaliingizia Taifa fedha nyingi. Lakini pia uchimbaji unaendelea kwa kasi na tukumbuke kwamba tunapopata mapato tuhakikishe mazingira yetu na yenyewe tunayaweka kwenye hali nzuri. Tusiangalie ukusanyaji wa mapato tu wakati mazingira yetu yanaharibika. Wachimbaji wetu wadogo wanaharibu mazingira sana kwa kutumia miti ambayo wanaifunga kama vile matimba kuingia kwenye mashapo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri ili tuweze kupunguza uharibifu wa mazingira haya basi Wizara ichukue angalau wachimbaji wachache iwapeleke nchi mbalimbali kama vile China na *South Africa* kwenda kuona namna gani wenzetu hawatumii miti, wanatumia utaalamu gani ama vifaa gani vya kuweza kujenga yale mashapu kutoendelea na kutumia miti, watumie utaalamu huo wa kisasa. Tutakuwa tumeokoa uharibifu wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana hili suala la uharibifu wa mazingira, sisi wachimbaji wadogo kwa kweli ni waharibifu wakubwa kwa sababu inapotokea sehemu kunaitwa lashi, watu wanachimba na zinapokata zile dhahabu wanaondoka wanaliacha lile eneo likiwa lina hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe kama kuna uwezekano, wakati uchimbaji huo unaendelea, waendelee kupanda miti ili iweze kusaidia kutengeneza mazingira hata ikitokea wameondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikupongeze tena kwa mara nyingine pamoja na Wizara yako. Ninamuomba Mheshimiwa Rais kama ananiona, kama kuna uwezekano basi Wizara hii atengeneze kautaratibu kazuri ka kutoa tuzo kwa viongozi hawa wenye taasisi hii kama vile Waziri, Naibu Waziri, Makatibu wake na wote kwa ujumla, taasisi hii angalau basi ipate tuzo kwa sababu tukiangalia kutoka 2017 mpaka leo 2023 mapato kupitia madini yamepanda kwa kiwango cha hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Amar.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha mchana, lakini tutaendelea na mjadala jioni ambapo tutaanza na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Nyongo na wengine wengi, *list* ninayo hapa.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja kutoka kwa Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kwamba kesho, Siku ya Ijumaa, tarehe 28, Aprili, 2023 kutakuwa na semina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji nchini mara baada ya kusitisha kikao cha Bunge saa saba kamili mchana katika Ukumbu wa Msekwa. Semina hiyo imeandaliwa na Wizara ya Maji, hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria semina hiyo muhimu.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala kwa hoja iliyoko mbele yetu ya bajeti ya Wizara ya Madini. Tutaanza na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Madini; lakini namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii tena ya kuweza kutupa nafasi ya kuchangia Bungeni leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kufanya kazi kubwa ya kuilea Wizara hii, na sasa tunaona maendeleo na ukuaji wa sekta unaendelea kuwa mkubwa. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa yeye, Naibu Waziri na wataalam kwa kusimamia sekta hii kiasi kwamba inaonekana ukuaji wake ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kwenye kumbukumbu kwamba mwaka 2020 ukuaji wake ulikuwa ni asilimia 6.7 lakini sasa mwaka 2021 inaonekana imekuwa inakwenda kwenye asilimia 9.6, maana yake kuna ukuaji, kuna *positive gain* hapo, kuna *positive growth*; kwa hiyo tunaamini kwamba kuna kazi kubwa wanayoifanya viongozi wetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mchango wa Pato la Taifa, napo nilikuwa najaribu kuangalia, inaonekana wamelinganisha vipindi ile *first quarter* ya mwaka ambayo ndiyo naona imekuja kwenye vitabu vyetu. Kwamba ukienda kwenye mwaka 2020 utaiona 6.7, 2021 utaiona 7.2 na mwaka 2022, kwa kipindi hiki utaiona ni 9.7. Sasa, hapa nilikuwa nataka kushauri, kwamba ikiwezekana wakati mwingine wanapokuja na taarifa hizi, kwa sababu leo tuko kwenye *quarter* ya tatu tunakaribia ya nne sasa basi tupate data za *quarter* ya pili ili data za *quarter* ya kwanza ambazo zinakuwa mpaka 9.7 zinaweza zikawa zimepitwa kidogo na wakati. Tungepata za *quarter* ya pili zingetuonesha uhalisia wa nini kunaendelea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napitia ripoti hii nikilinganisha ninaona kwenye bajeti ambayo walipata mwaka jana takribani bilioni 83.4 na mwaka huu wamepata 89.3. Sasa nikiangalia kwenye maendeleo, mwaka jana tulikuwa na asilimia 26.4, mwaka huu tuna asilimia 25.9 maana yake maendeleo pesa yake inazidi kupungua kwa maana ya pesa nzima inayotolewa lakini bado sekta hii inatakiwa ikue. Kwa hiyo nilitegemea kwa sababu sekta hii inatakiwa ikue basi pesa ya maendeleo mwaka jana ya iwe kidogo ya mwaka huu iwe nyingi. Mwaka huu inaonekana kama ni nyingi kidogo lakini *percent* yao kwa maana ya pesa ya jumla ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe tu hapo, kwa sababu ndipo mahali ambapo sisi tunaotoka kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo; nishukuru nimepata taarifa leo kwamba asilimia 80 ya madini yanayochangia kwenye Pato hili la Taifa ni dhahabu na mimi natoka sehemu wanayochimba dhahabu. Kwa hiyo nilitegemea kabisa hii pesa ya maendeleo inapoongezeka ndipo fedha ya *STAMICO* ilipo, ndipo fedha ya *GST* ilipo wanaoweza kufanya utafiti na kutupatia kanzi data ya madini yako wapi na watu wetu wakachimbe kwa urahisi. Huku

ndiko fedha ya *STAMICO* Ilipo, mahali ambapo wanaweza kununua vifaa vya kwenda kuwasaidia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lakini niseme tu kama changamoto, hata mwaka jana niliona *STAMICO* wamepata mitambo ambayo inasaidia wachimbaji wadogo lakini nikifanya sensa jimboni kwangu wanakochimba sana ni wapi sasa ambako *STAMICO* wameanza ku-*support* kwa mitambo ile wachimbaji wadogo, sipaoni. Kwa hiyo niwaombe sana Wizara, inawezekana tukawa na mitambo lakini kwenye utekelezaji, kwenye *implementation plan* kukawa kuna tatizo. Tumeona kuna mitambo ya bilioni nne lakini bado kwa wananchi hatujaona ile *impact* kubwa. Kwa hiyo niwaombe sana watu wa *STAMICO* waende na data za kutuonesha ni wapi wamewasaidia wachimbaji wadogo ili tuweze kupata mchango mkubwa wa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu cha pili ambacho nilitaka nikiseme hapa ni kile ambacho ndugu yangu Kigua alikisema hapa, kuhusu leseni. Mwaka huu tumeshatoa leseni 6,381 na malengo yalikuwa elfu sita mia moja kama sitini na kitu hivi, maana yake tumezidisha lile lengo, maana yake kazi inayofanyika ya kukata leseni ni nzuri sana. Changamoto niliyonayo kama aliyosema mwenzangu asubuhi, hapa kwenye Sheria ya *Mineral Right* na Sheria ya *Surface Right* kuna changamoto kubwa. Tunaonekana kabisa mchango kwa Pato la Taifa ni mkubwa na fedha ya madini ni nyingi lakini kiuhalisia wananchi wakaida wanaotoka vijijini wanazidi kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanazidi kuwa maskini kwa sababu gani? hawa wenye leseni wengi wanaotajwa hapa ni wale wanaoenda kuingia kwenye mfumo huu wa sasa wa kidigitali. Mwananchi wa kawaida kwa elimu ya kawaida huo mfumo hawaujui, na ndugu zangu wanaoshughulikia mtandao hata *3G* kule kijijini haipo anawezaje ku *access portal* ile ilhali *3G*

haipo? Kwa hiyo kimsingi wanaoweza ku-*access* ni watu wa mjini. Kwa hiyo leseni zote hizi zitakuwa ni za watu, wajanja wa mjini, na wale wananchi wetu kule chini wakiwa hawana leseni yoyote inayoweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye eneo hili, watu wetu wa ardhi na watu wetu wa madini fanyeni hii *surface right* na *mineral right* isomane, ikisomana maana yake tutapunguza haya malalamiko. Mimi mara nyingi huwa nina mifano ya wazi; nimebahatika kutembelea maeneo yanaitwa Kaseme, kata ya Kaseme pale kwetu. Moja ya hoja ambayo waliyokuwa wanazungumzia ni hii. Mtu jioni ameona vimacho macho vya dhahabu eneo lile, asubuhi akiamka anaambiwa kuna mtu alishaingia kwenye mfumo amekatiwa leseni tayari kwa hiyo eneo lile ni la kwake chini kule. Sasa yeye anabaki kuanza kubabaika anaambiwa analipwa shilingi ngapi hajui kwa sababu sheria hizi hazijulikani na elimu hatujatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu wa madini, hebu tujikite kutoa elimu kwanza kwa wananchi na tuwafundishe hii *portal* tunaingiaje. Kwa sababu leo hii nikimpigia mtu yeyote kijijini nikamwambia unaifahamu hiyo *portal* ya madini wanayoingia anasema hiki ni kitu fulani cha ajabu tu, hakijui. Hebu tuwape elimu hao watu ili kusudi na wao waweze kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo wamekaa miaka 20, kesho wanaambiwa *mineral right* kuna mtu anachimba anamwambia nitakulipa shilingi laki moja moja kila hekari yako moja, ana hekari 29 maana yake analipwa milioni mbili, huyo anayechimba anapata ela ya kutosha lakini huyu mtu anabaki kuwa maskini. Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu wa madini tutoe elimu kwa wananchi wale wa kawaida ili kusudi wajue nini wafanye kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaweza kupata maendeleo kwenye mdini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa malengo ambayo umeweka hapa, vipaumbele vyako. Umesema wazi kabisa kwamba unaenda kuwaendeleza wachimbaji wadogo. Nikushukuru vile vile nimeona unakwenda kujenga Jengo la Afisa Madini wa Mkoa wa geita kwa fedha nyingine inayobaki Wizarani. Nikuombe sana, wakati unalijenga hili vile vile tuhakikishe kwamba tunajenga uwezo wa wananchi wetu kuendelea kuchangia kwenye eneo hili. Tukifanya vizuri kwenye eneo hili la madini nina uhakika kuwa mchango wa Taifa badala ya kuwa asilimia kumi utakuwa asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Magessa. Mheshimiwa Riziki Said Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kunijalia na kutujalia sisi sote tukiweo hapa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamo wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Madini na Watendaji wa Wizara ya Madini. Mheshimiwa Rais tarehe 17 aliweka Saini mkataba mkubwa wa dola milioni 667. Mkataba huu unakwenda kuleta uchumi mkubwa katika Mikoa ya Lindi, Songwe na Mkoa wa Morogoro. Mikoa hii kwa muda mrefu ilikuwa inasemekana kwamba ina madini ya kutosha lakini ilikuwa bado kigugumizi. Sasa, kitendo cha Mheshimiwa Rais kufungua na kuingia katika mikataba rasmi kwa kweli tunaona kabisa Lindi kuchele. Naona Ruangwa kuna dhahabu, *graphite* na madini madogo madogo. Tunaona Liwale kuna dhahabu lakini ndani ya Selous kuna wachimbaji, ambayo tunaona wanachimba kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa Serikali itakuwa macho, wale waliopewa vitalu kule ndani wasitufanye shamba la bibi, tunataka tuhakikishe yanayopatikana ndani ya Selous au yale madini kama kuna wachimbaji wanajificha ficha, hasa watu wenye sura pana; nilipata nafasi mimi ya kuzungukia na nilipewa muda na watu wangu wa Habari *Conservation,* wa kutembelea maeneo ya *corridor* ya Wanyama tukakuta maeneo watu wanachimba, lakini *financer* wakubwa ni sura pana. Sitaki kutaja majina watasema Riziki umetaja mananii ya watu lakini tafuteni ni na sura pana wanajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 nikiwa Kamati ya *PIC* nilikuja na *recommendation* kuwa *STAMICO* ifutwe kabisa imeingia katika hasara ya nchi, lakini hawa *STAMICO* walikuwa wameingia katika hasara ya nchi kwa ajili ya mikataba ambayo wao haikuwahusu. Ilikuwa ni mikataba midogo ambayo imeifanya *STAMICO* wawe *paralyzed;* lakini leo nataka nitoe ushahuda wangu mwenyewe *STAMICO* inakwenda juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 *STAMICO* imeweza kupeleka gawio la Serikali bilioni 2.5, na mwaka huu tunategemea kupata bilioni tano kwa taasisi ambayo ilishakufa haikuwa na mishahara na haikuwa na uwezo wowote. Lakini, kwa kupitia Mkurugenzi Mkuu, kwa uwezo aliokuwa nao wakishirikiana na watendaji wa *STAMICO* sasa *STAMICO* ni taasisi moja wapo inayoongoza, na inafanya kazi kubwa ya kuleta Tato la Taifa. Hongera sana Mkurugenzi Mkuu Venant Mwase, endelea kufanya kazi, Watanzania tuna matumaini makubwa na wewe. Sasa hivi nenda Lindi kahakikishe kila kanda wanafanya *competition* ya kujua yako wapi madini ili watu wa pale waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kamati ya *LAAC* mwaka 2007 nikatembelea Geita. Ilikuwa kwamba katika mikoa sita

maskini na Geita mojawapo, leo nimeenda Geita nakuta mpaka *traffic lights* ziko barabarani. Nimetoka Geita, Katoro mpaka Bwanga watu wa kule sasa hivi unaona kabisa maisha yao mazuri. Niwapongeze Rais wa Madini Mr. Bina hongera sana kwa kazi kubwa unayoifanya kuwasimamia wachimbaji wadogo wadogo, ambao nao sasa wananufaika. Nimpongeze mwanamke shujaa Semeni John, huyu ni mwenyekiti wa wanawake wa wachimbaji wadogo wadogo. Tulikuwa kwenye mkutano mkubwa sana wa wachimbaji wadogo wadogo, kwakweli ule mkutano umetufanya tufarijike sana. Wanawake, vijana na wenye ulemavu ndio wanaoingiza *forty percent* ya uchumi mkubwa wa dhahabu; lakini hawana vitendea kazi, hawana mitaji; ni kundi ambalo linachimba katika mazingira magumu. Huko ndiko Serikali inapaswa ipambane na isimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri tulikuwa naye anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha tasnia hii inakwenda vizuri. Hongera sana Doto Biteko, mtoto msikivu, mwenye heshima, Mwenyezi Mungu azidi kukubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninazungumzia sekta ya chumvi. Mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani yote mpaka Tanga ni mikoa ambayo ilikuwa kando kando ya Bahari inashughulika zao la chumvi; hili zao lilikufa kabisa. Leo *STAMICO* wameamua kulifufua hili zao la chumvi kwa kutengeneza data ya kuhakikisha kwamba wanawajua wachimbaji wote wanafanya kazi gani ili kuweza kuingia katika soko la Afrika na *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chumvi inahitajika Rwanda, Malawi, Zambia mpaka Congo pamoja na Uganda. Kwa kweli akisimamia hili eneo na wananchi hawa wakanufaika na uchimbaji wao wa chumvi kwa kweli suala la umaskini Mikoa hii ya Kanda ya Pwani itakuwa imepungua; nimpongeze sana kwa kazi anayofanya. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, anafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja katika wachimbaji wadogo wadogo walemavu. Mimi ni shuhuda nilikwenda Mbogwe nikishirikiana na madini kwenda kugawa vifaa na mitambo kwa walemavu viziwi, wenye usikivu hafifu. Kumbe walemavu hawa mkiwatengea mazingira mazuri wanaweza kuleta uchumi mkubwa sana. Ningeomba baadhi ya Wizara zingine ziige mifano hii. Vile vile ningetamani mifumo iongee. Katika Wizara ya Wanawake tujue kuna wanawake wangapi wanachimba madini, hiyo naipa kazi Wizara; waje hapa watuambie wanawake hawa wanachimba madini. Lakini vile vile Wizara ya kazi wajue vijana wangapi wanafanya kazi ya kuchimba madini ili mafunzo yazidi kuendelea. Ninashukuru Waziri wa Fedha tayari ametoa bilioni tatu kwa ajili ya mafunzo kwa vijana. Hizi zikitumika kuwasomesha na kuwapa mafunzo maalum ninaimani baada ya miaka tunazungumzia utajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu? Tuna kanda ya kati ina madini, kanda ya kusini ina madini, kanda ya kaskazini tumeona Mererani kote kuna madini angalau kule kumeshapewa mwelekeo mkubwa. Matumaini yangu kwa sasa hivi Serikali iangalie, mikoa hii ambayo ina madini kwa wingi haya madini yote yanakwenda panya *road*, na katika kwenda panya *road* hatuoni manufaa ndio maana kama sasa hivi unaona *only forty percent* inakwenda kwa wachimbaji ambao wanaonekana wadogo wadogo. Ina maana madini mengi yanayotoka hapa yanaingia katika panya *road* yanaingia katika utoroshaji kwenda nje. Sisi wenyewe tukiwa tunategemea kuwa na matumaini makubwa sasa hivi tupambane nyumbani kwanza, mzalendo kwanza, Mtanzania kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wengine wanakuja misamaha ya kodi, misamaha ya mafuta yote wapewe, misamaha ya mitambo, inakuwaje wanashindana na watu ambao wanatumia vingondoli na majembe wakawa wanafika *forty percent*? Hawa wachimbaji wadogowadogo wakiongozwa

na akina John Bina, kina Semeni ninaamini kuwa watu hawa watatoka vizuri na wataweza kufanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali, na nishukuru sana Serikali, Mheshimiwa Rais katika mradi huu ambao umekwenda Mikoa hiyo, hasa mimi Lindi, nasema ninamuunga mkono kwa asilimia mia moja. Ninakwenda Lindi kusimamia wachimbaji wadogo wadogo. Wanawake na vijana sasa hivi ni muda mwafaka wa kuwaingizia uchumi. Hii tunayopata sasa hivi mwakani tutegemee kupata maradufu. Mheshimiwa Waziri nipe nguvu, niko tayari kama balozi wako kusimamia hili na wala sitakuangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya kusema hapa ninawashukuru sana na ahsanteni sana; Mungu Ibariki Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Said Lulida, tunashukuru sana. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mheshimiwa Kassim Idd ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Madini kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 Bunge hili lilitunga Sheria inayoitwa *Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act, 2017*, ambayo ni Sheria inayoeleza umiliki wa milele wa rasilimali na maliasili za nchi yetu. Na lengo la Sheria hii ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanatamkwa kwenye Sheria kwamba ndio wamiliki wa rasilimali za Taifa hili na maliasili zote. Niwapongeze sana Wabunge waliokuwepo wakati huo kwa wakishiriki kutunga Sheria hii. Kwa sababu ukweli ni kwamba Watanzania na wanachi wote, sisi ni miongoni mwao ndio, wamiliki wa milele wa rasilimali zetu. Lakini haitoshi kusema

kwenye Sheria kwamba Watanzania ndio wamiliki wa milele wa rasilimali na maliasili ya nchi yetu tukaishia hapo bila kuonesha kwa vitendo athari ya kimaendeleo inayotokana na umiliki wao wa milele wa rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na utangulizi wa Sheria hiyo ambayo imetungwa na chombo hiki kitukufu ambacho hata leo hii mimi nimesimama hapa naongea kwacho kwa sababu tukumbuke na tuone umuhimu wa chombo hiki kwenye Taifa hili. Kwa sababu kwenye chombo hiki kuna wawakilishi wa nchi nzima, Wabunge, Wawakilishi wa Majimbo yote Tanzania nzima wako kwenye chombo hiki. Maana yake uwakilishi wa Tanzania nzima wa hao wamiliki wa rasilimali za nchi yetu upo katika chombo hiki. Kwa hiyo, tunategemea pia kuona kwa namna kubwa wanaotajwa kama wamiliki wa milele wananufaika pia na rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza kuhusiana na Sekta ya Uziduaji *(Extractive Industry)* na namna ambavyo sisi wa kizazi cha leo tunatamani wasifanye makosa waliyofanya watangulizi wetu kwa kuacha mashimo ya dhahabu na almasi, wakati ukitoka tu kwenye mgodi nje kuna watoto wana shule wanakaa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa natambua jitihada ambazo zimefanyika mpaka leo kuna *CSR,* kuna miradi ambayo imetokana na uwekezaji ambao umefanywa kwenye Sekta ya Uziduaji. Hata hivyo bado, kama vijana na Watanzania ambao tunasema ndio wamiliki wa milele wa rasilimali zetu, tunatamani tushiriki katika *value chain* ya migodi, *value chain* ya madini yetu ambayo tunayo kwa sababu haitoshi kuitwa wamiliki wa milele, ni lazima tuoneshe na tuonekane kwa vitendo tumetajirika sisi binafsi kutokana na rasilimali tulizonazo kwenye ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015, Bunge hili lilitunga Sheria ya Uziduaji ambayo iliitwa *Extractive Industry Transparent and Accountability* na leo nitajikita hapo tu, uwazi na uwajibikaji kwenye mikataba ya Sekta ya Madini. Kwa wivu mkubwa sana, mimi kama mwakilishi wa chombo hiki kitukufu, nasikia wivu sana kama nitakuwa sijui nini kinaendelea katika makubaliano kati ya nchi yetu na mataifa mengine na kampuni nyingine za uziduaji kama haitajadiliwa kwenye Bunge hili kwa sababu tutajua vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wanaoshiriki kuingia mikataba hii ni binadamu, ndio maana tunahitaji vichwa hivi kutoka Tanzania nzima vishiriki katika kujua mikataba hii *line to line* ili tushauri kwa sababu hakuna mtu ana *bifu* na hii nchi, tunaipenda na tunataka rasilimali zetu ziwanufaishe Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Aprili nchi yetu imeingia makubaliano, wasiwasi wangu mkubwa sana athari ya Mikataba ya kutoletwa Bungeni imeanza kuonekana juzi. Waheshimiwa Wabunge wakiingia kwenye *tablet* zao *website* ya Kampuni inayoitwa *peak layer earth limite*d utaona mkataba wa Nguala - Songwe umesainiwa juzi hata mwezi haujapita. Kwenye Mkataba wale wa kampuni wanasema *project* ina-*expect* kutumia Shilingi Dola Milioni 320, lakini kwenye *website* ya Wizara inasema *project* inategemea kutumia shilingi Dola Milioni 439 *difference* ni Dola Milioni 119.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niamini ni *errors,* ni kukosea kwenye kuandika, lakini siamini kama nikukosea kwenye kuandika kwa tofauti kubwa kabisa ya fedha hizi ambazo ni sawa na zaidi Shilingi za Kitanzania Bilioni 276.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nisingezungumza hapa kama mkataba na mikataba ya *design* hii ikaletwa Bungeni tukajadili. Hakuna mtu ana *bifu* na mtu yeyote, hakuna mtu ana wasiwasi

na chochote katika nchi hii, bali tunataka tujue kwa sababu ya sheria ambazo zimetungwa na Bunge hili kwamba kila Mtanzania ni mmiliki wa milele wa rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu tuna mashimo ya *gold, tanzanite* na madini mengine tumeyaacha kule. Sasa hivi tunazungumza *critical Minerals, layer earth element* ni miongoni *mwa critical minerals,* ni kitu ambacho ni kipya na na tunakichukulia kama kipya, tunafikiri tunaweza kufanya kama tulivyofanya zamani. Sioni kama ni busara, kama ni sahihi kufanya kama tulivyofanya zamani. Natamani tuwe na jicho jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi hata Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabau za Serikali hana mikono kwenye kukagua mikataba ya madini inayoingiwa katika nchi yetu. *CAG* aliondolewa mamlaka kisheria ya kupitia hii mikataba na kuikagua. *The only provision* ambayo *CAG* anapewa ni ambayo ataombwa na *TEITI* kwenda kukagua mikataba hii tena ikitokea kuna hitilafu kwenye hesabu, si chini ya *one percent* kwenye hesabu ndogo ndogo ambayo ataomba na *TEITI.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kwanza, Ripoti za *TEITI* zote, kwa sababu *CAG* hana mamlaka kwenye ukaguzi wa mikataba, basi kwa sababu tumempa *TEITI,* basi wakati tunajadili ripoti za *CAG,* tujadili na ripoti za *TEITI* kwenye Bunge hili, ili sasa tupitie huko kwenda kuuliza nini kinaendelea kwenye mikataba yetu, kujua *in details what is going on* kwenye Sekta ya Uziduaji kwenye Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria ilitungwa na Bunge hili na sisi ni wajibu wetu kuitekeleza sheria. kwa hiyo, naomba sasa Sheria ya *Extractive Industry Transparent and Accountability* itekelezwe. Tuletewe mikataba iliyoingiwa na Serikali ili Bunge hili

kwa heshima yake lijadili kinaga ubaga na lijue mikataba ambayo Serikali yetu imeingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, *CAG* aruhusiwe kwenda kukagua mikataba kwa sababu sisi kama Bunge, *CAG* ndiyo jicho letu na ndiye tunamtegemea .

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kwa sababu sisi tumesema tunataka tutekeleze Sheria ya Watanzania ku-*enjoy* rasilimali zao, basi waziduaji na wachimbaji wadogo wa madini ni sehemu ya Watanzania ambao tunatamani washiriki na wao kiasi kusherehekea rasilimali ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa ninavyozungumza kuna mambo mawili. Kwanza, Serikali ilionesha nia ya kutaka kuwasaidia wachimbaji wadogo na kuna vitu wamewafanyia, lakini kuna *VAT* kubwa sana katika suala la umeme. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Madini watu wake wa migodi uunganishaji wao utasababisha watu wa madini waongeze kuchangia pato la Taifa, kwa sababu wanalipa kodi. Hata hivyo, kwa sababu wanarundikiwa madeni makubwa, wameunganishwa na umeme lakini wanatozwa *VAT* kiasi kubwa, kuna malimbikizo makubwa, wanashindwa kuendesha migodi, matokeo yake Serikali haipati pato na wachimbaji wadogo wanashindwa kupata pato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sasa Mheshimiwa Waziri atafute namna bora ya kuona namna gani anaweza kuwasaidia wachimbaji wadogo. Vile vile, hao hao wachimbaji wadogo kwenye upande mwingine kuna *tax exemption* walipewa kwenye vifaa vya kuwasaidia kuchimba madini, lakini wanaopewa *tax exemption* wanarudi wanakatwa tena na Serikali wakati wa kutoa vile vifaa bandarini. Kwa hiyo, sidhani ile nia bora ya kuwasaidia wachimbaji wadogo, kama tutakuwa tunaitekeleza kwa vitendo kama tunawapa kwa

mkono huu na tunachukua na mkono huu. Nchi hii ni ya kwetu wote na lengo letu wote tu-*enjoy* rasilimali za Taifa kwa pamoja na tuweze kunufaisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo atafuatiwa na Mheshimiwa Kassimu Iddi Iddi na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, naomba nitoe pongezi nyingi sana kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hasa katika usimamizi wa Sekta hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kutoa pongezi nyingi sana kwa Waziri wa Madini, ndugu yangu Mheshimiwa Dotto Biteko pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa kwa kazi kubwa wanayoifanya. Vile vile, niendelee kutoa pongezi kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ndugu yangu Kheri, wanafanya kazi kubwa kwa kushirikiana na Wakuu wa Taasisi zote ambazo zinasimamiwa na Wizara hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba hazidanganyi, tumeona jinsi gani Sekta ya Madini inavyozidi kupaa kwa kuongeza pato la Taifa kutoka asilimia 4.4 mwaka 2017 mpaka sasa hivi tunaongelea asilimia 9.7. Hii ni hatua kubwa sana, inastahili pongezi na kwa kweli kazi kubwa sana imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Madini tunaweza tukawa na madini yako chini ya ardhi na sisi Tanzania asilimia 90 ya madini tuliyonayo hatujayachimba. Pia madini yakiendelea

kukaa chini maana yake ni kwamba uchumi wake hatutauona katika mchango wa pato la Taifa.  Sasa nini kifanyike? Tunaona juhudi kubwa zinazofanyika, tuiombe leo Serikali, Wizara ya Fedha waangalie kwa jicho la kipekee hasa hizi Wizara ambazo zinazalisha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Wizara ziko hapa nyingi tofauti, Mheshimiwa Rais anatengeneza Serikali yake kwa kuunda Wizara mbalimbali, lakini tunatambua kabisa kuna Wizara za matumizi na tunawapongeza Mawaziri humu kwa kufanya kazi kubwa ya kutumia. tunawagongea makofi, wamejenga zahanati, madarasa, barabara na wamejenga na vitu vingine. Wizara zao zinafanya kazi ya kutumia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuangalie kipekee Wizara zinazokusanya fedha kwa ajili ya matumizi hayo na Wizara zinazokusanya fedha mojawapo ni hii Wizara ya Madini.  Wizara zinazokusanya fedha ikiwemo hii Wizara ya Madini, ni lazima tuzipe fedha za kutosha ili zilete fedha zaidi. Haiwezekani tukapata fedha nyingi bila ku-*invest* fedha kwenye Wizara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara ya Madini wanaipatia Bilioni 22 kwa ajili ya Maendeleo, leo tunawapa Bilioni 23, halafu tunawapa lengo la kukusanya trilioni 1.006, ni lazima tutambue kwamba ni lazima tuingize fedha kwenye miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunawawezesha wachimbaji wadogo wadogo ili kusudi wachimbe kwa tija, wapate fedha wao wenyewe, lakini wapeleke pato kubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wachimbaji wadogo ambao wanachangia asilimia 40, tuna wachimbaji wakubwa ambao wanachangia asilimia 60. Wachimbaji wakubwa ni wachacvhe lakini wanachangia kingi.  Hawa leo na kesho mmoja au wawili waki-*drop,* itatokea *shake* kubwa kwenye mchango wa mapato,

kwa sababu wanachangia kingi na wako wachache. Kwa hiyo, wawili au watatu kwa namna moja au nyingine ikitokea tatizo mmoja au wawili wakashindwa kuchimba, madhara yake ni makubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wanaochangia asilimia 40, ndio walioingiza ajira asilimia 80 ya uchimbaji na ndio Watanzania wengi wako kule wanachimba. Pia hii asilimia 40 wawili, watatu, wanne wakishindwa, *impact* haitaonekana kwa sababu ni wengi wako wachache wadogo wadogo wanachangia kingi asilimia 40. Tukiwawezesha hawa tuna hakika ni ajira ya Watanzania na wakati huo huo ndio watakuwa wazalishaji wakubwa na kuingiza fedha katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Tuendelee kuwapa fedha *GST* na *STAMICO* ili wajikite katika uwekezaji wa kufanya utafiti, kwa sababu utafiti ndio njia pekee ya kuwafanya watu wachimbe kwa uhakika na kuleta pato la Taifa. Wachimbaji wadogo wakichimba kwa uhakika, pato la Taifa litaongezeka. Hivyo basi, tunaomba *GST* wawezeshwe, waendelee kuongezewa fedha kwa ajili ya mikakati ya kufanya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya kitu kinaitwa *resource estimation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji sasa hivi wanatoka nje ya nchi na wengine wanatambua kuna dhahabu hapa, lakini hawatambui dhahabu hiyo ipo kwa kiasi gani na wa-*invest* kwa kiasi gani ili waweze kupata kipato. Tukifanya *resource estimation* vizuri kupitia *GST,* itakuwa ni rahisi kupata wawekezaji na watakuja kwa masharti nafuu na watachimba kwa uhakika kwa sababu tayari utafiti umefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *GST* leo wamekosa kibali cha kuajiri watafiti kwa maana ya watumishi wa *GST.* Naomba

nishauri, kwenye Sekta ya Afya pamoja na Sekta ya Elimu tulitoa watu wa kujitolea *volunteerism,* watu wa kujitolea wameorodheshwa wakafanya kazi kwenye hizo Sekta za Afya na Elimu. Niwaombe hata *GST* ikiwezekana wako vijana wengi wana hizo taaluma za utafiti, Serikali itafute fedha, wajitolee, waingie kule wafanye kazi za kujitolea bila kuajiriwa. Hawa wafanye, ikitokea nafasi ya kuajiri wawaajiri hao. Waende wakafanye utafiti watawasaidia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi ya kuongea. Kingine ni suala la ufungaji wa migodi. Ufungaji huu huwa unaanza wakati migodi inaanza. Mpango wa kufunga migodi pamoja na kulinda mazingira huwa ni mpango unaoanza wakati mgodi unaanza. Leo Mheshimiwa Waziri ametueleza hapa kuna baadhi ya migodi imezuiliwa kufunga kwa sababu hawajafuata tu taratibu. Niwaombe Wizara wawe karibu na wale wanaoanzisha migodi. Ile migodi mipya, wanapoanzisha migodi hapo hapo na *plan* ya kufunga iwepo. Leo ukienda Buzwagi kuna *pit* kubwa imeshindwa kufunikwa, ni kwa sababu inawezekana kabisa kulikuwa kuna utaratibu umekiukwa toka mwanzo wakati mgodi unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Liganga na Mchuchuma. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, leseni ya Liganga na Mchuchuma mwenzangu Mheshimiwa Profesa Manya alikuwa anazungumza hapa akaishia njiani. Liganga na Mchuchuma leseni zimetoka mwaka 2016, tuna chuma kingi zaidi ya tani milioni 150, tuna makaa ya mawe zaidi ya tani milioni 400 zipo zimekaa *dormant,* hazifanyi kazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu ameshindwa kuchimba kuna Sheria ya Madini, kwa nini Waziri asifute hizi leseni? Kwa sababu kutokuchimba kwa madini ya Liganga na Mchuchuma pale yale madini ya makaa ya mawe pamoja na madini ya chuma anayekosa fedha ni Waziri haingizi kwenye wizara yake.

Kwa hiyo, mchango wa Shilingi Trilioni moja, nina hakika ni mdogo kama tutajikita vizuri katika mipango yetu tutapata fedha zaidi. Kesi ya *NDC* na wale wawekezaji sijui Wachina Waziri aache waendelee na kesi, yeye afute leseni, ampe *STAMICO* achimbe, watu waendelee kufanya kazi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nyongo. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ili leo niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Madini.

Kwanza nianze kabisa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kujadili hotuba ya bajeti ya leo. Vile vile, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitapeleka shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika nchi hii lakini hasa katika Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Rais, Mama yangu Samia Suluhu Hassan ametuheshimisha wachimbaji wadogo wadogo kwenye Nchi hii

ya Tanzania. Historia inaonesha katika watu waliokuwa wakidharaurika katika nchi hii ilikuwa ni wachimbaji. Hata hivyo, leo hii unapozungumzia habari ya wachimbaji wadogo wadogo unaona kabisa ni watu wenye heshima zao, wanaweza kwenda wakakaa sehemu wakaonekana ni watu wenye heshima, wakawekeza, wanafanya mambo yao kisomi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Biteko anafanya kazi kubwa sana. Asubuhi hapa nimemsikia Mbunge mwenzangu akishauri Serikali waone kuwa na mpango wa kuweza kumpatia *certificate,* lakini nasema kama vyama vya wachimbaji vinanisikia huko viliko kwa maana ya *FEMATA, TAWOMA* na nimeona hapa chama kimoja cha wachimbaji vijana kiko hapa, wanafanya kazi kubwa kwa maana ya kusimamia wachimbaji vijana katika Sekta ya Madini. Kuna haja kubwa ya kumjengea sanamu Mheshimiwa Dkt. Dotto Biteko, ametufanyia kazi kubwa sana kwenye Wizara hii ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumza mchimbaji mdogo mdogo aliyekuwa akichangia asilimia 20 na sasa asilimia 40, sio miujiza. Ni mipango mzuri, mikakati mizuri inayosimamiwa na Dkt. Dotto Biteko chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nimpongeze hata Naibu wake Waziri na niwe wazi, katika Wizara ya Madini, Mheshimiwa Rais amefanya uchaguzi mzuri kabisa. Ukienda kwa Mheshimiwa Waziri ni msikivu na mnyenyekevu, ukienda kwa Naibu Waziri naye ni msikivu na mnyenyekevu, ukienda kwa Katibu Mkuu ndio usiseme meno 32 wakati wote sijui anachukia saa ngapi Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Wizara hii. Ukienda kwa Mtendaji Mkuu wa Tume, yuko vizuri, Kamishina naye yuko vizuri. Hiyo

inatufanya sisi wachimbaji wadogo wdogo kuwa na moyo wa kuwekeza na kuonesha kwamba Serikali kweli inatujali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana, leo hii tunazungumzia habari ya *STAMICO*. Utaona kabisa *STAMICO* hapo mwanzoni ilivyokuwa na sasa ilipo inafanya kazi nzuri sana. Wameanzisha miradi mbalimbali na leo hii wanazungumzia habari ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kutunza mazingira.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassim kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Kassim kwamba kwa wema wa Mheshimiwa Dkt. Biteko na mwenzake Mheshimiwa Kiruswa, leo ninapozungumza wananchi wa Nyamongo hawanywi maji ya sumu tena, wanakunywa maji safi ya bomba. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Biteko kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassim taarifa unaipokea?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii mimi naipokea kwa mikono yote miwili, Dkt. Biteko anafanya kazi nzuri sana, hata siyo Nyamongo tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mwita Waitara ukija Kata ya Bulyanhulu na Mheshimiwa Amar yupo pale Nyang'wale utaona fedha nyingi ya *CSR* ambayo inatumika kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Msalala tunazungumzia tumemaliza zahanati 34 kwa mpigo, yote haya ni matunda ya Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Biteko.

Tunazungumzia habari ya vituo vya afya hapa juzi nilizungumzia habari ya lami tayari wako *site* wanaendelea kumalizia taratibu za kuanza ujenzi wa lami kilomita 76 kiasi cha Shilingi Dola Milioni 40 yote haya ni matunda mazuri ya Mheshimiwa Dkt. Biteko chini ya uangalizi wa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu mpendwa kipenzi cha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka kuzungumzia hapa, naomba nishauri tuna Vyama vya Wachimbaji hivi ambavyo kazi yao ni kusaidia wachimbaji, niombe sana *STAMICO* na Mheshimiwa Waziri niombe sana vyama hivi hebu oneni namna ya kuvisaidia viweze kuwasaidia kwa kazi nzuri mnayoifanya. Leo hii tunazungumzia habari ya uchimbaji kuna wachimbaji vijana wapo lakini ukiwaangalia kutafuta nani anawasaidia vijana hawa huoni na ndiyo maana umeona kuna taasisi imeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia vijana. Leo hii utaona kuna watu wanauza madila nani anawasaidia madila leo hii ukienda utaona kuna watu wana-*plant* nani anawasaidia *plant?* Vyama hivi ni lazima vikae chini vione namna ya kuunda *reform,* waunde umoja na umoja huu utasaidia katika kuhakikisha kwamba inaisaidia Wizara ili iweze kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie habari ya wachimbaji kwenye Jimbo langu la Msalala, amezungumza Mheshimiwa Nusrat Hanje nimuombe Mheshimiwa January Makamba na hili nitalizungumzia tunavyokuja kuzungumzia suala la umeme, changamoto kubwa ya umeme inakwamisha shughuli za madini katika maeneo yetu, hilo nitalizungumzia nitakapokuja kuchangia kwenye suala zima la *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri wachimbaji wadogo wadogo hatuendelei kwa sababu ya kukosa mikopo. Leo katika hotuba yako nimeisikiliza vizuri, tumepongeza hapa mabenki yamefanya kazi kubwa ya kukopesha wachimbaji wadogowadogo, lakini nataka

nikwambie inawezekana takwimu hizi za ukopeshaji haya mabenki wanakopesha wachimbaji wakubwa, lakini bado kwa wachimbaji wadogowadogo kupitia imani ambayo wewe mwenyewe umeijenga bado hawakopesheki, hakuna benki ambayo inakopesha mchimbaji mdogomdogo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri na niombe *BOT,* tumeona *BOT* imetoa fedha nyingi zaidi ya Bilioni kadhaa kuyapa mabenki ili mabenki haya yaweze kuwakopesha wachimbaji wadogowadogo, lakini unapoenda mchimbaji mdogomdogo kukopa fedha kwenye mabenki haya haukopesheki mpaka wanakuomba aidha ufungue biashara nyingine au uwe na dhamana nyingine, wakukopeshe fedha zile kupitia mgongo wa biashara nyingine na siyo madini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kama wachimbaji wadogowadogo inapelekea wanakosa mitaji ya kuendeleza shughuli za uchimbaji leo hii utaona, akija hapa Mzungu na *briefcase* akapeleka *plan* kwenye mabenki haya anapewa mkopo lakini akienda ngozi nyeusi kwenda kuomba mkopo hapewi, mabenki haya yatueleze kama yana ushahidi yamempatia nani mchimbaji mdogomdogo watueleze waweke ushahidi hapa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest,* mimi ni mchimbaji ninachokisema hiki ninauhakika nacho, hakuna mchimbaji mdogomdogo ambaye kakopeshwa fedha na mabenki haya. Sasa kuna haja ya kukaa na mabenki haya niiombe *BOT* ikae na mabenki haya, kwanza ukiona *BOT* inawapa mikopo mabenki haya kwa asilimia ndogo sana, asilimia tisa na lengo la mikopo hii ni kutukopesha wachimbaji wadogowadogo lakini utaona wachimbaji wadogowadogo bado hawaaminiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Mheshimiwa Waziri kufanya kazi kubwa ya kuwapatia leseni wachimbaji wadogowadogo lakini bado leseni zao hazitumiki kama kigezo cha wao kupatiwa mikopo, kwa hiyo niombe sana na niombe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ananisikia waweke mkakati wa kuhakikisha kwamba wanakopesha wachimbaji wadogowadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii hapo zamani wachimbaji tulikuwa tunakopeshwa walikuwa wanakopeshwa wote kwa maana ya mikopo na baadae Serikali iliondoa, sasa wewe mwenyewe umetueleza Mheshimiwa Waziri kwamba wachimbaji wa sasa ni wa kisasa, hebu nikuombe sasa kwa sababu tayari wachimbaji wa sasa wako kwenye *reform,* mikopo iliyokuwa ikikopeshwa iweze kurudi sasa ili iwasaidie wachimbaji kuelekeza kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyongo amezungumza hapa Habari ya *GST*. *GST* inaendelea kufanya vizuri, niombe waendelee kufanya kazi kubwa kuzunguka maeneo yetu, waweze kuandaa ripoti wafanye *reserve estimate,* wawapatie wachimbaji wadogowadogo na Wizara mkitupatia hiyo mikopo wachimbaji wadogowadogo maana yake ni kwamba itaenda kusaidia katika kuhakikisha kwamba sekta yako Mheshimiwa Waziri inakua kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia habari ya ufungaji migodi hapa Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana pale Kahama tuna mgodi wa Buzwagi ambao umefungwa, *plan* iliyopo pale ni kwenda kufanya kuwa eneo la *economic zone* sikatai ni wazo zuri, lakini niendelee kuomba sana kwa sababu Kahama nzima inategemea uchumi wa madini na leseni ile kwa sababu hawa watu wanaenda kuiachia, na kwa kuwa wanaenda kuiachia bado ina madini ambayo wakipewa wachimbaji wadogowadogo wanaweza wakapata fedha

kupitia maeneo yale. Ninaomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana ikikupendeza hebu gaweni ile leseni sasa kwa wachimbaji wadogowadogo pale Buzwagi ili iweze kukuza uchumi wa Kahama Mjini na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya *GST* na *STAMICO,* leo hii utaona *GST* katika maeneo haya wanazo maabara za upimaji madini katika Jiji la Dodoma na niwapongeze Mheshimiwa Waziri wameenda kufungua maabara nyingine Geita. Sasa maeneo mengine mengi Mheshimiwa Waziri kama Chunya, Kahama ambayo ndiyo maeneo ambayo yanazalisha dhahabu kwa wingi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kuanzisha maabara kubwa kwenye maeneo haya ili tuwarahisishie wachimbaji wadogowadogo wanapoweza kuchimba madini yao waende wakapime sampuli zao kwenye maabara za Serikali ambazo zitawapa uhakika, kwa sababu wachimbaji wengi wanafilisika sana kwa sababu ya vipimo vya maabara hizi zilizoko mitaani ambazo hazina uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana watu wa *GST*..

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kassim muda wako umeisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga hoja kwa asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Madini. Namshukuru Waziri wa Madini, Naibu Waziri, Katibu na Viongozi wote wa Wizara ya Madini, wanafanya vizuri sana

kwenye Wizara hii, wameitoa mbali na sasa hivi inakua ilipotoka asilimia 4.7 mpaka hiyo asilimia Tisa sasa inaenda ni jambo la kupongeza sana. Ahsanteni sana kwa kuifanya Wizara ionekane ni Wizara ya maana sana kwa sasa hivi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa haya ma-"b" anayoweza kuweka kwenye Wizara ya Madini tumeona mikataba ya ma–"bi" na ma–"bi" inaongezeka maana yake yote ni maono yake katika nchi hii ya kuona madini yetu yatumike vizuri kutoka ardhini yaingie kwa wananchi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambayo anafanya Mheshimiwa Waziri Dotto, kusema kweli wachimbaji wadogo amewatoa mbali sana hawakuwa hapo, ametoa maeneo mengi sana amesaidia migodi mingi sana kwenye mazingira lakini nimuombe Mheshimiwa Dotto atazame maeneo kama matatu ya wachimbaji wadogo, wakiwemo wachimbaji wadogo wa Jimbo langu wanaitwa Nyabuzume na Nyaburundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni *PL* hizi leseni kubwa za utafiti zinachukuliwa na wachimbaji wakubwa wanakaa nazo miaka, hata kama hawachimbi wachimbaji wadogo wanazunguka hapo pembeni hakuna kupewa, wanakaa nazo miaka mingi, utafiti miaka mia, kwa hiyo nadhani hilo nalo uliangalie ili wachimbaji wadogo wanaozunguka migodi mikubwa au maeneo ya wachimbaji wakubwa waachie maeneo mengine kwa wachimbaji wadogo, hilo ni jambo kubwa sana kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *PML* hizi nazo ni leseni ndogo zinazokatwa wachimbaji wadogo, nao wamekuwa kama mafisadi na wenyewe. Wengine ana *PML* tano, 10, 40, 50 zinakaa kwa muda mrefu wenzao wanazunguka humu ndani hamna kitu, hata wale wengine viongozi wao nao wana ma-*PL*

ya kutosha, hilo nalo uende ulitazame viongozi wachimbaji wadogo wapewe maeneo yanayotosha kwa ajili ya uchimbaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni mitaji. Wamezungumza Wabunge wengi hapa, nikamsikiliza mwingine anasema twende tukamwambie Mheshimiwa Mwigulu Wizara ya Fedha itupe fedha, hizo ni ndoto! Kuomba Wizara ya Fedha ikupe mikopo ya wachimbaji wadogo hizo ni ndoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dotto nikuombe, mimi najiuliza hivi watu wa mbolea wanafanyaje amezungumza hapa Mheshimiwa Nyongo hapa, tunakopesha tunaleta mbolea tunagawa kwa wakulima tunaipa ruzuku mbolea maana yake hiyo ruzuku inaenda kutusaidia kwenye maeneo yetu inaleta chakula humu ndani. Sasa kwa nini hatutoi ruzuku kwa wachimbaji wadogo, ambao ndiyo wanaleta fedha kwenye nchi hii, wachimbaji wadogo ndio wanaoleta fedha hatuwapi ruzuku kwa nini sasa? Na hii kazi inatakiwa kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa dotto nikuambie kitu kioja nenda NMB benki, nenda CRDB benki nenda Benki ya Exim, nenda benki zote unazoona zinafaa uweke nao mkatabawa kukopesha wachimbaji wadogo. Mchimbaji mdogo asiende benki mwenyewe, umpeleke wewe ufanye kitengo humu kwenye Wizara yako, uende uongee nao wako tayari kuwakopesha wachimbaji lakini ukisubiri Wizara ya Fedha ikupe fedha na miradi mikubwa tuliyonayo ya mikakati hizo ndoto, hizo ndoto kama jina lako ni ndoto tu! nendeni CRDB, NMB kaa nao panga nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano, wanapoenda wachimbaji wadogo wanaambiwa kwamba vifaa unavyotaka ni Milioni 100, Milioni 100 wanataka asilimia 20, asilimia 20 hapa unazungumza milioni 200 au milioni 50 wanapata wapi hiyo Milioni 50? Unawaambia ulete nyumba, ulete kila kitu watapata wapi hizo nyumba zinatoka wapi? Hawakopeshwi! Kwa hiyo, wewe

chukua hicho kitengo chukua wachimbaji wadogo walete maandiko yao, *proposal* zao uzione, nenda kwenye mabenki ongea nao, mabenki wawakopeshe ninyi mtakuwa ni dhamana ya hawa wachimbaji wadogo, kwa hiyo naomba hili nalo ulichukue uweze kuliweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo lipo Mheshimiwa Dotto nakushukuru sana kwanza kwa kufungulia wale watu wa Kinyambwiga, wachimbaji wadogo wanapokuwa na migogoro mnawafungia kwa muda mrefu sana, mimi huwa najiuliza maswali mengi sana hivi ulishaona Wabunge tunaoshindwa kwenye uchaguzi? Ulishamuona Mbunge mzuri aliyeshindwa kwenye uchaguzi? Unajua anawakimbia hata watu hataki kuwaona, sasa kama kazi yako wewe inayokupa chakula au inayokuweka uwe na heshima ukishindwa unasononeka, kwa nini umfungie mchimbaji mdogo miezi sita, mwaka, anakula wapi? Kuna mamantilie wako hapo, kuna watu wa maji wanapeleka, kuna watu wa maziwa wanapeleka mnafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa madini unakua kwa asilimia 9.7 mpaka asilimia 10 inaenda, kama uchumi unakua na wachimbaji wadogo wanakuwa maskini maana yake nini? Maana yake haufunganishwi sasa na uchumi wa wachimbaji wadogo. Nikumombe Mheshimiwa Doto kwamba wachimbaji wadogo sasa umewapeleka mahali pazuri, uwasimamie wakue. Kadri uchumi wa madini unavyokua na wenyewe wakue sasa waweze kuendelea kwenye shughuli za kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna vitu vingi vya kujiuliza hapa wachimbaji wadogo wakipata madini mahali mkubwa naye anakata leseni anakaa nayo wanawakimbiza mnaenda kuwafungia, yaani wao wamekuwa kama vibarua, wakipata hapa madini wanahama wakipata madini wanahama hivi haitokei siku moja wakapata madini mkawapa? Mkasema sasa

tunawapa eneo hili lote, kwa hiyo sisi wachimbaji wadogo tukiwa tunapata madini maeneo mengine mnawagawia watu wengine wakubwa sisi tunakuwa kama vibarua tu. Ninakuomba kwenye hilo nalo ulitazame vizuri ili wachimbaji wadogo hawa wapate mitaji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la vifaa, kama ni mabenki basi kama ni Wizara ya Madini kwa nini isikope sasa, kopeni hivyo vifaa vya wachimbaji wadogo halafu ninyi muwape kwa sababu ninyi ndiyo mnawajua, kwa nini muwambie benki ziwape na hazina dhamana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kwamba ninyi kopeni hivyo vifaa vitafuteni, kwa mfano watu sasa wanataka kupima kufanya utafiti wa kutosha kujua hapa kuna madini wasihamehame, madini kama vifaa vile vya utafiti mita moja ni rola 130 ukifanya utafiti. Kwa hiyo unapotoboa matundu matatu ni dola kama 390, sasa dola kama 300 maana yake ni kwa hela ya kitanzania mchimbaji mdogo hawezi kufanya utafiti. Kwanini kama walivyosema *STAMICO, GS*T msiwape fedha wakawasaidia wachimbaji wadogo kuwapimia maeneo ambayo wanajua kwamba kuna dhahabu, hapa sasa wamekuwa wanatoboa hapa wanahama wanatoboa hapa wanahama sasa nchi nzima itakuwa matobo tu! Tutafute vifaa vya kutosha vya kuonesha kwamba hapa jamani kuna dhahabu muweze kutulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dotto ninakuomba baada ya bajeti yako kupitishwa hapa naomba uende Nyabuzume Jimbo la Bunda uende Nyaburundu Jimbo la Bunda, uwasaidie wale wachimbaji wadogo wapate mikopo kuna dhahabu pale mabilioni na mabilioni ya matani ya dhahabu iko pale tuwasaidie wapate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere. Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya hususani katika Wizara hii. Tumeshuhudia hivi karibuni tu kwa suala la madini ya kinywe kule Songwe na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Waziri Dkt. Dotto Biteko pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kihuswa. Vilevile Katibu wetu Mkuu Ndugu Kheri pamoja na wote wanaomsaidia na kwa ujmla Wizara yote ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu mwingine nisije nikasahau naomba niwaulize Wizara ya Madini, ni lini yule mwekezaji ambaye alisema anataka kuwekeza katika mgodi wa dhahabu kule Mpepo Wilaya ya Nyasa atakamilisha kulipa fidia zake na kuwaacha wananchi wawe huru wakaendelee na maisha yao maeneo mengine, kuliko hii hali ya kusubiri leo kesho, kesho hakuna kinachoendelea, naomba kwa kweli hilo nipate jibu kwa sababu ni suala ambalo linasumbua katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo nirudi katika masuala ya kitaifa. Rais wetu Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alisema namnukuu “usipokuwa na mjomba jijombeze mwenyewe” sisi Bunge hili hatuna mjomba mwingine wa kutujombeza bali sisi wenyewe, utakuta wadau wengine

wanasema Wabunge wanakaa mle wanalala tu hawafanyi nini? Jamani katika Wizara hii kuna kazi kubwa imefanyika. Nakumbuka miaka ya 2009 mpaka 2010 tulivyofikia kutunga sheria ambayo ilikuwa inajaribu kujibu matatizo yaliyokuwa yanawapata wananchi wa Mikoa ambayo inachimba dhahabu hususani Geita, tulipoenda kule Kamati yetu ya Nishati na Madini wakati huo tuliona huruma tulitoka machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wananchi ambao maeneo yao zinatolewa dhahabu zinasafirishwa kwa ndege huku na huku watu wanastarehe, lakini watu wake ni maskini sana. Ilikuwa inaumiza yaani ilikuwa haifanani maeneo yanayochimbwa dhahabu na hali halisi lakini leo ukienda Geita, Kahama, Shinyanga maeneo yote ya dhahabu kwa kweli unafurahi, unaona kwamba Wabunge walitimiza wajibu wao wa kutetea nchi hii, kuteteta watu wao katika kipindi chote kuanzia huko mpaka leo hii kupitia taasisi mbalimbali pia zilizokuwa zinatusaidia na leo sasa unaona matokeo ya nini maana ya madini kwa kipato cha mwananchi mmojammoja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Wizara kwa usikivu wao ambao waliujenga hatua kwa hatua, kwa sbabu mwanzo walikuwa wabishi ukiwaambia wanakwambia mkataba ni siri, hii haiwezekani, hili halipo lakini sasa hivi tunakaa tunajadiliana na mambo yanafanyiwa kazi yanakwenda vizuri, hiyo ndiyo maana ya Bunge katika kushauri Serikali *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo *STAMICO* pia ilikuwa ni moja ya mashirika ambayo yalikuwa yabinafsishwe, lakini tukasema hapana hebu tuliache tusichulie *STAMICO* kama ni shirika la faida moja kwa moja, kazi yake inayofanyika inasaidia kujenga uwezo katika nchi kwa kuwajengea uwezo wachimbaji wadogowadogo ambao sasa ni Watanzania na hatimaye watakua, leo *STAMICO* imekuwa ni kinara inaonyesha mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumeshuhudia *STAMICO* ikiongoza mapambano ya kuondoa uharibifu wa mazingira kwa kupanda miti, kusema kwamba lazima tupande miti katika maeneo ambayo tunachimba na maeneo mengine, lakini siyo hivyo tu imefikia kuweza kusaini mkataba wa Bilioni 55.2 wa uchorongaji, anaingia mkataba mkubwa na *GGM* ambayo ni kampuni kubwa ya uchimbaji. Huu ni mfano mzuri wa mashirika yetu kuigwa, kwa kweli nampongeza pia Dkt. Venance kwa kazi kubwa inayofanyika katika shirika hili la *STAMICO* ikizingatiwa na mimi nilianzia kazi *STAMICO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kilichopita cha bajeti nilishauri nikasema kwa nini *TANESCO* au Wizara ya Nishati haipeleki umeme *STAMIGOLD* kwa uwezo wao ili kuondoa hasara inayopatikana ya matumizi makubwa ya nishati ya *diesel* kwa kutumia *generator* wakati wangepata umeme wangepunguza hayo matumizi, leo nimefurahi kusikia kwamba Mheshimiwa Waziri anatuambia jana umeme umewashwa, hayo ndiyo tunayoyapenda mashirikiano kati ya Wizara na Wizara, tena nawapongeza sana Wizara ya Nishati lakini nawapongeza ninyi wenyewe *STAMICO* chini ya Wizara yetu ya Madini kufuatilia na kuhakikisha kwamba mnaondoa hasara hizo kama ambavyo mlishauriwa na Waheshimiwa Wabunge .

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nizungumzie kidogo juu ya suala la wadau tunaowahamasisha kuanzisha viwanda mbalimbali kwa ajili ya kuongeza thamani ya madini yetu. Mara ya mwisho wakati tumeenda Geita kama Balozi wa Wachimbaji Wanawake, tuliamua kumtembelea mwanakiwanda mmoja, Ndugu Sara kwenye Kiwanda cha *GGR*. Baada ya kufika pale, kitu ambacho tulikiona, hatupata picha nzuri sana. Yule mama tuliposema tunamsalimia ili tujifunze anachokifanya, alituambia kwamba jamani msinione hivi, mwenzenu saa hizi nipo kwenye *tension* kubwa sana. Nini? Watu wa *TRA* na watu wa Tume ya Madini wameenda kumkagua,

lakini jinsi ambavyo wanamsemesha, hawataki hata kumsikiliza vizuri. Yaani ni ile hali ya kama Polisi hivi sijui, na Polisi wenyewe sio wa siku hizi, wale wa zamani ambao walikuwa hawafuati ustaarabu. Eeh, nini? Hapana sijui nini! Kila wakati anafikiriwa kwamba mwanakiwanda ni mwizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuiache hiyo tabia. Sisi wenyewe kama hatuwezi kuwekeza, tunawaita *private sector* wasaidie kuwekeza, kwa nini hatuwajali? Kwa nini hatutumii lugha ambazo ni sahihi? Sikupenda suala lile, sikuipenda kabisa, na ndiyo maana tumesema lazima tuseme. Wale watu wamewekeza kiwanda kikubwa cha kisasa kabisa, lazima tuwajali, tuwaheshimu. Wawekezaji wote lazima tuwaheshimu, tuwasaidie, tuhakikishe wanapata dhahabu kwa ajili ya kusafisha kama ambavyo viwanda vyao vilianzishwa, lakini tukiendelea na mtindo huu wa kufikiria tu kwamba mimi naenda kukusanya mapato. Akifunga, utakusanya wapi hayo mapato? Utakusanya wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hatuwezi kukubali. Tunawaambia, Bunge hili msituone sisi sijui tumekuwa wapole, hatuna upole wa kuharibu rasilimali au kazi ambazo tunajua zitaleta manufaa makubwa kwa nchi yetu. Kwa hiyo, tunaomba sana, wale ambao bado wanaendelea kuona kuwa na vile viukiritimba vya kizamani, waache. Sasa hivi wameona mfano mzuri, Mama mwenyewe, Mama yetu, Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anavyosema namna gani tuwashughulikie wafanyabiashara; namna gani tuheshimu wawekezaji; kwa hiyo, ni lazima tuwe na tabia hizo za kuwaheshimu wawekezaji. Tutamfuatilia, mkiendelea kumfanyia fujo, tutawataja humu humu mmoja baada ya mmoja, hadharani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba *GST* waongezewe kiasi cha fedha za utafiti. Hawa wachimbaji

wadogo wadogo pekee yao hawawezi kuwekeza huko. Kama kweli tuna nia kama ambayo tumeanza nayo ya kuwasaidia, basi tufanye hivyo. Serikali ndio inayoweza kuwekeza fedha yake kwa kuchukua *risk* iliyopo na kujua kwamba baadaye huyu mchimbaji ataweza kunufaika yeye mwenyewe na pia kuisaidia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, *GST* isijikite katika baadhi ya maeneo tu. Tumegundua kwamba hayo madini yapo katika maeneo mbalimbali, ila haijajulikana. Kule Mbinga na Nyasa, tulikuwa hatujui kama makaa yangetusaidia kiasi hiki. Leo sasa hivi makaa ya mawe yamekuwa ndiyo chanzo kikuu cha fedha katika Mkoa wetu wa Ruvuma, lakini zamani tulikuwa tunaona ni ardhi tu tunaikanyaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, watu wamekuwa wanasema makaa ya mawe hayafai, ni nishati mbaya, tunakubali, lakini inakuwa ni nishati mbaya tu pale ambapo tunahitaji kutumia sisi kwa mambo mengine! Sasa hivi kunahitajika makaa ya mawe huko duniani, mbona sasa hatusikii, wanachukua kwa nguvu zote! Tumegundua kwamba kumbe tunakataa jambo pale tunapoona hatulihitaji sisi, lakini pale ambapo wao wanalihitaji, linakua ni suala la dharura, ni changamoto imetokea, basi leteni tu. Kwa hiyo, nasema kwamba tusiwe na mchezo huo wa kudanganyana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitoe wito na rai kwa madini mapya ambayo tunaanza kuyachimba, haya wanayaita *rare minerals,* au *critical rare minerals*; naomba sana, tusije tukaingia tena kwenye mtego ule ule ambao tulianza nao wakati tunaanza kuchimba dhahabu. Kwa sababu hayo hatujui tabia yake, hatujui gharama zake. Kwa hiyo, tusipofanya utafiti wa kutosha tutajikuta tunaingia mikataba ambayo leo tunafurahi tunasema kwamba mikataba hii ina faida kumbe ni hasara tu. Kwa hiyo, tuwe makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo la wageni waliopo Bungeni muda huu. Wapo wageni wa nne wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Mbunge, Waziri wa Madini kutoka Chama cha *Tanzania Youth Miners* kutoka Mkoa wa Geita ambao ni Ndugu Eliana Simon, Makamu Mwenyekiti; Ndugu Hamis Mohamed, Ndugu Ashraf Omary pamoja na Ndugu Peter Madem, karibuni sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuonesha dhamira kubwa ya kukuza Sekta hii ya Madini hapa nchini. Vile vile namshukuru kwani alipokuja Njombe nilimwomba amtume Mheshimiwa Waziri wa Madini aje Ludewa aweze kuzungumza na Wachimbaji wadogo juu ya kuwagawia vitalu vya makaa ya mawe. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Doto Biteko na Naibu wake, kwani Naibu Waziri aliweza kufika Ludewa, nimshukuru sana. Vikao vile vimezaa matokeo mazuri. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nashukuru sana kwa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kuikuza Wizari hii ya Nishati na Madini, kwa sababu namba zinamtetea. Tumeona sasa Sekta ya Madini inatoa mchango kwa asilimia 9.7 kwenye pato la Taifa. Jitihada ambazo amezifanya siyo ndogo, kwa hiyo, anastahili

pongezi sana. Kwa hiyo, tunamtia moyo kwamba aendelee kuhakikisha kwamba sekta hii inaongeza zaidi pato la Taifa. Kwa sababu tukiangalia Sekta ya Kilimo ina asilimia 26, Sekta ya Utalii ina asilimia 17. Kwa hiyo, nikiangalia madini tuliyonayo, na mwendo huu ambao Mheshimiwa Dkt. Biteko anao, naamini atasogea na sekta hii itakuwa na mchango mkubwa zaidi kwenye pato la Taifa, na vile vile kuzalisha ajira kwa wananchi. Ndiyo maana Wabunge wengi hapa wamechangia na kuona kwamba kuna haja sasa ya Serikali kuangalia sana wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na wananchi wote wa Ludewa kwa mapokezi mazuri ya Mwenge wa Uhuru. Nilikwenda huko, hamasa iliyokuwa mwaka huu siyo ya mfano. Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi na ninawashukuru. Naomba tunapowahamasisha awamu nyingine, wafanye kama mwaka huu. Kila mmoja aone jambo ni la kwake kama ilivyokuwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ile ya Mwenge, tulipita Kijiji cha Mkomang'ombe, wananchi walikuwa wanalalamikia sana zile fidia zao za Mchuchuma na Liganga. Naishukuru sana Serikali, mnatambua kwamba *exchequer* ilishatoka ya Shilingi bilioni zote 15, lakini nilipofuatilia *NDC* kwa nini hawaendi kulipa fidia? Ilionekana hawajapewa fedha zile za kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kumwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, namwona hapo, atusaidie wananchi waweze kupewa zile fedha, kwani wamezisubiri kwa muda mrefu sana. Kimsingi wananchi wale kwa Mkomang'ombe, Iwela, Kitongoji cha Malamba, wananchi wa Idusi, wanasubiri fedha hizi kwa hamu kubwa sana. Wananchi wale wa Kijiji cha Amani, wananipigia simu kila siku. Kwa hiyo, naomba kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshaidhinisha hizi fedha, wale *NDC* wapewe zile fedha za kufanyia kazi ili waende

mara moja tukamalize mgogoro na wananchi wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba sana, kuna hoja hii ya wachimbaji wadogo. Nilikuwa nasoma ukurasa wa saba kwenye ule Mpango aliowasilisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nikaona watu wa *GST* wamenunuliwa vifaa, mitambo kwa ajili ya kufanyia utafiti. Pia Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yake ule nadhani ni ukurasa wa 84 ameonesha kwamba hawa *GST* kwa mwaka huu wa fedha watakwenda kufanya utafiti wa madini Mkoa wa Njombe. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, naishukuru sana Serikali, kwani Wilaya ile ina madini mengi na hakuna tafiti ambazo zimefanyika ukiacha zile zilizofanywa na Wawekezaji wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Lupanga, kuna chuma unakiona kabisa na unajua ule mkondo wa madini umefika mpaka kule; maeneo ya Utilili, unakwenda mpaka Makete kule kwa Mheshimiwa Festo Sanga. Kwa hiyo, wakienda kufanya utafiti, tunaweza tukajua *potential* ambayo nchi hii tunayo, na tunaweza tukaweka mipango kwa ajili ya kuendeleza. Vile vile wananchi kule wanachimba dhahabu, *ruby*, *sapphire* na madini mbalimbali, hadi hizo *earth minerals* pale Mawengi zipo, lakini hakuna tafiti ambazo zimeweza kufanyika na kujua tuna madini kiasi gani, na je, yanafaa kwa uwekezaji wa kiwango kipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kwenda kufanya utafiti maeneo hayo. Hii itasaidia sana kuongeza ajira kwa wananchi, kwa sababu sasa hivi tuna vijana wengi ambao wamesoma na wengine walipelekwa nje ya nchi kwenda kusomea eneo hili la mafuta na gesi, wengine madini mbalimbali lakini waliporudi nchini hawajaweza kupewa ajira. Baadhi ya wananchi wamekuwa wakitusumbua sisi Wabunge. Kwa hiyo, tunavyokuza Sekta hii ya Madini hasa wachimbaji

wadogo, tunazalisha ajira nyingi zaidi, licha ya kuwa tunaongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba kule Ludewa wale wanaochimba makaa ya mawe, Serikali; namwona Mheshimiwa Jafo yupo, tuangalie sasa mpango wa kusimamia mazingira. Kwa sababu makaa ya mawe wote tunatambua kwamba yana sumu. Kwa hiyo, yanaweza kuleta hatari ya maji yake kwenda kwenye mito na mfumo mzima wa maji, hata haya maji ya chini ya ardhi. Tuweze kuwalinda wananchi kwa kushirikiana na wale watu wa *OSHA* na watu wengine kwa sababu unaweza kupita sehemu nyingine unakuta wananchi wanachambua makaa ya mawe kwa mikono. Hii ni hatari sana. Kwa hiyo, tuweke mpango mzuri wa kusimamia mazingira, kuangalia mfumo mzima wa maji ili kuweza kuwalinda wananchi wasiweze kupata maradhi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hata kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo; twende tukatoe elimu ili waweze kuujua vizuri huu mnyororo mzima wa thamani kwenye Sekta ya Madini. Waweze kujua, wawe na taarifa, tuanzishe *information centers,* waweze kupata taarifa ni namna gani wanaweza wakapata mitaji. Nina mfano mmoja wa mchimbaji yuko Kijiji cha Amani pale Ludewa, anaitwa Berege. Amehangaika, amemtafuta *geologist,* kamwandikia mradi mkubwa. Sasa anahangaika ili aweze kupata mtaji. Kwa hiyo, naomba Wizara hii iweze kuwaita hawa wachimbaji wadogo, iwape taarifa, wafanye nini ili waweze kupata hiyo mitaji kwa ajili ya uchimbaji? Kwa sababu wataajiri Watanzania wengine na fedha hii pia wanaiwekeza hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda sana kuishauri Serikali kama ambavyo Wabunge wengi wameshauri. Bajeti ambayo wanatengewa Wizara ya Madini

hasa watu wa *GST* ni ndogo sana. Hakuna nchi ambayo imeendelea bila tafiti hapa duniani. Kwa hiyo, ilikuwa ni vyema sana, hata kama ni kurekebisha sheria, weka pale sharti kwamba haya mapato yanayotokana na Sekta hii ya Madini; tunaweza tukasema, Bunge likapitisha sheria asilimia tatu hadi tano ziende kwenye utafiti zaidi wa madini, kwa sababu hii itatusaidia kufanya Sekta hii ya Madini iweze kutimiza malengo ya kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bila kuwepo kwa sheria ambayo itatubana, itatulazimisha kuongeza fedha kwenye eneo la utafiti wa kisayansi wa madini, nina hofu kama safari yetu inaweza ikawa na changamoto nyingi. Kwa sababu nchi hii ina mambo mengi, na fedha inahitajika maeneo mengi. Kwa hiyo, kama hamna sheria ambayo inatubana, inaibana Serikali kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa kisayansi, tunaweza tukakutana na changamoto kidogo. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Mheshimiwa Waziri atuletee hiyo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali waangalie eneo hilo. Kuwepo sheria kabisa ambayo inatubana. Hizi tafiti zitatusaidia sana kuweza kuongeza mapato na ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, linahusiana na eneo la madini ya dhahabu. Kule kwetu Ludewa kuna wananchi ambao wanachimba hizi *alluvial gold,* na vile vile zile za kwenye miamba. Hoja hii ya utafiti, ndiyo maana nairudia zaidi, ni vizuri wananchi wale wanaweza, na Mheshimiwa Waziri hata siku moja ukipata nafasi, nikakukusanyia wale wananchi, wakakutana na wewe ukawasikiliza changamoto zao, itapendeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto mojawapo nashindwa kuisema sana kwako kwa sababu inagusa pia Wizara ya Viwanda na Biashara. Wale watu wa *NDC,* vile vitalu walivyovigawa vya makaa ya mawe, wangeweka na mpango

mahususi kwa ajili ya wale wachimbaji wadogo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri wanakunukuu kabisa, kwamba ulikwenda kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na waliomba vitalu kwa ajili ya migodi yao ya shaba ambayo imechanganyika na dhahabu. Kwa hiyo, ukiwasikiliza, utaona namna ya kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema hivyo kwa sababu masharti yale yanayowekwa na *NDC*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Vestadus Manyinyi Mathayo na mchangiaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Henry Maganga Nicodemas.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalam katika Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kipekee kabisa na Naibu wake, watu hawa ni wasikivu sana. Mwaka 2022 nilipata malalamiko jimboni kwangu. Nilipoenda kuwaona, walinisikiliza vizuri na baadaye wakapanga safari. Kwanza nilienda na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini baadaye akaja mwenyewe Waziri. Kwa kweli tulifanya Mkutano mkubwa sana sana wa Wadau wa Makaa ya Mawe. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee

nampongeza Waziri na Naibu wake, wanaitendea haki sana Wizara hii wanayoiongoza. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kikao kile ambacho Waziri alikuja kwa wito wangu, kulikuwa na mambo mengi yamezungumzwa. Kwanza, tulizungumzia suala la *CSR;* na pili, tulizungumzia suala la *local content.* Mheshimiwa Waziri kwenye mkutano ule alitoa maelekezo mazuri sana, kwamba lazima madini haya yawanufaishe maeneo yanamochimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni sisi tumeanza uchimbaji huu wa makaa ya mawe. Nawapongeza sana wenzetu wa dhahabu, wameanza muda mrefu, na sasa hivi angalau manufaa kwenye maeneo yale yanaonekana wazi wazi, lakini maeneo yetu, bado wananchi walikuwa na manung'uniko na masononeko kwamba tunaona tu magari makubwa makubwa yanapita katika maeneo haya, lakini hamna kitu tunachokiona sisi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika tunaona Serikali sasa na Mkoa wetu wa Ruvuma kipato kimeongezeka sana sana. Tunaishukuru sana Serikali. Ila pale yanapochimbwa madini, bado wananchi wale hawajaridhishwa kabisa na namna ile inayobaki pale. Kwa hiyo, mwaka 2022 Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo pale na nadhani mliongelea suala kwamba mnatengeneza kanuni. Sasa pengine ni wakati muafaka Mheshimiwa Waziri ukasema ni hatua gani imefikiwa ya kanuni ile ili sasa na sisi wa makaa ya mawe tuanze kunufaika sawa na wenzetu wa dhahabu kama walivyonuifaika ikiwepo pia na lile suala la *local content*. Ni masuala muhimu sana katika uchimbaji wa haya madini, hususan madini ya makaa ya mawe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri najua unafahamu hiki kikao na maelekezo uliyotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Waziri alilozungumzia pale ni suala la leseni. Katika maeneo haya, ziko leseni zilizokwisha muda wake. Wapo wamiliki wamekaa na leseni hizi lakini hawafanyi kazi na muda wake umekwishwa. Kwa hiyo, kupitia kikao kile, Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwa wachimbaji wadogo. Nina orodha ya wachimbaji wadogo wadogo wanaendelea kufuatilia utekelezaji wa yale maelekezo yako. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, basi kama ziko hizo leseni, tuwatangazie wale wachimbaji wadogo wadogo nao wapate maeneo waweze kuchimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika, kwa uwezo pamoja na Naibu wako na Wizara kwa ujumla, mtalifanyia kazi hili haraka ili wananchi wale wa Mkoa wa Ruvuma nao wanufaike na rasilimali iliyopo katika mkoa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuliongea ni la Kitaifa zaidi, ni suala la uchimbaji wa madini haya ya chuma *(metallic minerals)*. Nchi yetu imebarikiwa sana na madini haya. Bahati nzuri yapo, na bahati nzuri yanatumika sana ndani ya nchi hii. Madini haya ndiyo yanayoenda kwenye viwanda hivi vya *cement*. Kwa wale ambao hawajui, utaona kama mawe hivi yamekaa humo barabarani, hayo ndiyo madini yanayoitwa *metallic minerals,* na kazi yake kubwa ni kwenda kutengeneza *clinker* kwenye viwanda hivi vya *ciment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wako wachimbaji waliokuwa wanaendelea kufanya hii kazi, lakini wanakatishwa tamaa na tozo zetu. Wanaochimba hii *metallic minerals* tumewawekea *loyalty* ya 6% pamoja na ushuru wa *inspection* wa 1%. Ukijumlisha wachimbaji hawa kwa jumla wanatoa 7%. Hii inakuwa tofauti na wachimbaji wengine wa madini kama ya *gypsum*, na madini mengine ya namna hiyo. Wao pamoja na makaa ya mawe, wao wanatoa 3% na *inspection* yao 1%. Kwa hiyo kule wanakuwa na 4% lakini wale kule wanakuwa na 7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki ni kikubwa sana, nina ushahidi wa baadhi ya maeneo wachimbaji hawa wameacha uchimbaji, wameona sasa bora tufanye shughuli nyingine kuliko kuchimba na kuendelea kuumia wakati faida inayopatikana humu ni kidogo sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri unalijua hili vizuri sana, lifanyie kazi ikiwezekana basi wote twende kwa, iende *flat rate* kwa sababu wote hawa wanachimba ni *minerals* hizi za viwandani, wote hawa wanachimba *raw materials* za viwandani kwa hiyo kwa vile hawa tumewa-*charge* kwa 3% basi na wale nao wa *metallic minerals* basi tuwapige nao kwa 3%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hapo hapo kwenye hizi *metallic minerals*, nchi yetu hii ina viwanda vingi sana vinavyotumia hii *metallic materials* lakini kinachoonekana sasa hivi hivi karibuni kuna kitu kimefanyika ndani ya nchi yetu. Ninakumbuka sisi miaka mitano iliyopita na hadi sasa hivi tulikuwa tuna-*promote* viwanda vyetu vya ndani. Sasa kupitia hiki kinachoenda kuendelea sasa hivi kinaenda kuharibu utaratibu huu wa kulinda viwanda vyetu vya ndani na wazalishaji wetu wa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema nini? Viwanda vyetu vinavyotumia hizi *metallic minerals* zimeingia na mpango wa kutumia *copper slug*. *Copper slug* naweza kusema labda kwa lugha ya Kiswahili ni pumba, pumba za *copper*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani *copper* ile inachimbwa huko inakochimbwa, inapelekwa huko nje, inaenda inachakatwa huko, yale mabaki mabaki yale yanarudishwa ndani ya nchi wanayatumia tena kwenye viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vile viwanda vilivyokuwa vinatumia hizi *metallic minerals* hizi, vinakwepa sasa kununua *metallic minerals* hizi chuma hizi, haya mawe unayoyaona na wewe unapita hii njia ya kwenda kama unaenda Manyara, kuna

mawe yanapatikana kuanzia hapa Maya Maya unaenda mpaka unapita Chemba hivi kuna mawe yanapatikana hapo. Yale mawe ni muhimu sana na ndicho chuma chenyewe kinachotumika watu wa viwanda vya *cement* wanayatumia haya kwa ajili ya uzalishaji wa *cement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanakwepa kuyanunua haya, wanakwenda kuchukua hiyo *copper slug* mbadala wa hii *metallic minerals*. Athari yake ni nini? Athari yake tunaenda kupoteza hadhi kwa hawa wananchi wetu, tunaenda kupoteza ajira, tunaenda kupoteza mali zetu ambazo tunazichimba humu humu nchini. Hawa wanaenda kuchukua haya na bahati mbaya sana sina uhakika Mheshimiwa Waziri kama tuna uchimbaji mkubwa wa hii *copper* hapa nchini. Najua *copper* zinazalishwa nje zaidi kuliko sisi wenyewe na pale jimboni kwangu *copper* ninayo lakini hatujaanza kuchimba lakini hii inayotumika sasa ni ya wenzetu, tuna wanufaisha wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa nia ile ile ya *local content* hapa tutakuwa tunaenda nje ya utaratibu wa *local content* kwa sababu tunajua lazima tuwape kipaumbele watu wetu na tunapowapa kipaumbele watu wetu ndipo tunapozalisha zaidi. Ndipo tunapotumia rasilimali zetu lakini pale tunapotumia hizi kutoka nje maana yake uchumi wote tunaupeleka wapi, nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri sijajua hili limetoka hivi vibali vimetoka kwako? Kwa sababu pale nyuma tulidhibiti hili hivi vibali vilikuwa havitolewi. Sasa aliyetoa hiki kibali kwa kweli sisemi kwamba haitendei lakini siyo sawa sawa. Lazima twende tuvilinde viwanda vyetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana muda wako umeisha naomba umalizie, muda wako umeisha. *(Makofi)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naunga mkono hoja lakini nikuombe sana Waziri suala hili ulitolee maelezo na ufafanuzi ili tunufaike ndani ya nchi hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Maganga Nicodemas.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi niweze kuchangia katika hii Wizara ya Madini. Nitaungana na wenzangu tu kumshukuru Ndugu yetu Waziri Biteko pamoja na Naibu Waziri. Kusema kweli kazi yao inaonekana na hasa pale ambapo wameweza kujitahidi kuhakikisha kwamba ndani ya muda mfupi wachimbaji wadogo wanaweza kuchangia kwa 40%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli katika nani yangu nitajikita tu kwa hawa wachimbaji wadogo maana ninawaona wako majirani zangu pale wa Buhemba naona ni namna gani wanahangaika. Wako majirani zangu wa Sirorisimba lakini hata kule kwa Kinyigoti. Tunaona kwamba ni kwa kiasi gani ambavyo wanapambana sana wanajitahidi lakini wanakumbana na vikwazo vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Wizara imejitahidi sana kuwasaidia lakini tunadhani inahitaji ifanye zaidi ya hapo. Uzuri wa wachimbaji wadogo kwanza uzuri wao ni kwamba wana *multiplier effects*. Yaani mchimbaji mdogo akipata, yaani utaona amejenga nyumba, akipata ameendelea kufanya biashara nyingine yaani ile fedha anayoipta anarudi ku-*reinvest*. Kwa hiyo, hii inasaidia sana katika kwanza mzunguko wa fedha lakini na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na wale wawekezaji ambao wanatoka nje wakubwa tunawahitaji lakini wao ni kwamba zaidi ya ile kodi ambayo tunabahatisha tunapata, hata *CSR* yenyewe wanatoa kwa mbinde sana. Kwa hiyo, tuna kila aina ya sababu na nikuombe Mheshimiwa Doto, umefanya kazi nzuri na kazi kubwa, nawewe kama kiongozi wa Wizara hii mojawapo ya kazi kubwa ya kiongozi ni kufanya mambo yafanyike. Sasa kati ya jambo moja ambalo unahitaji ulifanye hebu jipe malengo ndani ya miaka miwili, mitatu hawa wachimbaji wadogo sasa watoke 40% waende 60%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo ni jambo ambalo najua leo ukiamua Mheshimiwa Waziri Doto ni jambo linalowezekana sana. Wachimbaji wadogo hawa yako baadhi ya changamoto ambazo wanapambana nazo. Moja yaani yeye kwanza wao ndiyo wavumbuzi wa madini hasa ya dhahabu. Anachokifanya huwezi kuamini, mchimbaji mdogo anahangaika huko porini anakuja anakutana na mwamba, wa pili anakuja, mwingine anakuja mwisho wanakuwa wengi pale. Anatokea tu mtu wa kawaida anaenda pale na *GPS* anachukua *coordinates* akitoka pale anaenda kwenye *portal* tayari analipa shilingi 50,000 lile eneo linakuwa ni la kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wale wachimbaji wadogo waliokuwa wanachimba pale wote wanaondolewa, lile eneo unapewa wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli yaani tunawapa adha kubwa. Kwa hiyo, ombi langu Mheshimiwa Waziri ambalo linawezekana, hebu yeyote yule wachimbaji wadogo wakishaanza pale, kwanza wanatambulika mpaka kwenye vijji vile wanavyofanya kazi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inapotokea tukitaka kuwasaidia inapotokea kwamba kuna mtu ameenda pale

ameingiza kwenye *GPS* amepata *coordinates* na amechukua lile eneo, kabla hamjampa, hebu tuangalie nani alianza, ni wale wachimbaji wadogo au ni yeye. Kama ni wachimbaji wadogo ndiyo walianza, hebu tuwasaidie wale wachimbaji wadogo ndiyo waendelee kuchimba pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutawasaidia sana maana shida kubwa ambayo wanaipata ni kwamba wao yaani wakishatafuta, wakipata wanaondolewa hapo. Wakienda mahali pengine wakitafuta wakipata, wanaondolewa hapo. Sasa kusema kweli hii haiwasaidii sana katika kuwa kuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizao lao la pili ambalo wanakumbana nalo ni namna ya kupata ile miamba. Yaani wao wanakuwa tu ni kama waganga wa kienyeji. Anaenda anahangaika hapa miezi sita hajapata kitu anahama. Anaenda mahali pengine anahangaika hajapata kitu anahama. Mwisho anakuja kubahatisha kamchirizi kamwamba kidogo basi ndipo anapata hapo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nini kifanyike katika kuwasaidia? Natambua kwamba ndugu zetu wa *STAMICO* ndiyo *caretaker* wa hawa wachimbaji wadogo. Lakini ukiangalia leo majukumu waliyonayo *STAMICO* wanamajukumu mengi. Wana majukumu makubwa na kusema kweli wanafanya kazi nzuri sasa tukisema tena wao waendelee kuwa ma-*caretaker* wa hawa wachimbaji wadogo hiyo nafasi hawana kwa sababu wakifanya huku ni bure lakini sasa unaachaje uzalishaji wako halafu utumie muda mwingi kwa ajili ya kuwasaidia hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweza kufanya vitu viwili; moja, aidha tukatafuta chombo kingine kama labda *GST* wakawa wanafanya hiyo kazi ya kuwatafutia miamba. Maana unakuta yeye mchimbaji mdogo yule leo anachimba hapa, akikosa anaenda mahali pengine. Lakini kumbe ingekuwa mfano

leo ukija kama pale Buhemba watafiti wakaja pale kama ni *GST* au chombo, taasisi yoyote ile ikawaonyesha kwamba mwamba ni huu maana yake ni kwamba wangeweza kufanya kazi kubwa sana kuliko ambavyo wanahangaika hivi sasa. Kwa hiyo, kama ombi langu tuone namna ya kuwasaidia wale wachimbaji wadogo katika kutambua ile miamba halafu wao waendelee kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza yaani mchimbaji mdogo hata akipata mwamba tu wa sentimita 50 yaani huo tu umetosha kumtajirisha. Kwa sababu wanatumia muda mwingi kufanya kazi ya kubahatisha na ndiyo maana wanaendelea kupoteza na unakuta siku hizi wanakuja watu sijui tuwaite matapeli au ndiyo hivyo tena, wanakuja kwamba na vimashine vya kudanganya na anapitapita hivi nadhani ni *metal detector*, kakishasema hapa anaambiwa chimba hapa. Anaenda mita 30 hamna kitu, anaenda pengine hamna kitu, kwa hiyo hali hii nadhani haiwasaidii sana wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri kama utauchukua huo ushauri wa kuhakikisha kwamba tuna chombo ambacho kazi yake ni kuwatafuta yaani leo nikisema pale Sirorisimba uchimbaji wa pale unakuja unawatafutia.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hussein.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa mchangiaji kwamba ili waweze kufanikiwa hawa wachimbaji wetu wadogo, *GST* pamoja na *STAMICO* wapunguze gharama za utafiti. Mfano, mita moja sasa hivi wana-*charge* shilingi 432,000. Kwa kufanya utafiti wa mita 60 ni sawa na shilingi

29,000,000. Mchimbaji mdogo atazipata wapi? Kwa hiyo wapunguze hizo gharama ili wananchi wetu waweze kufanikiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mathayo taarifa unaipokea?

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo taarifa mimi naipokea kwa mikono miwili, kwamba inavyoonekana hawa watu wengi iwe *GST* iwe *STAMICO* na wengineo nadhani gharama wamechukua zile gharama za zamani zile ambazo wazungu walikuwa wanazileta huku kwetu hizo ndizo wamekuja wame-*copy* na ku-*paste*. Kwa hiyo, unakuta leo unapomzungumzia mchimbaji mdogo kwamba atumie utafiti hataweza ndiyo maana wanahangaika hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo leo sasa kwa kadiri tunavyoenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mathayo malizia muda wako umeisha.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nasema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Henry Maganga Nicodemas, mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa heshima siku ya leo tarehe 28 kuweza kufunga dimba la hii Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru wewe, nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ardhi na dunia kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hii Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mjumbe wa Kamati ya Madini, kwanza napenda nimshukuru Waziri Doto Biteko Mbunge wa Bukombe, jirani yangu. Nimshukuru pia msaidizi wake Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini pamoja na Katibu aliyeteuliwa hivi juzi wa madini ndugu yangu ambaye jina lake sijalikariri vizuri. Niwape shukrani za dhati ya moyo wangu bila unafiki. Nimshukuru Naibu Katibu wa Sekta hii ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli kabisa shukrani ninazozitoa ni za dhati siyo za kisiasa wala za kifitina. Mmekuwa msaada mkubwa sana kwangu. Mwanzoni tulikuwa hatutembei pamoja. Ilikuwa kata funua kata funua kwa ajili ya kero ambazo zilizokuwa kwenye hii Wizara ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifahamishe Bunge Tukufu hili kwamba kwanza hii Sekta ya Madini hapo nyuma tulikuwa hatufaidiki nayo sisi kama Wananchi wa Mbogwe. Kulikuwa na makampuni ya nje ambayo yalikuwa yananufaika pekeyake. Mheshimiwa Doto Biteko Awamu ya Tano ulipoteuliwa kuwa Waziri kulikuwa na migodi kwa mfano Nyakafulu likuwa imekaliwa na Kampuni ya *RUSROT*. Tulikuwa tunaona magari tu yanapishana. Mjie wetu wa Mbogwe Masumbo ulikuwa haujengwi. Mlipowatimua hao mabeberu wananchi wakaingia kuchimba na sasa hivi wilaya ina changamka kwa *speed* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Rais wa Awamu ya Sita Mama yangu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake anazozionyesha kwa wananchi wote wa hapa Tanzania. Lakini pia napenda niwape pole wachimbaji wenzangu ambao wanahangaika na mihangaiko ya hapa na pale kuchimba kwa nguvu zao wenyewe bila kuwezeshwa hata na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda basi leo nijikite kuishauri hii Sekta ya Madini kwa mambo machache ambayo Mwenyezi Mungu atanijalia kuweza kuyataja. Kwanza ifahamike kwamba ninaposema Mkoa wa kimadini Mbogwe nazungumzia wilaya tatu, ambapo Wilaya ya Bukombe imo, ambapo anapotokea Waziri mwenyewe. Nazungumzia Nyang'hwale ni wilaya ambayo tunaungana kwa pamoja kufanya Mkoa wa kimadini Mbogwe. Naomba niishauri Sekta ya Madini hakuna kosa tunalolifanya kama kuandaa hizi bajeti na kutokuweka vipaumbele vya hii mikoa inayotuzalishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika uzalishaji hapa kwenye Kapu Kuu tumeingiza zaidi ya shilingi bilioni 21 ndani ya mwaka mmoja lakini cha ajabu wale wakusanyaji wanaosimamia hizi shughuli hawana ofisi nzuri. Kwa hiyo, niiombe Sekta ya Madini itenge eneo na iweze kuwajengea watumishi wa madini wanaousimamia huu Mkoa wa kimadini Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze *RMO* uliyenipa Mheshimiwa Waziri ni *RMO* ambaye sasa hivi kausingizi sasa kana tulia maana tukero kila kakitokea kakero kwa wachimbaji nampigia simu sehemu fulani kuna mgogoro, anaenda. Ananisikiliza pamoja na wasaidizi wake nampongeza sana wajina langu ambaye anaitwa na yeye Maganga kama mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndugu zanguni huwa siyo mwanasiasa mzuri yaani huwa ninaumia sana pale unapomuona mtu anasimama kuzungumza uongo sehemu yoyote ile. Wamezungumza wenzangu kwamba ukiangalia maandiko yanasema tumewawezesha wachimbaji wadogo tumewawezesha lakini kiuhalisia wachimbaji wadogo hawajawezeshwa chochote kile. Hizi shilingi bilioni 21 ninazozizungumzia ambazo zimeuza mauzo zaidi ya shilingi bilioni 200 ni wachimbaji wenye moko ambao wanaingia kwenye

mashimo wenyewe. Serikali inaenda kuchukua pato la taifa na kuingiza kwenye Kapu Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu ukiona mazingira wanayoyaishi. Barabara hazipitiki, watoto wao hawana madawati kwenye mashule, huku Mbunge wao wa Jimbo la Mbogwe nazungumzia shilingi bilioni 200 zimeingia kwenye Kapu Kuu bila kuangalia fedha hizi zilikotoka. Ni kwa nini Serikali isitengeneze utaratibu wa kuwalipa ruzuku na kuwalipa posho wachimbaji hawa wadogo ili na wao waone faida ya kuwa na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi naweza nikasema haki vizuri haijakaa vizuri na ninaomba unilindie muda wangu nicheze maana bado muda mzuri sana hata nikipiga dakika 15 hamna shida ili kusudi niweke mchango wangu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye mabenki unakuta watu wanasimama huko kwenye Wizara ya Fedha wanasema tumewezesha wachimbaji lakini kiukweli wanamaliza viatu hawa wachimbaji kwenda kwenye mabenki na mikopo hawapewi lakini tukiwa kwenye makongamano na sherehe mbalimbali unaweza ukamwona mtaalam ana-*introduce* hoja akiwa anasema kabisa tumewezesha wachimbaji wadogo, huwa naumia sana. Kwa kweli hilo suala lishindwe na lilegee kwa Jina la Yesu nianomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba ni-*copy* na ku-*paste* mchango wa Mheshimiwa yule wa mzee wangu nanilii, mzee aah! jina nimelisahau yule wa Musoma yule. Mchango wake Getere umekaa vizuri sana. Amezungumza vizuri naomba niunganishe, ni-*copy* na ku-*paste* ndiyo maana nimesema hivyo. Mheshimiwa Waziri fuatilia mchango ule na niko pamoja na Getere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani wachimbaji waonekane wanathaminiwa kwenye hii Awamu ya Sita. Hatupendi kuona mazingira yale yaliyokuwa yanatupata miaka ya 1995, wachimbaji waki nanilii wakihila tu wawekezaji wanakuja wazungu kuwafukuza wachimbaji wadogo na kuwafanya kanakwamba wao ni wakimbizi hawako kwenye nchi yao. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri usiingie kwenye laana hiyo wewe. Natamani uweke historia hata kama ukiona mambo yamegoma sana yaani kung'atuka nalo ni neno ukiona mambo hayaendi kwamba sasa wachimbaji wanaenda kuanza kukosa haki zao unaachia ngazi rafiki yangu kabisa tunakuja kulima na kujipanga kufanya shughuli zingine huko Bukombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu tumeona sasa hivi kuna baadhi ya wawekezaji wakija hapa nchini hawawathamini wachimbaji wadogo wazawa. Wakifika wengine wanafikia polisi. Wanapokuta watu wamehila wanawafukuza kwenye maeneo yao. Hawafuati sheria za kuwalipa fidia wenye maeneo ambao wamekaa nayo maeneo miaka nenda rudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana kuanzia wewe kama sheria zetu haziko vizuri tuzirekebishe ili kusudi tuwajali watu wetu. Haiwezekani mtu amemiliki ardhi zaidi ya miaka 100, mtu anaingia kwenye mtandao tu akiwa Australia au Marekani anapewa leseni. Anakuta tayari kuna wananchi wanaishi vizuri pale yeye kwa kuwa ana leseni anakuja na mabunduki anakuja kuhamisha wananchi. Wanabaki wananchi wanalia. Sawa natambua kwamba ardhi ni mali ya Serikali lakini lazima kauzalendo tukaweke sasa. Hii ardhi ya Serikali kuna watu ambao wamemiliki zaidi ya miaka 100, unawaachaje? Kwa nini na wao wasiingizwe kama maeneo yao wamemiliki yenye dhahabu wasiingizwe kwenye leseni humo ili kusudi na wao waweze kufaidika na ardhi yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakujua una uwezo mkubwa kaka yangu. Kabla hata hujawa Mwenyekiti wewe ulikuwa Mwalimu wangu ulikuwa unanifundisha jinsi ya kuishi hapa Bungeni. Kwa hiyo, nikuombe sana kwa *power* uliyoipata tuweze kuwasaidia wananchi wetu waliotuchagua waweze kunufaika na rasilimali zao ili wawekezaji hawa wanaokuja kwa wingi wawafaidishe wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine hapa Mheshimiwa Waziri napenda nishauri, zipo kero ndogo ndogo ambazo zinaweza zikatucheleweshа zikatufanya hata kutukosesha usingizi tena. Kwa mfano, hizi kodi za matela ya punda, tunasema ni madini ujenzi, nakuomba Waziri hizi kero zingine ndogo ndogo ni kufuta tu ili wenye matoroli ya punda hata Bukombe huko pamoja na Bukombe na Nyang'hwale waweze kufanya shughuli hizi bure. Kwa sababu toka zamani ilikuwa ni bure tu lakini sasa hivi hizi fedha hata kwenye kapu lako huwa haziingii zinabaki halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uwaonee huruma wananchi wako ambao ni wachimbaji wako uwe tayari kama Bashe ambavyo huwa namwona anapambana na mabeberu yanapokuja kununua mazao na kuwadhulumu wakulima na wewe uwe mkali hivyo ili kusudi wananchi wetu waweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine naomba nishauri hata hii Wizara ya Madini. Niombe maeneo yenye migodi yote barabara nyingi hazipitiki na ni maeneo yana uzalishaji kila siku yanatoa pamoja na kwamba sasa hivi hali siyo nzuri sana. Serikali ione sababu ya kwenda kuweka zahanati ili wachimbaji hawa wanapoumia waweze kutibiwa kwenye maeneo ya karibu. Tumeshuhudia watu wanaumia wakiwa wanachimba wakipondwa hata kuvunjika mguu mpaka akafike kwenye kituo

cha afya anafika tayari ameshaathirika na kupata maradhi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali kwa vile inakusanya tozo kwenye haya maeneo iyape kipaumbele yawekewe zahanati pamoja na huduma zingine, barabara ziwe safi lakini pamoja na vijiji vile vinavyozungukwa vinavyoathiriwa na madini, Serikali iweze kutoa mchango mkubwa ili kusudi tuweze kuona faida. Haiwezekani kuna wilaya zingine humu nikiangalia zinachukua mabilioni mengi kwenye Kapu Kuu sisi tunaokusanya vingi tunatoka bila bila na kukaa kwenye maeneo chakavu tunabaki tunatukanwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana na kale kaswali kangu ka asubuhi nimeomba uwanja wa ndege. Watu wanahila kule kupanda ndege mpaka aende Mwanza zaidi ya kiometa 360. Mimi hapa nina marafiki wengi tundege tupo tudogo twingi tu hapa twa kuchukua lakini hakuna sehemu ya kutua mpaka ukashuke kwenye migodi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia hii Sekta ya Madini na Mheshimiwa Waziri kwa vile wewe ni wa kwetu kabisa na neno la Mungu linasema asiye wajali wa nyumbani kwao kubali kupambana huko kwenye vikao vya ndani na Mheshimiwa Rais umuombe na sisi tuwekewe kiwanja cha ndege pale Masumbwi mjini eneo lipo tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme tunafanya hizi shughuli kwa mujibu wa maelekezo ya Chama kwenye ukurasa wa 105 mpaka ukurasa wa 107 imefafanuliwa hii Sekta ya Madini kwamba tutafanya nini kuanzia mwaka 2020 mpaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana wataalamu wetu pale mnapoandaa hata hizi *proposal* muendane na mkataba wetu na wananchi kwamba tuliahidi nini kwa

wananchi? Tusiende tu yaani kupuyanga tu halafu tuwe kama vile hatujasoma wote humu. Tuwe tunaangalia mkataba wetu na wananchi ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tumeahidi tutawasaidia wachimbaji, tumeahidi tutawasaidia vifaa vya kuchimbia nashukuru nimeona ma-*caterpillar* wakati nasoma hotuba Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe kaka yangu, ninao wachimbaji pale Mbogwe nipe nafasi ya upendeleo wapatikane hata mabilionea hata watano pale kutokana na haya ma-*excavator* yanayomilikiwa na hili Shirika la *STAMICO* na Mkurugenzi wa *STAMICO* nina imani unanisikia. Pale Mbogwe kuna kila sababu ya kuweka *CAP*. Zikiwa zinachimba hizi *caterpillar* halafu tukawa na kiwanda *CAP* watu wanazalisha pale maana sasa hivi miundombinu tunayotumia ni ya *plant*. Tunachenjua huku tunakunywa sumu lakini tukipata *CAP* tunakuwa tunazalisha kwa haraka na pato litaongezeka zaidi ya 60%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine *GST*. Watu wa *GST* nimeona humu mmeongeza bajeti. Niombe sasa kwenye maeneo yangu hii migodi 88 ambayo wananchi wanachimba wenyewe iende ikafanyiwe *research* na mtuambie hii migodi dhahabu inapatikana kilometa ngapi kwenda chini ili wananchi hawa wawe na imani wanapokuwa wanapambana wajue kwamba tunazama shimo la urefu wa kilometa ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa na cha mwisho kingine niiombe sana Sekta ya Madini. Huwa kuna Kiswahili hawa wanasema kwamba samaki mmoja akioza, wote wameoza. Mheshimiwa Waziri usisite kuchomoa wale wabovu pale wanapoonekana wanakuchanganya, chomoa tupa chini safari iendelee. Hata Yona alitupwa akamezwa na samaki baadaye akaenda kuibukia kwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hizi bilioni ulizoziomba 89,357 sina kesi na wewe na wala sitashika shilingi. Nikuombe tu Mwenyezi Mungu akutangulie usiingie kwenye historia tena ya makaguzi makuu haya ya nanilii ya mafisadi nakuombea sana kwa Mwenyezi Mungu usije ukaingia huko wewe. Kila utakayemuona wewe uzuri wewe una mdomo ni mwanasiasa halafu ni mwalimu wangu, sema. Yaani najua ukisema mapema hata dunia inakuelewa siyo kitu kinaharibika wewe umenyamaza tu unalinda ustaarabu. Hakuna cha kulindana yaani wewe ukiona mtu anachanganya pasua ili safari iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na Bwana akubariki sana nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wa leo imekamilika hivyo tumefika mwisho wa shughuli yetu kwa siku ya leo na hivyo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.46 Jioni Bunge liliahirishwa Hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 28 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*